

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 8 Julai, 2009**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2008/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**

Randama za makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 171

### **Kutangazwa kwa Miji Midogo**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 17/09/2004 Miji midogo ipatato 90 ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 353 ambapo Mji wa Mererani ni mionganini mwa Miji iliyotangazwa ukiwa na wakazi wapatao 48,000.

- (a) Je, mionganini mwa Miji iliyotangazwa ni Miji mingapi imekwishaanza?
- (b) Je, ni Miji mingapi iliyopata ruzuku moja kwa moja ya kuijendesha toka Serikali Kuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya miji midogo ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopo kwenye Mamlaka ya Wilaya. Mamlaka hizi zinaanzishwa pale ambapo palikuwa na kijiji ambacho kimeanza kuendelezwa na kuwa na mazingira ya ki-mji. Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amepewa madaraka ya kutangaza kijiji au vijiji vilivyofikia sifa zilizowekwa kuwa Mamlaka za Miji midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganini mwa Miji midogo 90 iliyotangazwa kuitia gazeti la Serikali Na. 353 la mwaka 1994 ni miji 41 ilioanzishwa rasmi ikiwemo Mamlaka ya Mji mdogo wa Mererani. Mji huu ulizinduliwa rasmi tarehe 12 Agosti, 2008. Mamlaka hii ya Mji mdogo wa Mererani ina wajumbe 19, pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu ambaye ameteuliwa na Baraza la Mamlaka ya Mji mdogo. Aidha, vijiji vilivyokuwa ndani ya Mamlaka ya Mji mdogo vimefutwa na sasa kuna vitongoji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna miji midogo iliyokwisha anzishwa ambayo imepokea ruzuku moja kwa moja ya kuijendesha kutoka Serikali Kuu. Mamlaka za Miji midogo, bado zinaendelea kupokea ruzuku zinazopitia kwenye Mamlaka za Wilaya zilizomo kwa kuzingatia Bajeti zilizojiwekeea.

Mamlaka ya Mji mdogo wa Mererani haukutengewa fedha yoyote kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa sababu ilikuwa haijaanzishwa rasmi. Katika mwaka 2009/2010,

Mamlaka ya Mji Mdogo, wa Mererani imeandaa Bajeti yake ambayo imejumuishwa na ile ya Halmashauri ya Wilaya Simanjiro.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la pili.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa umbali wa kutoka Mji mdogo wa Mererani kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ni km 145; na kwa kuwa Mji huu wa Mererani una wakazi wapatao 48,000. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwapa ruzuku moja kwa moja ili miji hii iweze kuwahudumia wananchi hawa?

Swali la pili; kwa kuwa mji mdogo wa Mererani umepata neema ya kuwa mionganoni mwa miji iliyotangazwa kama eneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na kwa kuwa mji huu sasa unahitaji wawekezaji.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba ina boresha miundombinu ya kuwavutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na barabara kwa kuweka lami, barabara inayo toka *KIA* kwenda Mererani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupewa ruzuku moja kwa moja na Serikali; kwa mujibu wa Sheria mpaka sasa hivi Sheria yetu inasema kwamba miji yote midogo inapata ruzuku yao kuititia kwenye Halmashauri husika kwa sababu Sheria hiyo haijabadilika inabidi ruzuku hizo zipitie kwenye Halmashauri husika hadi hapo Sheria itakapobadilika. (*Makofi*)

Nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli umbali kutoka Mererani mpaka Simanjiro ni mrefu sana na ndiyo maana tumeuanzisha huo mji mdogo wa Mererani ili uweze kupanuka na ili baadaye uweze kujitegemea kuwa mji kamili na wakati ukiwa mji kamili utakuwa unapewa ruzuku moja kwa moja.

Kuhusu suala la wawekezaji nafahamu kabisa kwamba Mererani kuna uwekezaji na wawekezaji wengi wanavutika kwenda huko na miundombinu yake sio mizuri sana.

Lakini Mheshimiwa Dorah kama anavyofahamu kwamba barabara kutoka *KIA* hadi Mererani inaboreshwa mwaka hadi mwaka ili iweze kuitika vizuri na barabara hiyo inapitika vizuri. Ombi lake naomba nishirikiane na wenzangu wa miundombinu kuona kwamba kama kuna uwezekano wa kuweka lami kutoka Mererani hadi *KIA*.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile mji wa Mbinga una hadhi hiyo ya kuwa mji mdogo na kwa kuwa tangu mwaka 2004 wamekuwa wakijaribu kuanzisha Mamlaka ya Mji mdogo na bado hawajafanikiwa. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari hata leo kuongea na Mkurugenzi

kubaini ni tatizo gani linalowapata watu wa Mbinga hadi sasa kushindwa ku-*operate* kama Mji mdogo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba mwaka 2004 tulitangaza Mamlaka za Miji midogo 90 lakini mpaka sasa hivi iliyoanzishwa ni Mamlaka za Miji midogo 41 tu.

Hii ni kutokana na Halmashauri zenyewe kujipanga vizuri. Kama wameamua hata leo kwamba Mamlaka yetu iwe ina kuwepo, kwa sababu sisi upande wa Serikali tumeshatimizi wajibu wetu wa kutangaza ni wao katika Halmashauri husika kujipanga na kuamua kwamba sasa mji mdogo wetu tuuendeleze na *procedure* Wakurugenzi wanazifahamu Waheshimiwa baadhi ya Wabunge wanazifahamu na baadhi ya Mamlaka za Miji Midogo zimeanzishwa na sasa hivi zimekuwa zimefikia katika hadhi ya kuwa Mamlaka za Miji kamili. (*Makofi*)

Na. 172

**Kituo cha Afya Kikombo Kupewa Mgao  
wa Dawa na Vifaa**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kikombo ulikamilishwa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma zaidi ya miaka miwili iliyopita; na kwa kuwa utaratibu wa uanzishwaji wa kituo hicho ulikwishakamilika.

- (a) Je, kwa nini Serikali haijanza kupeleka mgao wa dawa na vifaa ili kukiwezesha kituo hicho kutoa huduma zinazostahili kutolewa na Kituo cha Afya?
- (b) Je, Serikali iko tayari kuanza kupeleka dawa na vifaa hivyo haraka ili wananchi waanze kupata huduma hiyo muhimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ujenzi na taratibu zote za uanzishwaji wa Kituo cha Afya cha Kikombo ulikamilika katika mwaka wa fedha 2007/2008. Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma tayari imewasilisha maombi kwa Waziri Afya na Ustawi wa Jamii ili kituo hicho

kiingizwe kwenye orodha ya vituo vya afya na kuweza kupatiwa madawa kulingana na hadhi ya Kituo cha Afya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maombi ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuititia kwa Mfamasia Mkuu wa Wizara hiyo, Kituo cha Afya Kikombo kilianza kupokea madawa ya stahili ya Kituo cha Afya kuanzia robo ya nne ya mwaka wa fedha 2008/2009 yaani mwezi Aprili hadi Juni, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imekuwa ikikitambua Kituo cha Afya Kikombo na kukinunulia dawa za ziada zinazohitajika ili kuwezesha wananchi kupata huduma zinazolingana na zile za Kituo cha Afya. Sambamba na jitihada hizo Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imepeleka watumishi wenye hadhi ya Kituo cha Afya akiwemo Daktari Msaidizi mmoja, Afisa Muunguzi mmoja pamoja na vifaa vinavyotakiwa.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo kwa kweli yanaleta matumaini wananchi wa Kikombo kwamba sasa watapata huduma za afya kwa uhakika zaidi. Pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili. Kwa kuwa majengo ya Kituo hiki cha afya yalikaa muda mrefu sana kabla hayajaanza kutumika. Baadhi yake haya majengo hivi sasa yana hali mbaya na hasa senyenge yake. Je, Serikali iko tayari kutoa fedha za ziada ili kuyakarabati majengo hayo?

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari hivi sasa kuja awe mgeni rasmi katika uzinduzi rasmi wa kituo hicho cha Afya ambacho tunatarajia kuufanya hivyo hivi karibuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi naomba ujibu kwa kifupi sana kwenda huko najua utakubali tu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hicho kituo cha Afya baadhi ya majengo yamekaa kwa muda mrefu bila kutumika, kwa hiyo yameanza kuharibika.

Nikubaliane naye kweli senyenge kwa kweli imeanza kuanguka. Niseme kwamba kwa kushirikiana na Manispaa ya Dodoma tutahakikisha kwamba tutakiboresha kile kituo cha Afya kwa sababu kinatoa huduma kwa watu wengi zaidi hata sisi Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine tunaweza tukapata huduma katika sehemu hiyo.

Kuhusu kuwa mgeni rasmi aliyepangiwa ratiba ni Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati mbaya katika ratiba hiyo haikuweza kutimizwa. Sasa kama Mheshimiwa Waziri

Mkuu ataniruhusu nikawe mgeni rasmi badala yake kwa sababu ile aliahirisha mimi niko tayari kuja na kukifungua kituo hicho rasmi. (*Makofi*)

Na. 173

### **Kuongeza Mtaji kwa Mikopo ya Wakulima Kupitia T.I.B**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kutoa mkopo kwa wakulima kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania(*TIB*) na kwamba wananchi wamefurahia uamuzi huo:-

Je, Serikali ina mtazamo gani katika siku za usoni juu ya kuongeza mtaji wake ulioanza kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.bilioni kwa kipindi cha mwaka 2009/2011?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa fedha na Uchumi, naomba kujibu swalì la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuiwezesha Benki ya Rasilimali *TIB* iendelee kubaki kuwa chombo cha muhimu katika Maendeleo ya kiuchumi kwa kushiriki kutoa mikopo kwa wakulima sambamba na wananchi wengine kwenye sekta zingine. Serikali itaendelea kuimarisha *TIB* kimitaji ili kuweza kutoa mikopo ya Maendeleo ya muda wa kati na mrefu. Hadi sasa Serikali imeshawekeza mtaji wa shilingi 35.5 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukuza sekta ya kilimo Serikali iliamua kutenga mahsusini shilingi bilioni 3.0 katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kwa lengo la kuwakopesha wakulima kupitia *TIB*. Ni azma ya Serikali kuendelea kuimarisha dirisha hili la kuwakopesha wakulima kwa kiliongezea mtaji zaidi mpaka hapo Benki ya Wakulima inayokusudiwa kuanzishwa itakapofunguliwa.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalì la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni Tanzania ilipata bahati ya kutembelewa na Rais wa Jamhuri ya watu wa China na aliahidi kuipa Serikali ya Tanzania fedha nyingi kwa ajili ya Maendeleo yake.

Je, hivi sasa Serikali iko tayari fedha hizo zitakapofika kumega fungu la fedha hizo kuzipeleka *TIB* kwa ajili ya kuongeza mtaji?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali yetu imekuwa ikifanya majadiliano na Serikali ya watu wa China kuhusu msaada kwenye sekta yetu ya kilimo lakini kipekee kuhusu jinsi ambavyo Serikali ya China wanawenza kushiriki katika

kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo inakusudiwa na hapa ni mambo mawili makuu ambayo yanazungumziwa.

La kwanza Serikali ile ya China itakavyotusaidia katika utaalam maana wana uzoefu mkubwa. Lakini jambo la pili ni kuhusu mtaji ambao utahitajita katika kuanzisha Benki ile na tunachotazama hapa ni kiasi gani na kwa namna gani Serikali yetu inaweza kushirikiana na Serikali ya watu wa China katika kuanzisha Benki ile na kwa njia hiyo kilimo kitakuwa kimeshapata chombo cha kukihudumia.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yameonesha kwamba dhamira ya Serikali ni kuiwezesha Benki hii iweze kufanya kazi vizuri na haswa kwa kuiongezea mtaji wake ambao utasaidiwa zaidi katika suala zima la shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kwamba kuna shilingi bilioni 15 za *EPA* zingepelekwa *TIB*. Napenda kujua hii fedha imeshapelekwa au bado?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika zile fedha bilioni 53. Serikali iliamua kwamba bilioni 40 zingekwenda kwenye kilimo na bilioni 10 zingekwenda mifugo na bilioni 3 zingekwenda *TIB* kwa lengo la kufungua dirisha la mikopo kwa wakulima mpaka sasa ni kweli kwamba Serikali imeshawapa *TIB* shilingi bilioni moja bado shilingi bilioni mbili. Lakini mahitaji ya *TIB* ni makubwa kuliko bilioni 3 zile. Kwa hiyo Serikali inachofanya ni kutazama uwezekano wa kuipa *TIB* nguvu zaidi kimtaji na tunakisia kwamba *TIB* kuweza kuwa na nguvu ya kutosha itahitaji mpaka kuwa na shilingi bilioni 150. Kwa hiyo, shilingi bilioni tatu sawa lakini Serikali inatazama mbali zaidi ya shilingi hizo bilioni tatu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ilikuwa bilioni tatu na sio 15. Tunaendelea na swali linalofuata kwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 174

**Kuwepo kwa Mashine ya kusafisha Figo  
Hospitali ya Muhimbili**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, mashine za kusafisha damu ndani ya figo katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili haifanyi kazi hivyo wananchi kulazimika kwenda hospitali binafsi ambako hulipishwa gharama kubwa na wengi wao hushindwa kuzimudu na kuishia kuomba misaada kwa jamii:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa mashine hii kuwepo ili kulinda maisha ya wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
**(K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge wa Ilala, naomba kwanza nitoe maelezo kwamba Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imekuwa haitoi huduma ya kusafisha figo na kwa sababu hiyo haikuwa na mashine ambazo Mheshimiwa Mbunge anasema hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya taarifa hiyo sasa naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo nchini, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeazimia kuhakikisha kuwa huduma hii muhimu inapatikana katika hospitali zote za Rufaa Serikali. Tayari huduma hii imeanza kutolewa katika hospitali ya rufaa ya Mbeya.

Aidha, hivi sasa Serikali inafanya maandalizi ya kuanzisha huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya vyumba vyta kutolea huduma yamekamilika na mashine 8 kwa ajili ya huduma hiyo tayari zimekwishanunuliwa. Mashine 7 kati ya hizo zimefungwa na moja imehifadhiwa kwa ajili ya dharura(*standby*).

Aidha, Madaktari Bingwa wawili tayari wameajiriwa baada ya kufuzu masomo yao katika fani ya Magonjwa ya Figo, kinachosubiriwa sasa ni kufunga mtambo wa kusafisha maji na fedha kwa ajili hiyo na mahitaji mengine zimetengwa. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya shughuli hii. Matarajio yetu ni kwamba huduma hii itaanza kutolewa katika mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namwonea huruma Naibu Waziri aliyejibu swal kwa sababu maswali la nyongeza yatamshinda kwa sababu siyo Wizara yake.

**NAIBU SPIKA:** Hapana huyu ni Daktari kabisa. Wewe uliza swal.  
(*Makofii/Kicheko*)

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hajui takwimu za pale. Kwanza naipongeza Muhimbili kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Lakini kwa hili Serikali isikwepe majukumu yake ya kujua mtambo huu nilioutaja upo na ni *the right machine* haifanyi kazi na wagonjwa wengi wanakwenda kutibiwa hospitali za nje kwa gharama kubwa sana; na kama Serikali sasa imeona kuna umuhimu.

Je, Serikali inajua ni watu wangapi wamepoteza maisha kutokana na mitambo hii kutokuwepo?

Je, Waziri mhusika hasa yule Naibu yupo tayari kuambatana na mimi kwenda kukagua hospitali hii na kutazama mitambo hii?

**NAIBU SPIKA:** Hilo la pili Waziri akija mtaambatana naye.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
**(K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kupokea shukrani zake. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Hospitali ya Muhimbili, mimi nimesoma pale, nimefanya kazi pale na nimekuwa nakwenda pale Muhimbili mara kwa mara kupeleka wagonjwa.

Hizi mashine ndiyo zimeagizwa sasa hivi na nafikiri wananchi wanafikiri hazifanyi kazi kwa sababu hazijaanza kufanya kazi na hizi mashine haziwezi kufanya kazi kwa kutumia maji ambayo yanatoka kwenye bomba sasa hivi ni lazima tupate mashine ya kusafisha yale maji kuondoa *chemical* zote ambazo zinasafisha yale maji na kuyafanya yawe na maji ambayo hayataleta *reaction* kwa mgonjwa anayefanyiwa usafishwaji. Naomba kusema kwamba ni mashine moja tu ndiyo inafanya kazi iko katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya lakini Muhimbili sasa hivi tutakuwa na hizo huduma mapema iwezekanavyo.

Naomba niseme kwamba kwa sababu hawa wagonjwa wanafariki kwa figo ni nchi nzima wala si Dar es Salaam tu ni vigumu kuweza kupata takwimu. Kutembelea Muhimbili mimi nitapeleka kwa Mheshimiwa Aisha Kigoda mtapanga safari na mtakwenda wote na utaona ile mashine ni mpya kabisa.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa upasuaji wa figo ni nyeti sana na unasababisha vifo vingi vya wagonjwa.

Serikali katika kufunga mashine mpya. Je, inaweza ikafunga mashine ya kuondoa mawe kwa kutumia *laser beam*?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**  
**(K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wagonjwa wengi ambao wanapata matatizo ya mawe kwenye figo.

Naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi kuna hospitali za *private* pamoja na Hospitali ya *KCMC* ambazo sasa hivi zinatoa huduma ya *lazer operation* na nafikiri kwa sababu ni jambo jema ambalo litatupunguzia hata matumizi ya madawa katika *theatre* zetu ninafikiri kwamba kwa hatua jinsi ambavyo Serikali itakuwa inapata pesa kama ilivyonunua hizi mashine nydingine basi wataangalia uwezekano wa

kuweza kununua hiyo mashine lakini kama uwezekano wa Bajeti utakuwepo.  
(*Makofii*)

Na. 175

### **Bajeti ya Miradi ya Umwagiliaji Muheza**

#### **MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-**

Kwa kuwa Wilaya ya Muheza ina zaidi ya miradi mitatu ya umwagiliaji katika Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*), kati ya miradi hiyo ni ya Misozwe, Potwe, Mkuzi/ Mindu na Mashewa; na kwa kuwa gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ni kubwa, mikakati ya utafutaji wa fedha na usimamizi wa miradi umekuwa chini ya Wizara ya ya Maji na Umwagiliaji kuititia Ofisi za Umwagiliaji za Kanda:-

- (a) Je, kuna utaratibu gani wa kuzitaka Halmashauri za Wilaya hasa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuona umuhimu wa kuingiza katika Bajeti za mwaka mahitaji ya fedha za miradi ya umwagiliaji?
- (b) Je, Serikali inashauri nini Halmashauri iwapo kiwango cha juu (*ceiling*) kinachotolewa chini ya Mpango wa DADPS ni kidogo zaidi ya mahitaji ya Bajeti ya mradi mmoja mkubwa wa umwagiliaji uliopo ndani ya Wilaya?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi tu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza dhana ya kupelekea rasilimali zake kwa wananchi kuititia Halmashauri za Wilaya kwa sekta mbali mbali kikiwemo kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Napenda kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe wa Muheza kwa kutumia Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*) wa mwaka 2002 katika kuibua miradi yao. Nazishauri pia Halmashauri za Wilaya nyingine ziendeleze tabia hiyo ya kutumia mipango inayoandaliwa na Serikali kama miongozo badala ya kuyaacha makabrasha kwenye madawati ya ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatumia ngazi tatu za kupendekeza miradi ya umwagiliaji inayogharamiwa na Serikali kama ifuatavyo:-

- (i) Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*): Katika ngazi hii, Serikali inashauri miradi yote ipitie katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya kijiji na Wilaya husika. Na katika ngazi hii miradi midogo midogo isiyozidi shilingi milioni 50 inapendekezwa na kujadiliwa.
- (ii) Mfuko wa Maendeleo wa Wilaya (*District Irrigation Development Fund*): Miradi yote ambayo gharama zake zinazidi shilingi milioni 50 lakini hazizidi shilingi milioni 500 inapendekezwa. Kinachotakiwa katika ngazi hii ni ushahidi tu kwamba wakulima na Halmashauri husika wamechangia gharama za uendeshaji kwa fedha taslimu au nguvu kazi na hasa kwa wakulima.
- (iii) Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Development Fund*): Katika ngazi hii miradi yote ambayo ni mikubwa hususan miradi ambayo miundombinu yake inaweza kuhudumia zaidi ya kijiji kimoja na yenye manufaa mengine zaidi ya kilimo cha mazao inapewa kipaumbele. Kwa mfano, ujenzi wa bwawa linaloweza kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kunywesha mifugo, ufugaji wa samaki, utunzaji wa mazingira na barabara za mazao na kadhalika ni mradi unaopewa kipaumbele. Hakuna *ceiling* ya gharama kwa miradi ya namna hii, kinachoangaliwa ni umuhimu wa mradi kiuchumi na kitaifa na fedha zilizopo.

Uamuzi wa kutenga fedha kwa miradi katika ngazi ya *DIDF* na *NIDF* hufanywa na Kamati maalum inayoundwa na wajumbe kutoka katika Wizara za Maji na Umwagiliaji, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Maliasili na Utalii, Viwanda, Biashara na Masoko, Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Baraza la Mazingira (*NEMC*). Kwa kufuata utaratibu huu, Kamati Maalum ya Wizara za sekta ya kilimo katika kikao chake cha tarehe 15 Juni, 2009 imetenga shilingi bilioni 23.8 kwa ajili ya miradi 94 ya umwagiliaji katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Fedha hizi zinatoka katika *Basket Fund* ya *ASDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa watalaam katika ngazi za kitaifa na Halmashauri za Wilaya kuwasaidia wakulima katika kuibua miradi inayofaa kwa kutumia vigezo vinavyotakiwa badala ya kuwaacha kufanya mapendekezo peke yao jambo ambalo linaweza kuwakosesha miradi mizuri kwa makosa ambayo sio yao. Wizara yangu itaenmdelea kuwapeleka watalaam kutoka Makao Makuu ya Wizara na Ofisi za Umwagiliaji za Kanda kusaidia katika uibuaji na uandaaji wa miradi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mwongozo na utaratibu mzuri sana ambao ameutoa. Na mimi napendekeza kwamba utaratibu huu uwe ndio mwongozo utakaopelekwa kwe nye Halmashauri zote hata Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupitia TAMISEMI. Sasa nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza, fedha zinazotoka katika Mifuko hii, ziko nje ya Halmashauri na zinasimamiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Na mara nyingi usimamizi wa utekelezaji wa miradi hiyo unafanywa na ofisi zao za Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ipo haja sasa ya kuimarisha ushirikiano kati ya zile Ofisi za Kanda na Halmashauri ili Halmashauri nazo zione kwamba mradi ule ni mali yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kumekuwa na matatizo kidogo katika upatikanaji wa hizo fedha na usimamizi wa kazi. Kwa mfano, sasa hivi katika mradi ule wa Misozwe, kipindi hiki ambacho mvua zimekatika watendaji wote na wale wanaosimamia utekelezaji wa mradi wameondoka na wamekwenda kufanya kazi kwenye mradi mwingine na hivyo kazi zimesimama. Je, hamwoni kwamba hii inaweza ikafanya gharama za miradi zikawa kubwa sana na hivyo fedha zilizotengwa siku zote zikawa hazitoshi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu naomba yawe mafupi!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotoka, Mheshimiwa Mntangi anasema ziko nje ya Halmashauri ya Wilaya. Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza, fedha hizi zinatolewa baada ya kujadiliwa na *Agricultural Lead Ministries* nilizozitaja na ndio maana unaona zinaendelea kutolewa hata sasa pamoja na kwamba tunakaribia kuingia katia kipindi kingine cha matumizi ya fedha.

Mimi nataka nimhakikishie kwamba fedha hizi zinapotoka, sisi lengo letu ni kwamba fedha hizi zifanye kazi katika miradi tu iliyokusudiwa. Bado tunaendelea kusema kwamba Kanda tunaziweka tu kwa ajili ya usimamizi wa kitalaam, lakini fedha tunazielekeza katika Halmashauri za Wilaya pale tu ambapo labda kutakuwa na haja ya usimamizi, basi tunapeleka pesa kwa ajili ya usimamizi katika ofisi zetu za kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ameongelea usimamizi kwamba wakati mwingine watalaam wanaondoka na miradi inabadki imesimama. Nadhani hili limempata katika mradi wake wa Misozwe.

Naomba nimhakikishie kwamba wakati mwingine tunalazimika kutuma watalaam kwenda kufanya kama *rescue operation* mahali pengine, lakini si lengo letu kuhakikisha kwamba mradi ule unakwama kwa sababu hiyo.

Naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mntangi ili tuweze kuangalia kama kuna tatizo ambalo limezidi kuwa kubwa, mimi nitahakikisha watalaam wanalirekebisha katika muda huu wa kiangazi.

Na. 176

**Barabara ya Dodoma – Babati**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** a liuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Bajeti ya 2008/2009 ilitenga shilingi bilioni 12 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati kwa kiwango cha lami:-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa lengo hilo?
- (b) Kwa kuwa dhamira ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ni kubwa sana. Je, Serikali haioni kuwa kiasi cha shilingi bilioni 12 ni kidogo sana kwa barabara hiyo yenye urefu wa zaidi ya kilomita 270?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyojibu Waziri wa Miundombinu kwenye hotuba yake ya Bajeti ni kweli kwamba Serikali katika Bajeti ya 2008/2009 ilitenga shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati kwa kiwango cha lami.

Kazi iliyofanyika katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 ni kutayarisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja na makalvati makubwa kwa barabara yote; kazi ambayo Serikali iliona ni vema kuanza nayo. Zabuni za kumpata Mkandarasi wa madaraja na makalvati makubwa zilitangazwa mwezi Mei, 2009 na kuwasilishwa mwezi Juni, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya ni mkandarasi mmoja tu aliyerudisha zabuni. Baada ya kupitia zabuni hiyo, ilionekana gharama ya ujenzi iliyokuwa katika zabuni ilikuwa ni mara mbili zaidi ya gharama iliyokuwa imekadiriwa, hivyo zabuni hiyo haikukubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali ilitenga shilingi bilioni 5.6 na pia imeazimia kutafuta fedha zaidi katika mwaka huu wa fedha wa 2009/2010 kufikia shilingi bilioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati. Hivyo, zabuni zitatangazwa upya kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira ya dhati kabisa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Degera, swali la nyongeza! Lingine halitaulizwa kwa sababu limezungumzwa sana kwenye Bajeti ya Miundombinu suala hili.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa

kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. (*Makofii*)

Lakini hata hivyo naomba niulize maswali ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma wamefarijika na uamuzi wa Serikali kuongeza Bajeti ya barabara hii.

Je, Serikali iko tayari kuwahisha ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

La pili; kwa kuwa mwaka jana, mwaka wa fedha mwaka jana 2008/22009, shilingi bilioni 12 zilitengwa na bado hazijatumika.

Je, hizo nazo zitaongezwa kwenye Bajeti ya mwaka huu ili ziweze kufika bilioni 57? Ahsante!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOANA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali, kama nilivyosema kwamba Serikali kwa kweli ina dhamira ya dhati kabisa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na dhamira hiyo imeonekana kwa Serikali baada ya kuamua kwamba itatafuta shilingi bilioni 45 kuhakikisha kwamba barabara hii inaanza mara moja.

Kuhusu fedha zilizotengwa, shilingi bilioni 45, fedha hizo ni jumla ya fedha fedha ya barabara nzima, kwa hiyo zitaongezewa fedha kiasi ili kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika. Zile bilioni 12 zilikuwa kwa ajili ya makalvati na hizo bilioni 45 inamaana kwamba ni kwa ajili ya ujenzi wa barabara nzima kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea! Hizi barabara zinatakiwa kungojea utekelezaji. Tumetoka kulumbana hapa kwamba ziko bilioni 5 kwenye kitabu cha Makadirio, bilioni 40 Serikali itatafuta na hizo ni za kuanzia madaraja, lakini wafadhili wanatafuta hela zingine za kujenga barabara hiyo kutoka Dodoma mpaka Babati. Hivyo ndivyo tulielezwa hapa katika Kiao cha Bunge. Kwa hiyo, tungoje utekelezaji.

Na. 177

#### **Mwongozo Juu ya Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa mwongozo gani kwa wananchi wa Kata za Gare, Kwai, Malibwi, Makanya na Mbwelo ambao wako tayari kushiriki katika ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika kata zao?

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijbu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufahamu umuhimu wa huduma za Mahakama kwa wananchi, Serikali inatoa mwongozo unaozishirikisha Halmashauri za Wilaya pamoja na wananchi katika ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo yao, na kwamba Halmashauri na wananchi walio tayari kushiriki katika ujenzi wa Mahakama wanashauriwa kuwasiliana na uongozi wa Mahakama kupitia kwa Hakimu wa Wilaya Mfawidhi ili kumwonyesha kiwango cha utayari wao katika mchakato mzima wa ujenzi.

Taarifa hizi za Halmashauri na wananchi zipelekwe kwa Hakimu wa Wilaya Mfawidhi ili Serikali ijulishwe ni kwa kiwango gani inastahili kuchangia ili kukamilisha ujenzi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwongozo huo ningemwomba Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, kuwaarifu wananchi wa Kata za Gare, Kwai, Malibwi, Makanya na Mbwelo kwamba wawasiliane na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Lushoto kuhusiana na kiwango cha utayari wao katika ujenzi wa Mahakama hizo ili Serikali iweze kujipanga kuchangia sehemu ya mchakato wa ujenzi huo.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali la nyongeza. Je, kama wananchi wa maeneo hayo wako tayari kujenga maboma mpaka mtambaa panya. Je, Serikali iko tayari kugharamia shughuli zilizobaki kukamilisha Mahakama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosemakatika jibu langu la msingi kwamba endapo wananchi watakuwa wamechangia na Halmashauri yao wakafikia kiwango ambacho wanaona kwamba ndicho ambacho wanaweza, basi, watashauriana au watapeleka maombi yao kwa Hakimu wa Wilaya Mfawidhi na uongozi wake na wale wataleta Wizarani na jibu litapatikana.

Lakini la muhimu ni kwamba mchango wa wananchi na wa Halmashauri uwepo na kutokana na mchango huo na utayari huo, basi Serikali Kuu itakuja kuona nini la kufanya katika kuwasaidia wananchi katika ujenzi wa boma hilo.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona. Tatizo ambalo lipo katika Kata ya Ngare ni sawa sawa na tatizo la Mahakama ya Mwanzo ya Wanging'ombe, imekuwa ni gofu. Je, Serikali inasemaje kuhusu ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Wanging'ombe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Swali jipyaa, kwani huyu hajui hata huko. Basi Mheshimiwa labda ulifika fika huko, hebu jibu. Labda ulifika! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri swali la msingi lilikuwa ni mwongozo gani Serikali inautoa kwa wananchi katika ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika kata zao. Kwa hiyo, mwongozo niloutoa ni huo huo kwamba wananchi na Halmashauri husika waweke mchango wake kwanza na wakishaonyesha utayari wao wa ujenzi wa Mahakama au boma, vyovyote itakavyokuwa, basi Serikali itakuja na kuweka mchango wake katika kuhakikisha kwamba hiyo dhana inakamilika.

Na. 178

### **Kuanzisha Viwanda vya Kusindika Samaki**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupe salaam za wananchi wa Biharamulo wanakusalimia.

**NAIBU SPIKA:** Nani anajibu? Hayo ni kinyume cha Kanuni zetu za Bunge!  
(*Kicheko*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ziwa Nyasa linamiliwi na nchi tatu yaani Malawi, Msumbiji na Tanzania; na kwa kuwa nchi hizo mbili wawekezaji wanaendesa viwanda vya kusindika samaki wanaovuliwa Ziwa hilo:-

Je, ni lini Serikali yetu itahimiza wawekezaji kuanzisha viwanda vya usindikaji samaki ili kuleta tija kwa wananchi waishio kandokando ya Ziwa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba sekta ya uvuvi ina mchango mkubwa katika kuendeleza viwanda, Wizara yangu imeendelea kuwahimiza wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya uvuvi ikiwemo yale ya Ziwa Nyasa kama inavyofanya katika mazao mengine ili kuongeza thamani ya rasilimali zilizopo hapa nchini.

Aidha, kupitia Mpango wa Maendeleo wa Kanda ya Mtwara, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya Ukanda huu ikiwemo barabara, reli, bandari na upatikanaji wa umeme ili kuwawutia wawekezaji katika maeneo hayo kuanzisha viwanda mbali mbali vikiwemo vya usindikaji samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba hakuna viwanda vyatya samaki kandokando ya Ziwa Nyasa, Ziwa hilo limekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi waishio kando kando yake kwa kujipatia kipato kutokana na uvuvi mdogo mdogo.

Aidha, takwimu tulizonazo zinaonyesha kuwa idadi ya samaki waliovuliwa imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutoka tani 8,500 mwaka 2005 hadi tani 4,353 mwaka 2008.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo na vyatya katika eneo husika ili kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Nyasa.

Namwomba Mheshimiwa Capt. Komba na Waheshimiwa Wabunge wengine amba majimbo yao yanapakana na Ziwa Nyasa waunge mkono jithada hizi za Serikali za kuhamasisha uwekezaji huu. (*Makofi*)

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Capt. Komba kwa jinsi anavyojali wananchi wake wa Mbinga Magharibi hasa wanaolitegemea Ziwa Nyasa kujipatia maendeleo. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imesema itaendelea kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika Ziwa hilo hasa katika viwanda vyatya kusindika samaki; Serikali inaweza kuniambia ni akina nani hasa hasa wamefuatwa katika jambo hili ili na mimi nisaidie?

Je, Waziri mwenyewe ambaye nina hakika hajawahi kutembelea eneo hilo, yuko tayari kwenda Ziwa Nyasa kule na kuona mandhari mazuri ya Ziwa lile na maisha ya watu wa kule ili apate morali wa kuwashimiza hao wawekezaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshuimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MKIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wawekezaji amba wamejaribu kujaribu kuwekeza kule amba ni wengi tu wanakuja, wanapitia katika taasisi zetu kama *Tanzania Investment Centre* na ni vigumu mimi kuwataja kwa majina, lakini ni kwamba wale wanajitokeza.

Tatizo linalokuwa pale ni kwamba lile Ziwa ukilinganisha na *Mozambique* na Malawi, kina cha pale ni kirefu kweli kweli, mita 250.

Sasa, samaki waliopo ni wachache na wanapajaribu kuwekeza kule inakuwa sio rahisi.

Lakini kwa sababu tunataka kuanzisha pale miradi, kuna mradi amba unaandikwa amba utawezza kuboresha hali ya uvuvi katika Kanda ile amba sasa hivi

mchakato wake unafanywa kati ya Benki ya Dunia na Ofisi ya Makamu wa Rais. Nafikiri tukishaboresha maeneo yale, uwezekano wa kupata mwekezaji kuwekeza ni rahisi.

Lakini viwanda tutakavyowekeza pale vitakuwa vidogo kwa sababu kiwanda kikubwa kama kile cha *Nile Perch* cha *Lake Victoria* kinahitaji tani 100 kwa siku, kwa hiyo kwa mwaka kinakula kama tani 30,000, ambapo lile Ziwa lina samaki ambao wanakadiriwa kuwa tani 168,000 tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Waziri kutembelea kule, mimi nafikiri Mheshimiwa hatakuwa na tatizo la kutembelea pale ili kujiona hali. Naamini kwamba Mheshimiwa kwa hiyo uvute subira, Waziri atatembelea yeze mwenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Sasa hapo kuna tatizo, Waziri sijui wa Viwanda au wa Uvuvi, sijui! Mheshimiwa Mpesa unakaa karibu na Ziwa hilo, swali la nyongeza!

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa *Mbamba Bay* na Kyela ni maeneo mazuri ambayo uwekezaji unaweza ukafanyaika hata wa viwanda vidogo, Je, Serikali itakuwa tayari kufikiria namna kuweka kiwanda sehemu za Kyela au Itungi ambako umeme upo na *Mbamba Bay* kwa sababu umeme unaelekea kwenda kule?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana maana yake swali lenyewe lilikua hata samaki wenyewe hawatoshi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakutakuwepo na matatizo kama Serikali itapata mwekezaji wa kuwekeza katika eneo hili la Kyela. Kutakuwa hamna tatizo, tutawahimiza ama tutawa-*encourage* kwenda kuwekeza katika eneo hilo.

Na. 179

### **Upungufu Mkubwa wa Maabara Shulenii**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inahimiza wanafunzi wajunge na masomo ya Sayansi kwa wingi; na kwa kuwa shule nyingi hazina maabara na hivyo kusababisha wanafunzi wengi kutofaulu vizuri katika masomo hayo:-

- (a) Je, ni shule ngapi za Sekondari zilizo na maabara nchini?

(b) Je, ni maabara za shule zipi zilizoboreshwa na kuwekewa vifaa vinavyoendana na mahitaji ya masomo yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua upungufu mkubwa wa maabara kwa shule za sekondari nchini ambapo shule 728 za sekondari zina maabara za masomo ya sayansi na shule 2412 hazina maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi.

(b)Mheshimiwa Naibi Spika, mabara za shule 36 zilijengwa na kuboreshwa kwa msaada wa feha za Benki ya Maendeleo ya Afrika, shule hizo ni pamoja na: Kilangalanga, Kitomondo, Mkongo – Mkoa wa Pwani, Mangaka, Nangwanda , Lukuledi, Mnyambe – Mtwara, Mbanga –Ruvuma, Matola – Iringa, Igunga, Kaliua – Tabora, Mogabiri, Manga – Mara, Chalao – Kilimanjaro, King’ori, Oldonyosambu, Makiba – Arusha, Kitoja – Singida, Mambwe, Kizwite, Inyonga – Rukwa, Malagarasi – Kigoma, Bumangi, Chato – Kagera, Galapo – Manyara, Kongwa – Dodoma, Matekwe, Mitole, Mahiwa, Mbekenyera – Lindi, Mwaya – Morogoro, Meatu, Runzewe – Sinyanga, Bwisya – Mwanza, Zingibari – Tanga na Kyela – Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa kuwa tatizo la ukosefu wa maabara ya sayansi katika shule zetu za sekondari ni kubwa sana, Serikali imeandaa mradi mkubwa wa kujenga na kufunga vifaa vya maabara katika shule zote za sekondari za Serikali hapa nchini. Gharama za mradi wote zinakadiriwa kuwa dola za kimarekani milioni 562. Tayari Serikali inajadiliana na washirika mbali mbali wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyonijibu Mheshiiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Je, ni sababu zipi zinazosababisha kushuka kwa kiwango cha elimu kwa vijana kutofanya vizuri pamoja na juhudzi zinazochukuliwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kupingana wala kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kiwango cha elimu kimeshuka. Isipokuwa, unapotathmini elimu, ziko au viko vigezo kadhaa vya kuviangalia na hili ni somo zima, kwa muda tulio nao hautoshi. Namkaribisha Mheshimiwa Mbunge ofisini kwangu, nitamwonyesha takwimu na tarakimu ziatakazomridhisha aweze kuona ni kwa kiasi gani tunesonga. Karibu ofisini kwetu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linahusiana na elimu ya Sayansi na sote tunaelewa kwamba kufaulu kwa vijana wetu katika masomo ya sayansi kumeshuka sana, ndio maana Wizara imeleta motisha kwa vijana hawa katika masomo ya juu.

Je, Wizara kwa kuwa inajua sababu zilizosababisha elimu hiyo kushuka ya sayansi. Je, ina njia gani mbali ya kuwapa motisha wanafunzi, namna gani ya kuwapa motisha walimu na kuondoa vile vikwazo ambavyo vinasababisha vijana hao wasifafulu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya yameelezwa vizuri kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufaulu vyema kwa masomo ya Sayansi ni kuwa na maabara na vifaa vyake ndani. Tumeeleza dhamira njema ya Serikali na mkakati ulio rasmi na hivi karibuni Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya elimu ame – *sign* mkataba wa kumkaribisha mwekezaji ambaye atatengeneza zana za maabara hiyo ni dhamira kwamba tunataka ufaulu

Mheshimiwa Naibu Spika, motisha tuliyotoa kwa wanafunzi waendelee na masomo ya sayansi ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwapatia ufadhili katika masomo ya elimu ya juu yaani *grate* ili wapate motisha. Na vivyo hivyo walimu wao tunaangalia utaratibu wa kuwa motisha. Tunafahamu mkono mtupu hulambwi (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaokoa muda tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, atauliza swali hilo.

Na. 180

### **Vitendo Vya Ukatili Dhidi ya Wanawake**

**MHE. ROSEMARY KASIMBI KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake kama vile kupigwa hadi kujeruhija vinaonekana kushamiri sana Wilayani Tarime; na kwa kuwa asasi za kiraia na zile za Mashirika mbalimbali zimeonyesha kukata tamaa juu ya harakati za vita dhidi ukatili huo ambaa sasa umeanza kuonekana ni jambo la kawaida.

- (a) Je, Serikali imechukua hatua gani za kukomesha ukatili huo?
- (b) Kwa kuwa ukatili huo umesababisha ulemavu wa kudumu kwa baadhi ya wanawake kama vile kukatwa mkono, miguu masikio na kadhalika.

Je, Serikali imechukua hatua gani kuwasaidia wanawake hao hasa ikizingatiwa kuwa ni walezi na watunzaji wakubwa wa familia?

## **WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, lenye sehemu (a) na ( b), naomba nitoe maelezo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake bado vinaendelea kuwepo katika jamii ikiwemo Wilaya ya Tarime. Takwimu tulizozipata kutoka Halmashauri ya Tarime zinaonyesha kuwa kuna matukio 23 ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyopotiwa kati ya mwaka 2008/2009 na kati ya hayo ni matukio 9 tu yaliyofungiwa kesi mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuandaa mpango wa Taifa wa kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa mwaka 2001 hadi 2015, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukomesha ukatili dhidi ya wanawake kama ifuatavyo:-

- Kutoa mafunzo kwa maafisa polisi wa jinsia zote kwa lengo la kuwapa uelewa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake ambapo walianzisha madawati ya kushughulikia maswala ya unyanyasaji katika kila kituo cha polisi wakianza na Mkoa wa Dar es salaam.
- Kuzindua kampeni ya kitaifa ya “kataa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na Albino iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24/5/2008. Tayari Wizara imeshapata gari la *cinema* ambalo linategemewa kuendeleza kampeni hii kuanzia kanda ya ziwa, ukiwemo Mkao wa Mara mwaka huu wa fedha. Hata hivyo mkakati endelevu wa kuzuia ukatili dhidi ya wanawake unahitaji ushiriki wa Jamii nzima.
- Wizara yangu ikishirikiana na *TBCI* imeandaa na imeanza kurusha vipindi vya Televisheni vyenye lengo la kuhamasisha wananchi kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake. Kipindi cha jinsia kinarushwa siku za Alhamisi saa 4.30 usiku na kurudiwa Jumatatu saa 4.05 asubuhi na kipindi cha familia kinarushwa siku ya jumanne saa 10.30 jioni na kurudiwa ijumaa saa 7 .30 mchana. Baadhi ya vipindi hivyo vinaonyesha ukatili wanaofanyiwa wanawake wa Mkao wa Mara ikiwemo Wilaya ya Tarime na vinalenga kubainisha matukio ya ukatili ili kuhamasisha jamii na wadau mbalimbali kushirikiana na Serikali kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto na Albino.

Aidha kitendo cha kumpiga na kumwumiza mtu ni kosa la jinai ambalo linachukuliwa hatua za kisheria kama makosa mengine jinai, hivyo natoa wito kwa wote wanaofanyiwa vitendo vya ukatili watoe taarifa polisi ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kutohukana na vitendo hivi vya ukatili baadhi ya wanawake wamepata madhara mbalimbali ya kisaikolojia pamoja na ulemavu wa viungo.

Hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua ni pamoja na kutoa elimu kwa kushirikiana na asasi zisizokuwa za kiserikali ili wanaofanyiwa ukatili huo watambue na kudai haki zao kwa muda muafaka pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya asasi mbalimbali zinazotetea haki za binadamu ziweze kufanya kazi vizuri.

Aidha kwa wale wanaopata ulemavu wa kudumu wamekuwa wakipata huduma kupitia idara ya ustawi wa jamii, Halmashauri na asasi zisizo za kiserikali zinazoshughulikia watu wenyewe ulemavu kulingana na uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kirigini kwa jitihada zake za kufuatilia na kupambana na ukatili dhidi ya wanawake katika Mkoa wa Mara. Aidha napongeza asasi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na mapambano ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake, na walemau wa ngozi.

**MHE . ROSEMARY K. KIRIGINI :** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Naibu Waziri, lakini vilevile niwapongeze *TBC1* kwa kampeni ya vita dhidi ya wanawake wanaoiedesha hivi sasa. Na ninaomba niulize swalii moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi iliyowekwa na Umoja wa Mataifa kuhusiana na haki za binadamu, na kwa kuwa kwa takribani miaka mingi sasa haki hizi za binadamu zimekuwa zikikiukwa na nchi yetu ya Tanzania sasa nina swalii dogo kwa Wizara je, ni nini nafasi ya Tanzania kwenye mtandao wa Kimataifa

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto naomba kumjibu Mheshimiwa Kirigini swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imeridhia na ku- *sign* mikataba yote inayohusika na haki za binadamu na imetengeneza mikakati ya kuweza kutekeleza hiyo mikataba pamoja na Itifaki ambazo tumeridhia.

Nafikiri sisi kama wadau au washirika wa Umoja wa Mataifa kama wanachama naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunawajibika kutekeleza yale yote ambayo tunakubaliana na wenzetu Ulimwenguni. Ndio sababu mpaka sasa hivi unaona kwamba katika kuitikia tumetengeneza ule mkakati wa “Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake,Watoto na Albino” na Serikali yetu ikiwa na nia njema inapambana sana na yale matendo yote yanayodhalilisha wanawake pamoja na walemau na ndio sababu Serikali yetu iliitisha kura za maoni na imeanza kuchukua hatua kwa wale ambao wameonekana wanahusika ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa Maswali umekwisha na maswali yameisha. Somo tulilojifunza Waheshimiwa Mawaziri mkijibu maswali *page* moja tunakwenda vizuri. Leo karibu Mawaziri wote walijibu maswali *page* moja *except* Wizara mbilli baadaye tutakuwa tunawataja kama mkizingatia gazeti la Mtanzania juzi limesema Wabunge mnaiba muda, kwa kuweka vitu ambavyo hamjaulizwa. Kwa hiyo, nakubaliana na lile gazeti kwamba muda mwingine tunapoteza mno kwa vitu ambavyo siyo vya lazima.

Wabunge wote hapa wanawajali wananchi wao. Sasa tuambie kila mtu anawajali wananchi wake. Kwa hiyo, tukienda namna hiyo tutakuwa tunaenda *speed*. Kwa hiyo, msijibu vitu ambavyo hamjaulizwa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni leo ni Wizara ya Mambo ya ndani kwa hiyo nitaanza na wageni wa Wizarra hiyo. Tunao watendaji wa Wizara wa Mambo ya ndani ya nchi ambao wapo kwenye *Spika's Gallery* katika eneo la Spika, kwanza kabisa ni Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa, karibu sana alafu tuna *Inspector General* wa Polisi Bwana Said Ali Mwema, tunae Kamishna Mkuu wa Magereza Bwana Augustino Nanyaro, Tunae Kamishna General wa Jeshi la zimamoto na uokoaji Bwana Mtwani Mohamed Kapamba, tunae Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Bwana Kinemo Kihomano, Tunae Kamishna Msaidizi Mwandamizi mwakilishi wa Kamishna wa Polisi Zanzibar Bwana Kennedy Kaseke, tunae Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar Bwana Mwinchumo Hassan Salum.

Waheshimiwa Wabunge Tunae Kamanda mpya wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma Bwana Zelotte Stephen, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu Bi Victoria Fovo, tunae Mkurugenzi wa Sera na Mipango Bi . Agnella Nyoni nadhani wale walioshuka kule, nawataja hawa kwa sababu hawa ndio *Gender* yenye, tunae Mkurugenzi wa Huduma kwa Jamii na adhabu mbadala Bwana Onnel Malisa, Mkurugenzi wa Idara ya malalamiko Bwana Augustino Dominic Shio, yupo Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa Bwana Dickson Mahimu. (*Makofi*)

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria na Usajili wa Ngo's Bwana F. W. P. Mushi, tunae Mhasibu Mkuu wa Wizara Bwana George Muhale, Mkuu wa Kitengo cha Habari Elimu na Mawasiliano Bwana Isack Nantanga, tunawakaribisheni sana leo ni Wizara yenu tunawatakieni Heri na tunawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo Wizara hii inafanya hasa katika Ulinzi wa Raia na mali zao na matatizo mengine yanayowapata Bunge litawasikiliza leo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Bungeni wengine ni kama wafuatao; wageni wa Mheshimiwa Damasi Nekei ambao ni Neema Ama Mwanafunzi wa Ifakara Sekondari School kutoka Morogoro, Neema yuko wapi? Wengine wamekwenda kwenye *Basement*, tunaye Mary Assumpta Nakei mwanafunzi wa Saint Teresa Sekondari School kutoka Arusha, tunao wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji Mbunge wa Manyoni Magharibi nao ni Potifa Yusuph Mchungaji, kuna Katibu wa Jimbo

Michael Mnyabahi, Tuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene ambao ni Julia Mginde Mwenyekiti wa Kata wa CCM Rudi, na mimi Rudi nimekwishafika huko.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Robert Maulia, Katibu Kata wa CCM Rudi, anao wageni wengi ningependa wageni wote wa Mheshimiwa Simbachawene wasimame maana wako wengi. Karibuni sana ameleta Wanachama wote hasa Rudi huko ndiko walikotokea, tunao wageni wa Mheshimiwa Professor David Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa jamii, ambao ni wanafunzi 25 wa udaktari kutika Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba BUGANDO Mwanza, Kiongozi wa msafara huu ni Bwana Paul Kasubi Nhinga, wapo hao? Karibuni sana tungependa kumwona kiongozi Bwana Paul Kasubi Nhinga yuko wapi? Asante karibuni sana madaktari wetu, tunao wageni wa Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga Mbunge wa Singida Kusini ambao ni Ndugu Iddi Maji ya Tanga Mwenyekiti wa CCM Kata ya Puma akifuatana na Ramadhani Kwilungi Diwani wa Kata ya Puma.

Waheshimiwa Wabunge, Samuel Daniel katibu Mwenezi wa Minyunge, Jumanne Mgunda Katibu Mwenezi Kata ya Puma karibuni sana, alafu tunao wanafunzi wa kituo cha mafunzo Chamwino ambao wapo 25 wanafunzi wa Chamwino wako wapi? Nadhani wako *Basement*, Wanafunzi wa shule ya msingi Minazini ambao wapo 37 wasimame kama wapo na walimu wao, kuna Mgeni wa Mheshimiwa Mathayo Manyinyi ambaye ni Mpwa wake yuko wapi? Hata jina hakumtaja.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli za kazi za Kamati Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Haroub Masoud, anaomba niwatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo ni 8/7/09, kutakuwa na kikao saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Saa saba mchana, halafu tuna Mwenyekiti Kamati ya Bunge Kilimo na Mifugo na Maji Mheshimiwa Gideon Cheyo anaomba niwatangazie wajumbe wake kwamba 1 eo tarehe 8 Julai, 2009 wakutane katika Ukumbi Namba 219 saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shelukindo anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo 8 Julai, 2009 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Namba 131 jengo la Utawala saa nane mchana. Kwa hiyo, wajumbe wazingatие muda na mahali panapohusika.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi, Hoja, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea, kujadili na kuitisha

makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rambirambi, naomba kuungana na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi wa majimbo matatu ambayo yaliwapoteza Wabunge wao katika mwaka wa fedha wa 2008/2009. Majimbo hayo ni ya Tarime, Mbeya Vijijini na Busanda kwa kuwapoteza waliokuwa Wabunge wenzetu Waheshimiwa marehemu Chacha Wangwe, Richard Said Nyaulawa na Kabuzi Faustine Rwilomba na Fares Kabuye Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pole, nawapa pole wananchi wa Mbagala Kuu Jijini Dar es Salaam kwa tukio la kusikitisha lililotoka tarehe 29 Aprili, 2009 la milipuko ya mabomu yaliyokuwa yamehifadhiwa katika ghalaa la silaha katika kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 20 na zaidi ya kaya 7,000 kukosa mahali pa kuishi baada ya nyumba zao kuharibiwa na mabomu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafa mengi yametokea zikiwemo ajali za barabarani, migodini, meli na treni ambazo zimeendelea kupoteza maisha ya wananchi. Nachukua nafasi hii kuwapa pole ndugu na jamaa wa marehemu na waathirika wote wa maafa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pongezi, nakupongeza wewe binafsi, Naibu wako, Wenyeviti wetu ndani ya Bunge na wale wa Kamati za Bunge pamoja na wasaidizi wao chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Nawapongeza pia Wabunge wenzangu wote kwa michango yao ndani na nje ya Bunge ambayo imelenga kulinufaisha taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba zao walizozitoa mapema katika mukutano huu wa 16 wa Bunge ambazo pamoja na mambo mengine zimetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2009/2010 na mwelekeo wa bajeti na hali ya uchumi kwa jumla kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kutoa huduma bora katika kudumisha amani, utulivu na umoja nchini. Dhima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji na kuwashudumia wakimbizi waliopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 na Utekelezaji Wake, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina majukumu 13. Ningependa kueleza majukumu hayo pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwanza ni kuimarisha usalama migodini. Jeshi la Polisi limeendelea kutoa ulinzi kwa kufanya operesheni, misako na doria kwenye maeneo ya uwekezaji ikiwemo migodi hususan katika Mikoa ambayo imekuwa na migogoro mingi. Hadi sasa askari wetu bado wanalinda mgodi wa Buhemba Mkoani Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la pili ni kuliimarisha Jeshi la Polisi kwa kuliongezea utaalam na zana ili upelelezi wa kesi ukamili haraka hivyo kupunguza muda wa mahabusu kukaa magerezani. Kama hatua ya utekelezaji wa jukumu hilo maofisa na askari 480 walishiriki katika mafunzo mbalimbali kuhusu taaluma ya upelelezi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika upelelezi. Aidha, askari wapya 205 walipata mafunzo ya msingi kuhusu upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tatu ni kuendelea kupunguza msongamano magerezani. Hivi sasa magereza yetu yana uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 27,653. Kwa kukarabati na kupanua magereza yaliyopo na kujenga magereza mapya na mabweni ya wafungwa katika vituo mbalimbali, Serikali imeongeza uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu kwa asilimia 22 kutoka wafungwa na mahabusu 22,669 mwaka 2006 hadi kufikia 27,653 hivi sasa.

Hata hivyo, bado msongamano upo, na juhudzi za kupunguza zaidi msongamano zinaendelea kuititia taratibu za Parole na kifungo cha nje. Tarehe 1 Aprili, 2009 kulikuwa na wafungwa na mahabusu 41,109 katika magereza yote nchini. Kati ya hao 20,360 walikuwa ni wafungwa, na 20,749 ni mahabusu, kama ilivyofafanuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2008 wafungwa 78 waliachiliwa kwa utaratibu wa Parole. Hata hivyo, idadi ya wafungwa wanaoachiliwa kwa utaratibu huu imeendelea kuwa ndogo kutokana na kwamba Sheria ya Bodi za Parole ya mwaka 1994 haiwaruhusu wafungwa wanaofanya makosa makubwa kuachiliwa.

Wizara ipo katika mchakato wa kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuifanyia marekebisho sheria hii kwa lengo la kupanua wigo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 9 Desemba, 2008 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa msamaha kwa wafungwa 7,553 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 47 ya Uhuru. Rais pia alitoa msamaha kwa wafungwa 3,247 tarehe 26 Aprili, 2009 wakati wa kuadhimisha sherehe za miaka 45 ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Aprili, 2009 jumla ya wafungwa 664 walitolewa gerezani ili watumikie kifungo cha nje chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Magereza, kama inavyoonyeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nne ni kushughulikia kwa ufanisi malalamiko ya wananchi ya kero ya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi. Hatua mbalimbali zimechukuliwa dhidi ya askari waliobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Askari 15 wamefukuzwa kazi na baadhi kesi zao zinaendelea katika Mahakama ya kijeshi na Mahakama za Jinai.

Aidha, Wizara imeunda idara maalum inayoshughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo vyake likiwemo Jeshi la Polisi. Katika mwaka huu wa fedha, idara inatarajia kuwa na sheria kwa lengo la kuipa nguvu ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tano ni kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea uwezo kitaaluma na zana za kisasa. Wizara imeweza kutoa mafunzo katika taaluma za upelelezi, intelijensia, usimamizi wa kumbukumbu za uhalifu, uchunguzi wa makosa yahusuyo fedha haramu, na uendeshaji wa magereza, na shughuli za zimamoto, uokoaji na uhamiaji. Mafunzo hayo yametolewa kwa watumishi wa Polisi 8,651, Magereza 1,671, Zimamoto na Uokoaji 60 na Uhamiaji 374.

Wizara imekamilisha ukarabati wa majengo na ufungaji wa kompyuta katika Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji Mjini Moshi, na imekamilisha maabara ya uchunguzi wa nyaraka ambayo imepatiwa msaada wa vifaa maalum toka Uholanzi. Chuo hicho kilizinduliwa rasmi tarehe 12 Desemba 2008 na mafunzo ya uhamiaji yameanza kutolewa kwa askari. Wizara itaendelea kuimarisha vyombo vyake vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la sita ni kuwahamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao na kuhakikisha usalama wao na mali zao. Katika kutekeleza jukumu hili, Makamanda wa Polisi Mikoa na Wakuu wa Polisi Wilaya na vituo wameendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana ya Polisi Jamii katika maeneo yao.

Aidha, Kitengo cha Polisi Jamii Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kimesambaza machapisho mbalimbali kama vile vitabu vya Mpango wa Ulinzi Jirani na Safiri Salama Tanzania na kitabu cha Falsafa ya Polisi Jamii/Ulinzi Shirikishi, kwa lengo la kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi. Vikundi 1,888 vya ulinzi shirikishi vimeanzishwa tangu mwaka 2005. Aidha, elimu ya kuhamasisha wananchi inaendelea kutolewa kupitia vipindi vya redio na runinga. Nashukuru kwa ushirikiano na moyo unaotolewa na wananchi katika kuanzisha vikundi vya kujilinda katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa askari wake. Katika taarifa ya programu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya *Research and Education for Democracy in Tanzania - REDET* ya mwezi Aprili, 2009 Jeshi la Polisi limetajwa kuwa ni mojawapo ya taasisi za Serikali ambazo wananchi kwa ujumla wanaridhika na utendaji wake wa kazi. Kituo cha Haki za

Binadamu katika taarifa yake ya mwaka 2008 pia kilielezea kwamba utendaji wa Jeshi la Polisi unaendelea kuboreshwa kwa kuanza kufanya kazi kwa kuzingatia miiko ya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la saba la Wizara katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kuvijengea mazingira mazuri vyombo vyala na usalama, na kutatua matatizo ya makazi na maslahi ya watumishi wake. Katika mwaka 2008/2009 Wizara imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, upanuzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara pamoja na Ofisi Kuu ya Uhamiaji Zanzibar. Wizara imeendelea pia na ukarabati wa nyumba, vituo, ofisi na mabweni ya wafungwa katika vituo mbalimbali.

Kupitia udhamini wa Serikali, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za askari Polisi Dar es Salaam na Zanzibar ambapo ujenzi upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeamua kuongeza posho mbalimbali za askari wa vyombo vyala na usalama vivilyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kiwango cha kuridhisha.

Lengo la nyongeza hii ni kuongeza mori wa utendaji. Ni matarajio yangu kuwa nyongeza ya posho hizi na maboresho ya makazi yanayoendelea yatawapa askari nafasi nzuri zaidi ya kuongeza ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la nane ni kuongeza uwezo wa taifa wa kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogondogo. Katika kukabiliana na uhalifu ukiwemo ujambazi, Jeshi la Polisi limeendelea kuimarisha Kitengo cha Intelijensia kwa kukipatia mafunzo na vitendea kazi. Doria za kutambua maficho ya wahalifu zimefanyika, ulinzi katika maeneo ya mipakani umeimarishwa kwa kuongeza idadi ya askari na kufanya operesheni za kudumu, na mafunzo ya utayari wa kukabiliana na matukio ya uhalifu yametolewa kwa askari. Kupitia mpango wa Polisi Jamii, Jeshi la Polisi limeweza kupata taarifa sahihi kutoka kwa raia wema ambazo ziliwezesha kuzima uhalifu na pale ulipotokea watuhumiwa kuweza kukamatwa.

Kikosi Kazi cha Taifa kilichoundwa mwaka 2006 kukabiliana na hali ya kutisha ya ujambazi iliyokuwa wakati huo, kimeendelea kukabiliana na uhalifu kwa kuendesha upelelezi wa matukio makubwa ya uhalifu na kufuatilia mwenendo wa uhalifu nchini na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuhakiki umiliki wa silaha ndogondogo ambapo katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009 kumbukumbu za silaha 10,643 zimeingizwa kwenye *database* ya silaha.

Aidha, Jeshi la Polisi liliendesa misako na operesheni za kusaka silaha, na silaha 424 na risasi 4,026 zilibainika kumilikiwa kinyume cha sheria na kukamatwa. Wizara

imeandaa mapendekezo ya kuwasilishwa Serikalini ya kutunga sheria ambayo itasimamia na kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha ndogondogo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la tisa ni kuandaa Sera ya Uhamiaji yenyе kubainisha masuala ya uraia na ukaazi katika mazingira ya kuelekea ushirikiano katika SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mchakato wa kuandaa sera hii ulikwishaanza mwaka 2007 na rasimu yake kujadiliwa na wadau mbalimbali. Wadau walishauri kuwa ni vyema majadiliano yanayoendelea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu *free movement of persons* na majadiliano ya UNIVISA katika Jumuiya ya SADC yazingatiwe katika sera hiyo. Majadiliano hayo bado yanaendelea. Hivyo, sera hii itakamilishwa baada ya majadiliano hayo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi ni kuanzisha na kutoa vitambulisho vya taifa. Mamlaka ya kusimamia na kuratibu utoaji wa vitambulisho (*NIDA*) iliundwa na Mheshimiwa Rais kupitia hati maalum iliyotolewa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watendaji wa Mamlaka hiyo wameajiriwa, na Kamati ya Uongozi imeshateuliwa na kuanza kazi.

Wizara imekamilisha hatua ya kwanza ya kumpata mkandarasi ambaye ataweka mfumo wa kutunza taarifa za watu watakaopewa vitambulisho. Hivi sasa maandalizi kwa ajili ya utoaji zabuni ya vitambulisho vya taifa yanaendelea sambamba na maandalizi ya miradi ya majoribio (*pilot projects*) ambayo itaanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwathibitishia Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwamba mradi wa vitambulisho utakamilika kwa kufuata sheria na taratibu, bila mizengwe, kwa uwazi unaostahili na bila upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi na moja ni kuongeza kasi ya kuwarejesha wakimbizi kwao. Utakelezaji wa jukumu hilo umekuwa na mafanikio.

Kati ya tarehe 1 Julai, 2008 na tarehe 30 Aprili, 2009 wakimbizi 69,687 walirejea kwao kwa hiari. Kati yao, wakimbizi 55,399 wamerejea nchini Burundi, na 14,288 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC* ).

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu zoezi la kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao za asili lilipozinduliwa mwezi Machi, 2002 hadi kufikia mwezi Aprili, 2009, jumla ya wakimbizi 390,599 walirejea nchini Burundi. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi, 2009, wakimbizi 65,418 toka *DRC* walikuwepo nchini walirejea kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi na mbili ni kuendeleza kampeni ya upandaji miti. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Jeshi la Magereza liliendelea kuboresha mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yake kote nchini. Siku ya upandaji miti kitaifa, tarehe 1 Januari, 2009, jumla ya miti 41,610 ilipandwa katika baadhi ya

maeneo yaliyokuwa yamepata mvua. Mradi wa kupanda miti kwenye eneo la jumla ya ekari 3,000 katika Magereza ya Idete-Morogoro, Isupilo-Iringa na Msalato-Dodoma, ambao unafadhiliwa na *NORAD* kwa ushirikiano na Wizara ya Maliasili na Utalii, unaendelea vizuri. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2009, jumla ya miti 742,092 ilikuwa imepandwa kwenye eneo la ekari 1,029. Mashamba mengine ya miti yalianzishwa katika magereza 10 katika Mikoa ya Mwanza, Singida, Kigoma, Iringa, Ruvuma, Shinyanga, Kilimanjaro, Rukwa na Mbeya. Hadi sasa idadi ya miti yote iliyopandwa ni zaidi ya 3.8 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumi na tatu na la mwisho la Wizara katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 ni kuendeleza vita dhidi ya dawa za kulevyta ili kuwakinga watoto wasiathirike na dawa hizo. Tatizo la dawa za kulevyta, limeendelea kuwa changamoto siyo kwa nchi yetu tu, bali kwa nchi nyingi duniani. Utandawazi, kukua kwa sayansi na teknolojia, kuongezeka kwa maingiliano ya watu duniani na upana wa mipaka ya nchi yetu, vyote vimechangia hali hii. Kati ya Julai, 2008 hadi Aprili, 2009, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, lilikamata watuhumiwa 514 na kilo 5 na gramu 331 za dawa za kulevyta za viwandani. Kilo 67,624 za bhangi na kilo 8,606 za mirungi vilevile zilikamatwa na watuhumiwa 6,501 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ulinzi na usalama. Aidha, ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, umesaidia sana katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya hali ya usalama nchini inatokana na takwimu zinazotokana na taarifa za vyombo vya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji. Kwa ujumla hali ya amani na utulivu nchini, imeendelea kuwa ya kuridhisha licha ya kuwepo kwa baadhi ya makosa kama vile mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaliyonekana kutishia usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuvishukuru vyombo vlivyo chini ya Wizara vya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji kwa ushirikiano wao na vyombo vingine vya dola kwa kutoa mchango mkubwa katika kudumisha amani na utulivu nchini katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, pamoja na changamoto zinazowakabili zikiwemo ufinyu wa bajeti, kuongezeka kwa mbinu za uhalifu, upungufu wa askari, uhaba wa vitendea kazi, uhaba na uduni wa makazi na ofisi, msongamano magerezani, majanga mbalimbali na uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizopo zinaonesha makosa ya jnai 506,030 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini katika mwaka 2008, ikilinganishwa na makosa 509,462 yaliyoripotiwa mwaka 2007. Idadi ya makosa ilipungua kwa kiasi cha makosa 3,432 sawa na asilimia 0.7. Jeshi la Polisi limeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na uhalifu zikiwemo kuendesha mafunzo ya utayari kwa maofisa na askari, kuongeza nguvu ya rasilimali watu katika Mikoa yenye upungufu wa askari mfano

Kagera, Mara, Kigoma, Rukwa na Tabora, kufanya doria za kutambua maficho ya wahalifu na kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kukabiliana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi, lina upungufu mkubwa wa nguvu kazi kwani idadi inayokubalika kimataifa ni askari mmoja kwa watu 450 (1:450), wenzetu wa Kenya wana uwiano wa askari mmoja kwa watu 821 (1:821), Tanzania ni askari mmoja kwa watu 1,300 (1:1,300). Hali hii inafanya maeneo mengine kutofikiwa na huduma ya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa makosa ya usalama barabarani, mwaka 2008 makosa yaliyoripotiwa Polisi ni 229,451, ikilinganishwa na makosa 230,751 yaliyoripotiwa mwaka 2007. Idadi ya makosa ilipungua kwa kiasi cha makosa 1,300, sawa na asilimia 0.6. Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani, kwa kushirikiana na wadau wengine, kimeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo operesheni za kukamata magari mabovu na kuyaondoa barabarani, kubaini mtandao wa kundi linalotoa leseni za udereva za bandia, kutoa elimu ya usalama barabarani kwenye mashule, ukaguzi wa leseni za udereva, magari na shule za udereva.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka 2008/09, ilipangija kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya shilingi 30 bilioni. Hadi tarehe 30 Aprili, 2009, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 28.8 bilioni sawa na asilimia 96 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliidhinishiwa shilingi 273 bilioni kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2009, shilingi 248 bilioni zilikuwa zimetolewa na Hazina na shilingi 231 bilioni zilikuwa zimetumika, ambazo ni sawa na asilimia 93 ya fedha zote zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2008/2009, nililieza Bunge lako Tukufu kuwa, kutohana na ufinyu wa bajeti, Wizara ingetumia fursa na rasilimali zilizopo ndani ya Wizara, kwa lengo la kutekeleza baadhi ya kazi badala ya kutumia wakandarasi. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza kimekarabati Chuo cha Polisi Kidatu - Morogoro na Kiwanda cha Ushonaji cha Magereza kilichopo Ukonga Dar es Salaam, kimeshona sare za askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Wizara itaendelea kuzifanya fursa hizi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilieza kuwa, Wizara itazingatia suala la jinsia katika maeneo yetu mbalimbali ya kazi ili kuona idadi ya watumishi wanawake katika utumishi wa Wizara inaongezeka kila wakati kulingana na majukumu na kazi zilizopo. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara ilitoa mafunzo kwa askari/watumishi 10,859, ambapo wanawake ni 1,069, sawa na asilimia 10. Pia Wizara iliwapandisha vyeo jumla ya askari/watumishi 3,875, ambapo wanawake ni 629 sawa na asilimia 16. Suala hili litaendelea kuzingatiwa katika mipango ya Wizara. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya kiutendaji iliyotukabili katika utekelezaji wa bajeti ya 2008/2009 ni kuchelewa kupatikana kwa magari kutokana na mchakato wa manunuzi unaofanyika kitaifa kuititia Wizara ya Miundombinu. Hali hii imeathiri kwa kiwango kikubwa, utekelezaji wa ahadi ya Wizara ya kupeleka magari kwenye baadhi ya vituo vilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi, limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola, pamoja na wadau mbalimbali ikiwemo majeshi mengine ya Shirikisho la Polisi la Kimataifa - *Interpol*, Shirikisho la Polisi la Nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika – *EAPCCO* na Shirikisho la Polisi la nchi za Kusini mwa Afrika - *SARPCCO*, kuititia ubadilishanaji taarifa za uhalifu na wahalifu, mafunzo, operesheni mbalimbali za pamoja na Mikutano ya Wakuu wa Majeshi na Wakuu wa Upelelezi wa Nchi Wanachama. Operesheni ya pamoja ilifanyika, iliyohusisha nchi za Tanzania, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi na Mauritius, kwa lengo la kukamata magari ya wizi, dawa za kulevya, dawa bandia, silaha haramu na wahamiaji haramu.

Katika dhana hiyo hiyo, mwezi Agosti, 2008 nchini Ethiopia, Tanzania iliweka saini Itifaki ya kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo, ambayo inahusisha nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika. Lengo la Itifaki hiyo ni kuziwezesha nchi wanachama, kushirikiana katika kuzuia na kupambana na wizi wa mifugo. Wizara imeanza mchakato ili Itifaki hiyo iridhiwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kutoa ulinzi kwenye maeneo yenye migogoro baina ya wafugaji na wakulima na mapigano ya koo. Serikali imeunda Kikosi Kazi kinachoongozwa na Jeshi la Polisi, kinacho jumuisha wataalam kutoka Wizara za Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katiba na Sheria na Ofisi ya Rais, Utawala Bora ili kufuatilia tatizo la migogoro ya mara kwa mara, inayotokea kati ya wafugaji na wakulima Mkoani Morogoro. Kikosi Kazi tayari kimekamilisha taarifa yake na kuiwasilisha Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine, limeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na uhalifu na tatizo la usalama barabarani. Kwa upande wa ajali za barabarani, tatizo bado ni kubwa na linahitaji nguvu za pamoja za wadau wote. Makosa ya mauaji ya Albino yameendelea kudhibitiwa. Katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Aprili, 2009 watuhumiwa 86 wa makosa ya mauaji ya Albino wamefikishwa Mahakamani na kesi zao zinaendelea kusikilizwa. Mwaka 2009/2010, Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na uhalifu na ajali za barabarani, mapigano baina ya koo, migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro katika maeneo ya migodi, ajali za majini na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2008/2009, Jeshi la Polisi limeanza utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha ulinzi wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2009 na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010. Maandalizi haya yanalenga kuongeza askari 7,000 na vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari na vifaa vya kutuliza ghasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeifanyia mapitio Programu yake ya awali ya Maboresho na kupanga programu ya miaka mitano (2009/2010 - 2013/2014), yenye mihimili mitatu ya Usasa, Weledi na Polisi Jamii. Programu hiyo ina maeneo makuu sita, ambayo ni mifumo ya kazi za Polisi, Sheria, Kanuni na Muundo wa Kitaasisi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), Menejimenti ya Rasilimali Watu, Miundombinu na Vitenda Kazi na Polisi Jamii/Ulinzi Shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba mbili katika Wilaya ya Bahi na nne katika Kikosi cha FFU Finya umekamilika. Mradi wa ujenzi wa nyumba 54 Dar es Salaam na sita Zanzibar upo katika hatua za mwisho; na ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa moja kila moja Wilaya ya Mwanga unaendelea. Katika mwaka 2009/10, ujenzi wa nyumba utaanza katika Kambi za Mabatini – Mwanza, Musoma, Kegonga na Nyamwaga Mkoani Mara, Ludewa - Iringa, Mtambaswala – Mtwara, Horohoro – Tanga, Muhukuru - Ruvuma na Byekera - Kagera. Pia ujenzi wa nyumba za askari utaendelea katika Kambi za Finya – Kusini Pemba, Tunguu na Unguja Ukuu – Kusini Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Dodoma, Morogoro na Mbeya na Vituo vya Polisi vya Makambako na Chato, upo katika hatua za mwisho. Miradi inayoendelea ni Vituo vya Polisi vya Wilaya za Mpanda, Ludewa, Newala, Bukombe na Meatu. Katika mwaka 2009/2010, ujenzi utaanza wa Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Upelezei wa Makosa ya Jinai Jijini Dar es Salaam, Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Mara na Manyara, Ofisi za Wakuu wa Polisi Wilaya za Bahi, Bagamoyo na Njombe na Ofisi za Wilaya za Kipolisi za Mbagala na Rarya. Vilevile ujenzi wa vituo vya Daraja “C” katika Kata za Kegonga Mkoani Mara, Muhukuru Mkoani Ruvuma, Horohoro Mkoani Tanga na Mtambaswala Mkoani Mtwara na Ofisi za Makao Makuu ya Kikosi cha Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Vyuo vya Polisi uliendelea katika Vyuo vya Dar es Salaam, Moshi, Zanzibar na Kidatu. Mwaka 2009/2010, ujenzi utaanza wa Chuo cha Upelezei Dodoma. Upembuzi yakinifu utaendelea kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati utaendelea wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nkasi, Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Rukwa na Pwani, Kituo cha Polisi Kati – Tabora, jengo la karakana ya vifaa vya mawasiliano, Ghala Kuu la Polisi Dar es Salaam, Zahanati ya Kambi ya Polisi Kunduchi na Ofisi ya Polisi Makao Makuu ya kutuliza ghasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Jeshi la Polisi limelipia magari 13 aina ya *Toyota Land Cruiser Pick-Up*, lori moja la maji taka, gari moja la kubeba wagonjwa na mabasi mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya kutokana na utaratibu mpya wa ununuzi, Wizara yangu haikufanikiwa kupeleka magari katika Wilaya zilizoahidiwa

katika mwaka wa fedha uliopita. Naomba kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wilaya zote zilizopangiwa kupata magari watapata kama walivyoahidiwa. Mwaka wa fedha wa 2009/2010, yatanunuliwa magari 22 aina ya *Toyota Land Cruiser Pick-Up*, lengo likiwa kuhakikisha kwamba Wilaya zote za Tanzania ziwe na magari ya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Jeshi la Magereza ni kuhifadhi wafungwa wa aina zote, pamoja na kurekebisha tabia za wale waliohukumiwa vifungo. Urekebishiwa wa tabia za wafungwa, hufanywa kuitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo na nadharia ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii. Programu hizo huendeshwa kuitia miradi ya ujenzi, kilimo na viwanda vidogovidogo. Mafunzo ya nadharia huendeshwa katika Chuo cha Ufundı cha Magereza Ruanda - Mbeya, Gereza la Wami Vijana na utoaji ushauri nasaha kwa kutumia walimu wa dini na Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha usafirishaji wa mahabusu kwenda mahakamani na kurudi magerezani, katika mwaka 2008/2009, yamelipiwa magari matano ambayo ni mabasi makubwa matatu na madogo mawili. Jukumu hili limeanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya za Kisarawe, Mkuranga na Kibaha Mkoani Pwani na litaendelezwa kwa awamu kwenye mikoa mingine kadiri bajeti itakavyoruhusu. Katika mwaka 2009/2010, Jeshi la Magereza linatarajia kununua mabasi makubwa mawili, madogo matano na *Pick-Up* tano kwa ajili ya Mkoa wa Pwani na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Magereza lilianza kutekeleza mradi wa uendeshaji wa shughuli za wafungwa nchini kote kwa kutumia mtandao wa kompyuta wa *Offenders Management Information System*. Utekelezaji wa mradi huu, utaendelezwa katika mikoa yote nchini kwa awamu kadiri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wapya 1,081 wameajiriwa baada ya kuhitimu mafunzo ya awali ya uaskari katika Chuo cha Magereza Kiwira Mkoani Mbeya. Mwaka 2009/2010, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri askari wapya 598.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza yenye ulinzi mkali umefanyika na unaendelea katika Magereza ya Karanga - Kilimanjaro, Lilungu - Mtwara, Gereza Maalum Isanga - Dodoma na Ukonga - Dar es Salaam. Lengo la mwaka 2009/2010 ni kuendelea na ukarabati katika magereza ya Maweni - Tanga, Uyui - Tabora, Karanga - Kilimanjaro, Butimba - Mwanza na Ukonga - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upanuzi, ujenzi na ukamilishaji wa mabweni ya wafungwa, ilifanyika katika Magereza ya Korogwe, Kahama, Isupilo, Mahabusu Tabora, Mafia, Kilosa, Bukoba, Ubena, Kigongoni, Mahenge, Mahabusu Songea, Singida, Ileje, Ludewa, Muleba, Geita, Kilwa, Njombe na Kingolwira. Katika mwaka 2009/2010, kazi hiyo itafanyika kwa mabweni ya wafungwa na ofisi za magereza 19 yaliyopo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Manyara, Pwani, Dar es Salaam, Kagera, Morogoro, Mara, Arusha, Mbeya, Iringa, Shinyanga, Ruvuma, Singida, Tanga na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uimarishaji wa mifumo ya maji safi na maji taka, iliendelea katika magereza ya Mwanga, Kibiti, Segerea, Nachingwea, Mafia, Kahama na Kikosi Maalum Ukonga. Mwaka 2009/2010, kazi hiyo itaendelea katika magereza ya Mwanga, Meatu, Mbanga, Kalilankulukulu, Kingurungundwa, Majimaji, Mkwaya, Kibondo, Hanang, Butundwe, Kiteto, Chuo Ukonga na Gereza Kiabakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia ya mazao na majengo imefanyika katika eneo la upanuzi wa Gereza la Mahabusu Segerea na eneo litakapojengwa Gereza la Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi. Upimaji wa maeneo umefanyika katika vituo vya Nzega, Mbanga na eneo litakalojengwa Gereza la Wilaya ya Chato. Maeneo ya magereza yataendelea kupimwa katika magereza kumi ya Ubena, Mkuza, Mwanga, Kibiti, Matongo, Ngwala, Kalilankulukulu, Rwamurumba, Kondoa na Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Jeshi la Magereza limelipia fedha za ununuzi wa magari ya aina mbalimbali 49 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa magereza. Uboreshaji wa mashamba umeendelezwa kwa kununua majembe 64 ya kukokotwa na wanyamakazi, *power tillers* nane, pamoja na mashine nne za kunyunyizia dawa kwenye mikorosho. Lengo la mwaka 2009/2010 ni kununua matrekta manane, *power tillers* nne, magari 22 na mashine moja ya kuvuna mpunga (*combine harvester*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magereza lilianzishwa chini ya kifungu Na. 3(1) cha Sheria Na. 23/1974 (*The Corporations Sole Establishment Act, 1974*). Madhumuni ya Shirika hili ni kuendesha programu za urekebishaji wa wafungwa kwa njia ya uzalishaji kupitia miradi ya kilimo, mifugo na utengenezaji wa vifaa toka viwanda vidogovidogo. Shirika lina jumla ya miradi 15 ya kilimo na mifugo na nane ya viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Shirika liliendelea kuimarisha viwanda kwa kufunga mashine mpya Kiwanda cha Viatu Karanga - Moshi na Uhunzi katika Gereza Ukonga. Ununuzi wa pembejeo umefanyika na Serikali imetoa ruzuku ya zana za kilimo kwenye mashamba ya magereza ya Mollo - Sumbawanga na Songwe – Mbeya. Ekari 1000 za mahindi zililimwa katika magereza hayo na magunia 6,678 ya mahindi yalipatikana. Ekari 450 za mpunga zililimwa katika shamba la Gereza Idete lililoko Ifakara – Morogoro na kupata magunia 2,846. Matarajio ya mwaka 2009/2010 ni kuweka nguvu zaidi katika Shamba la Kitengule Kagera ili kutumia fursa ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limeanza kuchukua hatua ya kuzalisha mbegu bora za kilimo katika Mikoa sita ya Morogoro, Arusha, Dodoma, Lindi, Manyara na Kilimanjaro, ambazo zitasambazwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limeanza kutumia makaa ya mawe katika Magereza ya Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa badala ya kuni. Utaratibu huu unatarajiwa kuendelezwa katika Mikoa ya Iringa, Ruvuma na

Rukwa. Mradi wa kutumia gesi itokanayo na tungamotaka (*biogas*), unaendelea vizuri katika Gereza la Ukonga. Katika Gereza la Keko, upo mradi wa kutumia gesi asilia kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa. Miradi hii inatarajiwa kuenezwa katika magereza yote makubwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limejikita katika utoaji wa ushauri nasaha, elimu ya kujikinga na maambukizi mapya kupitia waelimishaji rika, uhamasishaji wa kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari ili kujitambua na utoaji wa dawa. Ufuatilaji wa watumishi na wafungwa wenyewe maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI umefanyika na wanaendelea kupatiwa virutubisho na dawa za kupunguza makali ya VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Huduma kwa Jamii ambayo ni mojawapo ya adhabu mbadala wa kifungo gerezani, inaendelea kutekelezwa katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Shinyanga. Hadi kufikia mwezi Mei, 2009, wafungwa wanaume 831 na wanawake 158 wamefaidika na programu hii. Wafungwa hao wamekuwa wakifanya kazi kwenye taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itajikita katika kuimarisha muundo wa Idara ya Huduma kwa Jamii, kwa kuajiri Maafisa Majaribio (*Probation Officers*), ambao wasasimamia utekelezaji wa sheria zinazohusu adhabu mbadala za Huduma kwa Jamii, Huduma za Majaribio, Sheria ya Bodi za Parole na utaratibu wa kifungo cha nje. Watumishi 100 wanatarajiwa kuajiriwa na kupewa mafunzo maalumu na ununuzi wa vitenda kazi, zikiwemo pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, nchi yetu imeshuhudia majanga makubwa ya moto, ajali mbalimbali zikiwemo za barabarani, treni, vyombo vya usafiri majini na tukio la kulipuka kwa mabomu kwenye ghalala kuhifadhiwa silaha katika Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyoko Mbagala Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, limeendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto katika maeneo mbalimbali nchini. Ukaguzi huu umeenda sambamba na utoaji wa elimu ya kinga dhidi ya moto, majanga mengine au moto unapotokea na jinsi ya kutumia vifaa vya kuzimia moto. Katika kipindi cha Julia, 2008 hadi Aprili, 2009, jumla ya nyumba 582 ziliteketea kwa moto. Tukio kubwa la ajali ya moto ni lile lililotokea tarehe 23 Machi, 2009 kwenye hoteli za kitalii za *Paradise, Oceanic* na Malaika katika Wilaya ya Bagamoyo. Katika tukio hilo, madhara makubwa yalitokea hasa kwenye Hoteli ya Paradise, ambapo mali nyingi ziliteketea na watumishi watatu walijeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto lilifanyika kwenye maeneo 3,576. Ukaguzi huo pia ulilenga kutoa elimu ya moto kwa jamii na namna ya kutumia vizimamoto vinavyobebeka (*Portable Fire Extinguishers*), ambavyo vinawekwa katika maeneo ya kufanyia kazi au makazi. Zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa utekelezaji wa usimamizi wa Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji wa komandi moja na kuanzisha ofisi za Mikoa za Zimamoto na Uokoaji, unaenda sanjari na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Jijini Dar es Salaam, ambao umeanza katika bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, askari 60 walipatiwa mafunzo, ambapo askari 59 walihitimwa mafunzo hayo. Mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa watumishi 13 kwa lengo la kuwajengea uwezo kiutendaji. Askari wapya watano walijiriwa. Katika mwaka 2009/2010, mafunzo yatatolewa kwa askari 300 na askari 42 wataajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009, jumla ya wageni 680,168 waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 732,328 walioingia nchini katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Wageni 652,720 walitoka nchini, ikilinganishwa na wageni 681,750 waliotoka nchini katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Kwa ujumla, idadi ya wageni walioingia na kutoka nchini imepungua. Kushuka kwa idadi hii, kunaweza kuelezwu pamoja na mambo mengine ni kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009, wageni 10,682 walipewa vibali vya kuishi nchini, ikilinganishwa na wageni 11,356 walipewa vibali mwaka 2007/2008. Idadi ya vibali viliviyotolewa imeshuka kwa asilimia sita. Hii inatokana na baadhi ya makampuni au mashirika kupunguza nafasi za ajira au idadi ya watumishi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetoa uraia kwa wageni 146 waliotimiza masharti na kuyakataa maombi 41.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ikishirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (*UNHCR*), inaendelea kushughulikia maombi ya uraia ya Wakimbizi wa Burundi walioingia nchini mwaka 1972 na kuishi katika makazi ya Mishamo na Katumba Mkoani Rukwa na Ulyankulu Mkoani Tabora. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2008 hadi mwezi Mei, 2009, Wizara imekwishapokea maombi ya Wakimbizi wakaazi 51,876 toka Mkoani Rukwa na 20,523 toka Mkoani Tabora, ambayo yameshughulikiwa katika ngazi za Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa. Wizara inaendelea na zoezi la kuyapitia na hatimaye kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Watanzania 32 walipatiwa uraia wa nchi nyingine na hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995. Watanzania wengi wanaoukana uraia wetu ni wanawake. Kati ya idadi hiyo, wanawake ni 21 ambao ni sawa na asilimia 66 kutokana na wengi wao kuolewa na wageni wa mataifa mengine. Wanaume ni 11 waliopata uraia wa mataifa mengine, kutokana na ama kupata ajira ughaibuni au kutegemea kupata mafao yatolewayo kwa raia wa nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nchi yetu kuruhusu uraia wa nchi mbili, imekuwa ikijadiliwa ndani na nje ya Bunge lako Tukufu kwa miaka kadhaa. Bila shaka kutokana na ukweli kwamba, Tanzania ipo katika mageuzi ya kisiasa na kiuchumi na katika mageuzi hayo, kila njia inatafutwa ili kuharakisha maendeleo ya nchi. Serikali imekuwa ikilifanya kazi suala hili la uraia wa nchi mbili. Kwa kuzingatia kuwa uraia ni suala la Muungano, Serikali iliwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ ) ili kupata maoni yake. Baada ya kupata maoni ya awali ya SMZ, Wizara yangu imeendelea kulifanya kazi kwa lengo la kufikia muafaka juu ya namna ya kulishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Uhamiaji ilitoa jumla ya pasipoti 46,622. Kati ya hizo 44,586 ni za kawaida, 1,677 ni za Afrika Mashariki, 297 za Kibalozi na 62 za Kitumishi, ikilinganishwa na jumla ya pasipoti 69,521, ambapo pasipoti 66,339 za kawaida, 2,691 za Afrika Mashariki, 392 za Kibalozi na 99 za kiutumishi zilizotolewa mwaka 2007/2008. Jedwali Na. 7 linatoa mchanganuo wa huduma zilizotolewa na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, vijana 372 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali, baada ya kubainika kwamba, wapo kwenye nchi hizo kinyume cha sheria ikilinganishwa na vijana 382 waliorudishwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009, Idara iliendesha doria na misako yenyе lengo la kudhibiti wageni haramu nchini, ambapo jumla ya wageni 3,109 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikilinganishwa na wageni 3,252 waliokamatwa katika kipindi cha mwaka 2007/08. Mionganoni mwa idadi ya wahamiaji haramu waliokamatwa, 1,162 walitokea nchi za Pembe ya Afrika (Somalia 37 na Ethiopia 1,125). Kati yao 1,089 wamekwisharejeshwa kwao na 73 wapo katika magereza mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, ujenzi umekamilika wa nyumba ya makazi ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Manyara na ofisi ya kituo cha kuingilia nchini cha Mkenda Nakawale mpakani mwa Tanzania na Msumbiji Mkoani Ruvuma. Awamu ya kwanza ya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Uhamiaji Moshi imekamilika na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam, upanuzi wa Ofisi Kuu Zanzibar na ukarabati wa nyumba katika kituo cha mpakani cha Uhamiaji - Rusumo unaendelea. Miradi hii itaendelea kutekelezwa katika mwaka 2009/2010

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, askari wapya 192 wameajiriwa na askari/watumishi 374 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2009/2010, askari 150 wataajiriwa na mafunzo yatatolewa kwa watumishi 36.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Idara imelipia magari tisa na mwaka huu zitanunuliwa pikipiki 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Mei, 2009 walikuwepo wakimbizi 301,644 nchini. Wakimbizi 234,672 ni Warundi, 63,116 Wakongo (*DRC*), 1,529 ni Wasomali na 2,327 ni wakimbizi wa mataifa mbalimbali. Warundi wapatao 194,986 wanaishi kwenye makazi ya wakimbizi yaliyoko Katumba na Mishamo Wilayani Mpanda Mkoani Rukwa na Ulyankulu na Urambo Mkoani Tabora na wengine 39,686 wanaishi katika makambi Mkoani Kigoma. Katika kipindi 2008/2009, kambi moja ya Nduta iliyopo Wilayani Kibondo Mkoani Kigoma ilifungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia tathmini iliyofanywa mwaka 2007 kwa wakimbizi 218,234 waishio kwenye makazi ya Ulyankulu (Tabora), Katumba na Mishamo (Rukwa), wakimbizi 172,000 sawa na asilimia 79 walionesha nia ya kutaka kubaki nchini. Mchakato wa kuwatafutia suluhisho la kudumu unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuratibu ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo vya Wizara na pia malalamiko ya askari na watumishi wengine wa Wizara, ipo idara maalum kwa ajili ya kazi hiyo. Katika mwaka 2008/2009, idara ilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 104, mengi yakihu Jeshi la Polisi kuhusiana na ubambikizaji wa kesi na askari wa vyeo vya chini kulalamika kutotendewa haki katika suala zima la kufukuzwa kazi kwa askari hao. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeazimia kuanza mchakato wa kutunga sheria ambayo itaipa nguvu ya kisheria idara hii katika kutekeleza majukumu yake.

Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, jumla ya vyama 296 viliandikishwa na hii inafanya jumla ya vyama vilivyoandikishwa hadi sasa kuwa 5,722. Pia idara iliendelea kutatta migogoro ya vyama mbalimbali, vikiwemo sita vya kidini na vingine saba vya kiraia. Hata hivyo, migogoro hiyo bado inaendelea na chanzo kikubwa cha migogoro ndani ya vyama hivyo ni uchu wa madaraka na tamaa ya fedha mionganoni mwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, ili kufuatilia uhai wa vyama, zoezi la uhakiki limefanyika katika Mikoa 12 ya Mtwara, Lindi, Mbeya, Iringa, Mara, Mwanza, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Pwani na Morogoro na kubaini kuwa vyama vingi vinashindwa kutekeleza majukumu yake kutoptana na kuwepo migogoro ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha utendaji katika Idara ya Huduma ya Sheria inayosimamia pia usajili wa vyama vya kijamii, katika mwaka 2009/2010 inataraja kuwa na *database* ya usajili wa vyama, kuendelea kushughulikia migogoro ya vyama, kuhakiki utendaji na uhai wa vyama na kuelimisha vyama vilivyoandikishwa juu ya wajibu wao wa kulipa ada ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kwa kupitia na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara

ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2009/2010, pamoja na ushauri wao katika masuala mbalimbali yahusuyo Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, Katibu Mkuu - Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Elizabeth Nyambibo, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Inspeksa Jenerali wa Polisi - Ndugu Saidi Mwema, Kamishna Mkuu wa Magereza -Ndugu Augustino Nanyaro, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji - Ndugu Kinemo Kihomano na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji - Ndugu Matwani Kapamba, Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda wote, Askari, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao kwa ushirikiano wao, hotuba hii imeweza kuandaliwa na kukamilika kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani kwa nchi wahisani za Denmark, Canada, Sweden, Belgium, Libya na Uhollandzi. Vile vile kwa nchi za China, UAE na Marekani. Aidha, shukrani zangu iziendee Taasisi za Kimataifa za INTERPOL, UNHCR, IOM, NORAD, WFP na Benki ya Dunia, kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2009/2010 ya shilingi 395,345,819,200 kama ifuatavyo:-

Fungu 14: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	
Matumizi Mengineyo shilingi	3,080,000,000
Mishahara shilingi	1,246,343,000
Maendeleo shilingi	3,000,000,000
Jumla shilingi	<u>7,326,343,000</u>

Fungu 28: Jeshi la Polisi	
Matumizi Mengineyo shilingi	99,058,982,000
Mishahara shilingi	92,612,438,000
Maendeleo shilingi	22,870,815,000
Jumla shilingi	<u>214,542,235,000</u>

Fungu 29: Jeshi la Magereza	
Matumizi Mengineyo shilingi	52,000,000,000
Mishahara shilingi	48,238,639,000
Maendeleo shilingi	12,988,927,000
Jumla shilingi	<u>113,227,566,000</u>

Fungu 51: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	
Matumizi Mengineyo shilingi	4,500,000,000
Mishahara shilingi	1,629,483,000
Maendeleo shilingi	6,440,980,200

Jumla shilingi	<u>12,570,463,200</u>
Fungu 93: Idara ya Uhamiaji	
Matumizi Mengineyo shilingi	15,374,996,524
Mishahara shilingi	13,309,107,476
Maendeleo shilingi	18,995,108,000
Jumla shilingi	<u>47,679,212,000</u>

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kwamba, sehemu zote za hotuba yangu iliyowasilishwa leo asubuhi ambazo sikupata nafasi ya kuzisoma hapa leo, zipokelewe kama sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**MHE. MUSSA AZAN ZUNGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114 (11), naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kuliomba Bunge lako Tukufu liyapokee na kuyajadili Maoni haya na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya majukumu ya Kamati hii ni kupokea na kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuishauri na kuisimamia Wizara hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 21 Januari, 2009, Kamati ilitembelea Makao Makuu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupata maelezo kuhusu Mradi wa Jengo Jipyala Makao Mkuu ya Wizara hiyo. Aidha, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, tarehe 5 Aprili, 2009, Kamati ilipitia taarifa ya Wizara kuhusu mtiririko wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 02 Juni, 2009, Kamati ilikutana kupokea Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2008/2009, Kamati ilitoa ushauri kuhusu utendaji wa Jeshi la Polisi; Magereza; Zimamoto na Uokoaji; na Uhamiaji. Napenda kuliarifu Bunge lako

Tukufu kuwa, Serikali imetoa ushirikiano na imeendelea kutekeleza ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. Kwa mfano, Maeleo ya Waziri yalionesha kuwa, Serikali imejitahidi kuwapatia Askari Polisi, vitendea kazi kama magari, pikipiki na fulana za kuzuia risasi. Aidha, Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali imeongeza Bajeti ya Jeshi la Polisi ili kuliwezesha kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu nchini. Jeshi la Polisi limefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika jitihada za kuendesha operesheni za kudhibiti ujambazi na vitendo vya uhalifu ili kulinda usalama wa raia na mali zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa fedha wa 2008/2009, Taarifa za Serikali zilionesha kuwa, majambazi sugu na wahalifu wengi wamekamatwa. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, licha ya changamoto kadhaa zilizopo kwa Jeshi hilo. (*Makofî*)

Aidha, tulielezwa namna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilivyota mafunzo kwa askari 60 katika Chuo cha Magereza Kiwira – Mbeya ili kuongeza uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Kamati inashauri juhudhi hizi ziendelezwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri, alieleza Kamati Malengo ya Wizara kwa Mwaka 2009/2010. Kwa upande wa Jeshi la Polisi, Kamati ilielezwa mkakati wa kupunguza na kudhibiti uhalifu, mpango wa maendeleo ya askari na watumishi, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo na nyumba za askari, pamoja na mpango wa ununuzi wa magari 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa pia malengo ya Jeshi la Magereza kuhusu maendeleo ya watumishi, miradi ya maendeleo na ununuzi wa magari 11. Kuhusu Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, Mheshimiwa Waziri alieleza azma ya Serikali kuwezesha mafunzo kwa wazimamoto na waokoaji 300 na kuajiri askari wapya 42. Suala lingine muhimu lililoelezwa ni mpango wa tahadhari, ukaguzi na kinga ya moto katika maeneo mbalimbali, pamoja na maendeleo ya Watumishi na mafunzo. Kwa upande wa Uhamiaji, Mheshimiwa Waziri, aliarifua Kamati kuhusu mpango wa kufanya misako, doria na operesheni dhidi ya wahamiaji haramu, pamoja na lengo la kununua pikipiki 20 na kuendeleza ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo na nyumba za kuishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilielezwa kuhusu azma ya Serikali kuanza mchakato wa kufanya Marekebisho Sheria ya Uandikishaji na Utambuzi wa Watu ya Mwaka 1986. Kamati inasisitiza kuwa, mchakato huo uharakishwe sanjari na kukamilisha mchakato wa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza vyema majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 395,345,819,200. Kati ya fedha hizo, shilingi 174, 013,978,524 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 155,914,301,776 zimetengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 64,295,830,200 kwa ajili ya maendeleo.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inatarajia kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya shilingi 42.9 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2008/2009 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Baada ya kupitia mafungu yote matano, Kamati inaunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuliomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha maombi haya pamoja na maoni ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii na utekelezaji wa majukumu yake kwa mafungu yote kama ifuatavyo:-

Jeshi la Polisi:

Kwa kuzingatia utendaji wa Jeshi la Polisi na malengo yake ya Bajeti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati inashauri:-

- Tatizo la upungufu wa magari na nyenzo za utendaji kwa Jeshi la Polisi kwenye Wilaya mbalimbali nchini litatuliwe haraka sana;
- Elimu kwa Umma iendelee kutolewa ili kupunguza malalamiko kuhusu vitendo vya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi nchini. Aidha, suala la Ulinzi Shirikishi kupitia dhana ya Polisi jamii liimarishwe nchini kote;
- Serikali ikamilishe ujenzi wa Ofisi za Polisi katika Wilaya zisizokuwa na ofisi hizo, sambamba na kuandaa Mpango Mahususi wa ujenzi wa Vituo vya Polisi ngazi ya Kata nchini kote;
- Kikosi cha Polisi wanamaji (*Police Marine*) kiwezeshwwe kwa kupatiwa maboti yaendayo kwa kasi na yenyewe uwezo wa kuendelea kumudu vyema majukumu ya kikosi hicho;
- Maafisa na Askari Polisi waliokaa katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu wahamishwe, sambamba na kuhimiza uzingatiaji wa maadili kwa Maafisa wa Polisi wanaofanya biashara;
- Utaratibu wa Jeshi la Polisi wa kutoa habari juu ya matukio mbalimbali uboreshwe, kuepuka mkanganyiko kwa umma;
- Serikali iboreshe na kuimarisha huduma na miundombinu ya habari na mawasiliano ndani ya Jeshi la Polisi;

Jeshi la Polisi liongeze ukusanyaji wa maduhuli kwa kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Sheria mbalimbali nchini, hususan Sheria za Usalama Barabarani;

Jeshi la Magereza:

- Kwa kuzingatia utendaji wa Jeshi la Magereza na malengo yake ya Bajeti, kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Kamati ina maoni na ushauri kama ifutavyo:-
- Kwa kuwa Jeshi la Magereza likiwezeshwa ipasavyo linaweza kuongeza uzalishaji mali kwa kiasi kikubwa, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Jeshi la Magereza liwezeshwe Kifedha kwa kutumia Mpango wa Kitaifa wa Kuendeleza Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme ASDP*); (*Makofi*)
- Serikali iongeze kasi ya kurekebisha Sheria zinazosababisha msongamano Magerezani;
- Jeshi la Magereza liwezeshwe kifedha ili kuboresha huduma zake;
- Pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika kukabilianana na tatizo la makazi ya Askari Magereza, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iongeze kasi katika kutatua tatizo la makazi ya Askari Magereza.

Uhamiaji:

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha huduma za uhamiaji na kuongeza maduhuli yanayokusanywa mipakani, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-
  - Serikali iboreshe vituo vya uhamiaji kwa kuviimarisha sambamba na kuviwekea zana na vifaa vya kisasa vituo vyote kwa kuzingatia mahitaji;
  - Ujirani mwema baina ya Tanzania na nchi zinazotuzunguka utumike kudhibiti wahamiaji haramu wanaopitia mpaka wa Tanzania na Kenya; na
  - Umakini mkubwa unahitajika katika maamuzi ya kutoa uraia kwa wanaoomba ili kuzingatia mahitaji ya nchini.

Zimamoto na Uokoaji:

- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia katika utekelezaji wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji na Uhamishaji wa Vyombo vya Zimamoto na Uokoaji kutoka Serikali za Mitaa, Kamati inasisitiza utekelezaji wa ushauri wake kuwa:
  - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lijengewe Ofisi ya Makao Makuu badala ya kupanga;
  - Mafunzo ya Zimamoto na uokoaji yapewe uzito unaostahili; na

- Serikali iongeze juhudi ya kukiwezesha Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kwa kukipatia vitendea kazi bora na vya kutosha ili kuimarisha utendaji kazi zao kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepuka kukua kwa madeni ya wazabuni na askari, Kamati inashauri kuwa, utekelezaji wa Bajeti kwa kila mwaka wa fedha, uende sambamba na kukamilisha ulipaji wa madeni yote kwa mwaka huo. Aidha, Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe kuwa, idadi ya askari wa vikosi viliyvo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inalingana na mahitaji ya vikosi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Nawashukuru sana Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Mbunge, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Ndugu Patrick Rutabanzigwa, Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri, ushirikiano mzuri na maandalizi ya Taarifa zenye maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Inspekte Jenerali Said A. Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, kwa kuliongoza vyema Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, shukrani nazitoa kwa Kamishna Augustino Nanyaro, Mkuu wa Magereza nchini, Kamishna Msaidizi Mohamed Kapamba, Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Kinemo Kihomano, Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji, Askari wote na Watumishi wote wa Kiraia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Utekelezaji mzuri wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa ushirikiano, busara na michango yao ya kina katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii na kukamilisha taarifa hii kwa wakati ili iwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Kahalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mhangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru Dkt. Thomas D. Kashililah - Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano

na huduma nzuri sana. Aidha, nawashukuru kipekee, makatibu walioihudumia Kamati hii; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Stella Mlambo, kwa kuratibu vyema na umakini katika kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti. Sasa ntamwita Msemaji Mkuu toka Kambi ya Upinzani, ambaye ni Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Tunajiandaa kwa mwakani kuwa Mawaziri kamili.

**NAIBU SPIKA:** Hapana shaka unaelekea hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa hai na wenye afya na kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya Umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni ya 99 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa, kwa Chama changu cha Wananchi (CUF) na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe, Zanzibar, kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kuhakikisha kuwa, natekeleza majukumu yangu kama Mbunge kwa umahiri mkubwa ili kutimiza malengo na sera za Chama chetu na Taifa kwa ujumla. Aidha, naushukuru pia Uongozi wa Kambi ya Upinzani, chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Slaa, kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya Hotuba hii. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, ambaeo ni Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kutimiza wajibu wangu kama Waziri Kivuli wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama Nchini Tanzania, inaonekana sio shwari katika kipindi hiki kama ambavyo tulikwizhazoea, jambo ambalo lilifanya kila mtu kutembea kifua mbele. Matukio ya uporaji, yameanza kurudi tena mchana kweupe;

na hata baadhi ya wananchi kunyang'anywa haki zao za msingi kwa misingi ya itikadi zao. Jambo baya zaidi ni matukio ya kutisha yanayoendelea Mkoani Mara, Wilayani Tarime. Yote hayo, yanaendelea kuitia dosari historia yetu nzuri kwamba, Tanzania ni nchi yenyе amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la matumizi ya madawa ya kulevyahapa nchini ni jambo linalopelekeaa kupoteza vijana wengi, ambao ndio nguvu kazi ya nchi yetu. Mara nyingi vijana hawa ambao ni tegemeo kwa wazazi wao, pamoja na Taifa letu, hujiingiza katika wizi na hata kuambukizwa UKIMWI kwa namna moja au nyingine. Hata kiongozi wa nchi hii, Mheshimiwa Rais alikwishesema vigogo hawa wanafahamika; je, ni lini watu hawa watafikishwa mahakamani ili wajulikane na ni hatua gani za Kisheria zimechukuliwa dhidi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kwa nini hadi sasa hakuna hata kinara mmoja wa madawa ya kulevyahali yaliyofikisha katika vyombo vya Sheria? Masuala kama haya ndiyo yanayosababisha Watanzania walione Jeshi letu la Polisi kuwa linafanya kazi kwa *double standard*; wengine wanakamatwa na wengine wanalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalitaka Jeshi la Polisi lifanye kazi zake kisayansi kwa hali ya juu kabisa ili wale watakaobainika na dhambi hizi, wafikishwe katika vyombo vya Sheria nchini. Hii ndiyo njia ya kurejesha imani kwa raia na kuona kwamba, Serikali yao iko makini katika kulinda haki zao pamoja na rasilmali za nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mambo ya utawala ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka huu ni Sh. 6,129,483,000 tu. Hii inahusisha vitengo vifuatavyo: Wizara yenyewe, Uhamiaji, Zimamoto na Idara ya Wakimbizi. Wakati *Personnel Allowance (discretionary), Optional*, kwa idara tatu za Hazina zimetengewa jumla ya Sh. 3,338,850,000, ambazo ni sawa na asilimia 54.5 ya bajeti nzima ya mambo ya utawala katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba zetu za Kambi za miaka 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009, tumekuwa tukizungumzia suala la uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenship*). Majibu ya Serikali mara zote ni kwamba, mchakato unaendelea na huku muda ukiyoyoma. Je, mchakato huo ni lini utamalizika? Sababu nyingi za kutaka kuwepo kwa uraia wa nchi mbili tayari tulikwishesazieza. Faida za kiuchumi hakuna asiyeelewa na kama tunataka kuzifahamu zaidi, tuangalie jinsi nchi za wenzetu zinavyofaidika kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu yaliyosemwa na Mheshimiwa Waziri mwezi wa Juni, 2006: “*Sasa nieleze hatua tuliyofikia katika mradi wa kutoa vitambulisho vya kiraia. Tumemaliza hatua ya upembusi yakinifu na tumeandaa mchakato (Action Plan) wa kuanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu katika mwaka wa fedha 2006/2007. Baada ya kupata baraka za Serikali, itaitishwa tenda ili kupata Kampuni yenyе ujuzi na uwezo wa kuisaidia Serikali katika utekelezaji wa mradi*

*huu. Maandalizi mengine ya kupata jengo la mradi na watumishi wa mradi yameanza kufanyika. Vile vile zoezi la kuwatambua wageni wanaoishi huko vijiini na mijini na kuwaorodhesha, limeanza katika Mikoa ya mipakani na baadaye litaendeshwa katika Mikoa yote Bara na Visiiani, ikiwa ni mkakati wa kuzuia wageni wasipate vitambulisho vya uraia hapo zoezi la kutoa vitambulisho litakapoanza.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka huo wa 2006 hadi sasa 2009, bado mchakato unaendelea tu, kila siku tunaambiwa hadithi mpya kuhusiana na vitambulisho hivyo. Pesa za walipa kodi zinazidi kuwaneemesha baadhi ya watu katika kadhia nzima ya vitambulusho vya uraia. Je, Serikali inawatendea haki Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa, Waziri Mkuu atembee kwenye kauli zake kama alivyosema katika hotuba yake ya majumuisho ya hivi karibuni kuwa, yeye na Serikali watafanya kila njia kuhakikisha wanapunguza matumizi yasiyo ya lazima. RITA na NIDA zote ni asasi za serikali, lakini moja haiwezi kufanya kazi bila ya mwezake; kwa nini zisifanywe kuwa kitu kimoja au moja ikaondoshwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa RITA imeonesha uwezo mkubwa katika utendaji wake wa kazi; hivyo ni muhimu sana kwa wakala huu kupewa kazi zinazohusu uandikishaji na usajili. *Best practices*, nchi nyingi duniani kama vile Singapore, India, Korea kusini na Malaysia utaratibu wa kutumia wakala kama RITA, hufanya kazi zote zinazohusu uandikishaji. Lengo kubwa ni kupunguza gharama za uendeshaji na usumbufu wa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhana hiyo hiyo ya kupunguza matumizi, naomba Waziri atueleze kwa muda wote amba Mamlaka ya Vitambulisho imeundwa hadi sasa karibu miaka miwili; je, Serikali imepata nini au ndio tuseme watumishi wanalipwa mshahara bila ya kufanya kazi? Utawala Bora uko wapi hapa? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe ufanuzi kwa hili la watu kulipwa bila ya kufanyakazi. Aidha, Waziri atueleze Sh. 4,393,788,000 zilizotengwa kwa Mamlaka ya NIDA ni za kufanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi La Polisi, kwa kweli ndio tegemeo kubwa kwa usalama wa raia na mali zao. Hatuna budi kuwapongeza kwa dhati, kwa kazi nzito wanazokabiliana nazo usiku na mchana, bila ya kujali muda na mazingira ya kazi yenye. Hivyo ni vyema basi Serikali ikafanya juhudzi za lazima ili wapatiwe posho nzuri na kutengenezewa mishahara inayokwenda sambamba na hali ya maisha ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za taarifa ya maendeleo ya hali ya Umasiki (PHDR), iliyotolewa mwaka 2007, zinaonesha kuwa wizi wa mali za watu ni asilimia 52, matatizo yanayohusu ardhi ni asilimia 37 na matatizo ya madawa ya kulevyia ni asilimia 33. Mbali na takwimu hizo ambazo zinahusiana na usalama wa watu na mali zao, pia Jeshi la Polisi linalalamikiwa sana kwa vitendo vya kunyanyasa raia, watuhumiwa na wasio watuhumiwa, limekithiri mionganii mwa polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji huu umetajwa kama ukiukwaji wa haki za binadamu. Uchunguzi uliofanywa na taasisi ya Haki Elimu, umeonesha kuwa, baadhi ya polisi wamekuwa wakijichukulia Sheria mikononi mwao kwa kuwapiga wananchi na kuwafanya vitendo viovu, ikiwa ni pamoja na kuwabambikia kesi, limekuwa ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni lini Jeshi la Polisi limefanya kile kinachoitwa *Human Resource Auditing*? Tunavyoolewa hii ni kuangalia kazi anayofanya mtu imeongeza tija kiasi gani kwa taasisi na kutokuwepo kwake katika sehemu hiyo ni hasara gani inayoweza kupatikana kwa taasisi au kwa umma?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imeuliza hivyo kwa kuwa kuna askari wamekaa katika vituo kwa zaidi ya miaka 10, wakati RPCs, OCDs na OC-CIDs, wanahamishwa vituo vyao mara kwa mara. Je; ni sababu gani za msingi zinazopelekea askari wa chini ya ngazi hizo kutohamishwa kutoka katika vituo vyao?

Mheshimiwa Naibu Spika, askari polisi kupata uhamisho ni haki yao ya Kisheria, lakini inasikitisha sana kwamba, askari hawa huwa hawapewi haki zao za msingi. Hivyo basi, tunaomba kwamba, wale askari ambao hawajalipwa wapewe fedha zao katika kipindi hiki cha mwaka 2009/2010. Jeshi la Polisi mbali na kufanya kazi nzuri, lakini ndio watu wanaolinda uchumi wa nchi na vitega uchumi vyenyewe, hivyo tuangalie maslahi yao. Kwa kutoa mfano kwa hilo, inasemekana kuwa, wapo askari zaidi ya 300, ambao wamepata uhamisho kutoka Zanzibar na kuja upande wa pili wa Muungano na hadi hii leo ni zaidi ya miezi sita bado hawajapatiwa fedha zao za uhamisho. Je, hii ndiyo haki katika Jeshi la Polisi? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri leo atupe ufumbuzi kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari polisi kazi zao ni za kila siku, hivyo vitendea kazi bado ni kidogo, hasa ukizingatia mazingira na ukubwa wa nchi yetu. Ni vyema wakatafutiwa magari zaidi, pikipiki na kupewa mafuta ya kutosha katika kazi zao za kila siku. Wanapopata ajali kazini au kupata majeraha ni lazima uwepo mfuko maalum wa dharura ili wapatiwe matibabu ndani au hata nje ya nchi ikibidi kufanya hivyo na kwa hili sio tu kwa askari wa polisi, hata askari wa magereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mahabusu baadhi ya wakati wamekuwa wakinyanyaswa sana kuliko hata wafungwa. Hali hii imekuwa ikiwatatiza raia pale wanapohitaji msaada wa kipolisi au pale wanapokumbwa na matatizo na kushindwa kujitetea. Vitisho vinasababisha wananchi waogope vituo vyta polisi na hata polisi wenyewe. Hii imesababisha ushirikiano kati ya polisi na wananchi kuwa mgumu na hivyo kuwafanya wananchi kujichukulia Sheria mikononi mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia dira ya jeshi hilo, naomba kunukuu: “*Ni kuifanya nchi yetu kuwa yenye utulivu na amani, ambapo Utawala wa Sheria unathaminiwa na kuenziwa ipasavyo, kama umuhimu wa kuheshimu haki za binadamu,*

*umuhimu wa uwazi kwa jamii, umuhimu wa uaminifu, umuhimu wa uadilifu, umuhimu wa kuwaheshimu raia, na umuhimu wa kuwatumikia wananchi kwa uadilifu.”*

Mheshimiwa Spika, kwa matatizo hayo yote ambayo jeshi linatuhumiwa kuyafanya kwa raia; ni dhahiri yanaliondolea heshima Jeshi letu na kusababisha hata dhana ya Polisi Jamii kuwa ngumu. Aidha, ule msemo unaosema kuwa, kuingia polisi ni bure lakini kutoka ni kwa pesa, unapewa uzito na jamii kutokana na sababu tulizokwishazitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa, Jeshi la Polisi limekuwa likikwama katika kutekeleza mpango mkakati wake, kutokana na ufinyu wa bajeti. Kabla sijaendelea, naomba kurejea kauli za Viongozi wangu wa Kambi wakati wakiwasilisha Hatuba za Kambi kuwa, tatizo la nchi hii ni jinsi ya kuona viapumbele katika ugawanaji wa rasilimali chache tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali halisi ya Jeshi letu ni kweli kabisa lina uwezo wa kutoa huduma kama ambavyo majeshi mengine ya polisi duniani yanavyotoa huduma zao kwa jamii, lakini kilichokosekana ni kutokuangalia ukubwa wa nchi yetu, wingi wa watu na uhaba wa askari ukilinganisha na hayo niliyoyataja. Mfano, kwa kiwango cha kimataifa, askari mmoja ni kwa watu 450 (1:450), wenzetu Kenya ni askari mmoja kwa watu 821 (1:821), wakati sisi Tanzania ni askari mmoja kwa watu 1300 (1: 1300).

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia bajeti nzima iliyotengwa kwa ajili ya Jeshi la Polisi, kwa mwaka huu wa fedha ni Sh.191,671,420,000. Baada ya kujumlisha fedha zilizopangwa katika fungu la *Personnel Allowance (discretionary, Optional)* ni Sh. 17,212,858,247; ni fedha nyingi mno na fungu la *Personnel Allowance in-kind* ni Sh.19 bilioni, fungu la safari za ndani na nje ya nchi kwa Wizara mbalimbali ni Sh. 34,637,638,460 (Sh. 34.64 bilioni). Hizo zote zikijumlishwa ni Sh. 70,850,496,707 (Sh. 70.85 billion). Hizi ni fedha nyingi; hivyo ni vyema tukakata angalau asilimia 20 ya matumizi haya ili fedha hizo ziweze kutumika kwa ajili ya kuajiri askari wa jeshi la polisi ili upatikane ufanisi zaidi. Hasa ukizingatia ukuaji wa wawekezaji ambaa huhitaji huduma ya jeshi la polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatusemi kuwa safari za ndani na nje zisiwepo ila ni kuangalia hali halisi ya uchumi na sio lazima kila idara iwekewe bajeti ya safari. Kama ndio hivyo nini maana ya Serikali mtandao (*e-Government*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuwa, kama tunataka maendeleo kwa vyombo vyetu vya kutoa huduma zinazotakiwa au zinazotarajiwa kutolewa, hatuna budi kuangalia upya jinsi ya kupanga vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na matatizo hayo ambayo tunaona, Serikali kwa mujibu wa Waziri Mkuu kuwa watayashughulikia kadiri muda unavyokwenda, pia kuna upungufu wa wazi ambaa umeainishwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama vile malipo yaliyofanywa bila kuwepo nyaraka sahihi ya Sh. 74,000,000,

masurufu yasiyorejeshwa yanayofikia Sh. 131,000,000. Mapato yasiyo kusanywa ya Sh. 98,000,000. Hii yote ni dalili dhahiri kuwa, hata kile kidogo tunachopata, hakitumiwi vizuri na hii inasababisha malalamiko yasiyokwisha ya madai kutoka kwa askari wetu. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri suala hili pia liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, taarifa inaonesha kuwa, Jeshi la Polisi linadaiwa kiasi cha Sh. 23,354,120,000 na wazabuni mbalimbali wa ndani. Siyo vyema wazabuni hawa kucheleweshewa malipo yao kwa wakati muafaka. Tukifanya hivyo, tunachangia kuzoretsha huduma wanazotoa kwa askari wetu na hivyo kupelekeea kukosa mahitaji muhimu kwa askari wa jeshi la polisi. Tukumbuke kwamba, wazabuni hawa hupata mikopo kutoka katika mabenki na wanaposhindwa kurejesha fedha kwa wakati, huendelea kutozwa riba kubwa. Kambi inauliza kama Sera ya Serikali ni kutumia kulingana na kile ulichonacho (*Cash Budget*); hivi inakuwaje taasisi za Serikali zinatumia sera tofauti na hiyo? Tunamtaka Waziri atoe ufanuzi kuhusiana na suala hili la Jeshi la Polisi kuwa na deni kubwa kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Magereza ni mojawapo ya Idara muhimu katika Serikali yetu ya Tanzania, iliyopewa jukumu muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu. Dira ya Idara hii ni kuwa na mfumo wa kurekebisha raia waliopatikana na hatia ya kuvunja Sheria za nchi ili watokapo gerezani, wawe raia wema katika jamii yetu kwa kufuata taratibu na vigezo vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa, jeshi la magereza mbali ya kuwa chombo au taasisi ambayo ina jukumu la kurekebisha tabia za raia, pia jeshi hilo halikuachwa nyuma katika kadha nzima ya kuongeza kipato cha Idara hiyo kwa kuwa na miradi mbalimbali, kama vile kilimo, ujenzi, uashi, michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba zetu za nyuma, tulitaka kuelewa kwa nini magereza ambayo zamani yalikuwa yanasiyofikia kwa uzalishaji mkubwa kwa mazao ya kilimo, kwa sasa makambi hayo hayafanyi vizuri kiuzalishaji na badala yake yamekuwa kama magereza ya mateso zaidi badala ya kurekebisha tabia?

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Kilimo Kwanza iangalie zaidi kwa namna moja au nyingine, katika kufufua kilimo ndani ya Jeshi la Magereza. Hakuna asiyeelewa ni jinsi gani magereza walivyokuwa wanazalisha na kutosheleza mahitaji yao ya chakula na ziada. Magereza wanayo maeneo makubwa ambayo wanaweza kuzalisha kwa ajili ya chakula chao na hata cha ziada kwa ajili ya kuuza na kuisaidia nchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa kama kweli dira ya Jeshi la Magereza inatafsiriwa kwa vitendo na ni kweli vile vigezo vya Kimataifa katika kuhakikisha tabia za wahusika zinabadilika vinafuatwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ya Magereza kama zilivyo idara nyingine za Serikali, nayo ina matatizo ya matumizi yasiyofuata kanuni na taratibu za kisheria zilizowekwa. Katika Taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibitii Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonesha kuwa, jumla ya malipo ya Sh. 824,563,334 yalifanywa bila ya kuwepo nyaraka

sahihi kulingana na taratibu zinazotakiwa. Manunuzi ya Sh.119,875,376 yalifanywa kienyeji tu, bila ya kufuata taratibu zinazotakiwa kwa kuitishwa kwenye Bodi ya Manunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004. (*Makofi*)

Aidha, matengenezo ya magari ya idara yamefanya malipo ya jumla ya Sh. 205,404,964 bila kuitia kwa Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA), kinyume na matakwa ya Kanuni za Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona upungufu huo wote kuwa ni mojawapo ya uzembe unaoendelea kulitia Taifa hasara na hivyo tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa, uzembe huu unapatiwa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni suala la ndugu zetu wenyе ulemavu wa ngozi. Ni jambo la kusikitisha, kwa nchi kama yetu kuwa bado na watu wenyе fikra potofu na za kijinga eti watapata utajiri kwa kutumia viungo vya binadamu. Suala la kuvamiwa na hata kuuawa kwa ndugu zetu wenyе ulemavu wa ngozi (*Albino*) ni jambo lisilovumilika. Nawapongeza Askari wa Jeshi la Polisi, kwa kufanya msako mkali kwa kuwakamata na kuwakabidhi wahalifu hawa katika vyombo vya sheria. Ila Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa askari kuwa, wasichoke kwani inawezekana wahalifu wa aina hii bado tunao katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu ya mwaka 2007/2008, tuliulizia kuhusu kutoroshwa kwa mwanafunzi Mariam Farid, mwenye umri wa miaka 16 na mwalimu wake mwenye asili ya Uganda. Tuliambiwa kuwa, Jeshi la Polisi linashirikiana na *Interpol* kufuatilia kadhia hii. Je, hadi leo mbona kimya? Tunaomba kupata taarifa kamili za mtoto Mariam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Jeshi la Polisi, lisijiingize au kuingizwa katika siasa. Hii ni hatari kwa nchi. Vilevile wasikubali kupokea amri ya mkubwa yejote, itakayokuwa na malengo ya kisiasa. Polisi waachwe wawe walinzi kwa mujibu wa Sheria. Vinginevyo, tunaweza kuwajengea uhasama na raia na kupoteza hadhi ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, IGP, Mheshimiwa Nanyaro, Bana Kihomano na Makamishina, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazozifanya na sisi tuko nanyi bega kwa bega na tutaendelea kudai haki zenu mpaka mjisikie kwamba na ninyi ni Askari Polisi wa Kimataifa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Bwana Sanya.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, Wizara hii tunaijadili leo tu. Kwa hiyo, ninayo orodha hapa; waliochangia mara moja ni 8, waliochangia mara mbili ni 16, waliochangia zaidi ya mara mbili hata kutaja sitaji maana yake ni wengi mno. Tukijitahidi sana ni wachangiaji kumi tu. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Masolwa

Cosmas Masolwa, halafu atakuja Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, halafu atakuja Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, atakuja Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Mohamed Rajabu Soud atafikiwa asubuhi hii. Mheshimiwa Masolwa, tafadhali hama meza. (*Kicheko*)

**MHE MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi nianze kuchangia mada iliyo mbele yetu. Kabla ya kuanza, nitoe salamu za Wananchi wa Jimbo langu, ambao wanasema wanalaani sana mauaji ya Albino, ambayo yanaendelea mpaka sasa na wanasema Serikali isikae kimya. Waliofikishwa Mahakamani, wahukumiwe mapema ili uwe mfano kwa wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ambayo wamewezesha bajeti hii iweze kusomeka. Pamoja na pongezi hizo, ningependa kumkumbushia Mheshimiwa Waziri kupitia Naibu Waziri, kuhusiana na yule kijana wangu, Marehemu Koplo Suleiman Soud, kama tulivyozungumza naye; naomba afuatilie kwani mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa; na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali, hasa Wizara kuipitia Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, kwa uamuvi wake wa kujenga nyumba ya makazi ya askari Kituo cha Bububu, ambacho kitakuwa na jumla ya vyumba kama 16. Nasisitiza kwamba, jengo hilo sasa hivi limesimama, lakini nina imani baada ya bajeti kupita, jengo hilo litakamilishwa na halitachukua muda mrefu.

Pia ningemkumbushia Mheshimiwa Waziri kwamba, Naibu Waziri alipotembelea Bububu, nilimwonesha lile jengo ambalo kuna askari familia mbili wanakaa halijakamilishwa kwa kuweka umeme; ni la miaka mingi sana na aliahidi atachukua hatua, ninamwomba hatua hiyo ichukuliwe ili likamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kidogo juu ya suala la usafiri. Ni kweli Serikali inasema inakuwa na ufinyu wa fedha kwa ajili ya kununua usafiri kama vitendea kazi hasa polisi wetu hawa. Hata hivyo, ningeshauri iangalie mikakati ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa upande wa Zanzibar, kwa sababu katika Wilaya yetu ya Magharibi, kuna gari moja tu la *OCD* na habati mbaya sana, gari hilo huwa linatiwa lita tano tu za mafuta. Lita tano hazitoshii kwa matumizi ya *OCD* kutokana na matukio ambayo yanajitokeza. (*Makofii*)

Wilaya ya Magharibi ni kubwa na iko katika mfumo kama wa mji hivi na kuna matukio mengi sana, ambayo huwa yanajitokeza na katika kipindi kati ya mwezi wa pili mpaka wa tano, kuna matukio matatu makubwa ambayo yalijitokeza, ambayo yalisababisha watu kadhaa kufariki wakiwemo askari wawili wa KVZ. Matukio hayo mengine mawili yangeweza kuwashishwa tu kama askari wangkuwa na usafiri wakafika mapema. (*Makofii*)

Bahati mbaya sana, kutokana na ukosefu wa usafiri, askari waliokuwa wakifika pale tena kwa shida, yaani aazime pikipiki ya mtu, ndiyo anakuta tukio limekwishatoka na watu wameshaathirika. Naiomba sana Serikali, pamoja na ufinyu wa bajeti, ifanye mikakati kwa sababu usalama wa raia ni muhimu sana. Bila kuwa na raia hatutaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ajali barabarani. Usalama wa barabarani umeelewa kiasi, lakini mimi ningetaka kuelezea zaidi, kwa sababu watu wengi hivi sasa duniani wanakuwa kutokana na ajali za barabranii na inasemekana kwa mujibu wa Taarifa ya *World Health Organization*, watu zaidi ya milioni moja na laki mbili hufa kila mwaka kutokana na ajali za barabarani na zaidi ya milioni 50 wanapata majeraha na wengine kuwa na vilema vya kudumu. Kwa maana hiyo, nchi ambazo zinaongoza kwa ajali ni pamoja na Mabara ya Afrika na Asia, tukiwemo na sisi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti hiyo inaendelea kusema kwamba, endapo hatua za makusudi za kupunguza ajali hazitachukuliwa, ifikapo mwaka 2030 itafikia mpaka asilimia 65 ya ajali za bararani ambazo zitasababisha vifo na hivyo kuchukua nafasi ya tano katika sababu ambazo zinasababisha vifo vya binadamu. Sasa hivi vifo vya ajali za barabarani vinachukua nafasi ya tisa. Kwa hiyo, uone hapo jinsi gani wanavyokufa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marika ambayo hufa zaidi ni kati ya miaka 14 mpaka 29. Kwa mujibu wa takwimu ya *World Health Organization*, inaonesha kwamba, watoto wenyе umri kati ya miaka mitano mpaka 14, wanachukua nafasi ya pili kwa vifo duniani, ukilinganisha na sababu nyinginezo ambazo zinasababisha vifo duniani kwa mfano, UKIMWI na maradhi mengineyo. Halafu kuna rika la watoto kati ya miaka 15 mpaka 29, hili linachukua nafasi ya tatu. Marika mengine ni kati ya mwezi mmoja mpaka miaka mine, wana nafasi ya 14. Miaka 45 mpaka 49, nafasi ya nane na miaka 70 na kuendelea ndiyo wanachukua nafasi ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo nafasi nazitaja kwa sababu kuna maradhi fulani ambayo yanásababisha vifo, yameorodheshwa; kwa mfano, maradhi ya UKIMWI yanachukua nafasi ya ngapi. Sasa vifo vinavyotokana na ajali ndiyo hivyo kwa marika hayo. Utaangalia kwamba, rika kati ya watoto wa miaka 14 mpaka 29 ni watu ambao wako shulenii sasa hivi na ndiyo nguvu kazi ya nchi yetu. Mimi ningependekeza, pamoja na Usalama Barabarani kuwaelimisha watoto wetu mashulenii, lakini sasa tubadilishe labda kuwe na *sylabus* kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo, kwa ajili ya somo la Usalama Barabarani kama baadhi ya nchi zinavyofanya. Kwa mfano, Uganda kwa sababu kule ndiyo tunawatoa madereva, tunawatoa hawa vijana hawa raia, wapita njia, kwa hiyo, wakiwa wanajua hatua gani za kuchukua za kujikinga na Usalama Barabarani, itoke Elimu kutokana na Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti imeendelea kusema kwamba, ilifanya tafiti katika nyanja tano na wakatoa tathmini ya kila nyanja, waliangalia kwanza mwendo wa

kasi, yaani *speed*. Nyanja hii imeonekana kwamba, watu wengi wanapoteza maisha, yaani *risk* ni kubwa zaidi ya kupoteza maisha kutokana na mwendo wa kasi. Sisi hapa tumeshuhudia, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya mabasi mengi kupata ajali kutokana na mwendo wa kasi. Mimi mwenyewe hushuhudia jinsi gani basi linavyokupita wewe ukiwa na gari dogo kwa mwendo wa kasi. Sasa fikiria kama itatokea ajali watu waliomo mle itakuwaje? Kwa hiyo, moja hilo waliona kwamba *speed* kali inasababisha ajali.

Lingine ni kwamba, wanaendesa huku wakiwa wamelewa. Nay o imesemekana kwamba, *risk* yake ni kubwa kwa kupata ajali na inasemekana kwamba, kuna nchi ambazo zina sheria za *drink and driving*, ambazo zinamruhusu kiasi fulani cha pombe, yaani inaitwa *blood alcohol concentration* isizidi asilimia fulani, yaani isizidi *gramme* ziwe 0.5. Sasa katika nchi hizo, ajali wenzetu utakuta kwamba ni chache. Tanzania inaonekana kwamba, sisi tunazidi *a blood alcohol concentration* ya *0.05 grammes per litre*. Kwa hiyo, Sheria kama hii inaweza ikawepo, mimi siifahamu vizuri. Kama ipo basi iboreshwe zaidi, mtu ameleta, lazima aangaliwe amesha-*exceed* ile *amount* au haja-*exceed* kama ame-*exceed* basi hatua zichukuliwe zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine kilichoonekana, walichotafiti ni uvaaji wa *helmets*. Imeonesha ya kwamba, asilimia 40 mpaka asilimia 70, inaweza ikaokoa maisha kwa wale wanaovaa *helmets* na hiyo Sheria ni kwamba, siyo tu anayeendesa pikipiki, lakini mpaka na abiria wake. Zile *helmets* lazima ziwe *national standard*, yaani *recognized a national standard* au *recognized by international standards* hasa kwa upande wa Tanzania, inavyoonekana ninavyowaona zaidi ni wale waendesa pikipiki, yule anayeendesa ndiyo anayeruhusiwa kucaa *helmet*. Utakuta kwamba, hiyo *helmet* yenye haiko kwenye *standard*. Mwingine anavaa *helmet* kwa ajili ya kujikinga labda na jiwe litakalorushwa kule kwenye majengo na tunaona hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi sasa hivi wana pikipiki na wengi sana wanakufa kutokana na ukosefu tu wa Sheria Ndogo ya *Helmet*. Kwa hiyo, naomba Serikali ipitie tena upya kuhusu *specification* za *helmet* na uvaaji; kwamba abiria anavaa na mwendesa pikipiki anavaa, hii itatusaidia sana kwa sababu wanasema asilimia 70 ukipata ajali, basi asilimia 70 anaweza ukaepuka kujeruhwiwa kichwa, yaani *70 percent* ukawa ume-*prevent injuries* za kichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine walichogundua wenzetu walichofanya utafiti ni hii mikanda (*seat belt*), mikanda ya kwenye magari. Imeonesha kwamba, asilimia 40 ya nchi duniani kote ndiyo zenye Sheria hiyo. Sasa hizi *seat belt* zinaweza zikasaidia kwa asilimia kubwa kuепusha vifo kutokana na ajali. Tanzania imeonekana kwamba, sisi hatuna Sheria hiyo japokuwa kama ipo basi inam-*favour* zaidi madereva na abiria anayekaa mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ajiandae.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili, nawashukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, kwa hotuba yao nzuri tu waliyoitoa leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima ambalo nataka kulizungumzia hivi sasa ni kuhusu Sera ya Jeshi la Polisi. Kwa kweli ipo haja ya Jeshi la Polisi kuangaliwa upya, vimo baadhi ya vipengele vimepitwa na wakati, kwa sababu havimpi haki askari wa chini katika mfumo mzima wa kustaaful. Utaona kwamba, mfumo mzima wa kustaaful unaneemesha zaidi wale askari wa juu kuliko wale wa chini. Kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia hili suala ili kuhakikisha kuwa na wale askari wa chini wanapostaafu, angalau wanaweza kuyamudu maisha uraiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiliangalia suala zima, kwa mfano, Polisi au Askari *PC* mpaka *Serjeant*, wanastaafu kwa miaka mpaka 40 mpaka 45, yaani bado ni vijana. Askari kama huyu anastaafu anakwenda wapi wakati ambapo muda kama huu anawenza kufanya kazi vizuri tu? Kwa zile sheria ambazo zinambana, ambazo wanajidai ni sheria za hiari lakini uhiari huu unamdhilisha wakati ambapo anastaafu katika kazi hii ya jeshi. Kutoka Meja mpaka *Inspector*, yaani nyota mbili anastaafu miaka 50 mpaka 55, angalau hapa ni nafuu. Wakati huo huo, hawa wanaweza kufanya kazi, lakini ndiyo wenye maslahi mazuri wakati huu wa kufanya kazi. Halafu mwenye nyota tatu mpaka *IGP* wao, wanastaafu miaka 55 mpaka 60, hawa ndiyo wale wakubwa ambao wanaangaliwa. Ukiangalia mfumo mzima, askari walio wengi wako katika ngazi hii ya chini. Kwa hiyo, ipo haja hii Sera ya Jeshi kufanyiwa marekebisho baadhi ya vipengele. (*Makofi*)

Wakati mwingine, ukoloni ni mzuri, ulituachia hii Sera na Sheria, lakini wakati mwingine tuiangalie lazima iende na wakati tulio nao hivi sasa. Tumeongeza umaskini katika jamii zetu. Kwa sababu askari wanapostaafu ni watu ambao wanategemewa na jamii. Sasa tukiwaacha pekupeku hivi hivi, tunahakikisha kuwa wanakuwa majambazi badala yake tunawashutumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu uchunguzi wa kesi zetu. Kesi zetu zinachukua mrefu sana za ndani na za nje, ukiangalia wakati mwingine kesi zinakwenda kwa mashinikizo. Ukiangalia kesi mbili hizi; kwa mfano, meli ya uvuvi iliyokamatwa na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, mpaka wale Wafilipino walipogoma kula ndiyo kesi hii inashughuliwa. *IGP* ndiyo katoa tamko kuwa kesi hii itashughulikiwa na walipogoma kula ndiyo Waziri kasema kuwa, tutapata hela ya kuwarudisha kwao. Tunafanya kazi kwa mashinikizo, japokuwa nitajibowi kuwa sisi hatufanyi kazi kwa mashinikizo, lakini ukweli ndiyo huo au habari ndiyo hiyo. Tunafanya kazi kwa mashinikizo, yaani mpaka hali iwe imeshadhihirika ndiyo Serikali inachukua hatua. Suala hili zi suri. Ili tufanye kazi, tuhakikishe kuwa hakuna shinikizo, tunafanya kazi zetu kama kawaida. Kwa hili nashauri kuwa, tufanye kazi kama *system* inavyoruhusu na siyo kwa mashinikizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho kinanihuzunisha sana ni kufariki kwa askari. Askari anapofariki tunasoma risala nzuri, hotuba nzuri, ngonjera, huzuni, vilio na mambo mengine. Lakini akianza kudai mirathi ya wafiwa hapo kazi ipo, hapo kazi ndiyo inapoanza kudai mafao ya hao warithi ndipo shughuli inapoanza. Mimi ninao askari, baadhi yao wamenilalamikia sana na lazima nikufuate Mheshimiwa Waziri ofisini kwako. Kwa sababu ukiwapa hawa, anao Serjeant John, anao Serjeant Peter, yaani maelezo mengi kuliko vitendo vya wale waathirika wanaokabiliwa na hili tatizo. Kwa hiyo, ipo haja hili suala liangaliwe, tusiwe na huzuni, tuna huruma sana wakati wa mazishi, lakini hatuna huruma kuwaangalia warithi. Hili suala kwa kweli linaudhi na lazima tulifanyie kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Kwa sababu wale warithi wanategemea sana kwamba, watakachokipata kutokana na wale marehemu ndiyo kitakachowasaidia katika maisha yao.

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Wahasibu raia. Katika jeshi la polisi utashangaa kuwaweka wahasibu raia. Kwa kweli wananyanyasa hata raia, maana yake majibu yao hayaendi sambamba na wale askari. Kwa hiyo, kama wapo Wahasibu raia katika jeshi letu la polisi kwa nini tusiwaelimishe polisi wenyewe wakawa Wahasibu kuliko kuwafanya raia ni wahasibu ambao ukimpa amri anatoa maneno ambayo si mazuri kwa askari wetu? Kwa sababu yeye siyo askari, lakini majibu yake yanakuwa si mazuri katika kuhakikisha kuwa anatoa huduma kwa wale askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la mapunjo kwa askari wetu. Askari kama alivyosema Mheshimiwa Sanya, Wazanzibari wametoka kama 300, lakini walicholipwa nasema kuwa baadhi yao wamelipwa, baadhi yao hawajalipwa. Walicholipwa hakitoshi au hakiendi na ile kazi walioifanya au na taratibu zao na kanuni zao. Kwa hiyo, wamepunjwa sana.

Nasema askari kutoka katika sehemu ambayo ina Manispaa, yaani Mkoa ambao una Manispaa, wanapaswa kupewa shilingi 45,000, lakini wanapewa shilingi 25,000. Wengine ambao hawana Manispaa wanapaswa kupewa shilingi 30,000, lakini wanapewa shilingi 15,000. Kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia hili suala kuhakikisha kwamba, hayo mapunjo ambayo wanapunjwa askari wetu wanapatiwa hiyo haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu cheo cha Koplo. Unapopata cheo cha Koplo, wenyewe wanadai kuwa wanakwenda kusoma cheo cha Koplo, lakini cheo hicho unapokisoma ni *right* au ni vizuri kukisoma. Sasa wanashangaa kuwa, unapopata *Serjeant* vile vile unakwenda kusoma tena masomo yale yale ambayo ultoka Koplo unaingia *Serjeant*. Kwa hiyo, huku ni kupoteza hela ya Serikali tu. Ipo haja gani, kwani si kumpandisha tu, mbona maafisa wakitoka jiwe moja unaenda jiwe lingine unaenda tu bila ya kwenda kozi; kwa nini wao waende kozi? Kwa hiyo, wanashauri hii kozi ifutwe au kama ina maana zaidi kwa nini yawe masomo yale yale tu ambayo hayana tija yoyote? Halafu unadai kuwa wakati mwingine unakwenda kozi ya mafunzo fulani, lakini ukirudi hupewi ile kazi ambayo ulienda kusomea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liningine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, maafisa wamekutana na *IGP* mwenyewe Morogoro, wakatoa Maazimio mengi, likiwemo hili la madai kwa askari wetu. Maaskari wetu wanadai mambo mengi sana ambayo hawajalipwa, ambayo yakilipwa huenda yakawanufaisha askari wetu. Hili ni Azimio rasmi, wamelitoa wenyewe maafisa wa kijeshi lifanyiwe kazi. Mimi nashauri hasa kwa haya madai yanapotolewa, yaanze kwa askari wa chini yasianze kwa askari wa juu tena. Kwa sababu ukianza kwa askari wa juu, wale wale siku zote ndiyo wanaoneemeka kuliko wale wa chini ambao bado wanadai. Kwa hiyo, tukilipa haya madai ya askari, basi tuanze na wale askari wa chini, twende askari wa juu ambao tutahakikisha kuwa wanafanikiwa na wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka kuzungumzia ni kuhusu uhamisho wa askari. Askari wanakaa muda mrefu kituo kimoja bila kuhamishwa, yaani mtu anakaa kituo hicho anaoa, mwisho anaitwa babu au anaitwa mzee fulani kwa sababu hajahamishwa. Kwa hiyo, ipo haja ya askari wetu kufanyiwa uhamisho na ukimfanyia uhamisho umpe na stahili zake zote ili ahakikishe kule anakokwenda asiende kusumbuka.

Naingia katika Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja; Mheshimiwa Naibu Waziri alipotembea sehemu zote aliupenda sana Mkoa wetu, kwa sababu ni mkoa mzuri, ambao una sehemu za kitalii, alifurahi sana, ali-*enjoy* katika sehemu zile. Mapendekezo tuliyompa nafikiri afanyie kazi. *RPC* wetu hana Ofisi wala hana jengo, rafiki yangu anahama kuliko mtoto wa paka; leo Wilaya hii kesho Wilaya nyingine. Kwa hiyo, ipo haja ya kufanyiwa marekebisho, kuhakikisha anaishi mahali pamoja ambapo fanafaa kufanya kazi ili kuhakikisha kuwa anaweza kufanya kazi vizuri. Ofisi aliyonayo hivi sasa haikidhi haja kuwa ni Ofisi ya Mkoa. Kwa hiyo, ipo haja ya kuhakikisha kuwa inajengwa Ofisi ya Mkoa, ambayo inakwenda sambamba na wakati huu. Upungufu mwengine ni kwamba, askari hawana nyumba za kuishi, wanaishi uraiani. Ipo haja tulitatu hili halafu mafuta ambayo wanapewa kwa ajili ya magari, lita 200 kwa mwezi, hayakidhi haja iliyopo na magari ni mabovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine askari anaambiwa anakula rushwa. Lazima afanye hivyo, kwa sababu gari bovu na halitengewi hela. Anakamatwa dereva wa gari lile faili lake linafikishwa, ndiyo anatoa hela ya ziada, inatengenezewa gari la *OCD*. Kwa hiyo, ipo haja ya kuangalia kwa sababu hana kifungu maalum cha kuhakikisha kuwa anafanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la uhamiaji. Uhamiaji tulionao hivi sasa walivyoniambia, Jeshi la Uhamiaji wanajiuliza; kwani wao ni askari au ni jeshi la wokovu? Hawajajua mpaka leo kuwa wao ni askari, kwa sababu wanakwenda kwenye kozi za askari, lakini zile hatua za mfumo mzima wa uaskari wao unakuwa ni tofauti. Kwa hiyo, wanajiuliza kwamba je, wao ni askari au ni jeshi tu ambalo lipo pale la wokovu na kwamba Jeshi la Uhamiaji ni jeshi rasmi au ni jeshi tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa upande wa Uhamiaji, kuna baadhi ya mambo yanayotendeka wanasema si sahihi wala si mazuri, kutokana na Balozi zetu zilizopo nje. Balozi zetu zinatoa visa kwa wagani ambao wanakuja nchini, yaani taratibu zote za uhamiaji wanakuwa hawazifuati. Kwa hiyo, wakija huku nchini wanakuwa na utaratibu mpya, inaonesha wale Maafisa wetu wa Balozi zilizoko kule za Uhamiaji, zinakuwa hazina mafunzo ya uhamiaji kwa kuhakikisha wakiwa nchini hawasumbuki tena kuhusu yale masuala mazima ya Uhamiaji.

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Vituo vya Uhamiaji; ukiangalia sana mipakani na bandarini ni makontena, siyo ofisi utafikiri wanauza vipodozi. Utaona pale dirishani utafikiri mtu anauza vipodozi, kumbe ni Ofisi ya Uhamiaji. Kwa hiyo, mipakani, bandarini mote ipo haja ya Ofisi zetu za Uhamiaji kuzifanyia ukarabati au kuzitengeneza ziwe nzuri. Tulikwenda Horohoro, ofisi moja iliyopo pale mpaka uchungulie ndiyo umwone Afisa Uhamiaji; nasikitisha sana. Ukienda sehemu nyingine ya mpaka ule ule, wenzetu Kenya wana Ofisi nzuri. Kwa hivyo, inasikitisha wenzetu wanafanya kazi katika mazingira kama yale. Ipo haja hapo Zanzibar Bandarini ukienda kwenye Ofisi zake au ukienda hapo Dar es Salaam vile vile Ofisi za Uhamiaji ni kama sehemu tu alizowekwa yule Afisa Uhamiaji, wewe fanya kazi hapa kuna mwenyewe ili akija mgeni umpokee, hakikisha usalama. Kwa hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba, Ofisi zetu za Uhamiaji zinakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyoyazungumza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofifi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuchangia. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa ili na mimi nichangie katika Wizara hii. Wenzangu wameshasema mambo ambayo takriban yatajirudia rudia, lakini kwa sababu ndiyo ajenda yenye we itabidi lazima tuifanyie kazi.

**NAIBU SPIKA:** Ukirudia tu tutakupiga Kanuni.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Ukirudia tu tutakupiga Kanuni.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Ahsante na mimi nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wenzao, siyo kwa hotuba nzuri, lakini kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Taifa letu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niende katika suala zima la askari polisi. Tumekuwa tukizungumza vitu hapa, ambavyo inaonekana ama vinaachwa hapa hapa ndani au nashindwa kuelewa. Askari wanalamikia malimbikizo yao walipeni.

Wanalalamikia malimbikizo yao ya posho na mafao yao mbalimbali, walipeni ili hili jambo liishe. Kateni mambo mengine yoyote muwalipe, kwa sababu hawa ndiyo watu tunaowatuma, ndiyo watu wanaopoteza wakati wao na mara nyingine wanapoteza maisha yao. (*Makofi*)

Imesemwa na wachangiaji wanne waliotangulia; kuhusu uhamisho ningependa niseme hivi, najua kuna tatizo la fedha kuhusu uhamisho, toeni Waraka au toeni fomu kwa askari wote. Anayetaka kuhamishwa bila ya kudai pesa za uhamisho ajaze fomu ili mumhamishe. Kwa nini unamwacha askari anakaa kituo kimoja miaka 20? Mimi nawaauliza wale askari wakubwa wanaohusika na *administration* walipokuwa wadogo kweli kuna mtu amekaa kituo kimoja miaka 20 au 26? Haiwezekani, wahamisheni na kama tatizo ni fedha wapeni fomu, watakaoji-*commit* kuwa hawatadai mafao, wahamisheni mara moja. Kwa nini mnakaribisha malalamiko ambayo mnaweza mkayakabili? (*Makofi*)

Tatu, nije kwenye suala zima la vyeo. Bwana Shaban Robert alisema: “Kuwa na cheo ambacho hakioneshi tofauti ya ustahili huwa si cheo hicho.” Sasa askari wanalamika kuwa wengine wanapata vyeo, wanavivaa ndani ya nguo zao na mabega yao, lakini pesa hawazioni na inawachukua siku nyingi. Sasa cheo ambacho hukioni manufaa yake, mimi naita si cheo. Labda itakuwa kama ni haina maana, wapeni pesa zao kama mmewapandisha vyeo. Tena muwape mapema ili waweze kufanya kazi, wakiamini wanafanya kazi vyeo walivyopata. (*Makofi*)

Lingine kuhusu askari polisi, wanalamikia kuhusu makato. Kuna utaratibu wa kuwakata askari wadogo wadogo fedha, kwa kisingizio kuwa zinapelekwa kwenye Mifuko hii ya PSPF, PPF, lakini mwisho wa siku wanapostaafu hizi pesa hawazipati. Sasa sjui hizi pesa ama hazifikasi au hazisimamiwi vizuri? Ningekuomba Mheshimiwa Waziri na Timu yako, msimamie hizi pesa zinazokatwa zifike kunakotakiwa ili wanapostaafu wazipate. Kama hazifikasi basi msiwakate. Kwa nini unamkata mtu pesa yake anashindwa kutumia halafu hazipati?

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika kitu kikubwa sana katika Jeshi la Polisi tunalisifu sana ni nidhamu na ni kweli wana nidhamu. Mimi nitamke hapa kuwa, Askari Polisi hasa pale Makao Makuu, pana heshima na nidhamu ya hali juu sana. Ukienda kwa *IGP* na Wasaidizi wake wote wanakupokea, wanakusaidia na unaweza kuona shida yako imetekelezwa ndani ya dakika chache sana. Huku chini kuna askari wachache, wanavunja sifa nzuri na heshima nzuri ya Jeshi la Polisi. Hivi karibuni pale Zanzibar kuna Mheshimiwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, amekamatwa na askari wa Kituo cha Malindi, gari lake walimwambia kuwa halina bima. Bima anayo hajaibandika, kaitoa bima hii ninayo ni kweli sijafanikiwa kuibandika hii hapa. Askari kachukua maamuzi ya kumwita ndani, amethubutu kumpiga ngumi na mateke *Member* wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa unapompiga Mwakilishi mimi najiuliza; kapigwa yule kwa sababu anatoka Jimbo la Tumbe; hivi kweli angetoka Donge, angetoka Makunduchi au angetoka Amani angepigwa? Watu kama hawa wanaoharibu nidhamu nzuri ya Jeshi la Polisi ni vizuri

Mheshimiwa Waziri mka-deal nao hawa watu, kwa sababu wanaharibu sifa nzuri ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Tumeshapeleka maelezo kwa urefu sana kwa *Inspector General*, juu ya kijana huyu; maelezo yake, jina lake, siku aliyofanya tukio na kila kitu. Nategemea hatua zinazofaa zitachukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha, kumekuwa na malalamiko, mimi mwenyewe binafsi nimeshalisema muda mrefu hapa. Pesa za malipo ya askari wa Mikoa kama mnavyofanya katika *Vote* za Mikoa hapa Bara, fanyeni na kule Zanzibar kila Mko a upelekeeni *Vote* yake. Kwa nini unachanganya pesa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar? Matokeo yake wakubwa wakishakuwa pamoja mara nyingi wana kazi nyingi, wanawenza waka-*reallocate*, matokeo yake wale wanaokusudiwa katika Mikoa, haziwafikii na wanalamikia vitu hivi, vifanyieni kazi kama kuna namna ya kupeleka *Vote* kwenye Mikoa pelekeni.

Sasa nije kwenye *component* ya Usalama wa Raia. *Component* ya Usalama wa Raia ni *component* ya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini pia ni *component* ya Katiba ya Muungano. Sasa hivi kule Pemba, kunaendelea zoezi linaloitwa la Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura. Mimi sijui ni zoezi la uboreshaji au ufujaji wa daftari na ninasema sielewi kuwa ni uboreshaji au ufujaji kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, ukienda pale kituoni pana mazingira ya kutisha sana. Mimi ninavyojuu, Askari Polisi ndio wenye jukumu la kulinda usalama katika maeneo yoyote ambapo raia wapo. Wana jukumu la Kikatiba la kulinda usalama wa raia na mali zao. Ukienda kwenye vituo vya uandikishaji katika Jimbo lile la Konde, utakuta vikosi mbalimbali vyenye silaha vimezunguka vituo vile. Je, kuna hali ya hatari hapa ndani ya nchi na kama ipo kwa nini haitangazwi? Kwa nini tunawatisha wananchi katika vitu vya kawaida? Watu wetu mpaka leo wana tabia ya kuogopa askari, tutake tusitake. Hii inafanywa kwa makusudi, si bahati mbaya. Mimi nimeangalia katika uchaguzi uliopita wa Magogoni, mwezi mzima kabla ya kupigwa kura ile kulikuwa na kwata ya vikosi vyote wakiwemo Polisi. Mbona lile kwata sasa hivi halifanywi? Kwa nini tunawatisha watu bure tu kwa jambo la kidemokrasia? Hivi kweli huu ndio Utawala Bora, huu ndio Utawala wa Sheria au ndio Demokrasia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Konde ili uandikishwe kwa mujibu wa sheria ambayo mimi naiita ni sheria kandamizi sana, ni kuwa uwe na kitu kinachoitwa kitambulisho cha Uzanzibari. Vyombo vyote vinavyowajibika kutoa vitambulisho vya Uzanzibari, vimekuwa *sealed* kwa makusudi. Ukienda kwa Sheha, hupati hiyo barua ya kukufanya wewe uende kwa Mkuu wa Wilaya ukapate fomu. Ili ulalamike ni lazima upewe fomu na Mkuu wa Vitambulisho wa Wilaya au Mratibu ili uende kwa Mkurugenzi Unguja. Eti watu elfu tatu mpaka elfu kumi watoke Pemba kwa meli waende Unguja wakapeleke barua mmoja mmoja kwa Mkurugenzi wa Vitambulisho, lakini hiyo fomu huipati. Nina fomu hapa ya vijana waliofikia umri zaidi ya 900 karibu ya 1000, walioandikishwa Konde mpaka juzi Siku ya Jumatatu, ambayo ndio ilikuwa siku ya mwisho ni 130. Hii ni demokrasia gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unawazuia watu haki kwa makusudi, tunawa-*provoke* watu kusudi! Mimi ninajiuliza hii *provocation* ya namna hii ina malengo gani? Mimi bado nakumbuka yaliyotokea mwaka 2001; napenda niulize, tunawa-*provoke* hivi ili tufikie huko? Kwa nini tunakuwa hivi jamani? Hii ni nchi yetu sote.

Chinua Achebe anasema na ninapenda nimnukuu: “*An anger against brother is felt in the flesh and not in the bone.*” Tatizo la mwenzako ulione na ulisaidie tu. Nachukua fursa hii, kumwomba Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, ambayo inamuheshimu sana na anaheshimika sana nje na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati ni huu, wakati ni sasa, kulishughulikia suala hili. Hili suala ni kandamizi, ni zito, ni bayaa na linaweza likaifikisha nchi yetu mahali pabaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo nchi zinazoharibika ni kwa mambo madogo kama haya tu. Watu wanafika mahali wanasema basi liwalo na liwe, utawauwa lakini wameshaonesha na wao kuwa wana hasira. Kwa nini tunawafikisha watu huko? Hivi kweli tunataka tushinde chaguzi katika mambo kama haya mwaka 2010? Tunaringia mamlaka, mamlaka ni kitu kinachoondoka kama ambavyo tutaondoka sisi wenyewe. Mimi nimesikitishwa sana na vitendo hivi vinavyofanyika na tumeshatoa taarifa, hakuna kinachoendelea. Ninashtuka zaidi ninapomwona Jaji wa Mahakama ya Rufaa, ambaye kwa mujibu wa Katiba, anawajibika kutafsiri sheria; anaruhusu watu wanakoseshwa haki ya kupiga kura akiwa ni *Chairman* wa Tume ya Uchaguzi, hapa napata tabu. Hili siyo la leo, watu wanakoseshwa kuandikishwa kuanzia 2000, 2005 na hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu Daftari linaloandikishwa ndilo linalotumiwa katika Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano. Kama hivyo sivyo, hebu tuone basi kuanzia kesho, Tume ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano, ipeleke Daftari lake iandikishe kuanzia kesho. Kwa nini unawatumia mawakala wanakuandikia wapiga kura, wanawanyima watu haki ya kupiga kura *at the end of the day* wewe ndio unabeba lawama ile? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba niulize, anayezuwia ni Polisi au ni nani maana kama sio Polisi usiwahusishe hapa?

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirudie na nilisema kuwa, *component* ya usalama wa raia na mali zao ni *component* ya Jamhuri ya Muungano, kwa sababu kwa mujibu wa Katiba, haki ya kupiga kura, haki ya kuchagua na kuchaguliwa ni haki ambayo iko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Kinachofanyika kule kwetu ni kuwa, ili uweze kuandikishwa kuwa mpiga kura ni lazima upeleke kitambulisho cha Uzanzibari. Kitambulisho cha Uzanzibari, kimekuwa *sealed* hupati, ukienda kwa Sheha hatoi, ukienda kwa Mkuu wa Wilaya hatoi na ukienda kwa huyo mtu wa vitambulisho hatoi. Sasa wewe unasema watu wasafiri kwa meli, tiketi umezifungia ndani, mwisho wa siku kitakachotokea ni nini si utaondoka na meli tupu, ndio kinachofanyika. Tume inasema inarekebisha daftari, inawaandika wapiga kura,

watu hawaandikishwi, wanakwenda wanasumbuka, wanalia, wanateseka na sisi tunanyamaza kimya tu mpaka lini? Nakushukuru. (*Makofii*)

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi fupi hii ili na niweze kuchangia machache niliyonayo. Niipongeze tu Wizara hii ya Mambo ya Ndani, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, pamoa na timu yake yote kwa ujumla, kwa kazi nzuri tu wanayoifanya. Kwa kweli wana kazi ngumu, lakini kiasi fulani wanajitahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaanza matatizo yaliyoko katika Wilaya yangu. Nina masikitiko makubwa sana, kwa sababu wilaya yangu...

**NAIBU SPIKA:** Wilaya yako inaitwa nini sisi hatujui? (*Kicheko*)

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia Wilaya yangu ya Maswa, Mkoa wa Shinyanga. Nazungumzia tatizo lililopo ambalo ni kubwa. Wilaya ya Maswa, imekumbwa na wimbi kubwa sana la ujambazi. Ninapozungumza mahali hapa; wiki jana tu, wameuwawa watu wanne kwa kuchomwa moto.

Nataka niseme kwa nini limetokea jambo hili mpaka kufikia mahali pale. Wilaya ya Maswa, kutoka tarehe 01 Juni, kumekuwa na tatizo kubwa sana la uvamizi. Sina hakika kama Ofisi ya Waziri inafahamu jambo hili, kwa sababu limeathiri sehemu kubwa sana; kila siku wanaweza wakavunja maduka zaidi ya matatu au manne. Naongea maneno haya nikiwa na hata wakitaka kufanya mawasiliano, watapata habari hizi ambazo mimi ninaamini kabisa zingekuwa zimeshawafikia mezani kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi ninapoongea, wananchi na wafanyabiashara wa Maswa na hasa wajasiriamali wale wadogo, inafikia mahali wanapokuwa wamefunga biashara zao, inabidi wafunge na wabebe vitu ambavyo wanaona ni muhimu, ambavyo vina thamani kwao waende navyo nyumbani halafu kesho yake asubuhi warudishe. Jambo ambalo mimi sijawahi kuliona hata siku moja. Sasa nashindwa kuelewa, kwa sababu kuanzia mwezi wa sita mpaka sasa hivi ninavyoongea mwezi wa saba, tatizo bado liko palepale. Baada ya wananchi kuona kwamba, Jeshi la Polisi au wote wanaohusika kufutilia jambo hili wamekuwa kimya au ufuutiliaji wao hauleti manufaa na matunda hayaonekanai, ndio maana imepelekea sasa hivi wanapokuwa wamembabatiza mtu, wanamchoma moto na kusema kwamba, tumeamua kufanya hivi kwa sababu tunaona Serikali haichukui hatua yoyote.

Ninapata wasiwasi, inawezekana kuna mtu mwengine anaweza akachomwa moto lakini si jambazi, labda wamemuhi tu. Kwa hiyo, unaweza ukakuta kuna mtu mwengine anaweza akachomwa moto akauwawa ni jambazi, mwengine amesingiziwa, mwengine ni fitina na mwengine ni mambo mengine kama unavyojua. Kwa hiyo, ninadhani kwamba, hatua iliyofikia katika Wilaya ya Maswa ni mbaya kupita maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo niliposimama hapa ninachangia, Wazee wa Wilaya ya Maswa, wamekaa kikao kikubwa sana na Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kujadili jambo hili, wanafanyaje ili kuweza kuirudisha Wilaya ya Maswa katika hali ya amani. Niseme pia kwamba, Mwenyekiti wa Usalama, anayefuutilia pale Wilayani, ambaye ndio Mkuu wa Wilaya, anajitahidi kwa kiasi kikubwa sana. Ninachotaka kusema, naona kama ushirikiano wake unakuwa mdogo sana; Mkuu wa Wilaya kama Mkuu wa Wilaya, hawezi kuchukua hatua kufuutilia jambo hili mguu kwa mguu, wapo watu wanaohusika kufuutilia jambo hili mguu kwa mguu. Kwa hiyo, yeye anachokifanya ni kukaa na wale watu na kutoa maelekezo na kutafuta ushirikiano wa pamoja ili waweze kuona ni jinsi gani wanaisaidia Wilaya ya Maswa, iweze kurudi katika hali ya amani. Sasa inaonekana hakuna jambo linaloendelea.

Hivi ninavyoongea sijui, inawezekana hata jana wamebomoa, maana yake majuzi walibomoa, nilipata taarifa. Kila kinapotokea kitu tunafahamishana, kwa sababu na mimi ni Mkazi wa Maswa, nimetumwa kuwakilisha Wananchi wa Maswa, lakini pia ni Mwakilishi wa Mkoa mzima wa Shinyanga; kwa hiyo, chochote kinachotokea katika Mkoa wa Shinyanga, ninawajibika kukizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, nitakapomala kuzungumzia jambo hili, walichukulie hatua na wajaribu kufuutilia. Wilaya ya Maswa imevurugika, wananchi hawana amani, kila kunapokucha wanajadili majambazi, kukicha asubuhi wanauliza ni kwa nani kumebomolewa; ni nani kauwawa. Vijana wawili wafanyabiashara wazuri, mwezi Juni, walikatwa mapanga wakauwawa. Kwa hiyo, ninapozungumza ina maana watu sita walipoteza maisha katika Wilaya ya Maswa, mwezi Juni tu; ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hiyo, ninaomba nitakapokuwa ninazungumzia jambo hili, litiliwe maanani na lichukuliwe hatua. Ninaamini hata Wananchi wa Maswa wanasiliza, kwa sababu simu zimekuwa nyingi sana; wanalamika sana. Kwa hiyo, ninadhani mkishachukua hatua na wao watajua naam, Serikali imeshasikia na inatuthamini kwamba na sisi ni jamii mojawapo katika nchi yetu ya Tanzania. Ninadhani ujumbe umefika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninataka nirudi kwa Maaskari. Mimi ninadhani pamoja na kwamba, wenzangu wameongea, jambo wanadolizingumzia linagusa kila mahali. Ninadhani kwamba, ipo haja ya maaskari kuhamishwa kwa wakati unaofaa. Askari asikae mahali mpaka na yeye anaanza kuomba jamani sasa nataka kuhama. Ukiona mtu anaomba kuhama, ujue kwamba ameshaharibu. Anapoomba kuhama, Wizara inahusika vipi kumsaidia mtu huyu aweze kubadilisha kituo na kuweza kufanya kazi maeneo mengine? Mimi nilikuwa ninafikiri ipo haja ya maaskari kubadilishiwa vituo, waende wakafanye sehemu nyingine. Askari kuzowea mahali kwanza na yeye anaweza akachangia katika masuala hayo au la, wakati mwingine anaweza akachoka akaona ni jambo la kawaida; wananchi ameshawazowe, haogopi mtu yeyote. Ninadhani ipo haja ya kuwabadilisha maaskari. Kama watumishi wengine wanavyofanyiwa, basi na wao watendewe haki zao, kwa sababu nao ni watumishi ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninataka niongelee askari anapohamishwa kutoka kituo kimoja kwenda kingine, kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine au Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine. Ninadhani kwamba, na yeze atendewe haki kama watumishi wengine. Ahame apewe haki zake, msitangulie kumhamisha mkampakia kwenye fuso na vitu vyake na watoto wake, mkamwambia tangulia tutakulipa haki zako. Anatakiwa na yeze apate malipo yake pale pale. Hili limekuwa ni tatizo, askari hathaminiwi, haonekani kama ana umuhimu.

Ninataka niwaambie kwamba, askari wakitugeuka hata hapa ndani hakutakalika. Kwa hiyo, ipo haja ya kuona kwamba, askari nao ni wa muhimu, tena ni wa muhimu sana katika nchi yetu; anapohamishwa apewe haki yake. Ametoka kituo kwenda kituo, apewe haki yake; Mkoa hadi Mkoa, apewe haki yake, lakini asikopwe; wewe nenda bwana tutakulipa baadaye. Kwa nini afanyiwe hivyo? Mkubwa akihama siku hiyo hiyo anapewa haki zake zote, lakini huyu mdogo anaonekana hana maana wakati yeze ndio anafanya kazi usiku kucha, mchana kutwa. Mimi nadhani na wao tuwathamini kama binadamu wengine na wathaminiwe kama mkubwa anavyothaminiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema kwamba, askari wakati mwingine anawajibika kwenda kufanya kazi eneo lingine, maana yake askari ni mtu tu wa kuamrishwa wakati mwingine kwa sababu ndio mkataba wa kazi yake. Labda anaambiwa sasa ondoka mahali hapa kafanye kazi Chamwino kwa muda kadhaa. Anapoondoka mahali hapa, kwanza, hapewi fedha ya usafiri, kitu kingine ana haki zake za kulipwa kila siku; unapomtoa kituo hicho kwenda kufanya kazi kituo kingine kwa muda na kwa sababu kuna umuhimu wa kufanya kazi ile basi na yeze apewe nauzi, apewe posho zake na apate matumizi mengine anayotakiwa kuyapata katika eneo lile. Nilikuwa ninaomba jambo hili lifuatiliwe; ni jambo la kweli na ndivyo mnavyofanya. Naomba yafanyike mabadiliko ili angalau na wao waweze kujisikia vizuri. (*Mkaofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie suala la kufanya kazi muda mrefu. Askari anaweza akawajibika wakati mwingine kufanya kazi saa 24, labda anaweza akawajibika kufanya kazi muda ambaio sio wa kazi, anaitwa kwamba kuna jambo fulani limejitokeza njoo ufanye kazi. Ninachotaka kusema, kuna watumishi wengine wanapokuwa wanafanya kazi tofauti na muda wao wa kazi wanalipwa *overtime*, wanapewa pesa ya kufanya kazi tofauti na muda wa kazi. Hivi hili jambo ni kwa nini lisifanyike na kwa hawa maaskari wetu? Kwa nini nao wanapokuwa wanafanya kazi nje ya muda wa kazi wasilipwe *overtime* ya kufanya kazi kwa muda ambaio sio wa kazi? Maeneo mengine tunaona na Wizara nyingine tunaona wanalipwa tu. Wanasema hii *overtime*, wanasema sijui ni nini; ni kweli kwa sababu kafanya kazi muda usio wa kazi. Basi na hawa wanapokwenda kufanya kazi, ukimwita njoo kuna tukio limetokea sehemu fulani, anapokuwa anakwenda kule kufanya kazi, basi apewe haki yake kwa sababu amefanya kazi nje ya muda wake wa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yangu ninayotoka ya Maswa, kuna gari la Polisi ambalo lilikuwa limechoka sana, *STJ 887 L/110*, lililochukuliwa na Mfanyabiashara mmoja maarufu sana, lakini sitamtaja. Wizara ikitaka kufuatilia itamfahamu. Amechukua lile gari akiwa na maana kwamba, anakwenda kulitengeneza

liwe zuri hatimaye lirudi kufanya kazi Polisi. Lile gari toka limechukuliwa mpaka leo ninapoongea ni miaka mitano, sasa yule ametaifisha au amefanya nini? Kama ameshindwa kutengeneza arudishe lile gari. Kwanza, hatuwezi kukubali arudishe bila kulitengeneza, ikiwezekana anunue jipy, hawezi kukaa na gari la Polisi kwa muda wa miaka mitano akidai anakwenda kulitengeneza. Kwa hiyo, ninalolizungumza hili, Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, nilikuwa ninaomba baada ya hapa waulizwe wale watu, mfanyabiashara yule lile gari analifanya nini? Gari la Polisi linatakiwa lifanye kazi, alilichukua kwa staili ya kulitengeneza, lakini mpaka leo analo miaka mitano, sasa ni lake tena lile gari! Nilikuwa ninafikiri lile gari afikie mahali alirudishe na likija lije *order*, ikiwezekana anunue jipy, atajua mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia kuhusu matumizi yanayotolewa ndani ya Vituo vyetu vya Polisi, kwanza magari hakuna. Wilayani kwangu gari lililopo limechoka kweli kweli, likitokea tukio ukiwa karibu karibu gari lako unanyang'anywa. Mkurugenzi ataambiwa lete gari haraka, Mkuu wa Wilaya kama naye yupo karibu ataambiwa lete gari, kwa kweli gari hakuna, lililopo limechoka, hali ni ngumu. Pamoja na kuchoka kwa magari, lita 100 zinaletwa Wilayani eti zifanye kazi kwa muda wa mwezi mzima, jamani aibu! Gari haliwezi likafanya kazi kwa muda wa mwezi mzima kwa mafuta lita 100. Mimi nilikuwa ninafikiri, kwanza, jambo hili tunapolizungumza ni aibu, lita 100; haiwezekani. Wizara ibadilishe, hizi lita 100 hazifai ni aibu kuzitamka mdomoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bukombe, Mkoa wa Shinyanga, haina gari la Polisi. Gari la Polisi hakuna, kazi sio nzuri, halafu kama unavyojua, Bukombe uvamizi, majambazi, vurugu, patashika ziko kule kama mnavyosikia. Mimi nilikuwa ninafikiri kwamba, ipo haja Bukombe, wajaribu kuangaliwa kwa macho ya huruma jamani, wapewe lile gari na wao waweze kufanya kazi vizuri, ikitokea tatizo wafike haraka wanapotakiwa kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maswa tuna matengenezo ya Kituo cha Polisi. Tumetengeneza msingi, tumefyatua matofali, toka mwaka 2004, huo ni mchango wa wananchi. Kwanza, mimi ninasema wamejitalidi, wananchi ukiwaambia kuchangia Jengo la Kituo cha Polisi, wanasesma tunajenga kusudi watuweke ndani tujae kwa hiyo ni bora liwe kadogo ili wakose pa kutuweka. Kwa hiyo, ninawapongeza kwa sababu wamejitalidi kwa kazi waliyoifanya. Ninachotaka kusema, Wizara inasaidia nini hapa tulipofikia? Tunaomba tupate majibu kwamba, angalau mnatuchangia basi mabati na madirisha ndio ya gharama kubwa, mengine nadhani hata sisi tutajisaidia. Naomba mlichukue hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuzungumzia habari za Magereza. Magereza Wilaya ya Maswa, wamemaliza miti; ni jangwa sasa. Miti inakatwa kila siku, nikamuuliza Mkuu wa Gereza, vipi mbona unakwapua miti tu? Akaniambia pesa ninayoletewa haitoshi na ninakopaswa kwenda kuchukua miti ni mbali, wazabuni wanakataa, pesa hailipwi; sasa nitafanyaje? Wafungwa hawawezi kulala na njaa, wakifa nitaulizwa. Kwa hiyo, mama inabidi tu twende hivyo hivyo. Ninachotaka kusema, basi ongezeni pesa, kuna pori zuri kweli kule, tatizo pesa tu ni kidogo. Tuongezeeni kidogo ili

wazabuni wakafuate kuni kule maporini. Ninaomba hilo mlitchukue. Muda hautoshi hivyo hivyo tunakwenda haraka haraka. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuzungumzia vitendea kazi. Magereza wanapewa pesa ya kununua karatasi, sijui ream 2,000; hizo karatasi ziweze kufanya kazi mwezi mzima! Jamani, ninaomba muwasaidie askari magereza na ndio maana ukiwaangalia wanachoka mno, saa nyingine wanatoa vihela vyao kufanya kazi. Mimi nilikwa ninafikiria kwamba, hii pesa iongezeke, haitoshi kununua vifaa vyao kufanya kazi; wanaandika, wanafanya nini. Kwa hiyo, ninaomba muwasaidie angalau wawewe kupata mahitaji ya kufanya kazi. Wafungwa wana matatizo ya unifomu. Kwanza, wapo wale ambaو wamekwenda bila matatizo, lakini pamoja na hayo, wana haki yao ya msingi kuvaا vizuri wafunike miili yao, siyo kwamba mfungwa sasa anakuwa yuko gerezani huku kiraka, huku kwingine kunaonekana kumekaaje, inakuwa haipendezi. Mimi nilikuwa ninafikiria kwamba, kwa suala la unifomu jaribuni kuwaangalia. Sare mliyowachagulia ni nzuri inapendeza, sasa hivi sio kama zamani, wanavaa suruali. Kwa hiyo, jaribuni kuangalia na hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuongelea magari. Wizara ilitoa magari *Canter* mwaka 1999, pesa ya *service* hamna, matengenezo hamna, *vi-canter* vimechoka, yaani hakuna kinachoendelea, basi wanavyo wanahangaika navyo vinayumba yumba. Wakiwekwa mle wafungwa wanaweza hata wakawatoroka, *vi-canter* nya kusukuma sukuma, ninadhani ipo haja ya kubadilisha.

Tutafute usafiri mzuri angalau na haya Mawilaya yaweze kupata magari ya kuridhisha. Ninawapongeza tu kwa sababu sasa hivi kuna mabasi mazuri yanayotoka Segerea, lakini sio Maswa. Nimeambiwa sio Maswa, kuna mtu kaniambia unapongeza wakati sio Maswa! Ninapongeza kwa sababu ni nchi yangu, mmejitätahidi sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi angalau na mimi nichangie kidogo kwenye Wizara hii, ambayo ni muhimu sana kwa usalama na pia kwa uchumi wa nchi yetu. Siku moja nikafikiria, hivi nchi ingekuwa haina Polisi ingekuwaje? Jibu tunalo.

Nitumie nafasi hii kuwapongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, *IGP*, Makamishna Wakuu wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kutufanya tulale angalau, tuamke asubuhi na tufanye kazi ya kujenga Taifa. Nawapa pongezi na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwe tofauti kidogo; jana tulipokuwa tunasikiliza matokeo ya Uchaguzi Biharamulo, wengine tulifuatilia tukakuta ya kwamba, waliokuwa wamejiandikisha kupiga kura walikuwa 80,000, lakini waliokwenda kupiga kura ni chini ya nusu. Mimi nikajuliza; tatizo liko wapi; ni kudharau; ni kuona haya mambo acha yapite tu au ni uwoga fulani? Nilifikia uamuzi wa kudhani kuwa wengi

hawakwenda kupiga kura kwa sababu ya uwoga tu unaotokana na fujo walizokuwa wanaziona wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa, mwaka 1959, aliwahi kutukumbusha, aliandika kitabu kimoja kinaitwa *Barriers to Democracy*. Katika kitabu hicho alisema, adui mkubwa wa Domokrasia yeoyote ni uwoga. Ukiwa mwoga ndio haya yanayojitokeza, watu wanajiandikisha hawaendi kupiga kura, kwa kuogopa kwamba, wakienda watapigwa au watazomewa. Hali hii ikiendelea sijui nchi hii tunaipeleka wapi? Kwa nini tumefikia hatua hiyo?

Nalisema hilo kwa sababu kama kweli unataka kutumia demokrasia yako kwenda kuchagua watu, lazima uwe huru, bila vitisho vyovyyote uende ukapige kura. Leo nusu ya watu hawakwenda kupiga kura, uwoga. Hii tabia tukiilea, hali itakuwa sio nzuri. Mimi nataka niwapongeze askari wetu wa Polisi, kwa jinsi walivyoshiriki kuhakikisha kwamba, upigaji wa kura umekwenda vizuri, umemalizika vizuri. Nawapongeza wenzetu wa upande wa Chama cha Mapinduzi, kwa ushindi mkubwa walioupata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kusema yafuatayo:-

Tabia ambayo imejengeka ya watu kuanza kuchapana, kupigana na wakati mwingine hata kutafutiana nafasi ya kuviziana wakati wa kampeni, sio nzuri. Sisi viongozi ni chanzo cha vurugu zenyewe. Viongozi wa Vyama vya Siasa, lakini pia na sisi Viongozi ambao tuko nje, hatujasaidia wananchi wetu kuwapa elimu ya kutosha kuhusiana na mambo ya kura. Dawa na silaha kubwa ya kujenga demokrasia ni mambo mawili; la kwanza ni kalamu na karatasi.

Acha uwoga, lakini kalamu na karatasi ndio inakupa nafasi ya kwenda kuamua nani unayemtaka. Wenzetu wa upande wa vyombo vya habari, wanaitumia vizuri sana kalamu na karatasi. Unaona wanavyotuendesha puta, kwa kutumia karatasi na kalamu yao. Ukitaka kwenda kuchagua, tumia kalamu na karatasi, nenda kapige kura, unayemtaka ajulikane. Ndio maana nataka nirudie maombi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliwahi kuayasema; Viongozi wa Madehebu ya Dini pia watumie nafasi hii kuwapa elimu waumini wajue ya kwamba, wana haki bila kuogopa. Wasitishike na haya mambo, lakini kalamu na karatasi ndio itakayowasaidia kupata kiongozi anayefaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa naibu Spika, sasa nije katika suala lenyewe; kuna mtaalamu mmoja anaitwa Adam Smith wa zamani sana. Aliwahi kusema haya yafuatayo: Akasema; uchumi hauwezi kuendeshwa bila kuongozwa. Kuna mikono ambayo haionekani. Aliyeandika kitabu hicho, alikuwa na maana yake. Tunachotaka ni kumwambia Mheshimiwa Waziri, atusaidie mambo mawili; pamoja na hotuba nzuri uliyotoa, lakini ninataka nikuombe katika Mkoa wa Rukwa, bado hamjatusaidia sana.

Nalisema hilo kwa sababu kubwa mbili; kwanza; kumekuwa na malalamiko mengi sana ya askari wetu wanaopelekwa Mkoa wa Rukwa, wakipelekwa tunawasahau tunawacha huko. Madai yao yanachukua muda mrefu, sijui ni kwa ajili ya umbali?

Mko radhi kuwashughulikia watu wa karibu ambao ni Dar-es-Salaam, labda Morogoro au Dodoma, watu wanaokaa mbali wanasota muda mrefu sana. Mnampa wasiwasi *RPC* wangu, ambaye anafanya kazi yake vizuri. Ninataka niwahakikishie ni mzuri sana na anafanya kazi yake vizuri na ninampongeza.

Kila siku anajibu mapigo ya askari, namna ya kuwatuliza wakijua ya kwamba, iko siku haki zao watapewa. Naomba sasa katika fedha ulizopewa; la kwanza, angalia askari wako ambao wanakaa mbali, wapo katika mikoa ya pembezoni, uwape kipaumbele ili malalamiko yao uone namna ya kuwasaidia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nakuomba sana, kwa kipindi zaidi ya miaka 20 tumekuwa tukilalamikia mambo makubwa mawili; la kwanza ni mahabusu iliyopo pale Mjini Sumbawanga. Ile mahabusu ni ya tangu mwaka 1952, kabla ya uhuru na ilikuwa kwa ajili ya mahabusu 100 au wakati mwingine hata 120. Sasa ukienda kwa kweli ni aibu, kwanza, ipo katikati ya mji.

Ukiingia mle ndani na mimi kwa sababu ni Mbunge ninaruhusiwa Kikatiba na Kisheria, mara nyingi unapokwenda pale unashangaa jinsi wanavyoishi mle ndani. Mheshimiwa Waziri, ayatembelee Mahabusu haya yanatisha, si mazuri hata kidogo. Nataka aone namna ya kusaidia angalau ijengwe mahabusu nyingine.

Mheshimiwa Waziri, hilo ninaomba sana. Ninamwomba sana aangalie, tumepiga kelele karibu mwaka wa nne, lakini hatujapata majibu.

La pili, ni Gereza letu la Molo, ambalo linazalisha. Mimi ninalipongeza, linafanya kazi nzuri sana, linazalisha chakula cha kutosha. Ninashukuru mwaka jana mmewasaidia baadhi ya vifaa na zana.

Tunataka Gereza hili liwe la mfano; wasaidieni, wapeni vifaa vya kisasa zaidi, tupate *planters*, tupate *harvestors* wameshapata mkataba wa kuingia na *TBL* kuzalisha shahiri. Shahiri inataka uwe na mashamba makubwa, wasaidieni nyezo wafanye kazi yao vizuri na mimi nina imani watafanya kazi yao vizuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzagu wamezungumzia kuhusiana na *uniform* hasa za wafungwa , Gereza la Molo ambalo kwa bahati mbaya tangu lijengwe halijakamilika, zaidi ya miaka 30 mpaka leo, kuta zake bado ni mabati, *shame on us*, na baridi ya Sumbawanga wote mnaifahamu. Jana kama mliangalia hali ya hewa ilikuwa *degree* nne, leo unamwacha mfungwa anakaa katika Gereza la mabati, kweli ni haki za msingi za binadamu? Hana blanketi, yaliyopo nayo yamechanika, vilago anavyolalia ni aibu tupu, Mheshimiwa Waziri, naomba angalia mambo haya. Katika Gereza hilo, ninaomba sana mtume kabisa angalau Kamati ikalifuatilie, inasononesha kuona wanaishi katika mazingira magumu wakati wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wa Molo, wanafanya kazi nzuri sana ya kuzalisha, lakini wakishamaliza inatakiwa tuwape heshima, wale vizuri, walale vizuri, angalau asubuhi wakiamka wana nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtaalam mmoja anaitwa Napolioni, katika Vita Kuu ya Kwanza, alisema nguvu ya Askari iko tumboni, alikuwa na maana ngani? Askari anatakiwa ale vizuri, apate huduma nzuri, afanye kazi yake kwa raha mstarehe. Kwa vile binadamu haishi kwa kula tu, mazingira yale anayoishi, mambo ya posho, mambo ya kuwahashia usafiri, yale yote naomba kabisa myape kipaumbele cha kwanza. Mimi naimani kabisa Mheshimiwa Waziri, utaliangalia suala hilo na utatusaidia katika Mkoa wetu wa Rukwa, Askari wetu wako katika mazingira magumu na tunataka mtusaidie, ili angalau haya ambayo tunayasema yaondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni Ofisi ya *OCD*. Ofisi ya *OCD* pale Sumbawanga, ni ya zamani nadhani ilikuwa ni ya mwaka 1953, 1954. Sasa Sumbawanga ni Manispaa, leo *OCD* ana kachumba kamoja, halafu mnaendelea kujenga ofisi zingine za Wilaya ambazo ni kubwa, hata ile ya Mkoa, hivi kweli Waziri unaangalia ukweli wa mambo ? Msitufikishe mahali tukaanza kulalamika, msitufikishe mahali tukaanza kuipinga Wizara yako, ni mambo ya haki tu, tunataka haki itendeke pale ambapo inawezekana, tusaidieni tutekeleze hayo tuliyokuwa nayo. Nadhani Mheshimiwa Waziri, amenielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kamishina Mkuu wa Magereza, akaangalie tatizo tulilonalo kati ya mipaka ya shamba la Molo na vijiji ambavyo vinazunguka shamba hilo. Kuna kijiji cha Malonje, Sikawungu na Msanda Muungano, tulimalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na watendaji wote wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii, niipongeze Wizara kwa ahadi waliyoitoa ya ujenzi wa nyumba za Askari pale Ziwani. Napenda nishukuru kwa niaba ya Maaskari na watendaji wote kwamba, kazi hii imefanyika katika hali nzuri ya kuridhisha, japo bado tuna mahitaji lakini muungwana unapopata, unaambiwa ushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vyetu vingi vina matatizo ya vitendea kazi. Naamini tatizo hili ni tatizo la nchi nzima, lakini hata kama mtazaliwa kumi kila mmoja anasema, Mama yangu, hakuna anayesema Mama yetu. Kwa tafsiri hiyo, katika vituo vyetu tuna matatizo la gari na zaidi, Askari wanaopangwa doria hawana vitendea kazi. Kama mfuko mdogo, basi angalau simu zao watiliine vocha, waweze kuongea wakati wakiwa kwenye doria, pia itasaidia. Hii inatokana na kwamba naambiwa Sungura

mdogo, lakini kikipatikana kitu cha kusaidia, kinaweza kusaidia na mawasiliano yakipatikana, yatasaidia. Sio hilo tu, hakuna hata vitu vidogo vidogo, kama karatasi na vitu vingine kwa ajili ya kuandikia mambo yao ya kesi, vitu hivi vinasumbua katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi tunapata tatizo la kuwahudumia Wastaafu kutokana na ucheleweshaji wa kupatiwa viinua mgongo vyao. Ukweli tuna Askari wengi sana ambao mpaka hivi leo hawajapata kiinua mgongo. Mimi ninashauri sana Wizara ikatafuta takwimu za Maaskari wote, ili wajue huyu anastaafu mwaka gani, mwezi gani, ili waweze kupatiwa mafao yao mapema kuliko kuanza kuhangaika, nenda rudi na kama wale wetu wanaotoka Zanzibar, inabidi Mbunge utoe nauli ya kwenda na kurudi mara ya kwanza, mara ya pili, ya tatu, ya nne kiasi ambacho imekuwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba mtupunguzie kazi hiyo, jaribuni kuijandaa kuweka takwimu zenu ili muweze kuelewa mwezi anaostaa, mwaka gani, ili taratibu zao zianze mapema kadri iwezekanavyo ama sivyo, itakuwa kama tunawatelekeza watumishi ambao tumewatumia kwa kipindi kirefu. Askari wetu ni waaminifu, wana maadili ya kazi, lakini wanapomaliza, wanajisikia vibaya kwa sababu inakuwa kama thamani yao imemalizika baada ya kumaliza muda wao wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana huwa naomba utaratibu wa Askari wa Usalama Barabarani, wa malipo ya papo kwa papo ufuatwe huku. Wale Askari Trafiki wa Zanzibar, wakija huku basi nafikiri vyombo vyote huku vitakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamamo Mahakamani umezidi sana, unapanda baskeli bila taa, bila kengele, *no entry* unakwenda Mahakamani, daladala kule unaandikiwa kama ni watu kumi na nne, basi kumi na nne, kama ni ishirini, ishirini, akizidi immoja unakwenda Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta mrundikano umekuwa mkubwa sana Mahakamani, kiasi ambacho tunaweza tukaepuka kama tutakuwa na malipo ya papo kwa papo ili kupunguza matatizo haya. Leo kama utakwenda trafiki pale Malindi, utauliza hapa kuna mnada wa baiskeli? Zimejaa, watu wanasubiri wamalize kesi, wachukue baiskeli zao, ni jambo ambalo lilikuwa linaweza kufanyika kwa dakika kumi na likaondoa usumbufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudi kulisema hili kwamba, limekuwa kero tunaomba sana Askari ambao kwa kiasi kikubwa ni waaminifu, wanaweza kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na wakayapunguza matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kama utamchukua kuku ukamning'iniza kichwa chini miguu juu, basi ujue ni kosa kubwa na kifungo kinakukabili. Sasa mimi nafikiri Askari hawa tungewaleta hapa Dodoma, watu wa Dodoma wangemalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ninakuonyesha ni kwa kiasi gani wanauadilifu wa kufuata sheria zilizotungwa. Lakini pia, naomba hata hapa Dodoma tabia hiyo iondoke, kuwanyanya sasa wanyama, ukweli unawafunga kuku watano, sita, kumi, halafu unawaning'iniza kwenye balskeli, ukweli ni unyanyasaji wa hali ya juu, sasa hizo zote kwetu sisi ni kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa kutakuwa hakuna kukusanya yale malipo ya papo kwa papo, utakuta Mahakama ina kazi kubwa sana, msongamano mkubwa kiasi ambacho shughuli nyingine zinalala kwa mambo ambayo yanaweza kutekelezwa kwa dakika tano, kumi na yakawa yamemalizika. Kwa hiyo, naomba sana kuititia kwa Mheshimiwa Waziri, aliangalie suala hili ili tuweze kupata malipo ya papo kwa papo, watu tupunguze msongamano wa kwenda Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chuoni pale Ziwanu, walichukuliwa vijana wawili kutoka kwenye vyuo kwa ajili ya taaluma waliyokuwa nayo ya sheria, ili kuongeza nguvu katika chuo kile. Ukweli mmoja katika vijana hao wawili, ameacha kazi na ameacha kwa sababu ile taswira hasa aliyochukuliwa sivyo ilivyokuwa inatumika sasa angalau huyu mmoja aliyebakia apate matunzo. Hivi sasa analipwa mshahara mzuri, lakini hana *rank* yoyote, analipwa kutokana na elimu yake. Sasa kama hivyo ndivyo, hebu Wizara iamue basi kwa sababu hata *uniform* havai, mpeni *rank* inayostahili na mshahara anaopata ili naye ajijue, ama sivyo tutakuwa tunapoteza wataalam kwa njia kama hizo ambao tumewachukua kwa gharama, mtu anakuwa hajijui yuko katika hatua gani. Sasa kama ni mshahara tu, anapata vizuri lakini *uniform* pia havai sijui kwa nini havai *uniform* labda ni aibu kwamba, mshahara wake mkubwa hana hata *u-corporal* tunaomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la baadhi ya Askari wanaojitoa mhanga kupambana na majambazi na wahalifu wengine. Ukweli wamejaribu kufanya kazi hizo na wamepata maumivu, mpaka hii leo hawajapata hata kifuta machozi. Kwa taarifa zilivyo ni kwamba, wanaojitoa mhanga katika ushujaa, basi kuna kiasilimia kidogo wanakipata, sasa hawa hadi hii leo hawajapata kitu chochote kile cha kuweza kuwasaidia wakawenza kupata moyo wa kufanya kazi. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri, ujaribu kuyatafutia ufumbuzi mambo kama hayo madogo ambayo yana uwezo wa kupunguza baadhi ya matatizo kama tutayashughulikia vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Bunge lako hili, nataka kuzungumzia suala la vitambulisho lakini kwa kuititia Bunge lako hili, nataka kwanza nimwombe sana Mheshimiwa Shoka, kitambulisho chake kimekaa muda mrefu, anaitwa akakichukue, kwa hiyo angalau akifuatilie hicho cha U-Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi tena katika vitambulisho sasa vya Utanzania, sio vya Uzanzibari. Hebu kama hili zoezi bado ni gumu, basi tujitahidi angalau wale walioko kwenye mipaka yetu waweze kupatiwa vitambulisho, angalau unaweza ukamjua huyu ni Mtanzania, huyu si Mtanzania kama ni hali ngumu kiasi hicho ambacho tumefikia hivi sasa. Ukweli kama wale wa kwenye mipaka wanaoishi maeneo hayo wakiwa na vitambulisho hata haya matatizo ya kuibiana ng'ombe yanayotokea katika

Mikoa iliyo mipakani, yanaweza kupungua kwa sababu utamjua Mtanzania ni nani na aliyekuwa si Mtanzania ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi hasa kwa jamii ya wenzetu wa Kimasai, ukweli humjui Mtanzania wala Mkenya, sura wanafanana, kimavazi wanafanana, *hero, hero* wote hamna tofauti nyingine. Sasa ni jambo ambalo ninaomba Serikali ijitahidi kuwapatia vitambulisho hao ndugu zetu ambao wako mipakani, halafu ndiyo tuje huku mjini ili kupunguza mambo mengi ambayo tunaweza tukayapunguza yaliyokuwa hayana ulazima. Sasa kama uwezo wa kifedha bado mdogo, ninaomba sana Wizara ikajitahidi angalau kuwasaidia hawa wenzetu kupunguza matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofifi*)

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakupongeza kwa kunipa nafasi hii na leo kwa muda huu ni msemaji wa mwisho kwa kipindi hiki. Lakini vilevile nimpongeze Mkuu wa Majeshi ya Polisi, Waziri, Naibu Waziri na Makamanda wote wa Polisi pamoja na Uhamiaji na Magereza. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampa pole sana *IGP* Said Mwema na vilevile nampongeza zaidi *IGP* Said mwema, amelisababisha Jeshi la Polisi kukubalika katika jamii. Jeshi la Polisi, ambalo lilishatoka kwenye jamii, amejaribu kulileta na kuwa na uhusiano mzuri na jamii, nampongeza sana. Funga buti Said Mwema. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa jitihada zao za ufuutiliaji, lakini nina ombi mahususi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Waziri Mkuu msikivu. Hivi sasa ipo haja, Askari wetu kuwapa mafao yanayolingana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Lunch Allowance* sasa hivi Polisi wana haki wapate sawa, Waziri amekuja anatuambia ametayarisha mafao lakini hakutuachia bayana, atueleze Polisi haki yao iko wapi? Hawa si watoto wa kuku, hawa vijana wetu wapate haki sawa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Sasa hivi *ration* yao iwe shilingi 5000 kwa siku. Mimi mwenyewe nilikwenda *canteen* ya *central* pale nikala shilingi 3000, sikukijua nilichokula na kazi ngumu wanayoifanya Polisi hawa, Polisi katika mapambano na majambazi, humkuti ofisa utamkuta *Private, Corporal, Sergeant* ndiyo wanaopambana nao, leo kwa nini kila siku tunasema tunawapandishia, sema tu umewapandishia nini hapa tupate kujua. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Jeshi la Polisi, Ndugu Mwema ana matatizo makubwa anayopata kutokana na kwamba, hatumpi pesa za kutosha za kufanya kazi. Huyu kijana hili jina lake na baba yake vinalingana, ni mtu barabara kweli, mtulivu, ni ukweli uliokuwepo. Ukimpigia simu kama yuko kwenye kikao atakueleza nistahimilie na atakupigia. Kamanda gani anayeweza kufanya vitendo kama hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo Zanzibar, kuna Askari 250 wamepata uhamisho kupelekwa Bara, kwa sababu wamekaa muda mrefu hawajapandishwa vyeo, walipewa *u-corporal* na uhamisho Bara lakini haki zao hawapewi, kwa nini na watu wanafamilia, wana wake na watoto, lengo lenu wakafanye nini? Mnataka wafanye kazi au muwarudishe nyuma au waache kazi kabla muda wao haujafika? Hili nataka lisawazishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari haki zao wapewe, waache kulalamika hawana pakwenda, leo wanafunzi mnawapandishia, Polisi hamuwapandishi, kwa sababu wanafunzi wanaweza kugoma, Polisi hagomi, amepewa mafunzo na anaumwa na nchi yake, yejote anayekwenda UAskari ujue ni shujaa. Kazi ya UAskari ni ngumu sana, wapeni haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala mengine ya Askari wanaotoka *depo* pesa zao za kujikimu, kuna elfu 40, *depo* ya mwaka 2000, elfu 60, *depo* ya mwaka 2003, elfu 70, *depo* ya mwaka 2004 hela zao za kujikimu baada ya kutoka *depo* hamuwapi kwa nini? Kuna tofauti baina ya Bara na Zanzibar? Kwa nini hamuwapi haki zao wakati wanatiishwa saini? *IGP* nakwambia wametilishwa saini Askari wa Zanzibar, pesa zao hawapewi, nataka tupate maelezo kamili hapa juu ya haki za Maaskari hawa. Hii Sheria iko kwa Bara tu, kwa Zanzibar haipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *IGP* nakwambia tena, hili suala kutuwekea watu waliokuwa hawana maamuzi kuwa Makamishna, ondosha. Waziri nakwambia kutuwekea watu hawana maamuzi, msituwekee, wako vijana wasomi na wanaweza kufanya kazi. Huyu *IGP* anakwenda, anadanganywa tu, wanapiga *salute*, mzee tumefika, hawasemi jambo la maana, hawatetei matatizo ya Maaskari, hawasemi dhiki ya Maaskari, Askari wana dhiki, tegemeo letu sisi tulindwe, tulale salama, usalama wa raia uwepo lakini mbona hatuwalishi? Ng'ombe kama humpeleki machungani, kwa kumkaba atoe maziwa kila siku hutayapata utamuua ng'ombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linanihuzunisha sana, Naibu Spika, unaiona orodha hii, nataka uwe nayo na Waziri awe nayo na *IGP* awe nayo. Kuna wazee Askari wamekufa toka mwaka 1993, mwaka 2001 na mwaka 2004 lakini haki zao hawajapata. Mnajua haki ya maiti nyie? Urithi mnajua, dhiki yake na adha yake na hukumu ya Mwenyezi Mungu, leo tunakwenda kufuatilia haki hizi, tunakwenda pale palipo banda lile, mbuzi ukimweka hawesi kukaa, utatoka una mafua, wale Askari wanafanya kazi katika hali ngumu sana, banda la kuweka orodha za watu waliostaafuli, mafaili na kila kitu na ukienda unazungushwa, Mbunge mzima unazungushwa. *IGP* nenda kule ukaangalie hali halisi ilivyo hivi sasa, manyanyaso wanapata Maaskari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna ugomvi na baba yetu, ananiambia wewe mwanangu Mbunge mzima, ndugu yako toka alipokufa, pesa zangu sijazipata, nateswa tu, mnanigombanisha na mzee wangu bure, nyie tegemeo lenu nini? Waziri nakuuliza tegemeo lenu nini? Tunakwenda wapi jamani? Serikali ya Mapinduzi sikivu, Waziri Mkuu msikivu, kaeni muondoshe matatizo Idara ya Polisi, mnampa tabu Mwema. Huyu

jina lake linalingana, wazee wake wamejua kwamba, huyu atakuja achangie Taifa na jina ndiyo wakamwita hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoka Bungeni hapa, nataka watu hawa, pesa kama utakuwa umepewa, pesa hizi zilipwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, inakuwaje leo Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, pesa ya mafuta ilikuwa wanapewa shilingi milioni 20, sasa hivi wapewe shilingi milioni tatu hata kwa vespa, hazifai kwa kutoa huduma. Nawanong'onezeni uzuri na lipo hilo suala, mnawapelekea shilingi milioni tatu watafanya kazi gani wale?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viongozi wanataka *escort* ya Polisi, mafuta hakuna lengo lenu nini? Wayapate wapi, mnawapelekea shilingi milioni tatu! Leo la ajabu chuoni pale, mnampa pesa nyingi kuliko Kamishna wa Polisi, tegemeo lenu nini nyie? Mnaturepleka wapi? Japo kwamba, Sungura mdogo, pesa mnapata, Wizara ya Fedha wawape pesa Polisi wampunguzie makali Mwema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wanaopewa bakhshishi Zanzibar, mnawadhlumu. Kwa nini hamuwapi haki zao? Basi nawaombeni kile kitengo kinachoshughulikia habari ya fedha, wapeni uhuru wamalize na Hazina, maana yake ukienda Makao Makuu ya Polisi ni kuteswa. Mtu yale yale aliyosema Mohamed Rajab, ni kweli kabisa leo unafika kutoa pesa mfukoni, mimi nimekwenda na Mheshimiwa Ameir, kudai haki za Maaskari mara kumi. Leo mie nimekuwa mfanyakazi wa Polisi? Mie nilikuwa Jeshi bwana, wako Maaskari wameacha kazi tokea mwaka 2004 haki zao hamuwapi kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkija hapa mnipe jawabu kamili, sipendi kuchukua mshahara wa Waziri wowote kwa sababu kila mmoja ana wake, lakini kama sikupata jawabu leo, mimi nitakuwa mkorofu, kwanza, sijasimama hata siku moja hapa na haya, Alhaji Kagesheki, nakuonea huruma sana kwa sababu wewe mfuutiliaji, inabidi niongee kwa sababu naona uchungu hapana hata familia moja inayotoka Zanzibar ambaye hakuhusiana na familia yenye upolisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtoto wako Polisi pesa umchangie wewe, ushuhuda mie ninao kamili. Mwanangu alikuwa anataka vespa, fedha za vespa zimemshinda aendeje kazini? Nimetoa mfukoni mwangu kumnumunulia vespa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine na watoto mnawaweka miaka mingi hamuwapandishi vyeo. Askari anatoka kutoka *Private* anakaa miaka saba na hasa Zanzibar, kuna matatizo *IGP* Mwema, nenda Zanzibar ukutane na Maaskari, sio kukutana na viongozi tu, watakudanganya hawa *IGP* Mwema. Nakuambia juu ya sifa zako na pale Makao Makuu, pitisha fagio, tunakwenda taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza kabisa ultakiwa uniambie mimi, sasa unamwambia *IGP*, hawezi kukujibu hapa, unatakiwa uniambie mimi.

Sasa nafikiri amewasilisha zile karatasi alizokuwa anasema, kwa hiyo ofisi yangu itakabidhi kunakohusika halafu tutaendelea labda mchana Mheshimiwa anaweza kupata nafasi kuzungumzia hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sina chochote mchana huu, isipokuwa nasema mchana tukirudi, wafuatao ndiyo watapewa nafasi. Ni Mheshimiwa Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma na sana sana Manju Salum Msambya. Wengine mjiandae vizuri kwa hoja moja moja kwenye Kamati ya Matumizi. Kamati ya Matumizi unaruhusiwa hoja moja iliyoandaliwa vizuri kwenye mshahara wa Waziri.

Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06:59 Bunge lilahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **HOJA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, niliwataja wafuatao kwamba ndiyo wataendelea kuwa wachangiaji, nao ni Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Manju S. Msambya. Tunaanza na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, karibu!

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaomba nimshukuru Mungu sana kwa kuniweka mpaka muda huu kuweza kupata muda wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja yenye, ninapenda kwa niaba ya wananchi wa Morogoro Kusini kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuja Jimboni mwezi Juni kumalizia ahadi yake. Wananchi wanamshukuru sana na wanamkaribisha tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, sina budi kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, *IGP* na Maafisa wote wa Jeshi la Polisi na Magereza na wengineo, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hii mpaka tunao usalama wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi, naomba nimpongeze *RPC* wangu wa Morogoro, anafanya kazi nzuri sana, tena sana kwani ni kijana hodari na ana mawasiliano na uhusiano mzuri na Maafisa wake na watu wengine. Nashukuru sana kwa tabia yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye hoja na ninaomba niende moja kwa moja kwa yale ambayo yananigusa Jimboni kwangu. Nimekuwa ninazungumzia suala hili katika Wizara hii kwa muda mrefu sana, vitendea kazi kwa Polisi wa Jimboni kwangu. Nilikuwa ninaomba sana usafiri, Jimbo ni bayo sana na kubwa sana, lina milima na mabonde na nilikuwa ninawaomba sana sana viongozi wa Wizarani kusaidia Polisi wale angalau pikipiki ili waweze kufika sehemu ambazo ni ngumu sana. Inakuwa vigumu wao kufanya kazi bora kama wale majambazi na wezi wana vyombo nya uhakika lakini wao wanakwenda kwa miguu, kwa kweli ni kitendo cha aibu sana kuona Polisi wakifanyiwa hivyo na ninaomba tena leo, tafadhali sana hii ni mara ya tatu sasa mfululizo, ninaomba Polisi wa Matombo na Kisaki wapatiwe usafiri kwani ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimwombe Waziri au Naibu Waziri asiende mbali, yeye na mimi wakati tuko hapa tuandamane tu aende kwa siku moja akaone matatizo ya Matombo na atajua kwa hakika watu wale wanastahili huduma ya usafiri. Ile milima mikubwa na mirefu wao wanakwenda kwa miguu huwezi kuamini. Kule kuna madini na Wachimba Madini wa kila aina wapo huko kutoka kila sehemu, wanapokosa madini wanaingia kwenye ujambazi. Hivyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri uwapatie vijana wetu wale vyombo nya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la vituo nya Polisi katika Jimbo langu, ukiacha kituo cha Matombo na Kisaki, utaona kwamba Mvuha, Dutumi, Mungasi hakuna kituo na hizo ni sehemu ambazo zina umbali wa kilomita 50 au 60 mpaka 70, kwa hiyo, ni vizuri tukasaidiwa na Serikali. Lakini kimoja ambacho kiko Tawa kimebakia milango tu na niliahidiwa kwamba Jeshi la Polisi lingekwenda kuangalia na kuona jinsi gani wangeweza kutusaidia, tumekwishakijenga, tumepega lipu na tumekiezeka. Sasa naomba tafadhali sana hiki ni kituo ambacho kitusaidia sana Kibungo Juu, Tawa na Kibowa ambayo ni milima mitupu hiyo na sasa pale kuna soko kubwa pale watu kutoka Kenya, Uganda wanakuja na malori yao kuchukua matunda katika soko la Tawa, kwa hiyo, tukipata ulinzi itatusaidia sana. Naomba mtusaidie siyo tu kumalizia kituo kile na kutuletea Maafisa ili tupate ulinzi wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la nyumba za Maafisa hawa. Kwa kweli ukienda kungalia nyumba anayokaa Mkuu wa Kituo cha Matombo, nina hakika usiku akilala unaweza ukamuangalia kuititia nyufa za ile nyumba. Inatia aibu na inatia mashaka. Naomba Polisi hasa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, tafadhali sana nyumba ile itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko nyumba pale imeanguka Maafisa wale wametoka, wako uraiani na Maafisa wengine wako uraiani, wanakaa tu, pana nafasi pale, tunaomba tafadhali sana mtumalizie nyumba zile ili Maafisa wale warudi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, rumande ya Matombo si rumande hata kidogo, inatia aibu kwani kama wakizidi watu watatu basi inabidi kutoka nje, wanafungiwa na pingu nje na Askari inabidi alale pale mpaka asubuhi, si kitendo kizuri hata kidogo wanawenza siku moja wakamzidi nguvu wakaondoka. Naomba hilo mlitupie jicho sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo maalum ambalo liko kwenye Jimbo langu na hili limetokana na ndugu zangu wafugaji. Katika Jimbo la Morogoro Kusuni, wameingia wafugaji wa aina tatu yaani kuna Wamasai, Wasukuma na wale wanaoitwa Wamang'ati. Watu hawa hawapendani na hawapendani katika misingi nafikiri ya mila na desturi zao. Lakini zaidi kumeingia na wizi wa mifugo wa hali ya juu sana, kwa hiyo, unaweza ukashtukia vita tu ya ghafla wanapigana, Polisi hawana nyenzo za kwenda kumalizia matatizo haya. Wale wanaoiba, wanafanikiwa kwa sababu wanatorosha mifugo hiyo haraka sana na wengine wanafuatana mpaka Chalinze kilomita 198 huko kutoka sehemu zile ambazo mifugo imeibwa. Naomba wasaidieni Polisi wamalize tatizo hili kwa uharaka na kwa uwezo mkubwa, si vizuri kwa Polisi kubebe Bunduki mgongoni halafu akaomba lifti ya pikipiki au ya baiskeli wanawenza kumfanya chochote kile, ni vizuri kwa Polisi kuwa na pikipiki ama gari lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba sana na ning'ang'anie tena tupatiensi usafiri wa uhakika katika Jimbo la Morogoro Kusini, tuko mwisho, tuna matatizo makubwa vilevile kuna matatizo ya wanyama hata ikitokea vifo wale Polisi wanatoa taarifa tu kwa kutumia simu na simu si zao pengine ni simu za wananchi tu na inabidi wangoje hapo maiti mpaka Madaktari waje. Tafadhali sana wasaidieni. Ninakuahidi kuanzia sasa nitafuutilia ofisini kwa Mheshimiwa Waziri mpaka usafiri upatikane kwa Jimbo la Morogoro Kusini, utapatikana tu itabidi abane mahali atupe sisi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo lingine kubwa sana na tatizo hili ni kwa wale Maaskari ambao wameumia halafu wamapona na hawawezi kufanya kazi za kiuAskari, wanapewa kazi ndogondogo na matokeo yake Maaskari hawa hawapati *promotion* kwa sababu ya kuumia kwao. Tunaomba muwafikirie sana Maaskari hawa kwani kuumia kwao si kwa hiari yao na kama bado wako kazini wanastahili kupata *promotion* hata kama watakuwa pale kama Makarani, muwasaidie sana hawa Maaskari kwa sababu na wao wanaumia, wana familia na wako kazini, hili ni jambo muhimu sana kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye tatizo la kuanzisha vituo kwenye Jimbo langu. Nimeomba mwaka juzi, nilipewa jibu kabisa la uhakika kwamba nenda kaanzishe Wizara itasaidia. Nimeanzisha vituo vile na sasa inakuwa ni tatizo kwa sababu Wizara hata ukiwaandikia barua hawajibu. Tafadhali sana tena sana, naomba mjibu barua na ninaomba msaidie vituo vile mlivyoahidi na mimi nina hakika Waziri na Naibu Waziri, ni watu wasikivu, wanaelewa mambo haya na wanayaelewa matatizo haya. Sasa ninaomba mmoja wao wakati anajibu aahidi kwamba yeze mwenyewe atakwenda na mimi kwenda kuona matatizo ya ulinzi katika Jimbo lile labda ndiyo mtawenza kutufungulia vituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, niseme ahsante sana na ninakushukuru na pia ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani kwa kunipa nafasi hii na mimi kuongea mbele ya Bunge lako.

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uhai mpaka siku hii ya leo, nami nikasimama mbele ya Bunge lako tukufu kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuona jinsi Maaskari wanavyotaabika na makazi yao na jinsi wanavyohitaji makazi. Bajeti ya mwaka 2008/2009, alitenga pesa kwa ajili ya nyumba za Askari Polisi na mwaka huu kwenye bajeti yake nimeona pia katenga bajeti ya kujenga nyumba za Askari Polisi. Hii ni nzuri sana na hasa inawasaidia wale Askari wa pale Kigoto Mwanza na pale Mabatini kwani maisha yao tunayaelewa, ni chumba na sebule lakini chumbani, ni chumba na sebuleni pia ni chumba. Kwa kufanya hivi, atakuwa amewasaidia sana Askari wale ili waweze kuishi vizuri na familia zao na waweze kuongeza familia zao kwa mujibu wa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kitu kimoja ambacho nimejiuliza kwa muda mrefu nimeshindwa kukielewa. Tunapotenga bajeti ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi sijui hawa wa Jeshi la Magereza tunawaweka wapi? Kwa sababu sijawahi kusikia hata siku moja hapa kwamba imetengwa bajeti ya kujenga nyumba za Jeshi la Magereza, kwani na wao kuna vijana pia wanahitaji makazi, kuna vijana pia wanaishi nje ya Magereza katika nyumba za kupanga. Hivyo basi, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, iwafikirie Askari hawa wa Magereza naona wamesahaulika kwa muda mrefu angalau japo Sungura ni mdogo lakini tumle tukinawa mikono. Siyo wale wengine na wengine wale bila kunawa mikono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, angalau awape moyo Askari Magereza kwani na wao pia wanafanya kazi ngumu sana. Wanafanya kazi ya ulinzi pia kuwalinda wahalifu, mahabusu na wafungwa ambao wengine ni majambazi sugu, wengine wanaowalinda ndani ya Magereza yale ni watu wenye uwezo mkubwa lakini tukiamka tunawakuta salama wafungwa wote wapo, naomba muwafikirie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninataka kuongelea ni kuhusiana na kituo kidogo cha Polisi cha Kata ya Pasiansi katika Wilaya ya Ilemela Mjini Mwanza. Kituo kile sasa hivi kinaweza kikawa kinahudumia watu zaidi ya 20,000 kwa sababu kinahudumia Kata ya Pasiansi nzima, baadhi ya Kata ya Ilemela na Kata ya Nyamanoro na maeneo mengine jirani. Lakini kituo kile kinakuwa na Polisi wachache sana, pindi mtu anapopata matatizo akienda pale anaambiwa hatuna Askari kwa ajili ya kwenda kukamata wahalifu. Hii inasikitisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe imekwishawahi kunitokea, nikitoka Kiseke ni mbali, nikija Pasiansi halafu naambiwa niende Kirumba na wakati nakuta pale mhalifu anaendelea kufanya kazi yake hata mauaji yakinokwea pale kuja Askari inakuwa ni vigumu zaidi kwa sababu mpaka watoke Kirumba pale wanasesma hawana Maaskari wa kutosha. Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Naibu Waziri, Ilemela ni jirani na Jimbo lake, aliangalie suala hili kwa jicho la huruma kwa sababu Askari hawatoshi na ongezeko la watu ni kubwa na mji ule unaendelea kukua sasa hivi kwa kasi kwa sababu baada ya mwaka mmoja au miwili watu wataongezeka na kuwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna kituo kidogo cha Igogo kiko katika Wilaya ya Nyamagana. Kituo hiki kinahudumia Kata zaidi ya tatu au nne yaani zaidi ya wananchi 45,000 lakini kituo hiki kina Askari wachache sana kiasi kwamba Askari hawa wanashindwa kutekeleza kazi zao ipasavyo na pale ndipo inapofikia Askari wasiokuwa na maadili kukiuka Sheria za kazi zao na hata kufikia kusema kwamba kuna baadhi ya Askari wanapenda rushwa kwa sababu ni wachache na kesi zinakuwa ni nyingi na wahalifu wanakuwa ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Kata hii ya Igogo, kuna gari la Polisi ambalo ni bovu na hili gari likijitahidi likifanya kazi siku mbili basi siku ya tatu linarudi *garage*. Tunamuomba basi Mheshimiwa Waziri aangalie suala hili angalau kwa kuwa Kata hii inahudumia Kata nyingine zaidi ya tatu na watu zaidi ya 45,000 ili waweze kuwa na gari la uhakika la kuweza kufanya shughuli zao na kuweza kufanya kazi zao bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, nimeona ameongelea kuwaajiri watu 7,000 kwa ajili ya uchaguzi. Hii kidogo inanistua kwa sababu vijana 7,000 kwa faraja ni kwamba vijana wetu watapata ajira lakini kwa nini ajira hii isiwahi kwa sababu kuna shida ya Polisi ambayo haisemekani. Kuna kituo kidogo cha Polisi kimejengwa Kata ya Bugogwa, tangu kimejengwa kituo hiki kwa muda mrefu sana hakijapata huduma ya kupelekewa Askari wa aina yoyote. Sasa kwa nini hawa vijana 7,000 wasingeajiriwa mapema wakaanza kazi za wananchi mpaka wasubiri uchuguzi? Hivi Tanzania kweli tuna vita kweli vya kusubiri Askari 7,000 wakati wa uchaguzi? Hii inanisikitisha pamoja na kwamba vijana watapata ajira, vijana hawa walipaswa wapate ajira mapema ili waweze kuendana na shida za Askari Polisi zilizopo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wameongelea kuhusiana na Askari, kweli Askari Polisi mafao yao ya uhamisho si kwa Visiwani tu bali hata Bara Mkao hadi Mkao, Wilaya hadi Wilaya, Askari Polisi wanahamishwa. Kwa hiyo, tunaomba kitu kimoja angalau kupitia Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani, iangalie suala hili waweze hata kuwatengea malipo yao hata kwa awamu lakini wawamalizie malipo yao yote kwa sababu kumuongeza marupurupu Askari halafu akafikia sehemu hana anachokipata kulingana na haki yake halisi hii, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesemi kwamba Askari wetu wameongezewa marupurupu, lakini sijui Serikali inatumia kigezo gani baina ya Majeshi yetu kwa sababu kuna ambao wanalipwa shilingi 50,000/= kwa mwezi na kuna ambao wanalipwa shilingi

150,000/= kwa mwezi. Sasa sijui tofauti yake ni nini wakati watu hawa wote wanahemea katika soko moja. Tunaiomba sasa Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, ilifikirie suala hili na ijue kabisa Askari Polisi nao wana kazi kubwa sana na pia wao wanahitaji angalau malipo yao yaendane sawa kwa sababu wote hufanya kazi zinazoendana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwamba wakati wa Kamati Jumamosi nilitembelea eneo moja la Pemba, nilikwenda kuwaona vijana wa Bara ambao nilikutana nao barabarani wakanipeleka mpaka kituoni kwao yaani kituo cha Wete. Ombi waliloniomba ni kwamba wanamuhitaji *IGP* na hawa si Askari wakubwa ni Askari wadogowadogo, wakasema Mheshimiwa Waziri alipokwenda hakuwaona Askari wadogo wadogo, aliwaona baadhi ya Askari wakubwa, kwa hiyo, wanamuhitaji kwa sababu wana madai yao ya tangu mwaka 2003 wana haja ya kumueleza *IGP*. Pia walisema wanaomba mgawo wao uwe unapitia kwa *RPC* Mkoa na siyo kupitia sehemu nyingine yoyote kwani inakuwa ni vigumu sana kupata mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kuchangia kitu kimoja, hawa Askari wetu wanafanya kazi nyingi sana, wanafanya kazi za ulinzi wa raia na mali zao. Kwa hiyo, kama wanafanya kazi nyingi sana Askari hawa, wanatti amri wanapoambiwa inuka anainuka kulingana na mkataba wa kazi zao lakini napenda kuuliza kwamba pale wanapocheleweshewa madai yao je, Serikali kupitia Wizara wanawalipa na fidia? Kwa sababu pesa inakuwa imeshashuka thamani kwa wakati ule uliopita na kwa sasa hivi pesa inakuwa na thamani tofauti. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho aweze kunijibu hayo maswali yangu ambayo nimemuuliza na pia ninapenda kutoa ushauri awakumbuke Askari Magereza kwani hata Hospitali pia wamesaulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, JWTZ wana Lugalo, Askari Polisi wana hospitali yao lakini hawa Magereza wamekosa nini jamani? Sielewi walichokikosa! Ni muhimu basi na wao wakatengewa mahali pa kupata matibabu bila matatizo yoyote. Baada ya kufanya hili ni kwamba na wao watajiona wana haki sawa na Jeshi lingine lolote liwe la Polisi au hata JWTZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Riziki O. Juma.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake, kwa kazi nzuri sana anayoifanya pamoja na umri wake mdogo lakini labda niseme kwamba anajitahidi sana na anamudu kufanya kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze na kitengo cha ...

**NAIBU SPIKA:** Sijui uhame katika hiyo mashine?

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunibadilishia hii *mic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa *Police Marine* kule Zanzibar. Hivi karibuni tutakumbuka kwamba tulipata msiba mkubwa sana wa kuzama kwa ile Mv. Fatih. Ni msiba mkubwa kwa Watanzania na ni msiba mkubwa kwa Wazanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana *Police Marine* pale Malindi hawawezeshwi vizuri. Kuna Kitengo cha Uokoaji ambacho inaonekana hakitimizi wajibu wake vizuri jambo ambalo liliipelekea meli ile ambayo imezama bandarini yaani imeshafika lakini vijana wetu walishindwa kutumia nafasi ile kuwaokoa jambo lililopelekea Watanzania wale kuoza kabisa maana walishindwa kuokolewa hata zile maiti zao yaani zilizopatikana ni baadhi tu na hata kama kuna wengine waliopatikana basi tayari walishaanza kuoza. Tatizo ni kwamba Kitengo hakiwezeshwi vizuri na kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri akiangalie sana Kitengo kile na uokoaji ili msiba kama huu mzito, kwa sababu msiba huu tayari umeshatokea, wamekufa lakini ni vizuri sana wangepatikana wakazikwa wale watu. Ni jambo la kusikitisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nilizungumze ambalo limezungumzwa pia na wengi sana na ni jambo ambalo wanalilalamikia sana Askari wetu. Askari ndio usalama wa Rais, sote tegemeo letu tunawategemea wao watulinde ili tuweze kufanya shughuli zetu aidha za kimaisha, kiasasa au utendaji kazi, zozote zile tunahitaji ulinzi na kwamba kila mahali tunamuhitaji Askari. Lakini ni jambo la kusikitisha ni kwamba Askari hawa inaonekana tunawadharau kwani wanafanya kazi usiku na mchana, mvua na juu lakini wanadharauliwa kiasi ambacho kinatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wanapopewa uhamisho kwenda mahali pengine kama imetokea kupewa huo uhamisho basi anaambiwa nenda jitegemee, safirisha mizigo yako na baadaye utalipwa. Nina malalamiko mengi sana ambayo nimeletewa na Askari kule Wete Pemba kwamba kuna Askari kahamishwa tangu mwaka 1999 hadi leo hajapata mafao yake. Je, hiyo ni haki? Tunawatendea haki Askari? Mbona bila ya hawa Askari hatuwezi kufanya shughuli zetu? Mbona hawa Askari tunavageuza makopo ya chooni?

**NAIBU SPIKA:** Hiyo si lugha nzuri kwa Bunge!

**RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, nafuta.

**NAIBU SPIKA:** Sawa!

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana kwamba kitu ambacho una shida nacho, unakitafuta kwa hamu sana na unakitumia wakati ule wa kazi lakini ukimaliza kazi yako unakidharau kwani unakuwa umemaliza matumizi yako. Sasa sisi hatuwezi kwenda bila ya wao, ni lazima tuwatunze Askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hili kwa uchungu kwa sababu Askari wengi wanakuja na kutulalamikia jamani na wanalalamika kwa Wabunge na wakihisi

kwamba tutawafikishia madai yao au malalamiko yao yanafikishwa? Wabunge wengi wameyalalamikia hayo na ninamuomba Mheshimiwa Waziri afanye juhudzi zake basi ili ahakikishe ndani ya mwaka huu basi wanalipwa yale madai yao ili tuondokane na haya malalamiko yasiyokwisha. Tunawategemea sana hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Askari ambao wanalamikia Wahasibu wao kwamba wana wasiwaso posho zao nyine zinapelekwa lakini zinaishia mifukoni mwa Wahasibu, sina hakika Mheshimiwa Waziri, naomba ufuatilie kwa ukaribu sana uone kama kuna ukweli kiasi gani kuhusiana na hili kwa sababu huyu Askari ambaye tangu mwaka 1999 hajalipwa ana mashaka kwamba pesa yake imetolewa lakini haikumfikia yeze mwenyewe. Naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa ukaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko ya mishahara ya Askari kule Pemba. Zamani mishahara yao ilikuwa ikiipelekwa *NMB* moja kwa moja na mishahara inapotoka huku Tanzania Bara na wao kule moja kwa moja wanapata mishara yao kama kawaida. Kulipotokea mabadiliko kwamba mishahara iingie *BOT* Bara halafu urudi tena *NMB*, *NMB* tena watoe kisha ipelekwe *NMB* Pemba ni usumbufu mkubwa wanaoupata Askari wetu, naomba tuwaangalie kwa umakini sana ili usumbufu huu uweze kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkiwa alisema kwamba, *IGP* akutane na Askari. Mimi nimeombwa hasa na Askari, Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara yake kule Pemba, Askari walikuwa na matumaini makubwa sana kwamba, Mheshimiwa Waziri angekutana nao, bahati mbaya labda hakupata muda wa kukutana nao. Mheshimiwa Waziri, wanakuomba sana Askari Pemba, ukutanae nao, wana malalamiko yao na madai yao mengi sana ambayo pengine wanahisi kwamba, wakubwa wao hawayafikishi, ukienda mwenyewe wataweza kukuambia uso kwa uso. Naomba sana ulichukue suala hili kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninapenda nilizungumzie, ni suala la ajali barabarani. Inaelekeea ajali za barabarani Tanzania, zimekuwa nyinyi na za kutisha. Ukipanda gari mwenyewe una wasiwaso kwamba, jamani nitafika safari ninayokwenda? Huna hakika, ingawaje ajali inatokea popote Mwenyezi Mungu akiandika, lakini ajali nyinyi zina kusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali nyinyi zinachangiwa na Madereva wazembe na walevi. Naomba tuangalie sana wakati wa utoaji wa leseni, lakini pia Askari wetu wa barabarani waangalie sana Madereva wanapoendesha magari, je, wako wako makini? Hili ni tatizo ambalo linatupoteza Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu kazi ya Taifa inapotea kwa ajali za hovyo hovyo, ajali ambazo sio lazima, tunaweza kuziepuka. Je, vile vidhibiti mwendo vimeishia wapi? Tungekuwa na vile vidhibiti mwendo, basi vingetusaidia angalau kwa wale walevi, labda wakati mwengine vingeweza kuwa-control kwa sababu, ukiishalewa unaweza kufanya chochote, kwa hivyo, unaendesha gari kwa mwendo wa kasi, bila kujali kama umepakia watu, unahisi labda kama umepakia mawe au makumbi. Kwa hiyo,

naomba sana hili liangaliwe na Askari wetu wa Barabarani, kuhusiana na Madereva wazembe na walevi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la maandalizi ya uchaguzi...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuko Bungeni, punguzeni mazungumzo, kuna wengine wanatengeneza vikao hapa hapa. Mheshimiwa endelea.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ametaja suala la maandalizi ya uchaguzi, Mheshimiwa Mkiwa, alilusa hapa na alisema wana lengo la kuongeza Askari elfu saba (7,000). Nashauri kabla hatujaongeza hawa Askari elfu saba (7,000), kwa sababu hawa wanahitaji gharama za mafunzo, basi tuwalipe kwanza wale Askari wanaotudai maana wana madai yao mengi sana. Kwa hivyo, tuwalipe wale kwanza, baadaye ndiyo tuongeze Askari elfu saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kwa nini tuongeze Askari wakati wa uchaguzi? Kwa nini? Kulikoni? Mnaongeza magari na vifaa na vya kutuliza ghasia, kulikoni? Gari moja la maji machafu liko kule, king'ora kimekufa sijui kama Mheshimiwa Waziri, ameishalipelekea king'ora au viper? Liko kule FFU Finya. (*Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatutisha na linatutia mashaka kwa sababu kule Zanzibar inaonekana hili Jeshi la Polisi, lime-*deligate power*. Kwa nini nasema hivyo? Sasa hivi kuna Daftari la Uchaguzi linaandikishwa, lakini wanaosimamia pale ni JKU, Mgambo, KVZ, Zima Moto, ndio walipewa silaha pale, Askari Polisi inaonekana wao wanawalinda wale, wanawalinda wale KVZ, kwa sababu wapo Askari Polisi, lakini wanakaa kando huko, wanasubiri nini kitatokea wawalinde wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata mashaka kulingana na hali hii inavyokwenda. Nauliza tena, Jeshi la Polisi, kule Zanzibar lime-*deligate power*? Shughuli zake na hasa wakati wa uchaguzi zinafanywa na vikosi vya SMZ,? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipindi kulitokea kesi pale Piki, Askari walikwenda kufanya vituko ni JKU sijui Mgambo, sijui *Janjaweed*, sijui na nani, Askari Polisi wakatolewa kituoni na Kamanda, waende pale bila silaha, walipokwenda pale wale Maaskari walikuwepo wa SMZ, wana silaha, wao wakaishia kuandika majina na kuchukua mafaili, kipindi walichopigwa Mheshimiwa Khalifa na wenzake. Walikwenda na mafaili yao wakachukua majina, wakarudi, walishindwa lile agizo walilopewa na *RPC*, kwa sababu walitakiwa wale vijana wawachukue, waende nao kituoni kama kuna masuala ya kuhojiwa, wahojiwe kituoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea pale, walirudi wale Askari, mimi nikawakuta njiani, wakanambia Mheshimiwa usije ukaenda huko, wenzako wanapigwa kweli kweli. Nikamuuliza akina nani? Akanijibu ni fulani na fulani. Nikamwuliza nyie mnatoka wapi? Wanasema sisi tumetumwa na Kamanda, lakini

matokeo yake tulipofika tumeshindwa. Nikawauliza hivi ninyi mnashindwa na JKU na Mgambo? Nyinyi si Askari wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Jamhuri ya Muungano, mnashindwa na wale Mgambo? Kwa maana hiyo, ndiyo pale nilipotumia lugha ya kwamba, Jeshi la Polisi kwa upande wa Zanzibar, lime-*delegate power* kwa vikosi vya SMZ?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo, naomba niishie hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe machache niliyonayo katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikianza, naomba niwatoe wasiwasi wenzangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini mchango wangu kwanza nzungumzie...

**NAIBU SPIKA:** Kwani wana wasiwasi? (*Kicheko*)

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Wanaweza kuwa na wasiwasi Mheshimiwa.

**NAIBU SPIKA:** Haya wewe endelea tu.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nzungumzie hali ya usalama katika jimbo la Kigoma Kusini. Inaonekana Kusini ina matatizo matatizo kwa sababu hata Mheshimiwa Mwenegoha, amezungumzia hapa Morogoro Kusini, ndiyo hali hiyo hiyo na mimi katika miaka ya Tisini (1990), niliwahi kusema na wakati mwagine inatamkika vizuri kwa Kingereza “*The South is always poor and problematic*”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri, asaidie kupatikana kwa vituo vya Polisi katika Kata zifuatazo, ambazo ili mtu apate huduma ya Polisi inabidi atembee masafa marefu. Kata ya Ilagala, Kata ya Igalula, Kata ya Sunuka na hapa ndipo ninapotoka mimi lazima nitangaze maslahi, Kata ya Simbo, Kata ya Kandaga, Kata ya Mganza na Kata ya Mtego wa Noti (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya mengi yako mwambao wa Ziwa Tanganyika, sasa vituo vyenye Polisi au Kata zenye Polisi ni Kalya, Buhingu na Sigunga. Ukiishatoka hapo kwenda kwenye maeneo niliyotaja inabidi uwe umejiandaa kweli kweli. Najua Polisi wenzetu ni watu wana mafunzo, wana mazoezi, lakini kumtuma kwenda kituo cha mbali hakuna barabara na inabidi uende kwa usafiri wa maji, ni tatizo. Kwa hiyo, naomba maeneo haya yapatiwe vituo ili kuwe na ukaribu wa kufikiwa huduma za kipolisi, ambapo tumesema kazi kubwa ya Polisi ni usalama wa raia na mali zao, uwe na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nizungumzie ni kwamba, baadhi wamezungumza, wamewapongeza sana Polisi na mimi nawapongeza wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu sana, lakini tunayo lugha katika Serikali, ikitokea hitilafu mtu anasema, ni watu wachache kama Manesi, wanasesma ni Manesi wachache, Waganga wachache, kwa hiyo hata ukija kwa Polisi, unaambiwa ni Polisi wachache ndiyo wenye utaratibu huo mbovu. Sasa wakishakuwa Polisi wachache Kigoma, Sengerema, Singida na kwingineko, ukiwajumlisha wanakuwa wengi. Lipo tatizo la rushwa ndani ya Jeshi la Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, wanasesma baadhi, hawasemagi wachache, wanasesma baadhi tu.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Sawa, lakini mimi nadhani Kiswahili ni lugha yangu na ninailewa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lipo tatizo la Polisi, hasa Polisi wa Usalama Barabarani, utakuta wanasmamisha magari makubwa, malori, *ma-semitrailer*, lakini ni nadra sana Polisi hao kusimamisha magari madogo. Naomba pengine Mkuu wa Jeshi la Polisi kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, aniambie na hawezi kuniambia hapa, tunaweza tukakutana hata nje, ni kwa ushahidi gani alionao kwamba, gari dogo haliwezi kuwa, limechukua mihadarati? Utakuta wanasmamisha magari makubwa, wanakwenda kukaa mbele ya magari makubwa, anaongea kama ni Dereva wa basi, wanapangana vizuri anachukua chochote, lakini tunasema ni Polisi wachache, hao ni barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, wanasesma ni wachache, Dar es Salaam kwenda Arusha ni wachache, Dar es Salaam kwenda Mwanza ni wachache, ukiishawajumlisha ni wengi. Kwa hiyo suala hili la rushwa ya Polisi, ni kweli linapigwa vita na wanajitahidi kwa sababu, nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ipo Idara imeundwa ya kufikishiwa malalamiko, sasa ninaomba vilevile ipatikane Idara ya kuangalia mwenendo wa Polisi wa Usalama Barabarani, kwa sababu kadri wanavyofanya wanawatia mashaka raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la uraia wa nchi mbili. Mimi binafsi siliungi mkono japokuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, asubuhi amelizungumza kwa kulishabikia sana, mimi siliungi mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini siliungi mkono? Twende kwenye kauli zilizotolewa, kulitokea mgogoro ambao hata sijui ulianzia wapi, ulianzishwa na wenzetu wa Rwanda, ambao tumewakaribisha kujejunga na Jumuia ya Afrika Mashariki, wanakuja wanataka kuhamisha Makao Makuu kutoka Arusha, wapeleke Nairobi kwa kisingizo kwamba, Nairobi ni katikati, hivi katika hizi nchi tano, Nairobi ndiyo katikati au tungesema kwamba, Entebbe au Kampala ndiyo ingekuwa katikati? Unamkaribisha mtu sebuleni, anataka kuingia mpaka chumbani! Wanaojenga hoja ya uraia wa nchi mbili, pengine wanataka jamaa zao walioko nje wafaidike sana na suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nalipinga na wale walioko nje wenye kutamani kuja ambao hawana uhusiano na watu hapa, wanataka kuja ili waje wahodhi ardhi. Eeh! Kwa

sababu wameona ardhi ya Tanzania, haina mwenyewe. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba, napinga kabisa suala la uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa naibu Spika, uharamia katika Ziwa Tanganyika. Nawashukuru sana Wizara ya Mifugo na Uvuvu, ambao wameupatia Mkoa wa Rukwa, boti mbili kwa sababu ya doria, najua zitasaidia kwa kiasi fulani kupunguza tatizo, lakini mwambao wa Ziwa Tanganyika ni mrefu sana, wenzangu wa Rukwa wanafahamu, sijui unaanzia kijiji gani, kule Kasanga nafikiri, unakwenda mpaka Kagunga, mpakani na Burundi na hapo ndipo machafu yote yanapofanywa na maharimia kutoka *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliletewa boti la Polisi kwa ajili ya doria pale Kigoma, lakini lina zaidi ya miezi minane halifanyi kazi, na tumeambiwa kwamba, yale yaliyokwenda Rukwa yatasaidia. Mahala penye umbali, kama hizi Kata nilizoeleza umbali wa kupashana habari, kwa sababu hapa pengine hapana hata kituo, sasa mpaka habari iende Kasanga, irudie pengine Kalya, halafu hawa watu wa Kalya, ndio waende Kagunga, tungeomba ama lile boti la doria likabaratiwe au lipatikane jipya lenye uhakika wa kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la uraia na ukabila. Mkurugenzi wa Uhamiaji pengine atakuwa amesahau, mimi nimefika Ofisini kwake mara nydingi sana miaka ya 1990, vijana wa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma, pengine hawakupewa elimu nzuri ya kufanya kazi yao. Nasema hivi kwa sababu, wanashindwa kupambanua kati ya raia na mtu wa khabila fulani. Nitaomba nitaje kwa majina, humu tunaye Mheshimiwa Mbunge wa Rarya, Profesa Sarungi, yeye ni Mjaluo, yule mzee ni Mjomba wangu na anajua kwa nini nasema, ni mjomba wangu. Ni Mjaluo, Raila Odinga, Waziri Mkuu wa Kenya, ni Mjaluo, tatizo liko wapi? Huyu mmoja ni Mjaluo wa Tanzania, mwingine ni Mjaluo wa Kenya. Yuko ndugu yetu Edward Ngoyai Lowassa, ni Mmasai, yupo Saitoti wa Kenya, ni Mmasai, tatizo liko wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kongo-DRC, kuna khabila la Wabembe na mimi nawasiliana na Mbunge mmoja ambaye ni Mbembe, anaitwa Hanzuruni, tunawasiliana kwa simu kila mara na mimi ni Mbembe, lakini aliyewahi kuwa Rais wa Kongo Brazzaville, Pascal Lisuba, ni Mbembe, lakini utakuta watu wa Uhamiaji Kigoma, atakayekuwa Mbembe anahesabika ni mtu wa Kongo-DRC, nani kawafundisha hili? Kwa nini wanawafanya watu katika nchi yao waishi kwa matatizo? Tunao Wamasai, wako mpakani mbona hawasumbuliwi? Tunao Wajaluo wako mpakani, mbona hawasumbuliwi? Mpate mtu kwa tatizo lake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Rais hapa sisi, Rais wetu Mpendwa Mkapa, Mmakua na taarifa nilizonazo aliyekuwa Rais wa Malawi, alikuwa ni Mmakua, tatizo liko wapi? Sasa vijana wa Uhamiaji Kigoma, hawafanyi kazi yao kama inavyotakiwa. Mimi ninaomba Serikali ilitazame kwa undani kabisa suala hili, hasa Mheshimiwa Waziri, lifunulie macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza imelia, ngoja niende haraka. Mimi nilipokuwa Mkuu wa Wilaya, Handeni mwaka 2004 ilitolewa Sera ya Magereza ya

Kuhuisha Kilimo cha Mhogo na yakateuliwa Magareza Kumi (10) likiwemo la Handeni na Gereza la Ilagala ambalo liko kwenye Jimbo langu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie mkakati wa kuendeleza zao hili umefikia wapi, kwa sababu wenzetu wa Mikoa ya Kusini, kuna wakati waliwahi kupata fedha nyingi kutoka Ujerumanini kwa kuza mhogo, sasa Mgereza walichaguliwa kama ndio chuo cha mafunzo kwa zao la mhogo, ningependa nifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la Polisi wenye vyeo vya chini, wanajaariwa kama watu *temporary*, yaani kama vibarua hivi. Tungeomba na wenyewe waingizwe kwenye mfumo wa pensheni ili wawe na uhakika na raha ya kazi yao, vingenevyo watakuwa wanafanya kazi huku wamenyongea maana lazima wajilinganishe na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho japokuwa si kwa umuhimu, ni suala la wale wanaokwenda kuwasilisha kesi Mahakamani. Japokuwa sasa imefutwa lakini kwa sababu linaondolewa kwa awamu, bado wapo. Wenzao wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanapewa pesa ili waonekane nadhifu, karibuni shilingi laki tatu (Sh.300,000) hivi; lakini nimefahamishwa kwamba, hawa wa Polisi wanapewa takribani shilingi elfu hamsini (Sh.50,000), shilingi elfu hamsini, kwa maisha yalivyo sasa na mtikisiko wa uchumi wataonekana *smart* kiasi gani? Kwa hiyo, naliomba Jeshi la Polisi kuitia Waziri, liwezeshwe ili wale Ma-DPP wapate sare zinazolingana na hadhi yao, ili kuwafanya waonekane pale Mahakamani kwamba wana hali ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umesema kuna mwingine naye anapewa nafasi na mimi nisiwe mchoyo, natamka kwamba, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru kwa kuacha kuwa mchoyo Mheshimiwa.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, endelea.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Kanuni ya 64 (1) (a).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Riziki, alipokuwa anatoa mchango wake, alikuwa anazungumzia kuhusu Jeshi la Polisi kushindwa kufanya kazi pale walipotumwa kwa sababu walikutana na kikosi cha JKU au KMKM na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi za Polisi tunavyozifahamu hasa wanapopewa amri, huu ni udhalilishaji, naomba Mheshimiwa Mbunge, athibitishe kuhusu kauli yake hii au afute, kwa sababu kama kweli Polisi walishindwa, basi maana yake wameshindwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshajifunza na kwa wengine, unapoita Muongozo wa Spika, ni wakati yule anayehusika anazungumza, mtu ameshakaa huko unasema Muongozo wa Spika tena, Muongozo upi sasa? (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimeishajifunza sio kwa Hafidhi Ali peke yake, hata kwa wengine unakuta walishamaliza kuzungumza, wamekaa, wameenda zao nje, anasema Muongozo wa Spika. Muongozo wa Spika, unakuwa pale mtu anapozungumza, tunasimama Muongozo wa Spika, pale ndipo Spika ana-*catch the eyes*, kwa hiyo, si hivi.

Kwa hiyo, nitamwita anayefuata Maulidah Anna Komu.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa na mimi nafasi hata kama ni dakika chache, nitoe yangu machache niliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajali nyingi sana zinatokea sasa hivi, ajali hizi kama walivyoeleza wenzangu huko nyuma, maana unapokuwa wa mwisho kawaida kila kitu, unakikuta kimeishazungumzwa, zinasababishwa na uzembe na pia raia wetu hawaelewi Sheria za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mshangao wangu unakuja kwenye tabu hili la bajeti ambalo ni *Volume II, subvote* 2009, eneo la trafiki, nimengalia hakuna kabisa fungu lililowekwa kwa ajili ya *printing* na *advertisement*. Sasa mimi hili linanishangaza kwa sababu, nafikiri ingekuwa ni vizuri zaidi tukarudisha elimu ya mwendo wa usalama barabarani na pia tukaeleza kwenye TV na redio, tukawafunza watu wetu wakiona basi linakwenda *speed* ana haki ya kusimama na akikutana na Trafiki naye, atoe taarifa kwamba, hili gari linatembea kwa *speed*. Kwa hiyo, ninaomba baada ya hapa tutakaposhika mafungu, Mheshimiwa Waziri aniambie au kama wameweka eneo lingine, haya mambo ya pesa ya kusaidia kwenye mambo ya *advertising* ya matangazo ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa anatukanya kwamba, tusilee watoto wetu kwa video na TV, kwa sababu wanakwenda nje ya maadili ya Watanzania, lakini sasa kuna jambo ambalo linaendelea kutokea katika nchi yetu, tena si Dar es Salaam, si Mkoa gani, ni Tanzania nzima sasa hivi. Kuna wananchi wanaojiita wana hasira kali, hawa wananchi inachoonyesha kwamba, wamekosa kabisa imani na Jeshi lao la Polisi. Hili Jeshi lipo kwa ajili ya kulinda mali zetu na kutulinda sisi, kwa sababu wao wamekosa imani kabisa, wanaona hata wakimpeleka mhalifu mahali panapohusika hachukuliwi sheria yoyote, kwa hiyo, wanachukua sheria mikononi na wanafanya mambo mabaya sana, ya mateso mabaya sana kwa wale wanaokamatwa kwamba, ni vibaka na pengine wengine wala hawamo humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeishaona kesi moja mtu amefumanipa tu, ati amesimama na mke wa mtu, yule baba alikuwa anamvizia muda mrefu, alimnadi mwizi

palepale, watu hawajauliza kaiba nini, wala nini? Yule kijana alipigwa mwisho akatiwa na michongoma mikavu akatiwa moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu kama hivi vinapotokea vinakuwa ni vitu vya ajabu na kitu ambacho nakipigia mimi kelele, wakati jambo hilo linatokea watoto wapo na wanasaidia, wengine kushika mawe na wengine wanasogea kwenda kuzomea na kupiga. Sasa hawa watoto tunawafundisha nini? Tunawafundisha kwamba, baadaye na wao watakuwa ni watu wenye roho mbaya, wenye roho ngumu, kwa hiyo kupiga watakuwa wanaona ni kitu cha kawaida, kwa sababu hawajasoma kwenye TV, wala Video, wameona *live*, maneno ya wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba Jeshi la Polisi, ndugu zanguni, tafadhalini, chonde, chonde, chonde, hii pesa ndogo ndogo itatifikisha kubaya na naiomba Wizara na Serikali yote iwaangalia sana hawa Mapolisi, kama kuna uwezekano tutasema kila siku Sungura, Sungura, Sungura, hawi Tembo, ni Sungura tu. Tuangalie njia ya kuweza kuwasaidia hawa ili waweze kujimudu, waachane na visenti hivi ambavyo ndiyo vinatoa imani kwa wananchi kwamba, wakihongwa kidogo bwana, mhalifu asubuhi unamkuta barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nataka nizungumze hasa kuhusu magari, kuna kitengo maalum kilichowekwa kwa ajili ya matengenezo ya magari. Polisi wetu wanalamika sana kwamba, vifaa vya kufanya kazi ni vichache, havitoshi. Sasa, hivi vifaa havitoshi, lakini hapo hapo nimeangalia kwenye kitabu hapa, kwenye matengenezo ya magari hakuna pesa za kununulia vipuli, wala hakuna pesa ya matengenezo ya magari hayo, sasa haya magari yanatengenezwa kwa kutumia vipuli gani? *Medical Unit* wamewekewa dawa, lakini wao wanaoangalia vitu muhimu kama hiyo *medical*, kwa sababu *medical* inamuangalia Askari anapoumwa au mke wa Askari, au mtoto wa Askari na gari ambalo linakuja kunishughulikia mimi ninaposema kwamba, nimeingiliwa na majambazi litashughulikiwa na kipuli kipi? Sasa naomba pia Waziri aniambie kifungu gani ambacho imeweka fedha ya hivi vipuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa vitambulisho. Tunapopiga kelele humu ndani kuhusu vitambulisho, naomba tueleweke. Ni kitu muhimu sana, siku wanakamatwa Wasomali sijui wadudu gani wale, kule Kigamboni, nilikuwa maeneo hayo kwa sababu nina maeneo naishi kule mimi. Wamejazwa kwenye magari, wamekwenda wamekutwa kwenye mikoko wamejificha, wale waliweza kushikwa, wale ambao hawakushikwa, wamezagaa huku kwenye miji yetu hasa maeneo ya mipakani, tumejaza watu ambao si raia wa nchi hii na wanashiriki kwenye mambo mabaya sana ya uhalifu katika nchi yetu. Hivi vitambulisho jamani kuna siri gani? Kuna nini hasa kimejificha humu ndani ya hivi vitambulisho? Kuna matatizo gani, vitambulisho hivyo vinamaliza miaka utafikiri umri wa mwanadamu? Naomba sana Wizara inayohusika hii ya mambo ya Ndani, tuache kila kitu jamani tuangalie hivi vitambulisho, watu ambao wamejaa humu katika nchi yetu sio sote raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninashauri, zamani Mjumbe wa Nyumba Kumi, ambao mnao ninyi kwenye Chama Tawala, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, wahanishwe hawa. Zamani walikuwa wanapewa kabisa utaratibu wa kazi zao za kufanya, mgeni anaingia kwenye mtaa, ajulikane, yeze Mwenyekiti wa Mtaa, asione tabu maana kachaguliwa kwa kura za wananchi wale, aende akagonge mlango jamani nimeona mgeni hapa, ametokea wapi? Awe anajua wageni wangapi wameingia kwenye mtaa wake na wamekuja kufanya nini na wanaondoka lini? Wakishirikiana na Wenyeiti hawa, tutaweza kupata na kujua, akina nani ni wageni na wameingia wanataka kufanya nini? Kwa sababu hawa wanapokuja, wanafikia kwenye majumba yetu, hawafikii barabarani na hata kama wanalala barabarani kuna Askari wanafanya doria usiku, watawakuta, watawauliza ninyi mmelala hapa hamna pa kukaa? Kwa hiyo, naomba sana Wizara inayohusika ishirikiane na Wenyeiti hawa, ili tuweze kuwajua hao wageni wanaoingia na kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeja wageni, *permits* zinatoka kiholela, Wachina wanafanya kila aina ya kazi, mpaka tunawakamata kwenye ukahaba huko, tunawakamata huko vichochoroni huko, ni vitu vya ajabu viko kwenye nchi hii, sijui wenzetu hawa ambao tumewapa madaraka haya, kutuangalia kwenye mambo haya, wanafanya nini. Kwa kweli naomba, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, atujulishe kuna nini? Kama ni kusaidiwa jamani, basi tuisaidiwe mpaka na sisi tukasaidia mpaka vitu vya ajabu, tuisaidiwe lakini tusiambiwe na sisi tulipie kitu fulani, tusiwaonee haya hawa, wanakuja katika nchi yetu, wanachafua hali ya hewa, tuwafukuze, tuwatoe, kwa sababu sisi kwao hatuthubutu hata kuoa, ukienda huko ukisema unataka kuoa, unaambiwa, aah huku hapana, huku ni sisi kwa sisi tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Kwanza, nashukuru kwa kuokoa muda.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu unaofuata. Toka asubuhi, kumekuwepo na wageni katika nafasi ya Spika, *Speaker's Gallery*, bahati mbaya hatukuwatambulisha. Mmoja ni mwakilishi wa *UNHCR* Tanzania, anaitwa Bwana Yakoub Elhilo, yeze amefuatana na wenzake, mwingine anaitwa Profesa Rutinwa na mwingine anaitwa James Tremon, Karibuni sana, tumefurahi kuwa na sisi hasa wakati huu tunapojadili Wizara ambayo ninyi mnafanyia kazi, karibuni sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, endelea.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Kanuni ya 68 (1) na Kanuni ya 64 (1) (a).

**NAIBU SPIKA:** Inasema nini?

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Kuna Mbunge mmoja hapa, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, alipokuwa akichangia alisema kuwa, mimi sijachukua kitambulisho changu, mie kitambulisho changu ninacho. Ninaomba kwanza afute usemi wake halafu aniombe radhi. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mimi naona mmechoka kazi, kama una kitambulisho chako, tunafurahi, tutaaingalia baadaye utaratibu.

(*Hapa Mhe. Shoka Khamis Juma alinyoosha juu kitambulisho*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapa sio sokoni, ukinyoosha hivyo, sisi tutaonaje? Lete hapa.

Mheshimiwa Mbunge, kama unaomba utaratibu unasiliza, kama una kitambulisho chako wewe unawasilisha kwa Katibu, sio unaonyesha hivi hapa, mimi nitaonaje hivi? (*Kicheko*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitakileta hapo. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Yaani wewe unafikiri unaweza kutembea kuleta hapa, huruhusiwi mpaka umwambie Mhudumu. (*Kicheko*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu kwa kunijalia uzima ili nami niweze kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri pamoja na wataalam wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la wahamiaji haramu. Kumekuwa na wimbi kubwa la wahamiaji haramu katika nchi yetu. Maeneo yanayoingiza wahamiaji hawa ni Namanga, West Kilimanjaro, Rombo Tarakea Holili n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, ijapokuwa Askari wapo mpakani lakini bado wageni wanavuka na kuingia nchini Tanzania. Kuna watu ambao si waaminifu huwavusha na wakishaingia humu, huwa wanalipwa tena kwa dola. Hivyo, wahamiaji hawatapungua ikiwa Tanzania wenyewe ndio wamefanya kuwa mradi wao. Kuna haja ya kuwaelimisha Watanzania ili waelezwe athari za kuwaingiza wageni haramu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea Gereza la Manyara, nikawakuta wageni wengi sana. Kwa bahati nzuri, wale waliowavusha, walikamatwa. Hivyo, ni vema kuendelea kuimarisha ulinzi mpakani. Kwa nini Serikali isiongeze vituo vingi mpakani ili kudhibiti na zile njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Taveta ni hatari kwa wahamiaji haramu. Soko hili la Taveta lina-*operate* siku za Jumamosi ambapo watu wote kutoka Kenya Tanzania wanapita mpakani bila kuulizwa kitambulisho wakidai kuwa wanakwenda sokoni. Je, siku hiyo ya soko si ndiyo wahamiaji wengi wanapita mpakani wakijidai kuwa nao ni wazawa au Watanzania? Nasisitiza vituo mipakani viongezwe nguvu na viimarishwe zaidi na wale wanaowavusha kwa kuwafanyia biashara wathibitiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uingizaji wa miraa. Kwa kuwa nchi jirani ya Kenya ni wazalishaji wa zao hili na walaji ni sisi Watanzania, Askari wapo mipakani wanazuia lakini miraa inaingizwa nchini kwa wingi hasa Arusha, Singida, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga na kadhalika Kuna watu maalum wanafanya kazi hiyo. Kwa nini Serikali isisitishe zoezi la kuzuia badala yake walipe ushuru ili Serikali iingize mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uraia. Kwa kuwa Serikali imeweka Sheria ya kuukana uraia wa nchi yako ili uweze kupata uraia, je, wageni walioishi hapa nchini zaidi ya miaka 10 na ambao wamewekeza kwenye miradi ya kudumu ya maendeleo, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia uraia bila kukana uraia wa nchi yao?

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema. Pia nitumie fursa hii, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Lawrence Kego Masha (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Mheshimiwa Balozi Alhaji Kagasheki (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Kamanda *IGP*, Ndugu Said Mwema, watendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Makamanda na Askari wote wa Jeshi la Polisi, kwa shughuli wanazozifanya za ulinzi, usalama wa raia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana kutokana na majukumu yanayotokana na taasisi zake, kama vile Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji. Taasisi hizi ni taasisi nyeti kwa maana zinagusa jamii moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie na Jeshi la Polisi, nashukuru dhamira nzuri ya uanzishaji wa Polisi Jamii (*Community Policing*). Dhana hii ni nzuri sana kwani inasogea mahusiano baina ya wananchi na Jeshi la Polisi. Tangu kuanza kwa dhana hii, kumeongezeka hali ya udhibiti wa wahalifu ambao mara nyingi hujichanganya na jamii na hivyo kuwa vigumu kugundulika kutokana na jamii kuwa na hofu ya wahalifu na pia kuiogopa Polisi na hivyo wananchi kubaki katikati na hofu yao. Dhana hii imerahisisha wajibu wa mwananchi juu ya kushirikisha Polisi katika kujilettea ulinzi na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, bado kuna tatizo ambalo nalionna ni vema likaangaliwe vizuri sana ili kukomesha kabisa japo sio kumaliza kwa ujumla tatizo lakini kwa kiwango kikubwa kulikomesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado yapo matatizo kwa baadhi ya Askari wasio waadilifu ambao wanashirikiana na wahalifu (majambazi) katika matukio mbalimbali ya uhalifu. Naomba *IGP* na *DCI*, waandae utaratibu wa kuwashirikisha wananchi kupitia mpango huu wa Polisi Jamii, ili wananchi wawataje Askari wenye tabia za kihalifu na hawa, ni hasa wasiovaa magwanda (*Detective Police*), kwa kutokuwa na *uniform* huku wakijua sio rahisi kutambuliwa kutokana na kutokuwa na namba inayoonekana basi hutumia mwanya huo katika kujishirikisha katika vitendo vichafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri kushirikiana na *IGP*, *DCI* na Mkuu wa Utawala wa fedha wa Polisi, kuwatoa (kuwafukuza kazi) Askari wa aina hii bila kuwaonea haya kwa kuwa wanalitia doa Jeshi letu (tunahitaji Polisi wenye maadili) kadhalika katika hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Kitengo cha Upelelezi, kizingatiwe. Ni kitengo nyeti sana lazima Jeshi (*IGP*), aone umuhimu wa kuwapatia nafasi hizi wale Askari wasomi na wenye taaluma mfano vitengo kama *Fraud*, lazima awe msomi kwa kuwa kitengo hiki kinahusiana na suala la kugushi, kadhalika uhalifu kupitia mitandao (*cyber crime*), mauaji (*mudder*) na kadhalika. Maeneo kama haya, hayahitaji Polisi mzoefu hapa panahitajika mtu mwenye weledi (*professionalism*) na sio suala la kupapasa kwa kugezesha matukio yaliyopita. Kuendelea kupachika Polisi wa aina hii, ni hatari, tutaonea watu na kuwatia katika hatia pasipo uchunguzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uhamisho wa MaPolisi (kukaa eneo moja kwa muda mrefu). Ninao ushahidi, mfano Kituo cha Chang'ombe Temeke na *Police Central*, wapo Polisi nawafahamu tangu nasoma nikiwa mtoto na baadaye nikaja kumwona *IGP* Mwema akiwa *RCO* Dar es Salaam, akahamishwa kwenda Mbeya na baadaye *Interpol* na kurejea tena kuwa IGP lakini bado wapo katika vituo hivyo, sitaki nitaje majina, fanyeni uchunguzi (kukaa kwao muda mrefu wamegeuza vituo hivyo kama mali yao). Kadhalika tatizo hili lipo Mikoani, Wilayani na hata vituo vya Kata na kadhalika sio vema kuwaweka Polisi kituo kimoja kwa muda mrefu maana wanapakazia hata kulindwa eti na baadhi ya viongozi wa Jeshi Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya Vituo vya Polisi vya Shelui Ndago, Kinampanda na Misisiri. Vituo hivi ni sawa na mtu bubu kumpa kazi ya kuwasilisha mada katika semina wakati hataongea. Vituo hivi, ni vituo na vina Polisi lakini havina silaha kutokana na kutokuwa na sehemu ya kuhifadhia silaha. Kitendo hiki, mara zote hasa matukio yakitokea Polisi hawako yatari kwenda eneo la tukio kwa kuhofu usalama wao. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati akijumuisha mjadala, anieleze ni lini vituo hivi vitapatiwa silaha? Kituo cha Shelui, kwa nguvu za wananchi wamejitalidi wamejenga kituo, naomba Wizara imalizie hatua iliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kianzishwe kituo cha Polisi eneo la Tulya (ziwa Kitangiri) ambapo kuna Kata za Kidaru na Ntwike. Maeneo haya ni hatari sana kwa kuwa ni maeneo ya wafanyabiashara wa samaki hivyo mara zote kuna wageni wasiojulikana wanakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *IGP* awe macho na Askari wa Usalama Barabarani ambao wamekithiri kwa rushwa. Mbaya zaidi wanajihuisha na rushwa ndogo ndogo ambapo ni kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi ishirikiane na mamlaka husika katika kulinda na kudhibiti matumizi ya barabara kwa barabara za mijini mfano barabara za Dar es Salaam na kadhalika. Udhibiti huu utaongeza mapato ya Wizara na pia kutapunguza uholela wa Madereva na kufanya matumizi ya barabara kuwa na sura nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Kwa kuwa Waziri aliyekutangulia, aliahidi kujenga Kituo cha Polisi pale Kipatimu Kilwa kwa kuwa hali ya uvunjaji wa sheria umekithiri sana, je, Serikali inalifkiriaje suala hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Somanga Kilwa, kimeshajengwa kwa nguvu za wananchi kwa asilimia 75 na kwa kuwa ujambazi kati ya Ndunu – Somanga umekithiri, je, Serikali haioni busara kumalizia asilimia 25 iliyobakia?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii, kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kudhibiti uhalifu nchini na kushiriki katika uzalishaji chakula kwa kuwatumia Askari na wafungwa japo bajeti haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Gereza la Molo na uongozi wa Magereza Mkoa wa Rukwa, natoa shukrani za dhati kwa Gereza la Molo kupewa *planter*. Sasa Gereza hili linazalisha mbegu ya mahindi. Mwaka huu wamelima hekta 200 za mbegu bora licha ya kulima mahindi ya chakula. Hii ni hatua nzuri. Lakini nichukue nafasi hii kukumbushia ombi la *harvester* ili kazi ya *planter* imaliziwe na *harvester* kwa kuvuna mahindi kwa wakati bila wao kuchomewa mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbanano wa mahabus/wafungwa, ni mbaya sana. Kamati ya masuala ya Ukimwi ya Bunge, ilitembele Gereza la Ukonga na kushuhudia mahabusu wanavyobanana kama kumbikumbi hivyo wanalazimika kulala muda wote na kugeuzwa kwa amri kwani hakuna uwezekano wa kukaa. Mwezi Mei, 2009, katika Gereza hilo, Mahabusu na wafungwa walimuonesha Askari aliyemuwekea mfungwa biki mkunduni mpaka ikaingia yote. Japo uongozi wa Gereza ulisema Askari ataadhibiwa; mimi nasema vitendo kama hivyo ni unyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wanaowekwa selo wakiwa uchi, wana hatari kubwa ya kuambukizana Ukimwi. Nia ya Serikali ya kutaka wasijinyonge, ni nzuri lakini nashauri Serikali kujenga selo ya mtu mmoja mmoja ili kuepusha wafungwa hao kufanya *sex* na kuwa katika hatari ya kuambukizana Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya vizuri sana kuongeza Askari Mkoa wa Rukwa. Inasemekana vijana wengi wa mjini Sumbawanga huvuta bangi. Ni wazi Askari watasaidia kupunguza uhalifu huo na kujenga jamii yenyе akili timamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukosefu wa magari imara, upungufu wa mafuta, ni matatizo sugu katika baadhi ya Wilaya mfano Meatu, yenyе matukio mengi ya ujambazi, wizi wa mifugo, mauaji ya Albino, mauaji ya vikongwe na usafirishaji wa washtakiwa kwenda Gereza la Wilaya jirani. Kwa kuwa tatizo hili, tumeliripoti mara kwa mara, lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa na Wizara. Je, Waziri anawaambia nini wana Meatu wanaoibiwa na kuuawa bila msaada?

**MHE. FATIMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu kuhusu Wizara hii.

Kwanza, naomba niwaarifu kuwa, Gereza la Segerea lina matatizo makubwa ya maji. Inafika hatua wafungwa na maabusu wanakunywa maji mara mbili tu kwa siku, sio kila mfungwa anapoona kiu anapata maji ya kunywa. Hii ni hatari kwa wafungu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Magereza yapo katika hali ya kusikitisha. Niliwahi kutembelea Gereza la keko, nikashuhudia jinsi wanavyolala usiku, nilitoka machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona Polisi wamejiingiza ndani ya siasa, jamii ya ulinzi yote haitakiwi kujiingiza katika siasa. Polisi vijijini huwa wanapewa maagizo wakamate wananchi wasio na hatia hasa waliojiunga na Vyama vyta Upinzani. Kwa mfano, kuna Diwani wa Kata ya Mgembе kwa kupitia CUF, Polisi wamemkamata na kumbambikia kesi kuwa anaiba watoto na kuwauza Uganda. Kweli hii ni halali?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni la Askari Traffic na naongelea wale walipo Dar es Salaam. Askari hawa naomba wapewe semina namna ya kuwashughulikia Madereva wa daladala. Madereva hawa, wanavunja sheria na kusabisha ajali na vifo vingi. Madereva hao, wakikamatwa na kuadhibiwa basi wengine wangefuata sheria na ajali zipungue barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Askari mmoja kule kwetu Pemba ambaye alifariki kama miaka mitatu iliyopita. Ndugu na jamaa wamejaribu kufuatilia mafao ya marehemu huyu hadi leo hivi hawajafanikiwa. Amefariki akiwa ameacha watoto wengi wao wakiwa wadogo na wachanga. Naomba wafiwa wapewe haki yao ili waweze

kusomesha mayatima. Jina lake ni Hamadi Abeid. Namuuliza Waziri, hata haki lazima udai? Kama ndio, naomba nidai haki ya marehemu huyo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongozi nydingi kwa machapisho mbalimbali ya Polisi kuelimisha jamii. Naomba Majeshi mengine yaige.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliahidiwa kumalizia ofisi ya Polisi Wilayani Nkasi ya tangu mwaka 1983 ili ifunguliwe, naomba ahadi hiyo itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari la Polisi Nkasi, hatuna kabisa, naomba tupewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Uhamiaji mbona ahadi ya kuwa Jeshi bado haijatekelezwa, ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza Nkasi hawana gari na wanakaa mbali na mji. Pia hakuna mahabusi kabisa na Askari hawana nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo kuhusu hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau, naomba kwanza usafiri kwangu yaani Jimboni kwangu Bukene. Kama nikipata *Landrover* mbili yaani kila Tarafa ambayo ina Kata nane nane, *Landrover* moja, Tarafa ya Bukene *Landrover* moja na Tarafa ya Makalundi gari moja. Tarafa hizi ni kubwa sana na ziko mbalimbali sana maporini. Mfano kituo kiko Bukene Centre, tukio la wizi/majambazi likitokea Semembela au Maambali – Mbutu au hata Kahama ya Nhalanga, shida kufika na kuyakamata bila usafiri. Kuwa misingi hiyo, naomba kama siyo basi tupatiwe pikipiki. Naomba kusisitiza kwamba ijulikane gari/pikipiki hiyo inaletwa Bukene ili isiishie Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata nafasi kutembelea Gereza la Keko mwezi Mei, 2009 kama Kamati ya Ukimwi, mimi nikiwa mjumbe mmojawapo. Kitu ambacho niliona yaffaa, Serikali ibadili utaratibu wake ili kuepusha au kupunguza maambukizi ya Ukimwi, ni kupunguza wafungwa/mahabusu hapo, kwani wako wengi mno. Chumba kimoja wanalala zaidi ya watu wanaotakiwa kulala humo. Wanalala wamebebana kweli kweli. Sasa mtu anaweza, hana nia mbaya ila kwa sababu hana “kasoro” ile kitu inasimama kwa ajili ya kugusana hivyo mambo mabaya ya kufanyana, yanatokea. Kumbuka hapa kuna watu wa rika tofauti, ndio maana wanaambukizana magonjwa si ya Ukimwi tu bali hata magonjwa ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu hawa, wanapewa adhabu za kukaa uchi watatu au watano kwenye vyumba hivi na kwa kuwa hawajakutana na wake zao kwa muda, basi wanajamiiiana wao kwa wao. Askari walituambia wanawaacha uchi kwani wakiwa na nguo hutumia kujinyonga na wanawaweka katika namba tasa yaani 3,5 na

kadhalika. Lakini si tija, wao wanakubaliana kujamiihana katika *style* yao ya utatu au utano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vijengwe au vikatwe vyumba vidogo vidogo ili kila mtu anayepewa adhabu awekwe peke yake. Kwa wale wengi basi kesi zao zisikilizwe haraka ili watoke au wapewe kifungo cha nje. Kuna wengine wanawekwa kijiti/kalamu yote mkunduni na kadhalika. Nashauri adhabu kama hizi ziachwe kwani Magereza yetu lazima yafuate haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposafiri, utakuta matawi/majani ambayo yamewekwa kama alama kwamba kule mbele kuna gari bovu, lakini wakishatengeneza hawashughuliki kuondoa matawi/majani wakati mwingine ni makubwa sana kama chaka. Nashauri “*traffic*” wakague gari zote kama zina vifaa vyta kisasa vyta kuweka alama mfano ya ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia elimu inahitajika kwa wananchi wote watumaji wa barabara kama waenda kwa miguu, baiskeli na gari, hasa kwenye “*Zebra*” unakuta baiskeli zinaji –*overtake* mbili au tatu na gari inakuja. Lazima baiskeli ijue inatakiwa kuwa kando kando ya barabara na si vinginevyo hasa kwenye “*High way*” na “*Zebra*” na gari ikisimama unavuka haraka sio tena kwa maringo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na viongozi wenzake, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayofanya.

Aidha, nampongeza *IGP* na Makamanda wote wa Polisi, kwa kazi nzuri ya Kikatiba wanayofanya. Nakubali sifa “*image*” ya Polisi imeanza kuwasawili tangu uongozi mpya wa Jeshi uchukue madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo. Kwanza, utamaduni wa kuweka watu ndani halafu upelelezi ufuate zaidi Wilayani na Vijijini, utamaduni huu unasaidia sana kujaza Magereza na Mahabusu na wengi hawana hatia. Ukiondoa kesi kubwa za mauaji na majambazi, watuhumiwa wengi walio mahabusu kama Mafina Bariadi, wangeweza kuwa nje na huku kesi zao zinapelelezwa. Mtindo huu unachafua jina la Jeshi na ni chanzo cha rushwa. Napendekeza utamaduni huu uangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, operesheni za Jeshi, ni eneo lingine linalohitaji kuangaliwa upya. Operesheni ya Kilosa kuondoa wafugaji na baadaye wakakosolewa, siyo sifa kwa Jeshi, kwani Jeshi linaonekana ni la kisiasa. Jeshi kutumika kuondoa Masai Loliondo ili kumpisha mfanyabiashara kwa kuchoma makazi na kuwashamisha kwa nguvu bila kuwa na makao mbadala, inalipa Jeshi uadui na raia ambao Kikatiba wanapaswa kuwalinda wao na mali zao. Kama ni mgogoro wa kibashara, migogoro hii iende kwenye “*civil councils*” na si kazi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ukamataji hauna misingi inayoelewaka. Kama Mgodi wa North Mara ungekuwa unaendeshwa na Mtanzania na Serikali, halafu ikawa mgodi umetia sumu kwenye mito na watu wameumia na wengine kufa, operesheni funga mgodi ingekuwepo na Meneja angekuwa ndani lakini kwa hawa ni Wazungu, upelelezi kwanza halafu kukamatwa baadaye. Watu wote tu sawa mbele ya sheria mbona hii haionekani sana kwa wageni?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulisongeza Jeshi la Polisi kwa kuanzisha ulinzi shirikishi. Hii imesaidia kupunguza uhalifu katika mitaa/vitongoji/vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomuomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kuhusu vile vituo ambavyo vilijengwa katika miaka ya 1980 – 1990 kwa nguvu za wananchi. Vituo hivi vilijengwa kila Kata, kwa hiyo, kila Kata ilikuwa na kituo ambacho wahalifu walipelekwa. Hii ilisaidia kupunguza msongamano wa wahalifu katika vituo vikuu vya Polisi. Cha kushangaza vituo hivi sasa hivi vimetelekezwa, havitumiki na vimegeuka ni makazi ya vibaka na majambazi na vituo vingine hubomolewa milango na madirisha na kubaki magofu. Namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni sababu zipi zilizopelekea kutelekezwa kwa majengo hayo? Kisingizio ni ukosefu wa Askari kumbe Askari hao hao wanaokosekana muda wote huu wanaweza kupatikana kipindi cha uchaguzi! Kwa nini hao Askari wanaoandaliwa kwa uchaguzi, wasiajiriwe mapema na kupelekwa katika kata mbalimbali ili kufufua vituo vingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kupata maelezo kuhusu tatizo lililojitokeza hata wakati mwingine Askari wetu wa barabarani kupigwa kwa kuwachelewesa wananchi katika taa za barabarani. Cha kuchangaza kwa Jiji la Dar es Salaam halina taa za barabarani. Utakuta mara nyingi Askari wa usalama barabarani hawasimami zile sehemu zisizo na taa za barabarani, wanasimama katika mataa na hivi kusababisha misururu ya magari, kwa nini hawaachi taa za barabarani zifanye kazi yake wao wakasimame sehemu zisizo na taa ili waongoze magari? Namwomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu.

**MHE. KIDAWA H. SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kuwapongeza, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara, kwa kuandaa na kuleta bajeti hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, nalipongeza Jeshi la Polisi, kwa kazi nzuri inayofanya ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Jeshi letu hili linajitahidi sana kupambana na uhalifu wa aina zote, uhalifu mdogo na mkubwa. Kati ya uhalifu mkubwa unaosumbua na kukosesha amani wananchi, ni ujambazi na madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi, linapambana vikali na ujambazi na hivi sasa kwa kiasi fulani umedhibitiwa katika baadhi ya maeneo lakini hata hivyo bado tatizo hili lingalipo na linasumbua. Jeshi la Polisi, likijipanga vizuri linaweza. Yapo maeneo

korofi ambayo ni maarufu kwa matokeo ya ujambazi. Katika maeneo hayo, kuwekwe ulinzi mkali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mfano hai wa eneo la Manyoni ambapo mara kwa mara majambazi wanawavamia na kuwaumiza wapitao njiani. Juzi tarehe 5/7/2009, watumishi wa CCM walipokuwa wakirudi kutoka Biharamulo wamevamiwa, wamepigwa na kuumizwa na kunyang'anywa kila walichokuwa nacho kuanzia simu, pesa na kadhalika. Tunamshukuru Mungu kuwa hawakuwaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi, katika Kisiwa cha Unguja, huko Zanzibar, tatizo la wizi wa kutumia silaha za moto katika visiwa vya Unguja na Pemba, ni jambo geni kabisa. Wizi ambao umezoleka na unaojulikana ni wizi wa kutumia silaha za kienyeji kama vile visu, mapanga na sio bunduki, pistol na kadhalika na wizi hasa ni wa mazao, ndizi, nazi na vitu kama hivyo sio wa kuiba benki, *Bureau De Change* na maduka makubwa makubwa. Wizi wa majumbani ulikuwepo lakini ni ule wa kuvunja milango kwa kutumia tofali liitwalo Fatuma sio risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni zimetokea kesi kadhaa za ujambazi wa kutumia silaha za moto kule Zanzibar na kesi mbili ambazo zimetokea karibuni sana ni ile ya ujambazi wa kuua mtu mmoja katika soko la Mwanakwerekwe na nyingine imetoka katika kituo cha mafuta ambacho kipo jirani ya kituo cha Polisi hapo hapo Mwanakwerekwe, tukio ambalo Askari wawili waliokuwa wanalinda wameuliwa. La kusikitisha ni kwamba majambazi hawa hawakupatikana na kuadhibiwa kisheria. Zanzibar ni kisiwa na eneo lake sio kubwa, hivi kweli Jeshi la Polisi limeshindwa kudhibiti au kuwakamata wahalifu hawa? Hivi majambazi hawa wanawezaje kutoroka na matendo wameyafanya mchana kila mtu anaona. Naomba Jeshi la Polisi lijipange vizuri, lipatiwe vifaa vya kutosha vya mawasiliano mfano *radio call*, ili kurahisisha mawasiliano na kuwakamata wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa ya kulevyta, moja kati ya kero za wananchi, ni dawa za kulevyta. Vijana wetu wengi ambao ndio nguvu kazi ya Taifa, wanaathirika kwa kutumia madawa haya. Polisi iendelee kupambana na tatizo hili, wananchi wanalamika, hawaoni jitihada zinazofanywa na Serikali kupambana na tatizo hili na hata wanafikia kusema kwamba kwa kuwa watoto wa wakubwa hawaathiriki na tatizo hilo, ndio maana hawashughulikii ipasavyo, wanachukua jambo hili kama jepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya bandari na viwanja vya ndege na barabara zinazounganisha mataifa, zinajulikana hivi kweli tunashindwa kuweka ulinzi na uchunguzi wa kutosha wa kufuatilia madawa ya kulevyta yanayoingizwa nchini? Isitoshe maeneo yanayouzwa madawa haya kwa vijana humu ndani yanajulikana, ni uchunguzi mdogo tu wa Polisi utagundua haya maeneo. Kwa nini Jeshi hili halichukui hatua ya kufanya msako na kukamata hawa wahalifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazohusika na madawa ya kulevyta zifanyiwe mapitio na zirekebishwe ili wahalifu hawa wakikamatwa wapatiwe adhabu kubwa kwa

sababu ni wauaji, wanaharibu na kuua watoto wetu. Aidha, ofisi na maabara za Wakemia Wakuu Bara na Zanzibar zipatiwe vifaa vya kisasa na vya kutosha ili wafanye kazi zao za kuchunguza madawa haya kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Zanzibar, huduma za Jeshi la Polisi zinatakiwa ziende sambamba na ukuaji wa maendeleo na uwekezaji. Zanzibar sekta ya utalii inakua, maeneo mengi hasa ya fukwe yamejengwa mahotelii makubwa ya kitalii, katika maeneo hayo kunahitajika sana kuwe na vituo vya Polisi ili kuzuia uhalifu wowote wanaoweza kufanyiwa watalii lakini pia raia wanaoishi katika maeneo hayo. Aidha, zipo barabara mpya nyingi tu ambazo zimejengwa kwenye barabara hizo ni muhimu pia kuwa na vituo vya Polisi ili kuzuia uhalifu kutoka “*point*” moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kisiwa cha Pemba eneo la Mnarani Makangale, Tumbe, Kinyu na eneo ambalo imejengwa hoteli ya Mauntarif, maeneo haya yapo jirani na mji wa Shimoni Mombasa. Katika maeneo haya, kunahitajika ulinzi wa kutosha ili ukaribu huo usiruhusu raia wa kigeni na wahalifu kuvunja sheria kwa kuingia nchini kwetu bila ya kufuata utaratibu na kuweza kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada iendelee ya kujenga nyumba za makazi ya Askari. Mkoaa wangu wa Kaskazini, zipo nyumba 23 za Askari, ni idadi ndogo sana kulingana na idadi ya Askari. Hivyo, Askari walio wengi wanalazimika kuishi katika nyumba zao na jamaa zao za kukodi uraiani, sio jambo jema kwa Askari. Aidha nyumba zilizopo, zifanyiwe ukarabati wa mara kwa mara ili zioneshe taswira nzuri za Jeshi la Polisi. Ikiwa raia wanaishi kwenye nyumba nzuri na nzima kuliko Askari, Jeshi letu hilo linadhalilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linatakiwa liwe “*mobile*” kwa maana ya kufika katika maeneo ya matukio, sehemu za malindo na maeneo mbalimbali yanayohitaji ulinzi wa doria. Jeshi la Polisi maeneo mengi ikiwemo Zanzibar, hawana magari wala pikipiki za kutosha na hizo chache walizo nazo ni mbovu tunasema spana mkononi. Hivyo, Serikali ijitahidi kuendelea kupanga bajeti kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri kwa Askari vinginevyo wananchi wataendelea kulalamika utendaji wao kumbe hawawezeshwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta, ni muhimu katika utendaji kazi wa Polisi, la kushangaza ni kwamba bajeti ya mafuta kwa kikosi cha Polisi Zanzibar imepunguzwa kwa Sh. 27.9 milioni ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana. Mwaka 2008/2009 ilikuwa Sh. 356.9 millioni na mwaka huu 2009/2010 ni Sh. 329.9 milioni. Tunaongelea Jeshi letu lionezwe ufuatiliaji wa shughuli zake lakini tunawakata miguu kwa kuwapunguzia mafuta, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze sababu zipo zilizopelekea fedha za mafuta kupunguzwa badala ya kuonegezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ipo sehemu inayoshughulika na Mbwa Askari na mbwa hao wapo, lakini la kushangaza kama hakuna gari la kusafirishia mbwa hao kwenda katika maeneo ya matukio, hili ni tatizo. Polisi Zanzibar wapatiwe gari ili waweze kutoa huduma hii ya Mbwa – Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Polisi Marine Unit*, unit hii kwa upande wa Zanzibar inashindwa kufanya kazi zake ipasavyo kutokana na kukosa vitendea kazi, wana boti moja tu tena mbovu. Serikali iwatafutie boti walau ndogo ndogo “*fibre boats*” waweze kuzunguka na kufanya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, “*Identification Bureau*” kwa upande wa Zanzibar bado wanafanya kazi kwa kutumia mbinu za kizamani, kwa karne hii ya sayansi na teknolojia watafanya kazi kwa kubahatisha. Naomba Serikali ijithabidi kuwapatia zana za kisasa na wasifanye kazi kwa kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Polisi Zanzibar, chuo hiki kinachukua wanafunzi kinyume na uwezo wake. Kulitakiwa kichukue wanafunzi 100 sasa kinachukua watu 400. Hii inaonesha dhahiri kuwa kinahitajika chuo kikubwa zaidi chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi. Hivyo, kwenye bajeti ya mwaka ujao, Serikali itenye fedha za kujenga Chuo cha Polisi Zanzibar tena kiwe mbali na makazi ya raia, kwani kilichopo kipo katika makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kunahitajika kujenga ofisi ya kikozi cha FFU Zanzibar pamoja na nyumba za Askari nje ya makazi ya raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara pamoja na Majeshi yote chini ya Wizara hii, kwa kazi muhimu na ngumu sana kwa faida ya Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makazi ya Askari Polisi, nashauri mbinu na mipango mbalimbali itumike kushughulikia uboreshaji wa nyumba bora kwa Askari wote. Askari wetu wengi sana wanaishi kwenye nyumba duni sana. Haikubaliki! Hawa ni walinzi wa mali na rasilimali zetu. Hivyo, hatua za makusudi ziendelee kuchukuliwa za kuwajengea nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Shinyanga mjini, wanaishi katika vijumba vilivyojengwa wakati wa Mkoloni. Inasikitisha kuwa hadi leo karibu miaka 50 ya uhuru, makazi yao ni duni kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za afya kwa Askari. Kwa kuwa Askari, ni kundi maalum katika jamii, ni vema wakawa na maeneo maalum ya kupata huduma kama za afya. Hali bado ni mbaya sana kwa Askari wetu pamoja na familia zao kupata huduma bora za afya. Nashauri wajengewe zahanati/vituo vya afya kwa ajili ya kuhudumia Askari wetu. Mfano pale Shinyanga Mjini, Askari wanapata huduma za afya kutoka inayoitwa zahanati. Haikubaliki Askari wetu na familia zao kupata huduma duni za afya. Namwomba Mheshimiwa Waziri tushirikiane ili hatimaye kuwe na zahanati ya kisasa kwa Askari Polisi na kadhalika pale Shinyanya mjini. Namtakia kila la kheri.

**MHE. DR BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi Tandala (Makete), Serikali kwa kupitia swali langu la msingi lililohusu kuanza kwa Kituo cha Polisi cha Tandala kilichopo Makete, aliahidi kwamba kituo hiki kingeanza mara moja, kutokana na hoja za msingi kwamba, kukua kwa matukio ya ujambazi kijiji Tandala na wananchi wa Kijiji cha Tandala wako tayari kuchangia gharama za ujenzi kama vile vifaa vya ujenzi ili kukamilisha kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo hii, hakuna hatua yoyote ile iliyochukuliwa hata baada ya maagizo ya Naibu Waziri kwamba *RPC* Mkoa wa Iringa ahakikishe kituo hiki kinaanza kazi mara moja. Naomba maelezo ya Serikali kuhusu ufumbuzi wa tatizo hili linalowakabili wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa 100%. Pongezi kwa kazi nzuri kwa IGP na Jeshi zima la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu Jeshi la Polisi linawatumiae Askari wanaopata Diploma/Degree ya Ualimu kama taaluma? Taaluma hii inawasaidia kupanda vyeo?

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lawrence Masha, (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nch, kwa hotuba yake nzuri akiwa na Msaidizi wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Kagasheki (Mb).

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi yoyote, yanategemea mazingira ya amani yaliyoko ndani ya nchi. Nchi ikiwa salama, raia wake wana amani, basi hii ni chachu muhimu katika kuwezesha wananchi kujifanyia shughuli zao kwa ufanisi. Hali ya amani pia ni kivutio kwa shughuli za uwekezaji – wageni wanakuwa na uhakika kuwekeza, watalii wanafurahia matembezi yao na hivyo kuitangaza nchi kule ugenini kwa sifa nzuri ya amani na usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya nchi yetu, kwa hakika si shwari sana imekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu nchini. Uhalifu wa ulevi wa pombe na madawa ya kulevya na uhalifu wa ujambazi, nao umekithiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la ujambazi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, aliliweka kwenye vipaumbele vyake. Utulivu ulipatikana kwa muda mfupi, sasa tumerejea tulikokuwa. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ielewe kwamba, ni kweli jeshi letu la Polisi linaheshimika kwa kazi nzuri inayofanya, lakini katika maeneo yenye kero hasa kero ya rushwa, Jeshi letu la Polisi na Mahakama wametuhumiwa. Naomba viongozi wa Jeshi la Polisi waiweke sawa “*image*” ya Polisi panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Babati Vijijini, tumekuwa na maombi ya siku nyingi juu ya vituo vipyta vya Polisi vya Bashanet km 55 kutoka Babati, Dareda km 32 kutoka Babati, Gidas km 45 kutoka Babati, Galapo km 20 kutoka Babati na Magara km 70 kutoka Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maombi hayo, kituo cha Polisi cha Bashanet ni cha tangu mwaka 2002 mpaka leo. Serikali inatupa matumaini gani ili kukabili uhalifu katika maeneo haya yaliyo mbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya? Naomba Waziri anapojobu hoja za Waheshimiwa Wabunge, anisaidie, ni matumaini gani ananipa kwa ajili ya wananchi wa Babati Vijijini hasa Bashanet.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuajiri Askari Polisi. Utaratibu wa sasa wa kuajiri Askari Polisi na kuwapeleka CCP Moshi kabla ya kwanza kufanya kazi, ni mzuri lakini nashauri vigezo vinavyotumika sana vya namna ya kuwapata vijana hao havitoshi, kwani baadhi yao huwa wanahuksika kwa kushirikiana na watu ambaao ni wahalifu. Hivyo ni vema taarifa za mienendo/tibia zao, zipatikane kutoka kwa Mabalozi/Wenyevit wa Mitaa. Kwa kufanya hivyo, watapatikana Askari wazuri kuliko ilivyo sasa ambaao baadhi yao hupatikana na vitendo vya kushirikiana na wahalifu ingawa huchukuliwa hatua na viongozi wao. Askari wa namna hii hulitia doa Jeshi ha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi liendelee kuborosha nyumba za kuishi Askari. Kwa kweli nyumba za sasa zimepitwa na wakati, kwani ni ndogo mno ikizingatia kuwa wapo Askari walio na familia kubwa, wanaoishi kwenye nyumba zenye chumba kimoja tu kisicho na mlango, hilo husababisha watoto kujifunza mambo ambayo hayastahili kwa umri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwajengea Askari nyumba za *Full Suit* kama zilivyo huko Kibaha – yaani ujenzi wa kutumia mabati chini na kuezeka bati ni kuwatesa Askari kutookana na joto lilivyo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Askari ambaao wamekaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo, jambo ambalo linasababisha kuwepo kwa malalamiko dhidi ya viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nawasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ufuutiliaji wa matukio mbalimbali ya uhalifu bado mdogo, mfano leo ni siku 371 tokea bajeti ya mwaka 2008 na Waziri Mambo ya Ndani kumwandikia *IGP* afuutilie matukio matatu (3) Mkoa wa Singida:-

(a) Mwalimu Abraham Mongo wa Mitundu aliyeteswa na Polisi wa upelevi wa Manyoni;

(b) Bwana Mosi Mungulu wa Filimuli Muhanga aliyeoporwa ng'ombe 38 na Polisi – Manyoni; na

(c) Bwana Mghenji Senge wa Singida aliyedhulumiwa nyumba yake na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo hii hakuna hatua zilizochukuliwa kumaliza matatizo haya yanayonyooshewa vidole Jeshi la Polisi. Pamoja na Kamishna Mtweve na Kamishna Mangu, kuahidi kulishughulikia hakuna kilichofanyika. Nitapenda kupata maelezo kulikoni vinginevyo sioni ni kwa nini Kanuni 103(2) kisichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ahadi iliyotolewa ya kukarabati Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni mpaka leo ni kitendawili. Mheshimiwa Bakari Mwapachu aliahidi kuleta bati kukarabati kituo hicho mpaka leo jengo hilo linavuja, napenda kupata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wananchi hususan wafugaji, bado wanaonewa kwa kubambikiwi tuhuma za kuwakuomoa kutoa fedha. Matukio haya ni mengi katika Kata za Mgandu na Ipande ambapo Mgambo hushirikiana na Polisi kuwawekea wananchi hao bangi, mafuvu ya nyani, nyara/uganga wa kienyeji na hatimaye kuwahukumu kutoa fedha ili wawaachie. Je ripoti ya Jaji Chande kuhusu Ihefu iliishia wapi? Napendekeza ripoti hii iletwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, naomba gari la Polisi Kituo cha Itigi na Mgandu kati ya magari 22 yatakayonunuliwa mwaka mpya wa fedha. Kituo kiko kilomita 240 kutoka Manyoni – Rungwa na Kilomita 90 kutoka Rungwa – Chunya ambapo kuna mapori makubwa na uhalifu mwingu. Polisi wanashindwa kufuatilia matukio kwa kisingizio cha ukosefu wa usafiri (*Ratio Polisi 1: watu 1300*). Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Kijiji cha Kirurumo, Ukimbu kama majengo ya *Folk School* yanaozu tu, napendekeza paanzishwe J.K.T. au Chuo cha Polisi ukanda huu mpana kati ya Singida, Tabora na Mbeya. Naomba jibu kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, *Traffic* bado wanapokea “kitu kidogo” kutaka kwa Madereva na kuachia magari mabovu hivyo ajali zinaendelea kutokea. Mkakati uandalive kuvunja mtandao wa mafiga matatu (3) wa Traffic – Dreva – Wamiliki wa magari. Jeshi la Polisi linaweza kuuvunja mkakati huu na kupunguza ajali.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha, ambayo imetenga utekelezaji mzima wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Kwa namna ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa hapa Bungeni na ni mtendaji kazi anayejali maisha ya wananchi akishirikiana na Waziri wake katika kuhakikisha usalama wa wananchi unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Katibu Mkuu, watendaji wa Wizara kwa pamoja kuhusu utendaji kazi, katika Wizara kwa kushirikiana kikamilifu ukamilihaji wa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kaskazini Pemba, wanatoa pongezi kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kutokana na ujenzi wa nyumba za Polisi zinazoendelea kukamilishwa huko Limbani Wete. Tunaamini kuwa majengo hayo yatasaidia sana kuondoa ugumu wa makazi kwa Askari wa maeneo ya Mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi hizo, naiomba Serikali kuangalia uwezekano pale uwezo utakaporuhusu kuyakarabati majengo mengine yaliyopo *Police Line*, Wete, Konde na Matangatuani, kwani ni muda mrefu sana majengo hayo yapo katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ifuatilie kwa undani zaidi pale inapotoa fedha za Askari wanaopatiwa uhamisho au malipo ya posho kwani wakati mwingine huwa haziwafikii kama ilivyokuwakusudiwa hasa tukiangalia kuwa Askari wanafanya kazi ngumu bila kujali wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara iangalie kwa undani pale zinapotoka ajira na kutakiwa kila Mkoa utayarische vijana kwa ajili ya ajira hizo. Mara nyingi baadhi ya watendaji hufanya makosa ya kujaza nafasi hizo kutoka Mikoa mingine wanayotaka wao na kusababisha malalamiko makubwa katika Mikoa iliyofanyiwa upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wizara itakumbuka kuwa yapo maeneo ndani ya Mkoa huo ambayo hayana ulinzi wa kudumu na kusababisha wahalifu kupenya na kuingia kiholela nchini. Maeneo hayo ni Bandari ya Msuka, Bandari ya Tumbe pamoja na maeneo mengine ya bahari yaliyozunguka Mkoa huo kama Kinyu, Maziwa Ng'ombe na mengineyo. Naiomba Serikali iangalie namna ya kupeleka ulinzi wa kudumu katika maeneo niliyoyataja ili kuepusha ujambazi unaojitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara hii kwa jitihada zake za kulinda usalama na mali za raia. Napongeza vile vile kwa kazi nzuri ya kuzuia uhalifu. Niunge mkono mia kwa mia hotuba hii ila nina mambo machache nataka kutoa angalizo yashughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Askari. Katika hotuba yake, hakutaja chochote kuhusiana na ujenzi wa nyumba za Askari Mkoa wa Kaskazini Unguja. Hali ya nyumba za Askari Mkoa huo ni mbaya sana, sio nyumba ya Afisa wanazofanyia kazi, majengo yaliyopo pale yamerithiwa wakati wa ukoloni na kwa maelezo tuliyopata majengo yale yalikuwa ni nyumba za wafungwa na Askari. Ngome hiyo kwa sasa, Ofisi

ni nyumba za Askari, ni makazi yao. Uhalifu mkubwa unatokea kwa vile Askari wanaka pamoja na wahalifu uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya Polisi na stahili zao. Hivi tatizo ni nini Askari hawa hawapewi mafao yao na stahili kwa wakati. Mimi sifahamu kabisa ni kwa nini janga hili huwa linawasibu Askari wa ngazi za chini tu. Nadhani inatupasa tuelewe kuwa katika mfano wa kazi watendaji wa moja kwa moja ni Askari hawa wa ngazi za chini na sio wakubwa na viongozi wa juu. Kwa hiyo, kama hoja kwa kweli ni stahili/haki zao hata hawa wadogo wapatiwe stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari na vitendea kazi vingine. Itakuwa ni jambo la busara kwa Jeshi hili likajipanga upya kuwapatia Askari wake vitendea kazi vya huduma (mafunzo) na magari. Sasa sio wakati ule, hali ya nchi ki-uteknolojia na utandawazi vimepanuka kwa hali ya juu sana kiasi ambacho taaluma ya Polisi na vitendea kazi haviwezi kuwa hivi tulivyo au kwa mazoea. Kwa hiyo, tunahitaji tuende na wakati. Askari wetu wapewe magari yenye uwezo wa kukabiliana na hali halisi. Tuwape zana za mawasiliano, silaha za kisasa zaidi, pipipiki na kadhalika. Lakini kubwa zaidi panahitajika kuwa na Askari (kundi kubwa) wasiovaa sare, Askari Kanzu. Hawa ndio watakaokuwa ni mwingiliano na watu wa kawaida na kuweza kuzuia uhalifu kabla haujatendeka. Ulinzi shirikishi, sawa tunawapongeza, lakini ulinzi kwa kutumia Askari kanzu tunauhitaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpungeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya hapo Wizarani. Pia nimpongeze sana *IGP* Said Mwema, pamoja na wapiganaji wake wote, kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao na pia kwa namna wanavyowashirikisha wananchi kuititia Polisi Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, napenda nimsihi sana Mheshimiwa Waziri, *IGP* na Askari Polisi, viongozi mahiri, kubuni utaratibu wa ziada utakaotuwezesha kumaliza tatizo la mauaji ya Albino na ya vikongwe. Kumekuwa na taarifa zipatazo nne hivi kuhusiana na tatizo la mauaji ya vikongwe, ingawa pia sababu nyingi zilizotambuliwa katika taarifa hizo zaweza pia kuwa na mchango mkubwa katika kutambua na hatimaye kuondosha sababu zinazopeleke maaji ya Albino pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwezekana basi lifanyike Kongamano la Kitaifa ili kukomaza uelewa mionganoni mwa wananchi kuhusu sababu na mbinu za kupambana na mauaji haya ambayo hakika hayatazuiliwa wala kumalizwa na Polisi pekee. Jamii nzima lazima ifahamishwe namna ya kuweka mchango wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na nawapongeza sana kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao. Nimpongeze sana Waziri Masha, Naibu wake, Balozi Kagasheki, *IGP* Mwema na Wakuu wa Magereza, *Immigration*, Zimamoto na Askari wa kada zote, kwa kuonyesha nidhamu ya hali ya juu. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine, nikuombe na unipe jibu kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Kituo cha Polisi wa Wilaya ya Kwimba. Katika bajeti ya mwaka 2008/2009, niliuliza na nikajibowi vizuri kuwa suala hilo litazungumziwa lakini hadi leo kimya, naomba majibu tafadhali. Tuliomba tutumie wafungwa kujenga Ofisi hiyo, tunasubiri kibali ambacho nacho hakijapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika bajeti, niliomba gari kwa ajili ya Wilaya ya Kwimba ambapo gari mbili zilizopo, hazitoshii kutokana na ukubwa wa eneo la Wilaya yenye, inawezekana ombi halikutekelezwa kutokana na mfumo wa manunuzi kutokuwa mzuri. Naomba mara magari yatakapofika basi Wilaya ya Kwimba iwe moja ya Wilaya zitakazopata magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niliomba usafiri wa pikipiki mbili kwa Vituo vya Polisi vya Sumve na Malya, Mheshimiwa Waziri anayafahamu maeneo hayo vizuri zaidi, ni maeneo yanayostahili usafiri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa ujenzi wa nyumba za Askari wetu zilizoko Kilwa Road, huo ni ukombozi, ni heshima na ni kuthamini mchango na kazi wanayoifanya kwa nchi yetu. Naomba Serikali kupitia Wizara yako, ijenge nyumba kama hizo katika Mkoa wa Mwanza eneo la *Police Line* Mabatini. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumejjijengea utamaduni mzuri wa kuwaweka pamoja Askari wetu kuliko hivi sasa wametawanyika, wanakaa na raia inaweza kufikia hali ya kushawishika kufanya mambo nje na maadili ya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaliomba Jeshi letu la Polisi, liendeleee kushirikiana na wananchi (Ulinzi Shirikishi) na Sungusungu, ili kuendeleza amani na utulivu hasa suala zima la mauaji ya vikongwe na walemavu wa ngozi (Albino). Tunaipongeza Serikali, Jeshi la Polisi, wananchi kwa kukemea kwa nguvu zote suala la kuwaua walemavu wa ngozi hasa katika maeneo ya Mwanza na Shinyanga. Uzi ule ule, Polisi isilegeze Kamba katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia kuomba tena kuhusu ujenzi wa Kituo Kikuu cha Polisi cha Wilaya ya Kwimba, ni Wilaya ya miaka mingi, Ofisi ninayotumia imejibanza, haina hadhi ya Ofisi Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27/06/2009 katika Msitu wa Rwenzewe, Bukombe, mtoto wa kaka yangu akitoka kusindikiza gari la abiria, aliuwawa na majambazi. Mheshimiwa Waziri nilikueleza tukio hilo ukaniambia unasubiri *IGP* ambaye ulisema yuko Mara. Napenda kujua stahili ya Askari huyu marehemu PASCHAL

MATINDE FS91B, msimamizi ambaye ni baba yake mzazi atalipwa lini? Leo naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na ninawataenia kila la kheri katika utekelezaji wa yale mliyoyaainisha katika hotuba yenu.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba awali ya yote, kutamka kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ranya, napenda kutoa shukrani zao, kwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kusikia kilio chao cha miaka mitatu kuhusu uporaji wa mifugo yao na mauaji ya raia wasio na hatia unaofanywa na majambazi kutoka nchi jirani wanaotumia silaha za kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya unyang'anyi wa mifugo ya wananchi wa Ranya, yamesababisha dhiki na mateso makubwa kwa wananchi wetu. Wananchi wa Ranya wamefarijika sana na hatua iliyochukuliwa na Serikali kutohana na ziara za Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mkuu wa Polisi na timu yake kwenda katika vijji vya Mangore, Changunge, na Tutue. Kutohana na ziara hizo, vikosi maalum vya Polisi vimewekwa katika vijiji hivyo kwa ajili ya *operation* maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, wananchi wamenituma kufikisha maombi yao kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaomba Serikali iimarishe ulinzi wa mipaka ya nchi yetu katika Wilaya za Tarime na Ranya. Jukumu la Ulinzi wa mipaka ya nchi, ni jukumu la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Naomba ninukuu:-

*“(a) Kujenga Jeshi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa kwa ajili ya majukumu ya ulinzi wa nchi yafuatayo:-*

*(i) Kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya uvamizi wa adui; na*

*(ii) Kuandaa na kuongoza umma wa Watanzania katika jukumu la ulinzi wa Taifa dhidi ya adui.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanampongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi na Makamanda, kwa kuimarisha ulinzi katika vijiji ambavyo vimeathirika na ujambazi wa uporaji mifugo na mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaomba Vituo vya Polisi katika vijiji vya Mangore, Sudi/Changunge, Tafwe, Shirati, Panyako, Kogaja na Utigi viimarishe kwa kupatiwa Polisi wa kutosha, magari, vifaa vya mawasiliano ya nishati ya juu kwa ajili ya kuboresha

mawasiliano. Vilevile wanaomba mpakani Kirongwe, kifunguliwe Kituo cha Polisi na Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya uporaji mifugo Wilaya ya Rorya na Tarime, yanaendelezwa na maharamia kutoka nje ya nchi wanaotumia silaha za kijeshi kutokana na mipaka yetu kutokuwa na ulinzi. Naomba JWTZ lipelekwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha Kikosi Maalum cha JWTZ kwa ajili ya kulinda mipaka yetu, ni kwa ajili ya kutuliza au kukomesha mapigano ya koo. Serikali inalo jukumu la kulinda mipaka ya nchi yetu hasa mipaka ya Wilaya za Tarime na Rorya dhidi ya uvamizi, unaofanywa na maharamia/majambazi kutoka nje ya nchi yetu. Tangu mwaka 2007 – 2009, ng'ombe wapatao 2,500 wameporwa na kuvuka mpaka wa nchi yetu, wananchi 40 wamepoteza maisha yao. Wananchi wanaomba kufuta machozi au fidia.

Mheheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ambaye amefanya kazi nzuri kwa kutoa ushirikiano wa hali ya juu kuhusu maafa yaliyotokea Wilayani Rorya, atoe majibu kuhusu maombi ya wananchi hao.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na uwasilishaji mzuri wa bajeti. Naipongeza Wizara hasa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri hasa za mapambano dhidi ya majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo hayo ya pongezi, naomba niombe mambo mawili. Kwanza, naiomba Wizara iongeze Askari katika Wilaya ya Sikunge kutokana na uchache walionao na ukubwa wa eneo la Wilaya. Ombi la pili, ni la kuomba *Pay-master* ambalo nilikwisha lifikisha kwako Mheshimiwa Waziri na ukaahidi kulitafutia ufumbuzi lakini mpaka sasa bado halijatekelezwa. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuwaondolee adha Askari kuja Tabora km 71 kufuata huduma za fedha na pia wananchi wanaosafiri km hizo kuja kufuata ulipiaji wa mambo kadhaa yanayoambatana na shughuli za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kukushukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara na napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri, hata hivyo ninaomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kuhusu tatizo la usafiri kwa kituo kidogo cha Polisi Kwamtoro. Kituo hiki kilikuwa na gari lakini gari hilo limechakaa sana na hivi sasa liko juu ya mawe. Mheshimiwa Waziri aliwahi kuahidi kutoa pipikiki kwa vituo vya Kwamtoro na Mrijo

wakati Wizara inatafuta uwezekano wa kununua gari kwa kituo cha Kwamtoro. Ninasisitiza kuwa gari ni muhimu sana kwa sababu eneo la Kwamtoro lina matukio mengi ya ujambazi, wizi wa mifugo na mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuiarifu Wizara kuwa wananchi wa kata ya Kwamtoro kwa kushirikiana na uongozi wa kituo kidogo cha Polisi Kwamtoro, wameanza kufyatua matofali kwa lengo la kuanza ujenzi wa majengo ya Kituo kidogo cha Polisi Kwamtoro. Uamuzi huu umefikiwa baada ya kubaini upungufu mkubwa wa majengo katika kituo hicho. Kwa niaba ya wananchi hawa, ninaomba Wizara iwaunge mkono kwa kusaidia vifaa vya ujenzi vikiwepo mabati, saruji, mbao, misumari na kadhalika pindi ujenzi utakapoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi hii na ninaunga mkono hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ahsante.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, majambazi yamezidi Wilaya ya Mpanda, tunaomba msaada mkubwa kutoka kwenu. Pia Vituo vya Polisi, Wilaya za Mpanda bado ni vichache. Kituo cha Karema bado kina matatizo, tunaomba msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mpanda, magari ni machache, tunaomba msaada wa magari kwa sababu Wilaya hiyo ni kubwa sana na mapori ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maboti ya Ziwa Tanganyika kwa sababu maharamia ni wengi sana kutoka Zaire na Burundi, tunaomba kwa ajili ya doria.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya Maandishi, kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kagasheki (Mb), Katibu Mkuu, *IGP* Saidi Mwema, pamoja watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa na matumaini makubwa kuwa mchango wangu utajibiwa na Waziri pamoja na Naibu Waziri, kabla sijaanza kutoa ushauri na maombi ya wananchi wa Mkoa wa Singida na Taifa kwa ujumla, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuikumbusha Serikali ahadi iliyonipa kipindi Waziri wa Mambo ya Ndani akiwa Mheshimiwa Bakari Mapachu ya kujenga Kituo kipywa cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni na kukarabati kile ambacho kinatumika sasa hivi. Ninasikitika sana kusema kuwa hadi sasa ahadi hizi bado hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni, ni mbaya sana kwani bati zake huvuja sana wakati wa masika jambo ambalo ni kikwazo kikubwa

kwa Askari wanaofanya kazi hapo kwani huharibu kumbukumbu za majalada ya kituo hicho. Ninamuomba Mheshimiwa Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atafute uwezekano wa namna yoyote ili fedha zipatikane za kukarabati kituo hicho kabla ya masika ya mwaka huu hayajaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa jambo hili, watumwe watendaji kwenda kuujionea hali halisi ya kituo hiki na wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atoe maelezo yenge kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ahadi ya Serikali kukubali kujenga Kituo kipy Cha Polisi Wilaya ya Manyoni na kutuma fedha za kununua kiwanja, wananchi wa Manyoni walifurahi sana na kuwa tayari kushirikiana na Serikali kujenga kituo hicho pamoja na uongozi wa Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalosikitisha, ni kwamba Serikali imesahau kabisa ahadi yake kwani kupitia bajeti hii ya 2009/2010, haikutenga hata kiasi kidogo cha fedha. Ninaishauri Serikali kutafuta fedha za kuweka hata msingi tu ili ujenzi kamili uendelee mwaka wa fedha 2010/2011. Nategemea majibu kwa Waziri wakati akitoa majumuisho.

Mheshimwa Spika, napenda kupongeza Jeshi la Polisi Mkoani Singida chini ya uongozi wa *RPC* Selina Kaluba kwa jinsi wanavyojitahidi kudhibiti mwendo kasi kwenye magari ya abiria kwani mwaka 2008 waliingiza Tshs. 150,000,000/= kwa ajili ya faini ya magari ya abiria na mwaka huu kwa kipindi cha miezi sita tu wameshaingiza Tshs. 80,000,000=/. Hatua hii imesaidia sana magari ya abiria kupunguza mwendo na ajali kupungua Mkoani Singida,. Ninaombwa Serikali kuwapongeza Askari kwa kitendo hichi kupitia Bunge wakati Waziri anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ajali zimepungua, napenda kuishauri Serikali kuagiza magari yote ya abiria kuanzia sasa yawe na mikanda ya kujifunga abiria wakati wa safari. Hii itasaidia zaidi hata kama inatokea bahati mbaya maana ajali huweza kutokea hata kwa bahati mbaya mikanda itawanusuru abiria pamoja na dereva kutokuumia vibaya. Suala hili linawezekana ni Serikali kutoa agizo kama ilivyotoa wakati wa kuweka milango ya tahadhari/dharura. Ninasubiri majibu au maelezo ya Waziri wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wako Watanzania wakorofi, hung'oa mabango yenge alama za barabarani na kuwafanya Madereva kupata ajali kwa vile hukosa kufahamu hali ya barabara huko aendako. Ninaombwa Serikali kutoa maelekezo kupitia idara ya *TANROADS* kujengea nguzo za alama hizo kwa zege nzito ili Watanzania wakorofi, washindwe kuchimbua na kung'o'oa alama za barabarani. Jambo hili Singida limefanyika na linasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza Serikali kwani madai ya Askari yamepungua sana kwani wanajitahidi kupunguza mara kwa mara. Ninaishauri Serikali sasa kuanza kulipa wakati ule ule Askari anapohitaji mfano anapoenda likizo au safari ya

kikazi, hii itawatia moyo Askari na itaondoa malimbikizo makubwa na adha ya Askari kusafiri kwa taabu au kuanza kuomba rushwa kwa raia wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha helkopta ya Polisi kusaidia ulinzi Mikoani, kilisaidia sana Jeshi la Polisi kukamata wahalifu Mkoani Singida. Ninaamini hata Mikoa mingine pia. Ninaishauri Serikali zoezi hilo lirudiwe tena kwa kushtukiza litasaidia tena kwani uhalifu bado upo Singida hasa wa kuteka magari yanayotoka vijijini na kupita katikati ya misitu hata barabara kuu. Tafadhali Waziri atoe majibu ya maombi yangu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali jinsi inavyojitahidi kushirikiana na wananchi kujenga vituo vya Polisi Mkoani Singida ingawa bado zipo kata nydingi ambazo hazina Vituo vya Polisi na Kata hizo ndizo zenye kukabiliwa na ujambazi. Ninapongeza pia uongozi wa Mkoa kwa kupeleka Askari wa *patrol* kwenye maeneo hayo kitendo ambacho kinasaidia kiasi ingawa Askari wanakuwa na mazingira magumu posho hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ijitahidi kujenga Vituo vya Polisi maeneo ambayo ni mbali sana mfano Rungwa Wilaya ya Manyoni, Mugungira, Mwaru, Isuna Singida vijijini na Urughu, Kidaru, Mwangaza Wilaya ya Iramba na Kata zingine nydingi ambazo sijazitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Serikali pamoja na huduma inayotoa ya tiba kwenye zahanati zake, bado ipo kero kwa Askari kwani sio huduma zote hupata kwenye zahanati kwani hulazimika pia kwenda Mkoani na kuchangia fedha zao. Ninaiomba Serikali ione njia nzuri ya kuwasaidia kama vile kuwa na Bima ya Afya kwa Askari Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho, limekuwa la muda mrefu sana mpaka Watanzania wameanza kupata hisia tofauti tofauti na kuwapa nafasi Wapinzani. Ninaishauri Serikali kutekeleza hoja hii kwani kucheleweshwa sana haileti picha nzuri. Naomba Waziri atoe maelezo ya kufunga hoja hii tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa Serikali huwapa fedha za kodi za nyumba Askari wanaoishi uraiani lakini ni ndogo sana haziendani na hali ya bei za sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida kuna upungufu wa vidhibiti mwendo na simu za Polisi. Ninaomba tupewe zinasaidia sana kwenye matukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuunga mkono hoja hii, nasubiri majibu na bila kusahau ombi la magari kwa Wilaya zetu zote tatu kwani ni kubwa sana na vijiji vyake viko mbali mbali sana hata matukio kukabiliana nayo ni vigumu sana. Tumeomba Wilaya zigawanywe lakini bado Serikali haijatoa jibu. Kwa tahadhari ya uhalifu ndani ya Mkoa, ni vema kila Wilaya iongezewe hata gari moja moja ili linapotokea tatizo Askari wawe wepesi kwenda kwenye eneo la tukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa magari ya Jeshi la Polisi yanafanya kazi kubwa sana, hata huwa hayapumziki, ni vema yawe yanabadilishwa kila mara ili huduma ya magari iwe endelevu kwani hadi leo kuna magari ambayo yamekufa na mengine kuchakaa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninategemea majibu kwa Waziri wakati wa majumuisho.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Kwanza naanza kwa kulishukuru Jeshi la Polisi, kwa kazi nzuri wanazozifanya za kupambana na majambazi. Lakini niwapongeze Askari wa Unguja, kwa kusimamia ulinzi wakati wa uandikishaji wa uchaguzi na hata wakati wa upigaji kura zenyewe, nawapongeza sana kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia kuhusu Askari wanawake, Askari wetu wa kike wanafanya kazi nzuri sana, wanastahili kupewa pongezi za peke yao kwa utendaji wao hasa hawa Askari wa *Traffic* wanavyopitisha magari kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wastaafu na waliokufa katika Jeshi la Polisi, kuna ma-Sergeant sita ambao wamestaafu tangu mwaka 2005 mpaka hii leo hawajapata ufumbuzi wowote wa mafao yao, hasa huyu *Sergeant Yusuf Nasoro* ambaye alikuwa kocha wa Riadha yaani kila mara huwa anaambiwa aje Dar es Salaam, mambo yake tayari akifika huko huambiwa asubiri Hazina cheki karibu itatoka, karibuni mara saba kashaenda Dar es Salaam na kurudi. Mheshimiwa huoni kama hawa Maaskari wanapata usumbufu kwa haki yao? Wale Askari waliofariki wale warithi wao, wameshatimiza vitu vyote walivyotakiwa watimize, je, tatizo ni nini, hamuoni kuwa yatima hawa tunawatia unyonge?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Zanzibar ipo timu ya *netball* ya Askari wanaume na timu hii imeshaleta ushindi na kupeperusha bendera ya Tanzania nje ya Tanzania mara nne na mara zote hizo si Waziri wala *IGP* walau kwenda Zanzibar kuwapa hongera kwa kitendo hicho kizuri cha Kitaifa. Kwa kuititia Bunge hili, nakuomba Waziri, Naibu Waziri au *IGP* mwende Zanzibar mkawape moyo Askari hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamisho, inakuwaje Askari akitoka Mwanza kwenda Zanzibar analipwa mafao yake yote ya safari lakini Askari huyo huyo anapotoka Zanzibar kwenda Mwanza huwa halipwi posho yake yote ya safari? Mheshimiwa *IGP*, hebu hili suala ulichunguze kwa makini, kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, huku Zanzibar Mheshimiwa Waziri kuna hizi fedha za kujikimu ambazo hupewa Askari wanapotoka kwenye mafunzo ya awali. Fedha hizo, madhumuni ni za kujikimu na maisha wanapotoka mafunzo sasa pesa hizi kuna Askari tangu mwaka 2000, wenao wamepewa wao hawajapewa na wametilishwa saini ndani ya karatasi wakaelezwa hizo pesa ziko tayari na mpaka hivi sasa hawajazipata. Ninaomba hili nalo uliangalie vizuri na kulitafutia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vituo vya Polisi, vingi vya Zanzibar vibovu na wala havina vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme kwenyeV vya Polisi, ni muhimu hasa hizo siku tunazokwenda kwani ni siku ya uchaguzi ningeomba ifanyike jitihada ya umuhimu kwa kuvipatia vituo hivyo umeme, Radio call, pikipiki au baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushauri Wizara itafute mfadhili aweze kuwakopesha vipando Maaskari ili waweze kusaidia ufanisi wa kazi za Jeshi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yako. Nawapongeza pia Wataalam, Makamanda na Wapiganaji wa vikosi chini ya Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngorongoro, ni Wilaya ya mpakani na Jamhuri ya Kenya. Ni zaidi ya km 400 kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Arusha. Matukio ya uhalif, ni mengi na mengine, yanahusisha nchi jirani kama vile Wasomali, wezi wa mifugo, majangili, wachimbaji haramu wa madini yetu na kadhalika. Haya ni matukio mazito! Polisi hawana nyenzo za kazi, kuna magari lakini ni mabovu zaidi ya mwaka sasa. Bajeti ya kutengeneza ni ndogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Polisi kutokuwa na gari, wanakuwa omboomba kwa wawekezaji na makampuni yaliyoko maeneo yao ya kazi kama vile OBC, Kampuni ya Thomson na kadhalika matokeo yake ni manyanyaso na kunyimwa haki wananchi hasa kama wamegombana na mwekezaji. Naomba Askari wa Loliondo wapewe gari la kazi pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Loliondo ni la zamani sana, limejengwa wakati wa ukoloni katika miaka ya 1950's. Hata Mzee Jomo Kenyatta wa Kenya, aliwahi kufungwa katika Gereza hilo. Ni Gereza la kilimo na ujenzi. Wanahitaji lori la kupeleka wafungwa shambani na kusomba vifaa vya ujenzi mawe, mchanga na kokoto; pia majani ya mifugo na maji. Mkuu wa Gereza, Bwana Mwaisabila, ni mchapa kazi, mbunifu na amejitahidi sana kujenga nyumba za Askari na Zahanati. Anastahili kuungwa mkono na Wizara yako ili asikate tamaa. Naomba apatiwe lori na trekta kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya haina Ofisi ya Uhamiaji licha ya kuwa tuko mpakani na nchi jirani ya Kenya. Mwingiliano wa watu ni mkubwa wanaruka mpaka kupitia njia za panya. Tunategemea Afisa Uhamiaji kutoka Wilaya ya Karatu zaidi ya km 250 kutoka Loliondo Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro. Naomba huruma yako katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iharakishe ukamilishaji wa vitambulisho vya kitaifa kwa ajili ya Watanzania.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mambo machache kwenye bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara/Jeshi la Polisi, bado Askari Polisi wengi wa zamani hawajapandishwa vyeo. Nashauri jitihada zaidi zifanywe ili kuhakikisha kwamba Askari wote wa zamani wanapandishwa vyeo kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi sana kuhusiana na jinsi ajira zinavyofanywa ndani ya Jeshi la Polisi. Inasemekana kwamba ajira hutolewa kwa upendeleo kwa watoto wa wakubwa na ndugu zao. Hili kama kweli lipo, siyo zuri na linaleta picha mbaya kwa Serikali na Jeshi la Polisi kwa ujumla. Nashauri utaratibu unaotumika uwe wazi zaidi. Aidha, nafasi zinazotolewa kwa Mikoa basi ziwe kwa wananchi wa Mikoa hiyo na siyo kuchukua vijana kutoka Mikoa mingine kwenda kufanya usaili katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji wa Tunduma, Wilayani Mbozi, umekuwa kwa kasi kubwa na kwa sasa unakadiriwa kuwa na watu zaidi ya 40,000 (wakazi). Aidha, kwa wakati wa mchana, mji huu mdogo unakadiriwa kuwa na watu zaidi ya 100,000. Mji huu uko mpakani mwa nchi yetu na Zambia na ni kituo kikubwa sana cha biashara za aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na soko la Kimataifa la mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwingiliano wa watu wenyewe tabia na tamaduni mbalimbali, Mji huu umekuwa ukikumbwa na vitendo vya ujambazi mkubwa na mdogo na hivyo kusababisha Polisi kufanya kazi ya ziada ya kuufanya mji huo kuwa na utulivu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali iliyopo Tunduma ambayo mara kadhaa husababisha mapigano kati ya Polisi na raia na kutokana na kukua kwa mji wa Tunduma ambao upo mpakani na kutokana na ukweli kwamba Askari walipo Tunduma ni wachache sana na hivyo kushindwa kukabiliana na vurugu za mara kwa mara zinajitokeza katika mji huo, kwa msingi huo, napendekeza na kuomba ianzishwe Wilaya ya Kipolisi ya Tunduma ambayo itaongozwa na *OCD* na hivyo kupunguza mlolongo wa kuchukua maamuzi pale vurugu zitakapojitekeza. Lakini muhimu zaidi, tutauweka mji wetu kuwa salama zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi Vwawa – Mbozi ambacho awali kilianza kama kituo cha manamba wakati wa ukoloni, kina zaidi ya miaka 48 sasa. Kituo kina hali mbaya sana pamoja na nyumba za Askari Polisi. Nataka kujua Wizara inachukua hatua gani kukijenga upya na kukikarabati kituo hicho sanjali na kukarabati nyumba za Askari ambazo ziko kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Novemba mwaka jana, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotembelea

Wilaya ya Mbozi, aliahidi kukipatia gari Kituo kidogo cha Polisi kilichopo kwenye mji wa Mlowo. Kituo hicho kinahudumia Tarafa za Vwawa, Lyula na Igamba. Tarafa hizi zote zina matukio mengi sana na kituo kinazidiwa kwa kutokuwa na gari. Naomba kujua je, Wizara ina habari na ahadi hiyo ya Rais, kama wanayo wamechukua hatua gani? Kama hawana, je sasa watachukulia taarifa yangu kuwa rasmi na hivyo kuiweka ahadi ya Rais kwenye utekelezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilimwandikia Waziri kuhusu hali mbaya ya Gereza hilo na marekebisho yaliyotakiwa kufanywa, hata hivyo, hadi leo hakuna maendeleo yoyote. Gereza la Mbozi kwa sehemu kubwa limejengwa kwa ukuta wa tofali na tope. Ukuta huo siyo imara sana kutokana na kujengwa kwa tope. Naomba Wizara itenye pesa kwa ajili ya kununua saruji na mchanga ili kuimarisha ukuta wa Gereza hilo.

Aidha, naomba Gereza lipatiwe gari mpya kwani lililopo ni bovu na hugharimu pesa nyingi kwa matengenzo ya mara kwa mara. Ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kwanza, kumpungeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote waandamizi wa Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji, kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuimarisha usalama wa raia katika nchi yetu. Suala la usalama wa raia, ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii, kwa kiasi kikubwa Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi nzuri, ukiacha kasoro ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata nafasi ya kutembelea Gereza la Ruanda – Mbeya na kushuhudia mambo yafuatayo:-

Kwanza, uchakavu wa majengo – Gereza hili limechakaa sana, hasa selo za mahabusu, wafungwa na jengo linalotumika kupikia chakula. Gereza hili ni la toka ukoloni, hivyo natoa rai Serikali iendelee kutenga fedha kwa ukarabati kama wanavyofanya katika suala la uimarishaji wa huduma za afya.

Pili, madai ya wazabuni – Chama cha Wazabuni Mbeya wanayo madai ya muda mrefu ya kutolipwa kwa kupeleka huduma mbalimbali kwa Wizara hii. Asubuhi hii wamenijulisha kuwa baadhi yao wameanza kulipwa, inatia moyo sana, natoa rai wale wote ambaeo hawajalipwa walipwe sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Maaskari Polisi. Naipongeza sana Serikali kwa Ujenzi wa nyumba za Maaskari Kilwa Road na Zanzibar, ni kazi nzuri sana na iendelezwe kwenye maeneo mengineyo. Naomba sasa nguvu zote zielekezwe kwenye majiji makubwa, likiwemo jiji la Mbeya. Naomba sana mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba za Askari Polisi Mbeya, si vyema kwa Maaskari kuishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya Maaskari Magereza, yapo madai ya muda mrefu ya Maaskari wa chini na maafisa kutokana na uhamisho, safari, tiba na kadhalika. Naomba madai haya yalipwe haraka ili kutowavunja moyo Maaskari hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha Wilaya ya Polisi Tunduma, kutokana na vurugu za kila mara katika eneo hili la Tunduma, Wilaya ya Mbozi, ni vyema Serikali ikalitazama upya eneo hili. Utakumbuka hivi karibuni vurugu za tarehe 20/06/09, ambazo zilitokana na kifo cha kijana Mwachembe, aliyeuwawa kwa kupigwa risasi na Polisi, limekuwa jambo la kawaida kwa eneo hili, kwa wananchi kuchukua sheria mikononi. Inawezekana ni kwa sababu ya mpaka kati ya Tanzania na Zambia, mbona mipaka mingine ni tulivu sana, kwa nini Tunduma iwe hivyo? Kuwepo kwa Wilaya ya Kipolisi kutaimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kati/Kikuu cha Polisi Mbeya mjini. Jengo hili ni la muda mrefu sana, hata hivyo hali yake inahitaji kupakwa rangi ili liwe katika hali ya kupendenza.

Mheshimiwa Naibu Spika, doria zinazofanywa usiku na Maaskari, tunapongeza juhudhi hizi za Serikali, lakini imeibuka kero kubwa sana ndani ya jiji la Mbeya, kwamba wananchi hasa vijana wanakamatwa na kuambiwa ni wazururaji, wakipelekwa Kituo cha Polisi, hawatoki mpaka watoe chochote. Haya yanafanywa na Maaskari wasio waaminifu. Wazazi wanahangaika kutafuta pesa ya kuwakomboa vijana hawa vinginevyo hawatoki. Ni wakati gani mtu anaitwa mzururaji, fedha wanazolipishwa zinaingizwa wapi? Ninaamini ni Maaskari wasiokuwa waaminifu ndiyo wanaoendeleza kero hii, naomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa shughuli/kazi za Wizara hii pamoja na majukumu yake. Nampongeza Waziri, Naibu wake na uongozi mzima wa Wizara. Mchango unalenga kutoa mifano kidogo tu ili iangaliwe na kufanyiwa kazi ili kazi nzuri inayofanywa na Wizara ionekane zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya OCD – Mbinga. Kesi za aina hii ziangaliwe. Maoni ya wananchi wengi pale Mjini Mbinga kwamba jambo hili limefanywa na Polisi wenyewe. Lakini wananchi/vijana na wafanyakishara walikamatwa na kuzuiliwa kwa muda mrefu. Suala hili likigundulika ni kweli basi Jeshi letu hasa litakuwa limechafuka sana. Nashukuru sana kwamba wengi sasa wameachiwa. Naomba kesi za namna hii ziangaliwe si Mbinga tu bali nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi Mbinga wanakamatwa na hulazimika kutoa fedha ili kunusuru pipipiki zao, ni kama mradi. Ni kweli wengi wao pengine hawajasajili vyombwa hivyo, je, kukamata ni njia pekee, upo uwezekano wa kufanya kampeni Kiwilaya kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamisha malori barabarani, tabia hii ni kero. Hii inafanya kuwa na lori nchi hii ni balaa. Tuangalie uwezekano wa kufanya kazi hii vyema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wasikae muda mrefu kwenye vituo. Polisi wengine hukaa muda mrefu maeneo ya kazi. Ni vyema kufanya zoezi hilo kubaini tatizo ili kuwahamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za kufanya kazi. Juhudi za kufanya Jeshi letu kuwa la kisasa zaidi kwa kuiga zana kama magari, *computer etc.* Hali ya Polisi Mbinga na hasa Uhamiaji inahitaji kuangaliwa upya. Mtendaji wenu pale Mbinga amefanya kazi nzuri ninahitaji kumuunga mkono. Magereza zitumie *biogas technology*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatachia kazi njema na Mungu awabariki na kuwawezesha.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri pamoja na Naibu wako, Waziri Kagasheki (Mb) ni mchapa kazi mzuri sana, kitendo chako cha msimamo juu ya tatizo la mgodi wa Barack kule Geita, ni mfano mzuri wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu, ni kuwapongeza sana kwa kuniletea Kituo cha Polisi pale Ilembula – Njombe. Tunawashukuru sana, uhalifu sasa umepungua pia Mkuu wa Kituo na Askari Polisi wote, ni wachapakazi wazuri. Ila tunaomba mtusaidie gari la Mkuu wa Kituo kwa ajili ya kuwachukulia wahalifu. Sasa hivi tunapikipiki tu, wahalifu wengi hupelekwa Makambako au kuwachukua waliko hasa vijijini ni tatizo kubwa sana, kwani mhalifu huwezi kumpandisha kwenye pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana watumishi wote wa Wizara wakiwemo Mkuu wa Polisi nchini Saidi Mwema, Makamanda wa Mkoa na Askari Polisi wote nchini, kwa utendaji mzuri licha ya changamoto mbalimbali za upungufu wa nyumba, vitendea kazi na ubaha wa Askari Polisi.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Askari anapotuhumiwa kwa kosa la jinai huwa anafukuzwa kazi lakini baada ya kesi kuisha na kwa bahati nzuri Askari yule hakukutwa na hatia, Jeshi la Polisi huwa halimrudishi Askari yule kazini. Isitoshe kuna uonevu mkubwa sana Polisi wa ngazi za juu akituhumiwa kwa kosa kama hilo hulipwa nusu mshahara mpaka kesi hiyo iishe. Je, si heri kurudi nyuma na kutumia utaratibu uliotumika enzi za ukoloni?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hawapewi ruhusa za kujiendeleza kielimu katika vyuo mbalimbali. Ruhusa hiyo mpaka itoke kwa *IGP* na *IGP* kwa Tanzania nzima anatoa nafasi za Askari 80 tu kwenda kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hatupo katika kisiwa chetu wenyewe, Umoja wa *East Africa* unakuja, dunia ni kama ipo kwenye kiganja kimoja. Siku hizi upelelezi mwangi unatumia technolojia za kisasa bila elimu hawa Askari wetu wataweza kwenda na wakati? Nashauri kama Askari amepata ufadhili wa kwenda kusoma na ufadhili huu

unakuta kaupata kutoka Serikalini basi apewe ruhusa akajiendeleze kusiwe na kizuizi chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhaba mkubwa sana wa vitendea kazi kwa mfano hata karatasi ya kuandikia *RB* ni shida. Mfano hapa Dodoma Polisi wanatumia *Order Paper* kuandikishia namba ya kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Traffic Police* wanaendesa pikipiki bila kuwa na kofia maalum. Je, Askari huyu atamkamataje mwananchi asiyevaa kofia?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha Askari anapewa likizo ndefu ya miezi mitatu lakini halipwi mshahara wake. Hivi Wizara inafikiria Askari huyu mfano anatoka Rukwa aje mpaka Arusha, nauli yake na familia ambayo hulipwa baada ya likizo tena anachukua muda mrefu, hapa tayari ameshavuruga matumizi ukizingatia mshahara ndio huo wa 150,000/= bado makato! Wizara iangalie jinsi ya kuwalipa mishahara yao yote ya likizo ili wasumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwepo na wahamiaji wengi nchini ambao hawana vibali lakini hata wageni wanapoingia nchini, *Arrival Form No.TIF10*, moja ya sababu zinazoulizwa katika *form* hii ni kama mgeni anakuja kutafuta kazi (No. 3), hivi kweli mgeni anaweza kutoka katika nchi yake na kuja Tanzania na kupata kibali cha kufanya kazi *on arrival*?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wafanyakazi wengi wa kigeni wakifanya kazi ambazo wazawa wangeweza kufanya kwa mfano pale *Shopaz Plaza*, kuna Wahindi kutoka India wanafanya kazi ya kusimama nyuma ya (*Cash till*) za malipo kuchunga wale ma-*Cashier* wasiibe na kuna Wachina wengi tu wanafanya kazi kwenye *garage* kukwangua rangi za magari. Pamoja na soko huria na wawekezaji, hivi Uhamiaji wanatoa vibali kama hivi kwa wageni wakati Watanzania wanaweza kufanya kazi hizo? Je, Watanzania wanaweza kwenda India au China wakapata kibali cha ulinzi *supermarket* au kukwangua magari? Naomba majibu kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji itueleze wageni (*visitors*) watatozwa kiasi gani cha visa? Sababu *multiple* ilikuwa 100\$ na single entry \$ 50 ina maana sasa *single entry* ni \$ 25?

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Polisi kwa kweli yapo katika hali mbaya sana. Tukumbuke hawa Askari nao ni wanadamu na wanafamilia. Unakuta Kambi za Polisi mpaka leo nyumba zao ni za Bati kama waziitavyo (*Full Suit*) na ukizingatia hali ya hewa duniani ilivyobadilika, nyumba zile zina joto inapelekea Askari hawa kulala nje ya nyumba na hii inawapelekea kuumwa na mbu hata kuugua malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu, Askari hawa unakuta nyumba nne, wanashirikiana choo kimoja na bafu moja. Kila Askari ana familia, nyumba hizi za kambi pia hazitoshii Askari wetu. Askari wengine wanaishi uraiani, hii ni hatari kwa mfano Askari amekodisha nyumba ambayo mmiliki wake ni mhalifu (muuza gongo),

unadhani Askari huyu atamkamata? Au *Traffic Police* anakutana na mwenye nyumba kafanya kosa barabarani mfano tairi zimechakaa, je, atawea kumchukulia hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya Askari Polisi ni ya kima cha chini sana. Polisi wanalipwa shilingi 150,000/= kwa mwezi na *allowance* ya 50,000/= . Tukumbuke Askari hawa wana mikopo, akikatwa mkopo atabaki na nini? Je, Serikali haioni inawalazimisha Askari hawa kupokea hong?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kigezo gani kinachotumika katika Jeshi la Polisi katika kuwapandisha vyeo? Kuna Askari waliolitumikia Jeshi kwa zaidi ya miaka 20 na hawajawahi kufanya kosa lolote lakini hawajapandishwa vyeo!

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaondoa mabasi yote yenyе *chassis* za malori ambazo zinabeba abiria? Waliotengeneza *chassis* hizo sio wajinga kutofautisha chasis 2C mabasi na *chassis* za malori. Je, hii si ni sababu mojawapo ya mabasi mengi ya abiria kupinduka na kupata ajali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wanaolinda Bank za Biashara, je, ni kiasi gani Jeshi la Polisi linapata kutokana na kazi ya kulinda benki hizo? Je, wale Askari wanaolinda katika *bank* hizo wanafaidikaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wataalam wengi katika vikosi mbalimbali kama ujenzi, afya, wengi wakijisomesha hawapandishwi cheo na hii inapelekea Askari wengi wataalam kilikimbia Jeshi mfano Madaktari wengi wanakimbia na kupelekea Jeshi kuajiri Madaktari kutoka uraiani. Cha kusikitisha, wale wanaotoka uraiani wanalipwa mishahara mizuri kuliko Askari Madaktari. Wizara ifikirie jinsi ya kuwapindisha vyeo wataalam hawa na kuwapandisha mishahara ili wasirubuniwe na kwenda mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shauri la kijana Swai kutoka Moshi alichomwa moto hadi akafariki. Kijana aliymchoma anaitwa Jafari, anayejulikana kama (JJ). Ndani ya Bunge hili, Waziri alitureaza bado wanamtafuta. Ningependa kujua upelezezi umefikia wapi? Mpaka leo Jeshi la Polisi hawajatangaza au kuweka picha ya Jafari (JJ) kwenye gazeti ili kama yupo nchini wananchi waijulish Polisi. Naomba tujulishwe ni hatua gani zilizofikiwa.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia hotuba hii. Nikushukuru Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kagasheki pamoja na watendaji wote katika Wizara hii. Shukrani za pekee ziende kwa Mheshimiwa Kagasheki kwa ziara aliyoifanya hivi karibuni Jimboni kwangu Tarime, kufuatia fujo baina ya wananchi wa Rarya na Tarime, mapigano yaliyotokana na wezi wa mifugo na ziara aliyoifanya katika Mgodi wa North Mara kuangalia uchafuzi wa maji katika Mto Tigite yenye kemikali kutoka mgodini. Kwa niaba ya wananchi wangu, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa namna ulivyoiwakilisha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kuhusu Rushwa ambayo imeenea katika Jeshi la Polisi, kwenye Idara ya *Traffic Police*, Idara ya Upelelezi na kwenye Vituo vya Polisi katika Kata (out post). Baadhi ya Polisi, kazi yao kubwa ni kupokea rushwa kutoka kwa wananchi. Serikali ichukue hatua za kupunguza rushwa. Napenda kuishauri Serikali kuwa Askari wasikae kwenye kituo kimoja kwa muda na Askari wa *traffic* wawe wanahamishwahamishwa, Askari wanapokuwa mafunzoni wawe wanapewa mafunzo ya kila fani hasa *traffic*, kila Askari apate mafunzo hayo ili wawe wanapangwa na kubadilishwa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Tarime, Polisi, huwabambikizia wananchi kesi za mauaji (*murder case*) na kuna mahabusu wengi katika Gereza la Tarime utakuta kuna zaidi ya watu kumi wanatuhumiwa kuua mtu mmoja. Naitaka Serikali iunde Tume ya kuangalia hali mbaya ya Askari kuwabambikizia wananchi *murder case*. Kwa kuwa kuna mapigano Wilayani Tarime, kila mtuhumiwa anaombwa shilingi millioni moja na kama hauna hubambikiziwa *murder case*. Serikali lazima ichunguze ili nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze Mahakimu, Majaji kwa ajili ya kusikiliza kesi nyingi ili kupunguza msongamano ndani ya Gereza la Tarime. Gereza la Tarime, linahitaji matengenezo ya haraka maana ni muda mrefu halijafanyiwa ukarabati. Wafungwa wakati wa masika hunyeshewa na mvua, wafungwa na mahabusu wana haki zao kama binadamu, naiomba Serikali itenye fedha za kukarabati Gereza la Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ilivyoahidi kuwa itaanzisha Kanda Maalum ya Kipolisi katika Wilaya za Ranya na Tarime, ni vema Serikali itimize ahadi yake ili wananchi wasiokuwa na hatia wasiendelee kuuliwa na majambazi wa wezi wa mifugo, ambao wanashirikiana na majambazi kutoka Kenya wenye silaha kubwa mfano K47. Naishauri Serikali, Jeshi la Polisi wapewe silaha nzito na za kutosha ili kukabiliana na majambazi hao maana hutumia silaha nzito na mara nyingi Polisi huzidiwa nguvu. Vituo vya Nyamwaga, Burega, Nyantira na Kegonga, pawepo na Askari wa kutosha kuzuia wezi wa mifugo maana mara zote ng'ombe huibwa na kupelekwa Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pawepo na vikao mbalimbali vya viongozi wa vijiji, kata, tarafa kwa maeneo ambayo kuna vita vya koo. Vile vile pawepo vikao vya ujirani mwema baina ya Kenya na Tanzania katika ngazi ya vijiji, kata, tarafa, Wilaya, Mkoa pamoja na viongozi wa kitaifa kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri Mkuu na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa dini wawe na maombi kwa ajili ya wananchi ambao wanakuwa na mapigano ya mara kwa mara. Pale ambapo hakuna Makanisa, viongozi wa madhehebu mbalimbali wajenge Makanisa, Misikiti ili kueneza neno la Mungu, hii itasaidia sana kuleta amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa koo ambao jamii inawaamini, wawe wanakutana mara kwa mara na kuhubiri amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari za Kata, ziwe za bweni katika maeneo yenye mapigano ya koo ili wanafunzi wanaofaulu waweze kuishi shulenii kwa kuchanganyikana koo na koo, kata na kata, tarafa na tarafa hii itasaidia vijana wetu kuishi bila ubaguzi wala uhasama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari walipwe madai ya posho wanazodai pamoja na kuongezewa mshahara maana kazi wanazofanya ni ngumu na katika mazingira magumu.

Baada ya kusema hayo, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini nashauri, vitendea kazi kwa Askari Polisi, ni vichache hasa magari na mafuta. Pale ambapo gari ipo hasa Wilayani, mafuta hakuna, kwa hiy, *patrol* ya Polisi ni ngumu kufanyika. Wahalifu wapo siku zote, wanapungua wakati pale ambapo ulinzi unaimarishwa, tuache tabia ya kuimariswa ulinzi pale ambapo matukio tayari yametendeka. Jukumu la Polisi ni kulinda raia na mali zake na pia jukumu la raia ni kuwapa Polisi taarifa sahihi za uhalifu pale unapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya Albino, ni kosa kubwa na mauaji ya kikatili kwa imani ya uchawi. Mauaji haya yanailetea Tanzania fedheha kubwa. Polisi na vyombo vingine vya usalama vinaweza kumaliza mauaji haya ya aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka yetu bado iko wazi, maeneo mengi hasa Kigoma na Rukwa. Kwa hiyo, wageni wanaingia kiholesha. Uhamiaji waongezewe fedha, wajenge Maofisi mazuri mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado rushwa ni tatizo kwa Askari wa barabarani yaani *Traffic Police*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto linatakiwa kuimariswa pamoja na kupewa vifaa kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa kasi na majengo yameongezeka sana na Watanzania wengi hawajui kutumia vifaa vya zimamoto. Mafunzo ya mara kwa mara yatolewe kwa raia hata Wabunge.

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nichangie Wizara hii kwa kufikisha ombi la Askari Polisi Pemba (i.e Askari wanaofanya kazi Pemba) wamenituma kumuomba *I.G.P* Mwema, awatembelee Pemba, wanamuhitaji sana kutokana na matatizo mbalimbali ambayo yanawasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi hili limekuja baada ya juhudii zote za kutaka matatizo yao yatatuliwe kugonga mwamba. Wameniambia kwamba haja yao ni *IGP* Mwema na si vinginevyo. Napenda kupata jibu rasmi juu ya ombi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi walioko Pemba, wanakabiliwa na matatizo makubwa ya kutolipwa malimbikizo ya madai yao mbalimbali. Miiongoni mwa madai hayo ni pamoja na posho za safari wanaposindikiza wahalifu na posho za likizo. Kwa

bahati mbaya, madai haya ni ya muda mrefu tangu mwaka 2003 hadi leo. Hili ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara kwanza kuondoa ule mtindo wa Wizara hii kuwataka Askari kujigharamia safari hizo kwa minajili ya kuwalipa baadaye, jambo ambalo halitekelezwi. Lakini la pili ninaomba Wizara ichukue hatua ya kuwalipa Askari hao madai yao haraka iwezekanavyo ili kuwaondolea usumbufu Askari wetu. Fedha za matumizi zipelekwe kwa Ma-RPC Zanzibar badala ya kupitia kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu uliopo hivi sasa wa fedha za matumizi ya Jeshi la Polisi kule Zanzibar kupitia kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar unaleta usumbufu mkubwa kwa sababu fedha hizo zinapofika katika Ofisi ya Kamishna zinakuwa hazigawanywi ipasavyo katika Mikoa ile mitano ya Zanzibar. Kwa bahati mbaya, ile Mikoa miwili ya Pemba ndiyo inapata shida zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pendekezo ambalo linaungwa mkono na Polisi wenyewe kwamba utaratibu uliopo hivi sasa ubadilishwe na kuanzia mwaka huu wa fedha, Makao Makuu ya Polisi iwe inagawa fedha za matumizi kwa Jeshi hilo na kupelekwa moja kwa moja kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa. Tukifanya hivyo, tutaweza kuondoa malalamiko kadhaa ya madai ya Askari na pia matumizi ya uendeshaji katika Ofisi za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Zanzibar kunajengwa Makao Makuu ya Uhamiaji. Jengo hili limechukuwa muda mrefu sasa bado halijamalizika. Tatizo sijui liko wapi? Uhamiaji Zanzibar wanalahimika kutumia masurufu wanayokusanya kuendeleza ujenzi huo kwa maana ya kwamba fedha hizo zitarejeshwa kutoka Makao Makuu Dar es Salaam, bahati mbaya, hali haikuwa hivyo. Naiomba Wizara hii kuchukuwa hatua za makusudi kumaliza ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya uhamiaji Zanzibar na kadhalika kurejesha fedha yote ambayo ilitumika kuendeleza jengo ambazo ziliahidhiwa kurejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata wasaa wa kuchangia hoja hii na naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na uongozi wake, kwa ujumla kwa juhudzi zao katika kufikia malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nipongeze vyombo vyatilini na usalama katika juhudzi zao ambazo zimevezesha kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vyatilini na hasa kupitia Polisi Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Wizara kuboresha eneo la nyumba za makazi kwa Askari Polisi Mkao wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimwia Waziri alivyoeleza kuwa mwaka huu tunajiandaa kwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, naiomba Wizara kuupatia gari Mji Mdogo wa Nanyamba ili kuwezesha Polisi wa Kituo hicho kufanya kazi zao kwa ufanisi hasa kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi Nanyamba, kwa kawaida huwa na gari kwa miaka yote kutokana na unyeti wa eneo hilo lakini sasa hivi kituo hicho hakina gari kwa zaidi ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza Jeshi la Polisi kwa ushirikiano mkubwa walionipa pale nilipohitaji kuwapa elimu ya ujasiriamali na kuwa nao pamoja kinamama hao na kupata mafunzo hayo na sasa kuwa ni kinamama wa mfano kwa kuanzisha benki kwa maana ya VICOBA na wanakwenda vizuri nampongeza Waziri , Naibu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Magereza mengi, hakuna vifaa au huduma nzuri katika maeneo hayo, uchafu ni mwangi sana na hata kusababisha maradhi mengi. Lakini kwa nini Magereza haya yasiwe na muda muafaka wa kutia dawa za kuuwa wadudu hata kwa miezi sita sita tu? Tukumbuke, kifo ni sawa na jela maana iko siku isiyojulikana waweza fika huko lazima tukubali Magereza yetu yawe katika hali ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la uraia kwanza lianzie Magerezani ili wahalifu hao wanapotoka wawe na mwamko tofauti. Mafunzo Gerezani; itasaidia sana hasa vijana wanapopata elimu mbalimbali kwa muda wote wanapokuwa ndani. Kuwepo kwa masomo hayo, itasaidia vijana hao kuwa na elimu hata ya useremala, ufundi bomba, umeme kufyatua tofali na hata ujenzi kuliko ilivyo sasa watokapo bado hawawezi kufanya chochote zaidi ya uhalifu kuliko kutumia ujuzi ambaa labda wangepata wangefanikiwa kuacha uhalifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatisha sana kuona ujambazi unafanywa mchana na hata kusababisha watu kukosa raha hata kidogo. Naomba Jeshi hili kushirikiana na wananchi wanapotoa taarifa ya mhalifu, kuifanya kazi lakini kuwepo na usiri wa kupata taarifa kwani kutoa taarifa ni mojawapo ya ya sababu inayosababisha wananchi kukosa imani na kubaki na siri zao bila kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Polisi na Wakuu wa Vikosi vyote, kwa kuandaa na kuwezesha hotuba kusomwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilipongeze Jeshi la Polisi, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kupambana na wahalifu na kuwezesha wananchi kuishi katika hali ya amani na utulivu. Nawaomba waongeze bidii katika kudhibiti wahalifu wanaoibuka mara moja ili kukomesha tabia hiyo maana wahalifu wanajulikana kwani wanakamatwa mara nyingi na kuachiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kuendeleza mkakati wa kilimo ambao ulifanyika kufuata kanuni za kilimo itasaidia kupata chakula cha kulisha Magereza nyingine zisizo na maeneo ya kilimo na kupunguza tatizo la chakula nchini. Nashauri kila Gereza lijenge maghala ya kutunza chakula. Vile vile vyombo au Jeshi la Magereza liongezewe fedha na viwe vituo vya uzalishaji wa chakula na mazao mengine ili mradi wawe na pembejeo za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza posho za Askari ili kuwapa motisha Askari waweze kuongeza juhudzi kazini. Ombi, posho hizi zipelekwe kwenye mishahara yao ili waone kweli posho zimeongezwa na ziweze kuwasaidia kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho limekuwa la muda mrefu na linaendelea kutolewa taarifa. Naomba Serikali ifanye juhudzi ili vitambulisho hivi vifike mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iongeze juhudzi za kufundisha wanawake angalau ifikie asilimia 30%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nyumba za Askari zijengwe katika Wilaya ya Bahi ili kuwawezesha kuishi Bahi ikiwa ni pamoja na kukamilisha Kituo cha Polisi na nyumba ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa ya vikosi vya ulinzi na usalama chini ya Wizara hii hususan Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Kikosi cha Zimamoto na Uhamiaji. Tunaomba waendelee na jitihada zao ili kudumisha amani na utulivu uliopo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, napenda kuwasilisha maombi ya wananchi wa Jimbo langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Manyoni haina Jengo la Kituo kikuu cha Wilaya, hii ni dosari kubwa. Ombi langu ni kwamba tushirikiane kujenga kituo hicho. Mwaka 2009/2010, wananchi tumejipanga kuanza kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi huu. Mimi kama Mbunge wao, nimenunua mashine ya kufyatulia matofali ya mfungamano (*Interlocking blocks*) moja kwa moja kwa Jeshi la Magereza.

Mashine hizi zitasaidia sana kufyatua tofali, Wizara inaombwa kutuunga mkono katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi (W), kuna tatizo kubwa la usafiri. Tunaomba kati ya magari mapya 22 yaliyopangwa kununuliwa na Wizara, moja lipangiwe Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la *Radio Calls* kwa vituo vyatya mbali na Makao Makuu kama Iteka, Makanda, Chikuyu na pia Kintinku, wapewe nyingine mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kilimo – Chikuyu (Manyoni), lina majengo machache na hafifu, hasa nyumba za Askari na Mabweni ya Wafungwa. Tunaomba hatua kwa hatua, majengo hayo yaboreshwe ili Gereza liwe mfano wa ujenzi wa nyumba bora kwa wanavijiji wanaolizunguka Gereza hilo. Kwa kuwa Gereza hilo ni la kilimo, basi lipatiwe zana bora za kilimo kama trekta ndogo za *power tiller*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka 2009/2010, ahsante.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia 100. Wizara na vyombo vyote vyatya dola vinafanya kazi nzuri pamoja na mazingira magumu wanayokabiliana nayo.

Tafadhali naomba nichangie tatizo la malipo ya uhamisho ya Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Mlalo. Madai hayo ni ya toka mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa mujibu wa Sheria na siyo kuendeshwa na wanasiasa wachache kwa kuwalazimisha kuchelewesha kukamilisha ushahidi kwa makusudi, kuwapandikizia kesi wananchi wasiokuwa na hatia na kusababisha msongamano wa maabusu ndani ya Magereza ambao husababisha ongezeko la bajeti ya chakula na mahitaji mengine bila ya sababu yoyote ya msingi. Haya yapo katika Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Kilwa na Lindi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itupie macho Mkuu ili kuepuka matatizo ambayo yanaweza yakatokea pindi wananchi hawa watakaposhindwa kuvumilia juu ya unyanyaswaji huu. Ahsante, nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi na Magereza kwa wale wanaoenda likizo baada ya miaka mitatu mitatu, kwa siku 90, wanaomba mabadiliko ya kwenda siku 30 (mwezi mmoja) kwa sababu huwa fedha za likizo hazikamiliki, akili huchoka kupita kiasi kutokuwa na mapumziko kwa kipindi kirefu, wanashindwa kufanya mambo yao ya ujenzi

na ya kimaendeleo kwa kukosa nafasi na hudhalilika wawapo ndani ya likizo kwani huishiwa hadi nauli ya kurudia katika sehemu zao za kazi, huwa na shida na kadhalika. Naiomba Wizara wakati wa kurekebisha Sheria za Wizara hii, iliangalie suala hili.

**MHE. MOHAMED HABID J. MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Mkoani Pemba limejengwa mwaka 1928. Huu ni mwaka wa 81, vivyo hivyo Mtambile na Kengeja. Mkoani kuna choo kimoja cha shimo na wamechimba wenyewe. Mwaka 2007/2008 Sh. 550,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya ukarabati majengo ya Polisi mwaka 2008/2009 Sh. 630,000,000/= zilitengwa mwaka huu Sh. 400,000,000/= zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri haya majengo mazuri ambayo yameishi tokea mwaka 1928 ambayo yameja nyufa vyoo vyote vibovu, anihakikishie safari hii *rehabilitation money* zitatumika Wilaya ya Mkoani Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafao ya *transfer*, masomoni, wanaofuata wahalifu, manung'uniko, malalamiko ni mengi mno kuhusiana na kuhujumiwa kwa askari wa ngazi za chini mafao yao katika aina zote tatu nilizozitaja hapo juu kitabu au taarifa ya mwaka 2006/2007 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ukurasa wa 284 malalamiko hayo yamelezwa kwa Inspeka Jeneral wa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naongeza la ziada ambalo halikutajwa katika malalamiko hayo, lakini mimi nimeliona na tena ni zito la uvunjaji mwingine wa haki za binadamu, nalo ni kumpa au kumweka askari katika chumba kimoja (*Quarter*) yeye, mke wake watoto wake watatu au zaidi na kufanya haki ya mama na baba zisiweze kufanyika usiku. Huu ni uvunywaji wa haki za binadamu unaofanywa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja tu ya *OCD* ifanye kazi kwa Wilaya nzima: Je, hii ni sawa? Kweli wahalifu watakamatika? Kwa nini Wakuu wa vituo Mkoani, Mtambile na kengeja wasiwe na usafiri hata wa pikipiki?

Ajira za Polisi kwa rushwa na upendeleo, zimegubikwa na rushwa, watu wanatakiwa kutoa chochote, watu wanaajiriwa kwa misingi ya itikadi na ukabila (*reference*' idadi ya Makunduchi – Polisi huko Zanzibar ni kielelezo cha kutosha).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo Mheshimiwa Waziri Masha huamini nenda kafanye tathmini ndogo tu mtagundua kuanzia ngazi za Kamishna hadi *private*. Hivi wengine sio Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa polisi bado wanaogopwa vijijini hakuna ushirikiano, wanatisha watu: Je, huo ndio mfano wa kupata ushirikiano na raia mwema?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba kila Polisi mmoja anatumikia watu 450 yaani 1: 450. Ikiwa kuna upungufu wa askari katika Mikoa mingi huku Tanzania Bara: Je, ni kwanini Pemba na Unguja kuna askari mmoja kwa kila watu 50 (1:50)?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini kila wakati wa kuandikisha daftari la kupiga kura na wakati wa kura kunaongezwa askari ili kutisha watu wasijiandikishe? Hiyo ndio kazi ya Polisi kutisha watu? Je, huo upungufu wa askari Tanzania Bara wasipelekwe tena sehemu nyingine zenyne machafuko kama vile Tarime na Rarya kwenye machafuko badala yake wanaongezwa Pemba ambako kuna amani na utulivu? Je, ni kwa nini hivi sasa Konde na Micheweni amani imechafuka kwa kupelekwa Polisi? Wametumwa na wewe Mheshimiwa Waziri wakafanye fujo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongeze katika mchango wangu wa maandishi kwamba kuna matukio ya ujambazi yaliyofanyika mwaka 2008. Chokocho saa sita usiku ambapo watu wenyе silaha walitumia boti wapatao wanane walimwonyesha mwenye duka na kupora mali yote na kuondoka *untouched*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009, pia wamempora mfanyakishara mmoja huko kijiji cha Chanjaani Michenzani Mkoani Pemba (Maashir) na wakapora.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio yote hadi hivi leo hakuna aliyekamatwa hata kwa tuhuma. Je, askari hawana mafunzo? Je, ni suala la vitendea kazi? Je, ikiwa polisi hawana gari, watamuudu kweli kumiliki boti? Ahsante.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kukabiliana na kumudu majukumu ya kila siku ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatao ndio mchango wangu kwa Wizara hii:-

Kwa muda mrefu wilaya ya Tandahimba imetenga maeneo kwa ajili ya Ofisi ya *OCD* na Magereza. Lakini cha kusikitisha hadi sasa hakuna bajeti yoyote yenye nia ya kuanzishwa ujenzi wa viwanja vilivyotengwa na Halmashauri. Kumbukeni kuwa Tandahimba sasa ni Wilaya kamili ni vyema vyombo vyya ulinzi na usalama vikakamilishwa ikiwa ni pamoa na ofisi na vitendea kazi nyingine.

Kwa kuwa *OCD* - Tandahimba ana gari moja tu linalosaidia kwa patrol na mambo mengine : je, upo mpango gani wa kuwapatia gari lingine ili kuimarisha ulinzi na usalama kwani tunapakana na Msumbiji na gari hilo ukipata tatizo hali huwa mbaya?

Hali ya maslahi ya askari polisi wa Tandahimba haivutii motisha wa kazi hii mgumu. Kwa mfano, askari waliahidiwa asilimia 10 ya kodi ya pango kwa Tandahimba askari wote wanapanga kwa nyumba za watu binafsi na wala hakuna aliyepatwa asilimia ya kodi ya pango. Ni kwa nini posho hii isitolewe?

Kuna tatizo la jeshi kukosa vifaa kama vile *stationeries*, hivi Wizara inashindwaje kuwasaidia vitendea kazi hata *stationeries* ambazo ni muhimu na sio za gharama kubwa kama karatasi ? Ingawaje nguvu kazi kwa Jeshi la Polisi kwa nchi ni askari mmoja watu 1300 (1:1300) lakini Tandahimba hali ni mbaya zaidi kwani ina nguvu kazi ya 1:7000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wizara ichukue jitihada za kupunguza tatizo hili kwa *special consideration*. Hali ni mbaya. Tafadhalii wapunguzie mzigo mzito askari waliopo Tandahimba angalau kwa kuwaongezea askari kwa kituo kikubwa cha Tandahimba na vituo vidogo vidogo nya Katani.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu *Inspector General*, Makamishna wote wakuu wa Idara na askari katika kutekeleza vyema majukumu yao nchini. Nawatakia heri katika kusimamia usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatoa faraja kwa Wizara/Serikali kuendelea kuboresha makazi ya askari na posho mbalimbali. Natoa rai kuwa posho hizo zitolewe kwa muda muafaka na bila upendeleo katika kugawa hizo nyumba mpya zilizojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi, natoa pongezi kwa Wizara kuchukua hatua za kukomesha mauaji ya albino ingawa wauaji hao wanaendelea kubuni mbinu mbalimbali mpya za kuendeleza mauaji hayo kama ilivyotokea hivi karibu huko Mwanza Ilemela. Nashauri elimu iendelee kutolewa kwa wananchi ili waweze kuendelea kushirikiana na walinzi wa usalama katika maeneo yao katika kutoa taarifa za uhalifu huo na mwingineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ajali za barabarani bado ni nyingi nchini na mionganii ya sababu ikiwa ni udhaifu wa baadhi ya askari wa usalama barabarani kukubali kupokea rushwa na kuwaachia madereva wabovu kuendelea na safari zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2008/2009 Serikali iliarifu kuwa Jeshi la Polisi la nchi yetu inapaswa kuwa na wasomi wa utaalamu mbalimbali. Hati hivyo inashangaza kuona kuwa askari wetu wanapopata nafasi za kusoma inakuwa vigumu kupata ruhusa ya kwenda kuijendeleza kimasomo. Je, sababu ni nini? Ni vyema wahusika wakaelimishwa ili vijana wetu wasikatishwe tamaa kwani kwa sasa kuna mwamko mkubwa wa vijana kuijendeleza kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na maoni ya Kamati kuhusu kuongezea Jeshi la Magereza pembejeo na zana za kilimo, kwani wao kama taasisi ambayo ina uhakika wa nguvu kazi muda wote, itaweza kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza kwa kuzalisha chakula chao na ziada kuuza nje mazao yaliyoongezwa thamani kwani wafungwa wengine wana taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono ushauri wa Kamati kuwa kikosi cha Zimamoto kuongezewa vitendea kazi bora kwani ni aibu inapotokea kwamba hata maji ya kuzimia moto huo ni taabu. Naamini wataalam wetu wana uwezo wa kufanya kazi lakini tatizo ni vitendea kazi haba.

Baada ya mchango wangu huo naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence K. Masha na Naibu wake Mheshimiwa Hamisi S. Kagasheki kwa hotuba yao nzuri sana. Nampongeza pia Katibu Mkuu Patrick Rutabanzibwa kwa kazi nzuri. Aidha, nawapa pongezi *IGP* - Saidi Mwema na Wakuu wa Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kwa kazi iliyyotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu napenda kuishukuru Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kuendeleza ujenzi wa nyumba za makazi ya Polisi Wilayani Mwanga. Nyumba hizo zimefanya maisha ya Polisi kuwa bora na familia zao kuishi vizuri. Aidha, katika mwaka 2005/2006, Jeshi la Polisi lilishirikiana na wananchi wa Mwanga kukamilisha Kituo kidogo cha Polisi Lang'ata (eneo la Nyumba ya Mungu) wa Kituo kidogo cha Msangeni Ugweno, kwa kutoa mabati, *cement* na nondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ahadi ya Jeshi la Polisi ilikuwa pamoja na kutusaidia kukamilisha kituo kidogo cha Kisangara na kituo kidogo cha Polisi Usangi. Katika kutoa mchango wao, wananchi wa Mwanga wamekamilisha ujenzi wa kuta zote (katika vituo vyote viwili) na kupiga rafta kama hatua ya kwanza ya kupanua. Kwa hatua iliyofikiwa, tunaomba msaada wa vifaa vya kumalizia vikihusisha mabati, *cement* ya sakafu na neru, *ceiling board*, rangi, misumari na kadhalika. Vifaa hivyo vimekadiriwa kugharimu Shilingi milioni nne Shilingi milioni mbili kwa kila kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutanguliza shukrani zangu za dhati.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEQYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri na watendaji wote. Nampongeza *IGP* - Said Mwema na Makamanda wote wa Mikoa kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya *albino* ni janga ambalo tunalo hivi sasa. Tunaishukuru Serikali kwa kura za maoni na kesi zipo Mahakamani. Lakini naomba nizungumzie ukubwa wa tatizo hili, ile mizizi inatakiwa ing'olewe na mizizi ni hawa wanaotoa pesa kwa ajili ya kutaka viungo. Naamini Jeshi la Polisi linaweza kabisa kufuatilia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi zinaendelea, tunaomba upelegezi uharakishwe ili hukumu ifanyike ili wale wanaotaka kuendelea kuua waogope.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi kwa *albino* ni wa Watanzania wote kwenye maeneo yao na Jeshi la Polisi jukumu kubwa ni lao, usalama kwa raia. Ahsante.

**MHE. MASOVO ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa daftari la kudumu la wapiga kura limeanza kuboreshwa Wilaya ya Micheweni Jimbo la Konde – Pemba tangu tarehe 6 Julai, 2009 Jeshi la Polisi ni vyema likajipange zaidi juu ya kukabiliana na vikosi vya SMZ ambavyo vimeanza kufanya fujo kwa kuwatawanya watu kabla hawajafika katika foleni jambo ambalo sio tu kuvunja sheria bali wanapelekea kuwatisha watu kupata haki yao ya kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya hali ya kukiuka sheria vikosi vya SMZ nilitoa kwa vyombo vya Polisi pamoja na Wizara husika, lakini bado sijapata jibu Jeshi la Polisi na Wizara kwa ujumla lina mpango gani kukabiliana na vikosi vya SMZ vinavyotumika na wanasiaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kuongezeka kwa ajali za barabarani, baharini na kwenye maziwa, majeruhi na vifo vya Watanzania. Je, Serikali (Jeshi la Polisi) lina mpango gani wa kushirikiana na *SUMTRA*, *TRA*, Shirika la Bima, Shirika la Viwango, Wizara ya Miundombinu katika kukabiliana na magari yanayotembea barabarani yasiyo katika viwango vinavyostahili pamoja na kubaini madereva wanaotembea kwa mwendo wa kasi na wengine wakiwa wamelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la uhaba wa vyombo vya uokoaji vilivyo katika viwango bora ili kutoa huduma mara tu inapotokea ajali baharini au kwenye maziwa, hivi Wizara ina mpango gani juu ya kuboresha huduma hii muhimu ?

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji vyeo kulingana na ukuaji au kupanda kwa mshahara, hivyo ninaishauri Serikali upandishwaji wa vyeo uende sambamba na kupanda kwa mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupata ufanuzi, ni kwa nini kuna ucheleweshaji wa kupata haki za Maafisa na Askari wa vyeo mbalimbali walioumia kazini na wanaosubiri fomu za *LDI* 306 za makisio kutoka ofisi za kwenda kwa daktari. *LDI* 329 kutoka ofisi ya kazi Mkao wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mkakati gani wa kuwapatia fedha zao wastaafu mbalimbali pamoja na familia za Marehemu amba walifariki na hadi leo familia hazijapata haki zao na wengine hawapewi pensheni za Marehemu hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Polisi Makao Makuu Kusini Pemba linavuja sana, ni chakavu na ahadi nyingi zimetolewa lakini hakuna matengenezo yoyote. Sambamba na hilo Kituo cha Polisi Kengeja jengo ni bovu ni la zamani tangu mkoloni na Serikali haioni ni vyema kuhama kabisa katika jengo hilo kuepukana na aibu ya hali ya jengo lilivyo na je, Wizara ina mpango gani wa kukarabari Kituo cha Polisi cha Mtambile Pemba Jimbo la Mtambile ?

**MHE. TATU NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba mdhibiti nidhamu ya askari hasa wanaofanya kazi katika Vituo vya Polisi kwenye vijiji na Kata wanaotumia uaskari wao zaidi kuliko sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameonyesha udhaifu wa utendaji kwa kushika sheria mkononi. Wanaotuhumiwa kuomba na kula rushwa kwa wananchi huko vijijini kuliko kutoa huduma. Tatizo hili ni kubwa hasa jimboni kwangu, walikokaa sana katika vituo, zaidi ya miaka mitatu. Sio vyema wakaendelea kubakia ili waondokane na mazoea ya maeneo na kukiuka maadaili ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwa kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara pamoja na askari wote. Pongezi maalum zimwendee *IGP - Said Mwema* kwa kuliendesha Jeshi la Polisi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina matatizo na Wizara hii, ila ipo haja ya kuikumbusha Wizara hii juu ya kero kadhaa hasa za Jimbo la Morogoro Kusini. Lakini haitakuwa sahihi kuzungumzia Jimbo tu bila ya kugusia mambo kadhaa ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ni utata wa uraia wa nchi mbili, kufuatana na maelezo ya Serikali. Suala hili linazungumzia Tanganyika na Zanzibar. Lakini hili siyo linazungumziwa, bali ni uraia wa Tanzania na nchi nyingine. Serikali inawajibika kutoa maelezo zaidi juu ya suala hili. Kama Serikali imekwama kwa sababu yoyote, ni vyema Serikali ikawa wazi badala ya kulizungusha suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie masuala ya jimboni kwangu Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hii nimekuwa ninalisemea kila mwaka, lakini suala hili ni gumu sana. Jimbo la Morogoro Kusini ni jimbo kubwa sana. Hivyo, Polisi kufanya kazi ya kupanda milima kwa miguu kufuatalia majambazi ambao wao wana zana za usafiri zilizo bora na za kuwawezesha kutoroka haraka toka maeneo ya matukio ya uhalifu. Polisi Jimboni ni muhimu kupewa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo hili la Morogoro Kusini lina kituo kimoja cha Polisi tu. Hapa naomba nitoe ombi rasmi la vituo jimboni.

(a) Kituo cha TAWA – hapa wananchi wamejitolea sana na bado kumalizia kwa kuweka milango na sakafu ndani, ninaomba Polisi sasa wamalizie kituo hiki.

(b) Ninaomba Wizara sana kujenga kituo kikubwa cha Polisi pale Mvuha kwani Mvuha ndipo Wilaya ya Morogoro vijijini inapohamia. Hivyo Makao Makuu ya Halmashauri/Wilaya inahitaji Polisi wa Wilaya kuwepo.

(c) Makazi ya Polisi pale Matombo yanatia aibu kwa jinsi yalivyochakaa askari wengine wapo katika nyumba za raia. Huu mchanganyiko wa raia na askari kule vijijini

ni mbaya sana kwani kuna tabia ya kuwa jirani mno na wapangaji wenzake na kumheshimu baba mwenye nyumba hata kama itatokea kuwa mtu huyu ni mhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Morogoro Kusini kumezuka tatizo maalum. Tatizo hili ni la wizi wa mifugo. Wafugaji walioingia jimboni wamekuja na makundi makubwa ya ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawa ni wa makabila matatu. Wamasai, Wasukuma na Wamang'ati. Makabila haya matatu ndiyo yenyenye mgogoro mkubwa wa wizi wa mifugo. Wizi huu wa mifugo unakua sana na kila siku wezi hawa wanaongezeka na mbinu zinaongezeka. Polisi hawa wa jimboni, wakati wanapopata taarifa wezi wanakuwa wamekwishatokomea sehemu mbalimbali. Wezi hawa huwa wanakamatwa sehemu za Ngerengere ama Chalinze ambako ni mbali na Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo naongelea Wilaya ya Chunya. Wilaya tatu za kwanza kuanzishwa nchini mwetu ni Chunya, Handeni na Ujiji – Kigoma. Kwa bahati mbaya sana mpaka leo Wilaya ya Chunya haina jengo la Ofisi ya Polisi ya Wilaya. Hii ina maana hata mahabusu hakuna pa kuwaweka, mpaka wapelekwe Mbeya zaidi ya kilomita 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa hoja ni lini Chunya itatengewa fedha za ujenzi wa ofisi?

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwentezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Masha - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri - Mheshimiwa Kagesheki pamoja na Watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa uwasilishaji wa hotuba na utengenezaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze *IGPG* - Mwema, makamanda na wapiganaji wa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanywa na Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza kuondoa kasoro zinazolikumba Jeshi la Polisi likiwemo la makazi, vitendea kazi, pamoja na kurekebisha malipo ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri ambayo yameelezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kuliangalia

jengo la mbao lililoko katika majengo ya Wizara yake ambalo mna nyaraka muhimu sana za wastaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hilo ni bovu, mchwa washalimaliza nyaraka (*documents*), pamoja na wafanyakazi wanaofanya kazi katika jengo hilo hawako salama. Ninaomba nyaraka na wafanyakazi wahamishiwe sehemu nyingine na jengo kujengwa jipya. Waswahili wanasema, kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa katika Jeshi la Polisi. Kwa masikitiko makubwa kuna baadhi ya askari wa jeshi hili wanavitia doa jeshi kwa kujishughulisha na vitendo viovu nya rushwa kwa kudai kitu kidogo. Vitendo hivi hasa hasa viko katika askari wa barabarani (*traffic*) na kutusababishia ajali nyingi za barabarani, kwa sababu madereva huwa hawaogopi tena, upakia abiria kupita kiasi, mwendo wa kasi na wengine huendesha magari wakiwa wamelewa na hakuna hatua inayochukuliwa kutokana na kitu kidogo alichopewa askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mkuu wa Jeshi hili atupie macho kitengo hiki bado uwajibikaji wake sio mzuri na unaleta hasara kwa Taifa kwa kupoteza nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwa mzima na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchangia bajeti napenda niulizie baadhi ya mambo na namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malimbikizo ya fedha za askari polisi hasa wa Kisiwa cha Pemba, wenye wanaofanya kuwa fedha hizi hazifiki na zaidi zinakwama Polisi Makao Makuu – Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho za polisi ni ndogo, kwa nini Serikali haiwaongezei angalu wakapata kuishi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewesha kesi, kwa nini kesi zetu zinachukua muda mrefu kwa mfano mtu anaweza kuwekwa rumande zaidi ya miaka kumi: Je, mtu kama huyu uliyemweka rumande kwa miaka yote hiyo, ikithibitika kuwa hakuwa na kosa lolote Serikali mtu kama huyu inakuwaje au ndio basi tu anarudi kwake akiwa ameshakufa kimaisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini polisi wetu hasa wa Zanzibar wanajishughulisha na siasa kwa kuwasaidia Chama tawala wakati wa uchaguzi na ni kwa nini wao hawawi katikati baina ya vyama lakini na wao wanajishughulisha kikamilifu? Ushahidi upo mkiutaka. Hata ukiwapa watu wanaoharibu changuzi, basi hawafanyi chochote ilimradi iwe ni watu wa Chama tawala.

**MHE. DANIEL NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, ningependa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi (W) Kasulu cha Wilaya kili jengwa kwa msaada wa *UNHR*. Bila shaka ofisi inahitaji fedha za kurekebisha jengo hili ili liendelee kuwa na hadhi inayohitajika.

- (i) Ukarabati maeneo yenyenye nyufa kubwa;
- (ii) Samani ya ofisi – viti, meza na kadhalika; na
- (iii) Vitendea kazi – *computer, printer, stationeries* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Heru – Ushingo ni mpakani kati ya nchi yetu na Burundi, kuwepo Kituo cha Polisi chenye hadhi ni jambo la muhimu sana (*priority matter*). Sisi Halmashauri ya Wilaya tumejipanga vizuri, tumekusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, matofali, mchanga na kadhalika na zaidi tumetenga eneo maalumu kwa ujenzi wa kituo hicho cha kisasa ambacho pia kitajumuisha nyumba za askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Polisi/Wizara ya Mambo ya Ndani itaamua kuunga mkono juhudii zetu?

Tunahitaji yafuatayo kutoka Wizarani:

- (i) Ramani ya jengo la polisi la kisasa;
- (ii) Ramani ya nyumba za polisi (*Structure* ya “*two in one*”);
- (iii) Fedha za ujenzi – hata kama fedha hizi watapewa kikosi cha Jeshi la Magereza;
- (iv) Fedha kwa ajili ya kupima eneo ili liwekewe alama “*Beacons*”.

Mahitaji hayo ni muhimu ili kuunganisha nguvu ya wananchi. Ninahitaji Wizara itekeleze sehemu yake ili kazi ianzé.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Jeshi la Polisi Wilaya ya Kasulu (*Kasulu - Central Police* na vituo vyake) zinahitaji ukarabati. Nyingine hata zina hatari ya kuanguka. Tafadhali rekebiseni hali hii au zungunzeni na *UNHCR* ili wafanye/tusaidiane kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kasulu lipo mjini sana. Ninapendekeza gereza hili lihamishiwe nje ya mji. Kwa mfano, hapo nyuma zilikuwepo juhudii za kuhamishia gereza hili katikati ya vijiji vya Heru – Ushingo – Kigadye. Eneo hili bado lipo na ni vizuri Gereza la Kasulu lihamie sehemu hiyo. Hatua ya awali ambayo Jeshi la Magereza linawenza kufanya ni kutuma fedha Kasulu kwa ajili ya upimaji wa eneo hilo. Halmashauri ya Wilaya tulishazungumza jambo hili upimaji uanze sasa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yenyeye matatizo maalum ya kiusalama katika nchi yetu ni pamoja na Wilaya ya Kasulu. Napendekeza kwa Wizara tuongezewe askari. Taarifa hizi zipo hadi kwenye Ofisi ya *IGP* – Dar es Salaam. Ni lini askari wataongezwa katika Wilaya ya Kasulu na hata Kibondo/Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kasulu inahitaji *OCS* Mwenye sifa. Kituo cha Kasulu Mjini chenye eneo kubwa hakina ofisi hiyo. Wamekuwapo wanaokaimu kaimu bila tija iliyokusudiwa. Tuleteeni sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri polisi wengi ni safi, lakini wapo wachache sana wanaoharibu sifa nzuri ya Jeshi la Polisi. Nashauri *strongly* hatua za nidhamu zichukuliwe haraka kwa wachache hao wasiofaa.

Kwanza, chunguzeni tabia ya polisi kubambikiza kesi kwa wananchi wa Kasulu, Makere, Manyovu na Heru – Ushingo.

Pili, chunguzeni kwa umakini tabia za rushwa au vitendo vinavyopelekea vitendo vya Rushwa katika Wilaya yangu ya Kasulu na maeneo tajwa hapo juu.

Tatu, chunguzeni dhuluma, vitisho ambavyo baadhi ya Askari Polisi wanawafanya wananchi. Mimi na *OCD* wa Kasulu tumefanya vikao vingi vya mashauriano juu ya mambo haya. Namshukuru *OCD* Kasulu, ananipa ushirikiano stahili.

Mwisho, ulinzi shirikishi ni kitu kizuri sana. Naomba uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWINCHOUM ABDULRAHMAN MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja na pili naipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanya hasa Waziri Masha na Naibu wake Mheshimiwa Kagasheiki, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Idara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa vitambulisho vya Taifa, naelewa mradi huu una sehemu (*component*) zaidi ya kumi lakini lililo la umuhimu zaidi kwa kuanza ni sehemu (*component*) mbili. *Printing* na *Database*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kwa umuhimu wake uliopo tujikite katika maeneo hayo mawili. Watalamu wamshauri vizuri Waziri wao na fedha kidogo sana zinahitajika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi una mpango wa miaka minne, hivyo twende kwa awamu na kutizama vipaumbele katika awamu hizo, nashauri tuanze na ‘*Printing and Database*’.

Mheshimiwa Naibu Spika, umma unatuona hatufanyi kazi/tunasuasua. Turekebishe kasoro zilizopo na nashauri ili kuondoa dhana mbaya na utata vyombo vya ulinzi na usalama vishirikishwe katika mchakato huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni muhimu Kamati ya Bunge iende kujifunza kwa wenzetu waliofanikiwa ambao ni pamoja na Kenya na Rwanda. Wenzetu wa Uganda nao wameanza, si shani wakatutangulia (ari, nguvu na kasi inahitajika kwenye mradi huu) tutawapa nafasi wapinzani kutupiga nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata fununu kwamba mradi huu unataka kuhamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa nini iwe hivyo kila mradi uende huko? Dar es Salaam huko vitambulisho viende huko. Tusimpe mzigo Waziri Mkuu kama hili ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri hii kwako ni heshima na historia kwa Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuijenga upya Kigamboni (kuipanga): Je, Jeshi la Polisi lina mpango gani? Wasilianeni na Wizara ya Ardhi na wa-accommodate kwenye mpango wa mji mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tuna tatizo la mawasiliano ya ki-polisi, naomba boresheni mawasiliano kazi zifanyike kwa kiwango. Vile vile tupatie Honda za doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la ukoselfu wa fomu za kuomba *passsport* Wilayani Temeke na sasa imekuwa ni kero. Ni tatizo dogo lishughulikiwe kwa umuhimu, pia suala la kuanzisha Ofisi ya Uhamiaji Kigamboni nalo ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa limo kwenye mpango, naomba kuelewa limefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Kimbiji imetupwa na haizalishi kwa kiwango kinachotarajiwa na wala hakuna mifugo kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeni na fogeni kissasa, pelekeni wanajeshi wa kutosha na zana za kilimo na mifugo tuone matunda ya kambi hiyo.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, napenda kusema kuwa, pamoja na askari kuongezwa marupurupu, lakini ni ukweli usiopingika kuwa madai ya awali ya askari hawajalipwa kama vile likizo, safari za kazi, askari wanapokwenda masomoni, kwani hutakiwa wajilipie na baadaye Serikali iwarejeshee. Lakini hadi hii leo mambo sio shwari kwani hawarejeshewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumwuliza Waziri, Askari Polisi amesoma katika bajeti yake kuwa watajengewa nyumba, lakini naomba kuuliza kuwa mbona sijasikia hata siku moja kuwa Askari Magereza wanajengewa nyumba? Hii ikoje? Naomba wakati wa majumuisho nipewe ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika naona Jeshi la Magereza limeachwa nyuma sana, kwani Jeshi la Polisi na hata JWTZ wana hospitali zao, lakini sio Jeshi la Magereza, kwani Serikali hailioni hili na hata wao wakakumbukwa. Pia posho zao ni za chini ukilinganisha na Jeshi la JWTZ. Jeshi la Magereza ni Sh. 50,000/= kwa mwezi, ambapo ni Sh. 1,770/= kwa siku. Lakini JWTZ ni Sh. 150,000/= kwa mwezi, ni kigezo gani ambacho kinatumika kwa kuweka madaraja tofauti kwa posho za chakula ? Naiomba Serikali iwaongezee Askari Polisi na Jeshi la Magereza ili nao wapate posho ya Sh. 150,000/= kwa mwezi kama ilivyo JWTZ.

Kuhusu kupanga au upangaji wa nyumba, wafanyakazi wa Uhamiaji na Askari Polisi hulipiwa pango, lakini Jeshi la Magereza hujilipia wenyewe. Pia napenda kuuliza PCP, pale katika Wilaya ya Illemela Kata ya Bugogwa pamejengwa Kituo cha Polisi, lakini hakifanyi kazi na kinatumika na sungusungu. Malalamiko ni mengi kuhusu kituo hiki kutoza watu gharama sana kwa raia, pesa ya ukamataji, mtu umeibiwa unaambiwa toa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba polisi kama hawawezi kuhudumia kituo hicho, basi kifungwe. Ahsante.

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Usalama wa Raia. Nawapongeza pia viongozi wa majeshi ya Polisi, Magereza na Uhamiaji kwa jitihada kubwa wanazofanya licha ya upungufu mkubwa wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuendelea kuuliza na kushauri juu ya mambo yafuatayo kama nilivyofanya katika bajeti za miaka 2003/2004, 2004/2005, 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 bila ya mafanikio!

Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya ya Gereza la Wilaya ya Muheza na nyumba za Maofisa wa Magereza Muheza. Nilimkaribisha aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo Mheshimiwa Chiligati kutembelea Muheza na aliona fedheha kubwa ya hali ya Gereza la Wilaya ya Muheza na nyumba za tope na makuti zinazovuja za Maofisa wa Jeshi la Magereza Wilaya ya Muheza. Hivi kweli ndio stahili halali ya Maofisa wa Serikali kuishi katika nyumba duni kama zile za Muheza! Jeshi hili na Wizara itaendelea kukaa kimya mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kusafirisha mahabusu, kutoka Gereza la Maweni kila siku kuja katika Mahakama ya Wilaya Muheza. Kwa kuwa Gereza la Tope la Wilaya ya Muheza ni dogo, mahabusu wengi hupelekwa Gereza la Maweni Tanga wastani wa kilomita 30 kila siku kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za usafiri sh.100,000/= kwa siku wastani kwa mwaka, siku 320 ni Sh. 32,000,000/= wastani kwa miaka kumi iliyopita ni Sh. 320,000,000/=. Je, Serikali haioni kwa upeo ukubwa wa gharama hizi kwa kutotekeleza mapendekezo yanayotolewa kwa sasa miaka tisa mfululizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muheza ilipokuwa pamoja na Wilaya mpya ya sasa ya Mkinga ilikuwa na vituo vitano vya Polisi. Viwili Jimbo la muheza (Muheza Makao Makuu na Amani) na Mkinga vituo vitatu. Baada ya mgawanyo, bado Muheza ina vituo viwili (Makao Makuu Muheza na Amani). Kituo cha Amani kipo kilomita 30 kutoka Muheza Mjini – Makao Makuu na hakina vifaa, gari wala pikipiki na nyumba hazina ukarabati.

Eneo la Amani ni eneo la utalii, uchimbaji wa madini na mashamba makubwa sana matatu ya chai. Bado nasisitiza na kurudia hoja ya kuimarishwa kituo hicho cha Amani na kuongeza kituo kingine maeneo ya Kata ya Mtindiro au Kwafungo, maeneo ya uzalishaji mkubwa wa machungwa, soko kubwa, barabara nzuri, shule tatu za sekondari, Mtindiro Kwafungo na Songa na idadi kubwa ya wafanyakishara wa machungwa wanaosafirisha nje ya nchi Kenya na Uganda. Uhalifu unavutia sana maeneo hayo kutokana na biashara hizo kubwa kufanyika kwa wakulima wengi kwa fedha taslimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano mzuri kati ya askari wa ngazi zote ni muhimu kwa jeshi la polisi popote nchini. Nashauri viongozi wakuu mtafiti juu ya malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi wakihofu kutokuwepo kwa uhusiano mzuri kati ya viongozi na askari polisi wa chini katika wilaya ya Muheza. Mnavyo vyombo vinavyoweza kutathmini hali hiyo. Mfano, baadhi ya wafanyakishara wa *Bar* hukatazwa kuweka muziki wa kawaida wakati wa saa za biashara (kabla ya saa tano usiku).

Hali ya jumla ya utendaji kazi wa Polisi Wilaya ya Muheza. Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi wilaya ya Muheza. Wamefanikiwa kupunguza uhalifu na ujambazi ulioibuka kutokana na uchimbaji haramu wa dhahabu maeneo ya Tarafa ya Amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekuwa wavumulivu kukosa umeme katika Kituo kipywa cha Polisi Wilaya ya Muheza kutokana na *TANESCO* kukosa uwezo wa kuwafikishia umeme kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaendelea kuwa wavumulivu kwa kukosa maji eneo la Kituo kipywa cha Polisi. Wamefanya jitihada kupata fedha na kuchimba kisima kuitia Wizara ya Mambo ya Ndani na Usalama wa Raia (nawapongeza sana).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL LUAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu, *IGP* na Watendaji wote kazi nzuri ya kuandaa bajeti na kuiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole askari na wananchi wa Bukombe kwa matukio ya ujambazi/utekaji wa magari kwenye barabara zinazopita maeneo ya msituni. Mfano, kifo cha Askari Paschal Matinde aliyeuawa na jambazi tarehe 27 Juni, 2009 kati ya msitu wa Runzewe (Bukombe) – Bwanga (Chato) Bwana alitoa na Bwana ametwaa jina lake libarikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, *IGP* na timu yote kwa ujumla kwa kuendeleza ukamilishaji wa Jengo la Polisi (W) kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 22 Ibara 49.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itenge fedha za kukamilisha jengo hilo. Namshukuru *RPC* kwa jitihada anazofanya za kukamilisha ufunguaji wa kituo kidogo cha polisi Lulembela. Naomba, kasi iongezwe ili kianze haraka sana kwani eneo hilo tunajua hali yake kiusalama. Wananchi wamejitoa sana kujenga kituo hicho tusiwakatishe tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi zisizokamilika/ubambikizaji kesi, katika ukurasa wa 39 Ibara 88, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa nini kesi hazikamiliki? Tunataka ushahidi gani? Kama uongozi wa CCM Tawi na Serikali ya Kijiji, Tawi wameandika barua kutetea. Jeshi linaendeleaje kusema upalelezi bado? Mfano kesi No. MC.19/2008 – USH 695/2008 ya Ndugu Anthony % Julius na wenzake, mbona haikamiliki? Nimemwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wapo wananchi wengine wenye kesi za uonevu kama vile Mzee Kasuluba wa Mjmwema (Uyovu) Ndugu Majaliwa % Andrew, Charles % Mayala na Majuto % Stephano wa eneo la Kasosobe – Bwelwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuutilie na iwatendee haki wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ujambazi, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kukubali kushirikiana na Jeshi la Polisi: Kwa nini Polisi msikubali kushirikiana? Kwani maeneo ya Ushirombo – Runzewe, Runzewe – Bwanga, Runzewe – Nyakanazi – Nyakahura na maeneo mengine ili tulete amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nahisi wanaofanya ujambazi huu ni waasi toka nchi jirani. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie gari Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la motisha kwa Askari wa Bukombe. Askari hawa wanafanya kazi kubwa sana. Mimi sio rahisi kupongeza kwa sababu mnajua Bukombe. Nadhubutu kuwapongeza kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ukiondoa wachache wasio waadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa Bukombe kwa taarifa zangu wamefanikisha kukamata bunduki ya kivita, majamabazi waliolipua Ushirombo *SACCOS*. Kikubwa sana wamekamata mtandao wa mauaji ya *albino* ambao ulishusha heshima ya Taifa letu. Sina taarifa kama wamepongezwa kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie mambo yafuatayo:-

(1) Kwa nini kesi za ubambikizwaji haziishi hasa zinapokuwa zimefika Ofisi ya *RCO*?

(2) Kwa nini askari wa Bukombe hawapatiwi motisha? Kama wanapewa ni wangapi wamepata motisha ya aina yoyote tangu mwaka 2008/2009?

(3) Kwa nini msiunde kikosi kazi cha kufanya upelelezi kesi za Bukombe kama alipounda kikosi Mheshimiwa Rais za kufutilia masuala ya usalama?

(4) Je, mko tayari kuomba JWTZ wakalinde maeneo ya Ushirombo – Runzewe – Bwanga na kadhalika? Ama kuwekwa Kambi ya JWTZ Bukombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuwawezesha Jeshi la Polisi kupambana ipasavyo na ujambazi ambao kwa kiasi kikubwa umepungua. Ili Jeshi hili liweze kumudu kabisa mapambano haya, Serikali iwaongezee Polisi vitendea kazi hasa magari na *helicopter* ili kurahisisha ufuutiliaji haraka watuhumiwa wanaotoroka kwa kutumia vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ianzishe kikosi maalum cha kudumu chenye magari na helikopta kwa ajili ya *ku-track* baadhi ya wafugaji wanaohamisha na kuficha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa. Kwa njia hii, madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira unatokana na mifugo yatadhilitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajali barabarani, hasa katika jiji la Dar es Salaam, Wizara itilie mkazo zaidi kwa Jeshi la Polisi kuweka askari wengi zaidi nyakati za msongamano mkubwa wa magari wawakamate madereva wote hasa daladala wanaochomekea wakiwa katika foleni. Adhabu nyepesi kuliko zote ni kuyafanya magari yanayochomekea ku-*park* pembeni kwa masaa matatu na faini juu. Kwa njia hii, madereva hawatatatmani tena kuchomekea na hata abiria wanaozoea kumchochea dereva

wao achomekee huku wakijua Polisi wa barabarani watawachelewesha safari endapo gari lao litakamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya askari katika mji mdogo wa Mikumi yako katika hali mbaya sana. Naiomba Wizara ichukue kilio hiki muhimu katika “highway” ya Dar es Salaam – Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi, Mikumi hali yake ni duni mno. Ikizingatiwa uwingi wa matukio ya ajali na uhalifu mkubwa katika maeneo jirani, pamoja na Mbuga za Wanyama – Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naiomba Wizara ipange utaratibu mzuri wa kuwatengea mgao unaofaa kwa mafuta ya magari kwa Vituo vya Polisi vya Mikumi na Ruhembe, Wilaya ya Kilosa. Ilivyo sasa, inawalazimu wananchi kuchangia mafuta kabla ya kupewa huduma inayohitaji usafiri. Njia hii haileti ufanisi katika utendaji na ufuatiliaji na upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kuongeza posho za Askari Polisi ili kuwamotisha kwa kazi ngumu inayowakabili ya kulinda na kuhudumisha usalama popote walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kuboresha Wizara na Taasisi zake hasa Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi limeimarika na hivi sasa, hasa kwa sisi wanasiasa, Polisi wamejitahidi sana kuzingatia haki za binadamu. Polisi waliokuwa Biharamulo wamefanya kazi nzuri sana licha ya matatizo madogo madogo wakati wa uchaguzi. Busara ya Polisi iliokoa umwagaji damu.

Naomba Waziri ampe pongezi *IGP* kwa uhodari wa Polisi hawa. Hata hivyo, malipo ya askari wadogo ni tatizo. Polisi walio kwenye operasheni walipwe Sh. 3,000/= kwa siku. Posho za watumishi wengine ni Sh. 40,000/= kwa siku. Iweje Polisi wadogo walipwe kidogo namna hii? Hili ninaomba nipatiwe majibu ya kina kwani siwezi kukubali Polisi wadogo waonewe. Mheshimiwa Waziri naomba majibu ya malipo kwa siku kwa polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji wa Kalinzi katika Mkoa wa Kigoma ni mji unaokua kwa kasi sana na niliomba Kituo cha Polisi pale. Ninaomba majibu kama tayari Kalinzi Kituo cha Polisi kinajengwa. Ujenzi wa barabara ya Mwandiga – Manyovu na ujenzi wa Kituo cha Mizani pale Kalinzi kunapelekeea mahitaji ya Polisi zaidi. Ninaomba Kituo cha Polisi Kalinzi kiimarishe na kuwa kikubwa ili kuendane na ukuaji wa mji wa Kalinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko ya wapiga kura wangu waliokuwa Askari Polisi na kufukuzwa kazi kwa kuonewa. EX D.3481 - PC ZUBERI na EX. E 3993 - PC DISMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malalamiko ya askari hawa yamefikishwa kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Kagasheki na majibu yaliyokuja ni kwamba mafaili yamepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa askari Mahakama imewaona hawana hatia. Ninaomba wapiga kura wangu wapewe haki yao, walipwe mafao yao haraka iwezekanavyo. Dhuluma kwa raia ni doa kwa Jeshi la Polisi. Ninaomba Waziri asaidie wapiga kura wangu walipwe mafao yao kwani wamefukuzwa kazi kinyume cha taratibu za Jeshi la Polisi. Ninaambatanisha barua mbalimbali za madai yao. Ninachoomba ni wapiga kura wangu walipwe mafao yao.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpogeza Mheshimiwa Laurence Kego Masha - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri - Mheshimiwa Balozi Khamisi Sued Kagasheki, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujuu pesa zilizotengwa kwa ajili ya vitambulisho vya uraia (Taifa) zimetengwa katika fungu gani? Kama pesa hazijatengwa maandalizi ya miradi ya majoribio (*Pilot projects*) ambayo itaanza kutekelezwa kuanzia 2009/2010 yatakelezwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi cha ujenzi wa Jeshi la Magereza linafanya kazi nzuri na tumeshuhudia kazi zao walipojenga nyumba za kuishi Mkoani Dodoma. Nashauri kikosi hiki kitumike sasa katika kujenga nyumba za Serikali. Hospitali, shule na kadhalika na kama wataalamu hawatoshelezi ni bora wakaajiriwe wenye utaalamu zaidi ili kuimarisha kikosi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa na urasimu uliopo Wizara ya Miundombinu kutokana na mchakato wa manunuvi kama hotuba ya Waziri ukurasa wa 18 aya ya 41 inavyosomeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara nyeti kama hii ni vizuri kuomba kibali cha kununua magari na vitendea kazi vingine kuliko kusubiri Wizara ya Miundombinu wasioelewa unyeti na umuhimu wa magari kwa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo wa mwaka huu wananchi walipiga kura za siri za maoni kwa lengo la kuwafichua wahalifu, wauzaji wa madawa ya kulevy, wauaji wa maalbino na kadhalika. Mpaka sasa wananchi hawajapata matokeo.

Je, upigaji wa kura za siri umeisaidiaje Serikali katika kupunguza uhalifu? Je, kuna watuhumiwa waliokwishakamatwa kutokana na upigaji wa kura za siri?

Mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa katuongoza vizuri. Pia nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kuwasilisha bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa umma wanatakiwa wasikae katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu ili kuepukana na kufanya kazi kwa mazoea na hivyo kusababisha kupungua kwa ufanisi wa kazi. Je, kwa Jeshi la Polisi utaratibu ukoje au wao wanatakiwa wabakie katika kituo hicho hicho kwa muda wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri ya kupambana na uhalifu wa aina mbalimbali yakiwemo ya ujambazi, lakini vitendea kazi walivyonyavyo havitoshi na havikidhi vigezo. Hivyo ni vyema wakapatiwa vitendea kazi vilivyo bora na vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Jeshi la Polisi yaboreshwe kulingana na kazi zao za kila siku za kawaida na zile za matukio mbalimbali yanayojitokeza yakiwemo ya maafa na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Polisi hayaridhishi katika baadhi ya maeneo jambo ambalo linakuwa ni kero kwa askari hao, hasa ikizingatiwa kwamba wanaishi pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, lakini wakati wa uchaguzi, Jeshi hilo hutumiwa kinyume na ule wajibu wao wa kulinda raia na mali zao badala yake wanawanyanyasa, kuwadhalilisha na hata kuwabambikizia kesi baadhi ya wananchi hasa wafuasi wa Chama CUF hasa kule Zanzibar. Jeshi la Polisi linaonekana kuwakosesha haki zao wale wa vyama vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna majanga ya moto yanayotokea mara kwa mara Jeshi la Zimamoto linapaswa kupatiwa vitendea kazi vilivyo bora na vya kutosha ili waweze kupambana na majengo mbalimbali kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa mujibu wa Katiba ya nchi pamoja na sheria na wasijilingize wala kuingizwa katika mambo ya siasa. Kwa kufanya hivyo, kunasababisha wananchi wakose imani na jeshi hilo. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa vizuri hotuba ya Wizara hii na kutuletea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo raia wengi sana kutoka nchi za jirani wanaingia kwa kupitia mipaka yetu. Ni hatari sana kwa usalama wa Taifa letu. Silaha kubwa, nzito za aina mbalimbali zinaingia nchini na ndizo zinazotumika kufanya uharamia na ujambazi hapa nchini. Hakuna Mtanzania mwenye uwezo wa kumiliki *submachine gun (SMG)* na wala hairuhuswi. Lakini kila leo silaha hizi zinakamatwa zimefanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifa kwamba baadhi ya askari Polisi wamekuwa wanaazima silaha kwa majambazi usiku kwa makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la baadhi ya Polisi kushirikiana na wahalifu hasa waporaji na vibaka. Hali hii inasikitisha na ndio maana vibaka hawapungui na kila leo wanaongezeka. Taarifa hizi wale vibaka wanazungumza wenyewe na askari wenyewe ukienda kuripoti tukio pale Polisi wanasema tunawajua vibaka hawa hadi wanapokaa. Vibaka wakishapora wanapeleka fungu fulani kwa askari Polisi ili wawalinde pindi wakamatwapo. Hili ndilo linalosababisha na wananchi kuchukua hatua mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali na hasa Wizara hii ifanye uchuguzi wa kina kubaini askari hawa wasio waadilifu. Mimi nina mifano hai ya karibuni. Raia anaibiwa mali zake, anaripoti Polisi. Polisi anamwambia tunaomba utoe pesa tuweke mafuta kwenye gari ili tufuatilie tukio lako. Kweli jamani hii ni halali?

Mheshimiwa Naibu Spika, tena raia huyu ambaye kaibiwa hata pesa hana hata senti anaambiwa aende kutafuta pesa alete ili wapewe vijana wafuatilie mali zilizoibowi. Raia wakisema Polisi wanakula na wahalifu, wanakosea? Kwa nini Polisi wawafahamu wezi, wajue wanafanyia wapi wizi wao, wajue mpaka makazi yao kama hawali nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ubambikaji kesi kwa raia ni tatizo katika maeneo mengi sana. Wananchi wasio na hatia wanabambikwa kesi mbaya na kwamba hana uwezo wa kujitetea anafungwa.

Askari wanatumiwa na wanasiasa kukandamiza raia wasiokuwa na hatia na hasa wa Vyama vyta Upinzani. Askari anapewa *order* na *OCD* na *OC CID* aende kumkamata raia bila kuwa na uhakika kakosa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kama haitaangaliwa ni hatari kwa usalama wa nchi. Hawa askari kwanza ni wachache sana, wananchi wakiamua kuwarudi hawataweza kuishi na familia zao kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari ni walinzi wa amani na usalama, wasiwe wanasiasa na wasitumiwe na wanasiasa. Nashukuru.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP, DCI* na watumishi na askari wote kwa jitihada wanazofanya za kulinda mali na kuhakikisha usalama kwa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo bado uhalifu umekuwa mkubwa sana. Hivi sasa hasa majambazi wanaotumia silaha, maeneo ya Jimbo langu hasa Tandale, Mkwajuni kuja Magomeni kwenye msitu wa Kifo, Mwananyamala, Kigogo, naomba sana Jeshi hili la Polisi lizidishe juhudhi kupambana na uhalifu. Makundi ya wahalifu wakiwa na silaha za moto, mapanga, visu na kadhalika, wanawavamia wananchi majumbani mwao na maeneo ya biaashara na kupora mali zao bila hata kukamatwa, wengine wanavizia magari kwenye foleni na kwenye *traffic light* na kupora vitu mbalimbali. Uhalifu huu umeanza kushamiri sana hivi sasa. Tafadhalini chukueni hatua haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya Askari, bado naendelea kusisitiza ujenzi wa nyumba za askari hasa Magomeni Polisi, Kijitonyama Mabatini, *Oysterbay*, askari wanaishi kwenye mabanda kama ya kufugia kuku. Namwomba tena Waziri atembelee vituo hivyo nilivyovitaja akaone askari wanaishi vipi. Hii ni mara ya pili naomba afanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu matababu ya askari, kuna matatizo kwenye hospitali za Serikali kwa kukosa dawa. Inabidi askari akanunue dawa kwenye maduka ya dawa, lakini askari huyu harudishiwi pesa alizonunulia dawa, tena akiwa na cheo cha chini ndio kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Ma-RPC waache tabia ya kuwa kama watangazaji wa mpira. Ni wepesi sana kwenda kwenye vyombo vya habari na kutangaza uhalifu uliotokea na mikakati ya kuwakamata wahalifu. Kazi kubwa ya Polisi ni kuzuia na kupambana na uhalifu kabla haujatokea, hii ndiyo sifa ya Polisi, mikakati na mipango ya kupambana na uhalifu ni siri ya Jeshi na sio vizuri kuitangaza maana wahalifu wanaweza kupata mbinu za kukabiliana na mikakati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atueleze kile kituo kidogo cha Polisi pale Jangwani, wanafanya kazi gani? Maana askari anakaa pale ni mmoja na hana silaha na eneo lile lina uhalifu mkubwa sana hasa usiku. Umeme hakuna, watu wanaabiwa, wanaauawa katika eneo hilo.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na nikathubutu kushika kalamu kuandika mchango wangu japo mdogo kuhusu hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Jeshi la Polisi ni makubwa na nyeti sana katika nchi yoyote ile duniani. Kwani jukumu la kumlinda raia na mali zake ni moja kati ya majukumu muhimu ya Jeshi la Polisi. Kwa mantiki hiyo basi, ni lazima Jeshi letu lipatiwe vitendea kazi vya kisasa ili kukabiliana na kazi hiyo pamoja na ufinyu uliopo wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwakani tutakuwa na Uchaguzi Mkuu nchini, ni vyema Mheshimiwa Waziri atueleze wakati wa majumuisho: Je, yale magari ya

maji ya kuwasha wameagiza mangapi? Nauliza hivyo kwa sababu katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri hakutamka lolote kuhusiana na magari ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira katika Jeshi la Polisi bado linaendeshwa kwa kuzingatia itikadi za vyama. Nasema hivyo kwa kuzingatia mchakato unaofuatwa kule Zanzibar na hasa Pemba. Utaratibu ni kupata barua (au kibali) kutoka kwa Sheha ambaye kama sio mfuasi wa chama kinachotawala, hupati kibali chake. Kwa hiyo, ni kusema kwamba kama kijana hajajiunga na chama hicho, basi ni vigumu kupata ajira ndani ya Jeshi la Polisi kwa kule Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko yasiyokwisha juu ya baadhi ya Polisi nchini mwetu kwamba wanakula rushwa katika kutekeleza majukumu yao na hasa wale wa usalama barabarani na watu wamesema kwa kiasi fulani suala hilo ndilo linalochangia ajali za barabarani. Tunaiomba Wizara izidi kulikemea suala hili pamoja na ugumu wa kupatikana ushahidi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi huko vijijini kutokana na uduni wa kuelewa mambo, huwa wananyanyaswa au kutopatiwa haki zao. Huwa wanabambikizwa kesi ambapo hutakiwa kutoa pesa kadhaa ndipo apate kuachiliwa. Kwa maana hiyo, anaweza kuwekwa ndani au kuwekwa Gerezani kwa zaidi ya siku tatu au zaidi ili kupewa muda jamaa zake kuleta pesa zinazohitajika. Huu ni uonevu. Ni vyema Wizara kufanya ukaguzi wa kushtukia sio tu Vituo vya Polisi, bali hata Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameleezea ndani ya hotuba yake kuhusu mazingira ya kazi, askari wetu wa Jeshi la Polisi na wale wa Magereza, lakini ipo haja ya Serikali kutoa umuhimu zaidi juu ya makazi ya askari kuboresha, posho zao na hata mishahara pale hali inaporuhusu maana wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ujambazi nchini bado haijatengemaa. Bado majambazi wanavizia vizia kuona na kupima hali ya ulinzi na mikakati iliyopo ya kuwasaka. Kwa kweli ni watu wenye maarifa makubwa sana. Sasa hapana budi juu ya Serikali kupitia Wizara hii kuandaa mikakati mipya na ya kitaalamu kila siku ili kukabili ana na mitandao ya ujambazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata wasiwasi, hivi hawa majambazi wanapata wapi silaha ambazo wanazitumia katika shughuli zao? Wakati mwingine napata mashaka ya kukubali kwamba wapo baadhi ya askari wetu wanashirikiana na majambazi hawa na kama ni kweli, Serikali itapata shida kuweza kumaliza kabisa janga hili la ujambazi hasa ikizingatiwa kwamba hali ya Jeshi Polisi kama ilivyo katika jamii wamo wengine ni watovu wa nidhamu, hivyo kusababisha Jeshi letu la Polisi kudhaniwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na timu yake Wizarani kwa jitihada kubwa wanazofanya kuimarisha usalama wa raia na mali zao japo bado kuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, bajeti ni nzuri na hivyo naiunga mkono. Hata hivyo baada ya bajeti kupita kwa leo naomba Wizara iyafanyie kazi mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama Kahama bado ni mbaya. Hii inatokana na uhaba wa askari, vifaa na ukosefu wa maadili kwa askari polisi. Ninaomba haya yafanyiwe kazi.

Askari wa vituo vya Kagongwa na Isaka wengi hawana uadilifu, kuna taarifa za uhakika kuwa *OCS* wa kituo cha Kagongwa sio mwadilifu na tayari wananchi wameomba ahamishwe. Hali hii pia inamhusisha *OCS* wa kituo cha Isaka. Tafadhali sana, hawa askari wahamishwe mazoea ya eneo yanaathiri sana uadilifu na utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPEN J. GALINONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya Wizara. Hata hivyo, nina machache ya kuchangia.

Kwanza Wizara hii ina *role* kubwa sana ya kuhakikisha amani na utulivu. Lakini siyo siri kwamba uhalifu umevuka mpaka kiasi kwamba hata Polisi wenyewe wanaohusika na mauaji baina yao (soma habari za Kilombero, Mbanga na kadhalika). Watu kuchukua sheria mikononi ni dalili ya umma kutoridhika na nguvu ya dola. Madawa ya kulevyta yana vinara wanaojulikana lakini hawakamatwi. Rushwa na ujisadi sasa ni jambo la kawaida. Nashauri Wizara ijiulize mapungufu yako wapi na tufanyeje.

Pili, baada yamsimamo huo wa jumla, naomba nitaje mambo mawili yanayohusu Jimbo langu la Kalenga kama ifuatavyo:-

(i) Kalenga ni Makao Makuu ya Kata na Tarafa lakini hayana *Police Post*. Kituo kiko Tosamaganga Kata hiyo hiyo, lakini uhalifu, hasa mauaji ni makubwa. Naomba kituo cha polisi pale Kalenga.

(ii) Shirika moja liitwalo *HEAR* lilifanya utapeli katika Kata yangu iitwayo Magulilwa kwa kuwaibia wananchi zaidi ya Sh. 20,000,000/=. Polisi iliwakamata lakini hakuna kilichofanyika. *RPC* (wakati huo Mr, Nyombi) anafahamu sana. Shirika la aina hiyo kwa jina *COEL* nalo lilitapeli Kata kadhaa. Halikuchukuliwa hatua ingawa sasa limetoweka. Naomba hatua zichukuliwe.

Mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Polisi maeneo yenye bandari bubu. Jimbo la Dimani ni jimbo linalozungukwa na banari bubu

zisizopungua 15 na linatumika kituo cha Mazizini ambacho ni kimoja tu lakini kituo hiki hakina gari hata moja na hii ni mara yangu ya tano nazungumzia juu ya suala hili. Jimbo hili limekuwa likitumika sana kwa kupidishia bangi, madawa ya kulevy, TV, baiskeli za wizi na hivi sasa kuna wasiwasi na silaha pia zikawa zinapitishwa wakati huu tukielekea uchaguzi mwaka 2010. Naomba sana Wizara yako ikipatie kituo hiki cha Mazizini gari maalum ili ihudumie maeneo haya ya Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji silaha kwa watu binafsi, nimeshawahi kuzungumzia juu ya suala hili na Naibu Waziri akajibu kuwa atafanya ufuatiliaji kwa kujua ni akina nani hasa ndio wanaohusika na rushwa ya utoaji wa silaha kwa mtu ambaye sio mhusika na ombi lilopelekwa. Nina maana, hivi kwa mfano mimi Hafidh Ali nimeomba kupatiwa silaha na kufuata taratibu zote, lakini inapofika hatua ya mwisho ya kutolewa silaha hiyo kwa mhusika, silaha hiyo hupewe mtu mwingine katika njia ya rushwa kwa kutumia taratibu za mwombaji mwingine? Suala hili bado sijapata taarifa ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya kukabilina na uhalifu Zanzibar, Zanzibar, uhalifu umeendelea kuongezeka na askari polisi wanashindwa kukabiliana nao kwa sababu usafiri hautoshi. Nafikiri ingekuwa vyema kama ilivyo Bara kuwe na usafiri maalum kwa kitengo cha kukabiliana na ujambazi pale Zanzibar ili wakati wote wawe tayari kukabiliana na ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uraia wa nchi mbili, bado hatujafikia wakati muafaka wa kutekeleza suala la Mtanzania kuwa na uraia wa nchi mbili kutokana na uhalisia jinsi ilivyotokea muungano wa Tanzania upande wa pili wa Tanzania kwa maana ya Zanzibar bado hakujawa shwari kwa sababu bado wapo watu wanaoshabikia suala hili kwa faida yao ili watumie mwanya huo kuleta fujo katika chaguzi za kule Zanzibar. Lakini wajue kuwa Mtanzania mwenye uraia wa nchi mbili bado haijsaidii Mtanzania huyo kuwa mpiga kura kwa sababu Katiba ya Zanzibar haitoi kibali cha mtu huyo kuwa mpiga kura mpaka awe na kitambulisho cha uzanzibar kitu ambacho hupewa Wazanzibar wanaoishi Zanzibar na siyo vinginevyo.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara na wale wote walioshiriki kuitunga bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti hii kuwa nzuri lakini bado tunahitaji bajeti ijayo iongezwe zaidi ili Jeshi letu la Polisi liimarike zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Jeshi letu la Polisi maslahi yao ni madogo sana kutokana na kazi zao, kwa hivyo, tunahitaji yaboreshwe na vile vile wapatiwe vitendea kazi nya kutosha, nyumba za kuishi ili waondoke kukaa uraiani wapatiwe magari ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya *FFU* Matangatuwani, majengo yao ni mabovu sana. Ni aibu kukaa askari hao na ni hatari. Kwa hiyo, naomba iboreshwe kwa baajeti hii ya mwaka 2009/ 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Polisi iliyoko Konde, majengo hayo ni mabovu na yanatisha. Ni aibu kuambiwa kuwa nyumba zile zinakaa askari wetu, tunawahatarishia maisha yao katika kituo hicho kwa hiyo waonewe huruma kwa bajeti hii, waangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari polisi ni haki yao kupata uhamisho. Kwa nini hawapewi? Askari anakaa miaka nenda miaka rudi mpaka anazeeka hapewi uhamisho. Wkipandishwa cheo pia hawapewi nyongeza zao za fedha, wanabaki na cheo kwenye nguo zao tu. Ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wanapofikia wakati wa kustaa fuwanahangaika sana kuhusu pensheni yao na wengi wao wanafuatilia mpaka wanaku fa hawajapata mafao yao na hapo askari anapokufa, basi warithi wa Marehemu kama watoto au mke tunaomba wasihangishwe, wapewe kwa muda muafaka ili wapate kuanza maisha mapya. Naomba liangaliwe kwa uangalifu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza. Askari wa Magereza nao wana matatizo sana. Kwanza hawana vitendea kazi, hawana makazi mazuri, nyumba zao wanazoishi ni mbovu, hawana usafiri, magari yao mengi ni mbovu, Askari wa Maagereza ni lazima wapewe vifaa vya kutosha kwa sababu wana kazi ngumu ya kukaa na wafungwa kwa sababu wafungwa wako tofauti. Wengine ni majambazi, wengine ni wahalifu. Hawana huruma, wanaweza kumgeuka askari na kumhujumu. Basi lazima tuwe na imani ya kuwaongeza mishahara yao pamoja na posho waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU S. N. MAHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri. Naomba kuchangia yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vingi havina *stationery*. Mshitakiwa anapaswa kununua karatasi mwenyewe, hii haitoi picha nzuri ya kiutumishi.

Ukosefu wa magari katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya unasababisha polisi kutumia magari ya watuhumiwa au ya wenye kesi zao. Hili nalo halipendezi. Mfano, Wilaya ya Mkinga sio siri inahitahji kupewa upendeleo hata ikibidi kupunguza kupeleka mipakani kama ilivyo Mkinga. *OCD* anafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa huruma kubwa, mamwombea gari tena gari nzima sio mbovu au kuu kuu. Mkinga ni mpakani mwa Kenya na Tanzania, Tanga/Mombasa, mpaka huo hupitisha watu wa aina mbalimbali, wahamiaji haramu, madawa ya kulevyta, biashara za magendo, wavuvi haramu kutoka nchi jirani, majambazi wa magari na kadhalika. Kwa kweli bila usafiri wa kuaminika amini usiamini atashindwa kutimiza wajibu wake.

Nakiri kupokea barua yenyenye kuelezea kuwa mnafanyia kazi, nawasihi mpatieni gari, Mkinga kugumu sana. Askari barabarani wa Dar es Salaam baadhi yao wamezoea rushwa, hawana hata haya namna wanavyolazimisha. Mifano mingi ipo, naweza kuwasilisha kama itabidi. Baadhi yao lugha zao chafu mfano, “Mumeo atakukuta sello”, “umeiba gari ya mumeo kwenda nje atakupa talaka”, Maneno haya yanahusu nini kwa kosa lolote lile liwalo kama sio kudhalilishana? Nashauri wafanyiwe *counseling* ili wawe na lugha nzuri. Walio wengi ni wachapakazi ninawapongeza wote, hongereni sana.

**MHE. VEDASTUSI MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri yeye binafsi, Naibu wake pamoja na jeshi letu kwa kazi nzuri ya kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba za Askari Polisi ni kubwa na wanaishi kama wakimbizi. Naomba baada ya Bunge hili tuandamane kwenda Musoma na tuone jinsi ya kuwasaidia kupunguza tatizo hili kubwa. Wanatumia fedha zao kufuata wahalifu mbali na inachukua muda mrefu kurejeshewa. Serikali itamalizaje tatizo hili ?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini fedha wanazokusanya kiasi kisibaki kwa ajili ya ukarabati mdogo pamoja na samani za ofisi kama viti na meza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo yao, zipo vile vile changamoto walizonazo polisi kama ifuatavyo:-

- Polisi wanababisha kero ndogo ndogo kama kuwakamata wachuuzi wa samaki wakidai wana sumu huku hawana utaalamu wala vyombo vya kupimia.

- Polisi wanaweka *barrier* barabara ya Ramadi Musoma wakiomba fedha kwa wafanyabiashara wanaopeleka chakula Musoma pamoja na kuwa na vibali.

- Polisi wanafunga vituo mapema kuanzia saa 12.00 za jioni na uhalifu mkubwa unatokea usiku na hii ni kero kubwa kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu Serikali imejipanga vipi kupunguza matatizo hayo ambayo ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuruhusu vijana wa boda boda kusafirisha abiria na kujipatia ajira. Napenda kufahamu ni lini vijana hawa watapewa mafunzo ili ajali za barabarani ziweze kupungua na pamoja na kupunguziwa gharama za usajiri wa leseni ?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza Mishahara yao bado iko chini, Serikali imojiandaaje kuwasaidiaje? Uniform za askari magereza bado ni tatizo kubwa

kwani askari wanadiriki kubadili sehemu ya ndani kuwa ya nje kwa kuwa zimechakaa. Wizara imejiandaaje kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wawapo Magerezani ni vipi Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba wanapata mafunzo ili baada ya kifungo wawe na ujuzi wa kuendesha maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada kubwa za kuwatumikia wananchi na ni vyema ukatambua wananchi tunaona zaidi mapungufu kuliko mafanikio. Nasema msife moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Ahsante.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kipekee kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nalipongeza sana Jeshi la Polisi akiwepo *IGP - Mwema*, makamishna wote na watendaji wote wa Jeshi hili. Kipekee pia, naomba nimpongeze sana *RPC Sirro, OCD* wa Kilindi na Ofisi yake yote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri Kilindi ni wa taabu sana. Gari moja *Landrover* liko njiani wiki mbili na wiki mbili lipo *grounded*. Ipo pikipiki moja, hivyo utakimbiza jambazi kwa pikipiki? Naomba katika magari 22 nasi tufikiriwe kupata gari moja, kama itashindikana, basi tupewe hata hayo yatakayobadilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo zamani palikuwa na *Police Post*, tulikuwa na askari wanne tu. Hivi sasa tuna *OCD, OCS, OC – CID*, maaskari sita, hakuna ofisi, posti imekuwa ndogo sana. Tunaomba tusaidiwe kujenga Kituo cha Polisi.

Makazi ya askari kuanzia *OCD*, wanakaa uraiani, jambo ambalo si sahihi. Wananchi wako tayari kuchangia nguvu zao.

Kwa niaba ya wananchi wa Kilindi naomba kwa heshima nikumbushe kwa mara ya tisa ahadi aliyotoa Mheshimiwa Chiligati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kutoa mabati kwa Kituo cha Polisi cha Kata ya Kikunde. *RPC Sirro* kwa uchache wake amechangia bati chache yeche binafsi, baada ya kuona jitihada za wananchi. Naomba basi ahadi hii ikamilishwe. Naibu Waziri Aboud akiwa Dep. Min., aliahidi kutekeleza aidha na Naibu Waziri – Mheshimiwa Kagesheki, nimemkumbusha mara kadhaa. Eneo hili ni muhimu kwani wachimbaji madini haramu ni wengi sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe wote walio mahabusu sio lazima kuwa ni wahalifu. Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje/Usalama ilipata fursa ya kutembelea gereza la Keko. Mahabusu walitoa malalamiko yao kuwa Wabunge wengi wamekuwa wakienda na kuwasikiliza kana kwamba ni maonyesho bila kutekeleza hata tatizo moja. Walisema wamechoshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malazi ni *against* haki za binadamu kabisa, wamesongamana sana. Hakika haistahili. Kumbuka hawa sio lazima kuwa ni wahalifu.

Kuhusu chakula, tulishuhudia wahalifu waliokamatwa kwenye meli ya uvuvi, wanakula *breakfast* ya nguvu, chakula cha mchana na cha jioni. Bali wale mahabusu wa ki-Tanzania wanakula mlo mmoja usiovumilika. Wakauliza, wale wameshtakiwa kuwa ni wahalifu wamevua bila kibali, hivyo ni wizi. Sasa wanasesma wao wanashaktiwa kwa wizi, kwanini pawe na tofauti ya chakula? Mamlaka ilituarifu kuwa wale wanahitaji kuwa *treated according to international standards*. Hili Mheshimiwa Waziri unalisemeaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, *paragraph* ya 25 ukurasa wa 11 inatia matumaini kuwa shughuli inaendelea na *paragraph* ya 26 inaonyesha sura tofauti kana kwamba mambo sio shwari. Binafsi ninaomba Waziri utueleze kwa uwazi tatizo ni nini kama lipo. Kama hakuna, ni nini kinaendelea? Inaogopesha kuzungumzia waraka wa *Cabinet* wakati *procurement process* imeanza. Sasa hivi tunataka kuona vitambulisho, haijalishi kuna vikwazo gani, ‘*what we need is*’ vitambulisho. Naomba ufanuzi juu ya suala hili nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Wizara yake yote kwa kazi nzuri katika mazingira magumu. Ahsante.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Aidha, natoa shukrani na pongezi kubwa kwa Hotuba ya Mheshimiwa Lawrence Kego Masha (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Askari Polisi wanaokaa barabarani. Kuna wanaofanya kazi zao vizuri, lakini kuna wanaofanya kazi zao vibaya na wanaleta kero kwa wananchi na wanaweza wakasababisha CCM tukanyimwa kura kwa ajili ya kero hizo.

Mfano, magari yanasmamishwa sana barabarani kwa kilomita chache sana. Hii ni kero na wanaonewa ni wenye magari madogo. Nasema hivi kwa sababu siku moja nilipanda gari dogo, nilisimamishwa zaidi ya mara 12, lakini wanachosema si maneno ya kikazi. Utakuta gari haliendi kasi, lakini unaambiwa gari linaenda kasi sana weka pembeni; kwa wewe toa Sh. 20,000, lakini angekuwa mwingine angetoa Sh. 40,000! Mimi nikamwambia sitoi hata senti tano. Nikatoa kitambulisho changu akasema basi Mheshimiwa nenda. Nikamwambia kumbe ndivyo

mnavyofanya? Nami nasema naomba mfuatilie sana jambo hili, kwani ukiona kipindi cha *Ze Original Comed* kinaigiza, ujue jambo hilo lipo angalieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Askari Polisi anapofariki. Polisi wa kawaida anapofariki, linatolewa gari la kumpeleka kwao kwa ajili ya mazishi, lakini kinachonisikitisha, hawatoi chakula wala chochote. Hivyo, mwili wa marehemu unapofika nyumbani, ndugu wanaanza kuhangaika kama marehemu hakuwa mfanyakazi. Naomba Askari Polisi anapofariki ahudumiwe kama wanavyofanya JWTZ, wanatoa chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie askari Magereza. Kilimo Kwanza kianze Magereza. Yapelekwe matrekta ya kutosha na zana zote zinazotakiwa, kwani hawa wafungwa ni binadamu na wanatakiwa wafanye kazi za kuzalisha kwa kissasa ili watakapotoka huko, waweze kujitegemea kama walivyofundishwa gerezani. Aidha, wapewe mahitaji yote ya kawaida kuanzia chakula, uniform na sehemu ya kulala na nguo za kujifunika, kwani gerezani ni “Mtakuja” kila mtu anaweza kwenda bila kutegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze FFU, kwa kazi yao nzuri wanayoifanya, nasema hongereni sana.

Mwisho, nawashukuru sana kwa gwaride wanaloofanya katika sherehe mbalimbali. Binafsi wananifurahisa sana FFU, Askari Polisi wa kawaida na Magereza. Aidha, nawashukuru Askari Polisi wa Magereza Wanawake. Naomba muwapeleke kozi na masomo mbalimbali ili nao washike nyadhifa za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU K.P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Napenda kuitumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na kwa kuisoma vyema sana. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii, ambaye kama Waziri wake ni mtu rahimu, mpenda watu, hana makundi na yuko karibu sana na watu wa aina zote. Bila shaka, sifa hizi za Waheshimiwa Mawaziri hawa, zinachangia katika utulivu wa Jeshi la Polisi tunaowaona sasa. Waendelee na umakini huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza watendaji katika wizara hii hususan kwa michango yao katika kuboresha hotuba ya wizara hii bila shaka ushirikiano wao ndani ya wizara umechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi mbalimbali, napenda kutumia fursa hii, kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri na za kizalendo linalozifanya, kudhibiti uhalifu nchini hasa siku za karibuni. Nchi yetu ilikuwa imeanza kufikia hatua ya wananchi kukata tama, kutokana na uhalifu jinsi ulivyokuwa umeanza kukithiri. Mauaji ya Albino wasiokuwa na hatia, yalichochea wasiwasi na mashaka ndani ya jamii. Hali

inazidi kuwa bora na wananchi wameanza kusahau machungu hayo. Hii yote imetokana na juhudi za makusudi za Jeshi la Polisi. Hongera sana. Nawaomba waendeleze juhudi wasilegeze kamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali na Wizara hii ni kuhusiana na miundombinu ya Vituo vya Polisi; ni vyema Wizara ikaangalia ukaribu wa Vituo vya Polisi na wananchi. Vipo Vituo vya Polisi, licha ya kutokuwa na vyombo vya usafiri, lakini viko mbali sana. Kwa mfano, Kituo Kidogo cha Polisi cha Hungumalwa Wilayani Kwimba, kiko karibu km 30 kutoka Makao Makuu ya Wilaya na km karibu 80 hivi kutoka Kijiji cha Shilina. Kituo hiki hakina chombo cha usafiri. Nilikiombea gari au pipipiki, nikaahidiwa zaidi ya mwaka mzima uliopita. Aidha, niliomba Serikali ijenge Kituo Mwamashimba kama km 30 kutoka Hungumalwa. Jibu nililopewa halikuwa la kuridhisha sana.

Naomba Wizara itafute fedha za kujenga Vituo vya Polisi. Jukumu la ulinzi wa raia na mali zao ni jukumu la msingi la Serikali. Kuwategemea wananchi wajenge Vituo vya Polisi, hasa katika maeneo ambako wananchi wamekatishwa tamaa na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi, kutokana na rushwa na ubambikizaji wa kesi; ni kutegemea muujiza! Hali hiyo ndiyo iliyoko katika Tarafa ya Mwamashimba Wilayani Kwimba. Bado ninaomba Serikali, iangalie upya uwezekano wa kujenga Kituo cha Polisi katika Tarafa hiyo ili kuliweka Jeshi hilo karibu na wananchi na wananchi wawazowee polisi ili wawaone kuwa ni walinzi wao na mali zao, badala ya kukutana nao katika matukio tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu wa Wilaya ya Kwimba yako Ngudu na ndipo kilipo na Kituo cha Polisi cha Wilaya. Wilaya hii ni kongwe na nyumba za makazi ya polisi ni ya zamani na hayakarabatiki, ikiwa ni pamoja na Gereza la Ngudu na nyumba za maaskari Magereza.

Ninaisihi Serikali ijenge nyumba za makazi ya askari wote hapo Ngudu na Gereza jipya la Wilaya Ngudu. Namwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, waje watembelee Kwimba ili wafike na kujionea wenyewe, ubovu wa nyumba za maaskari hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, majanga ya moto hivi sasa yanazidi kuongezeka kadiri maendeleo yanavyoongezeka. Ninaomba Serikali ijpange kwa mambo yafuatayo: Kila Wilaya iwe na gari moja la zimamoto - Kikosi cha Zimamoto; Wananchi wengi iwezekanavyo katika mafunzo ya mgambo na sungusungu, wapatiwe mafunzo ya kuzima moto.

Napongeza sana hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhusiana na ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto.

Naipongeza Serikali kwa hatua inazoendelea kuzitekeleza katika uratibu wa maombi ya wageni wanaoomba uraia Tanzania. Eneo hili ninayo yafuatayo:-

Kwanza, nimpongeze kwa dhati Ndugu Kihomano, kwa kazi nzuri azifanyazo katika Idara ya Uhamiaji. Ninaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kumtumikia ye ye katika nafasi hii.

Pamoja na pongezi hizi, ninalo moja kwa wakimbizi wanaoomba uraia:-

Wakimbizi wako katika makundi mawili; wapo wanaoishi kwenye makambi. Hawa hawajakaa nchini kwa muda mrefu na wakati wowote wanaweza kurejeshwa makwao. Hawa hulishwa, hawalimi wala kuwekeza katika lolote; na wapo wanaoishi kwenye makazi. Hawa wanaruhusiwa kuwa na nyumba zao, mashamba yao na vitega uchumi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kuongelea hiki cha pili. Kikundi hiki wanapoomba uraia, wanapewa masharti ya kuacha nyumba zao, vitega uchumi vyao na mashamba yao na kutakiwa kuhamia maeneo mengine kama maombi yao yatakubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa maelezo. Kwa nini kuna utaratibu huo? Lengo lake ni nini? Je; ni kuwafanya wasiombe uraia hata kama wangependa kuomba? Je, utaratibu huo hauashirii dhuluma kwa watu hao: Mtu amekaa nchini hapa kwa miaka mingi, amezeekaa hapa, kajenga hapa, ana mashamba yake na huenda anaendesha vitega uchumi vyake kwa utaalam mkubwa kuliko wananchi wanaozunguka, kiasi kwamba hata kama wakiachiwa wengine hawawezi kuviendeleza vyema. Kunaweza kukawa na sababu, naomba ufafanuzi; kwa manufaa yapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana niliomba gari la Kituo cha Polisi Kamachumu, lililoegeshwa Polisi Wilaya Muleba. Inasemekana kwamba, tatizo lake lilikuwa ni turbo, kama ni kweli; kwa nini hamlitengenezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushe pia Kituo cha Mpakani – Mtukula. Mwaka jana nilieleza kwamba, pale mpakani mwa Tanzania na Uganda, upande wa Tanzania, panatia aibu. Uhamiaji wana ofisi ndogo sana, haiipi nchi yetu heshima. Mbaya zaidi, hawana hata umeme, wanapata shida. Wakati huo huo upande wa pili wana umeme, wana majengo mazuri kweli panapendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijipange vizuri ipaangalie pale mpakani mwetu na Uganda. Waganda wengi ndio wamejenga kwetu, matokeo yake hata watumishi wetu wanapanga katika nyumba za Waganda (*foreigners*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali ijenje nyumba za kudumu za Watumishi wa Serikali hasa mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iboreshe na hasa ijenge kituo kizuri cha Polisi pale mpakani kwetu Mtukula na Uganda na watumishi wapate nyumba za Serikali za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunalo tatizo kubwa la vitendea kazi kwa polisi. Vituo vyetu vidogo vidogo vikiwemo Muhutwe na Kamachumu, viangaliwe ili vipatiwe usafiri, nyumba na mahali pazuri (ofisi) pa kufanya kazi. Vituo hivi viko karibu sana na mipakani, kwa vyovoyote ni Wasaidizi Wakuu wa Vituo vya Karagwe, Ngara na Misenyi, ambao wakati wowote wakihitaji msaada wa karibu ni yule wa kituo kinachokufuata; wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiimarihwe Kituo cha Kasindaga, ambacho kiko karibu sana na pori lenye ujambazi wa uharamia unaotishia abiria na mali zao. Kituo hiki kikiimarihwa, kitasaidia sana kukabiliana na matatizo hayo. Ikiwezekana kipewe vifaa vya kisasa zaidi maana kiko mpakani au niseme katika Kituo cha mapambano na ulinzi 100%, saa 24, kisaidiwe. Nashauri Mheshimiwa Waziri akakitembelee ili apate nguvu ya hoja ya kikitazama kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba askari asikae katika kituo kimoja kwa muda mrefu sana, maana inapotokea hivyo, wakioa/wakiolewa hapo hapo wakapata wakwe, mashemeji na mawifi, kazi inaanza kuwa ngumu. Kutokana na ugumu wa kazi, wakati mwingine baadhi yao wanatumia wenyeji wao kilitia aibu Jeshi la Polisi kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa. Ninao ushahidi ukitakiwa naweza kuutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchangwo wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hotuba yake nzuri, yenye dira na matumaini kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko ya askari wetu hasa Zanzibar kwamba, wanapokwenda safari au uhamisho, hawapatiwi posho zao kwa wakati muafaka na hivyo, kupelekeea mrundikano wa madai usiomalizika, kutokana na kupuuza ama kudharau madai hayo kuwa makubwa kiasi cha kushimdwa kuwalipa askari haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni madaraka mikoani; kwa nini basi mafungu yote yasikae kwa RPC ili kuepusha usumbufu usio wa lazima?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomwambia askari aende safari ajitegemee unatarajia nini wakati baadaye huwezi kumlipa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini askari tunawaacha kwenye eneo moja la kazi kwa muda mrefu bila kuhamishwa jambo ambalo si utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aende Pemba na akutane na maaskari ili akae nao kikao, wamweleze matatizo yao kwani wana matatizo mengi sana na ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna askari ambao wamehamishwa tangu Agosti, 1999 mpaka leo hii hawakulipwa hata zile pesa za mizigo waliambiwa wakachukue *invoice* pale Azam Marine na wakafuata taratibu zote na wakaahidiwa fedha ikiingia watalipwa gharama zote lakini hadi leo hazijaingia pesa hizo na kwa wakati huo zilikuwa Sh. 98,500 tu; je, leo ni kiasi gani? Mimi naamini pesa hizo zimetoka, lakini inawezekana zimeingia mfukoni mwa wajanja.

Zamani ilikuwa askari wa Zanzibar/Pemba ukiingizwa NMB, mara unapotoka hazina na baadaye NMB Chake Chake. Sasa utaratibu huo umeondoshwa. Hivyo, njia inayotumiwa sasa ni ya usumbufu mkubwa sana kwamba, mshahara wote wa Zanzibar uingie BoT kwanza pale Zanzibar, urejeshwe tena NMB Tanzania Bara na baadaye utumwe tena NMB Chake Chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na Mungu atawasaidia kuyaondoa yale makero ambayo bado ni malalamiko makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakupongeza kwa hotuba yako nzuri. Pili, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa nyumba nyingi za Askari Polisi zikiwemo za Wilaya ya Mpwapwa hazijafanyiwa ukarabati; je; ni limi nyumba hizi zitafanyiwa ukarabati? Je, mwaka huu wa fedha ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa nyumba mpya za Askari Polisi ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

Kwa kuwa Askari Polisi wa Wilaya ya Mpwapwa wanafanya kazi katika mazingira magumu na hususan Askari wa Usalama Barabarani hawana chombo cha usafiri; je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia pikipiki moja ili iwasaide askari hao?

Kwa kuwa katika Bajeti ya 2008/09 Serikali iliahidi kulipatia Gereza la Mpwapwa gari jipy;a; je, kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa hadi sasa?

Kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Maafisa Upelelezi hapa Dodoma; je, ahadi hiyo ya Serikali imefikia wapi na kama ipo ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa kazi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MANJU SA. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natamka kuwa naunga mkono hoja kwa lengo la kumpatia Waziri uhakika wa kutimiza majukumu alijoipangilia na kupangiwa. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninayo machache ya kuzungumzia hasa upande wa Jeshi la Polisi na hususan Kitengo cha Usalama Barabarani. Kadhalika, nitapenda kuzungumzia kuhusu huduma za doria tangu nchi kavu na majini, hususan eneo la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi kutokana na utendaji wa Jeshi la Polisi, unaoelekea kuwa bora kila siku. Pongezi zaidi ziwaendee Inspekte Jenerali Said Mwema, kwa ubunifu alioingia nao katika Jeshi, ambao umelipa hadhi kubwa Jeshi letu la Polisi. Sasa hivi mtazamo wa jamii kuhusu polisi ni wa matumaini makubwa. Kadhalika, jamii inapongeza juhudhi za ushirikishwaji kwa Makamanda wa Polisi wa Mkoa na Wilaya, zinazofanywa na Mheshimiwa Saidi Mwema. Hata hivyo; ni vyema haya kayafanya kwa polisi wa ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo lugha kuwa ni polisi wachache ndio wanaoharibu jina katika kadha ya rushwa. Binafsi, lugha hii siiafiki. Jeshi au Serikali inapobaini polisi wachache, inabidi ifahamike kuwa hawa polisi wachache wanapatikana maeneo mengi ya nchi yetu. Itambulike kuwa, wanapokuwa polisi wachache wanapokea rushwa, kwa mfano, katika maeneo ya Dar es Salaam, Arusha, Tabora, Songea, Iringa, Kigoma, Mwanza na kadhalika, ukijumlisha wanakuwa sio wachache tena, bali ukijulisha maeneo niliyoyataja hapo wanakuwa polisi wengi. Eneo la usalama barabarani, ndilo limekithiri sana.

Ninashangazwa na kusikitishwa na mambo mawili yafuatayo yanayofanywa na polisi barabarani:-

(i) Ikiwa yamefuatana magari makubwa (malori) na magari madogo; askari wa usalama barabarani hupenda kusimamisha magari makubwa (malori/semi trailer), kwa lengo la kukagua na kuyapekua. Magari madogo (shangingi/saloon), huachwa yakapita tu. Hapa magari makubwa huwa ni kitega uchumi cha polisi hawa wa usalama barabarani. Yanasimamishwa ili kuwaneemesha askari wa usalama barabarani. Hivi kwa nini magari madogo hayakaguliwi? Hivi tuna uhakika gani kama magari madogo na hasa usiku hayasafirishi silaha, mihadarati na watu wahalifu? Ni mara chache sana magari madogo madogo kukaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipinga Serikali kuruhusu uraia wa nchi mbili. Wapo wanaonyemelea kupata uraia wa Tanzania kuliko Watanzania wanavyotamani uraia wa nchi nyagine. Wale wanaotushinikisha kushughulikia suala la uraia wa nchi mbili, wanatamani na kunyemelea rasilimali zetu ikiwemo ardhi. Kisingizio cha kupata wawekezaji wa uhakika, hakina msingi. Wananyemelea ardhi tu. Tujikumbushe wale waliowakaribisha kuijunga na Jumuiya ya Afrika Mashiriki, sasa wameanza kutaka kuleta mabadiliko hasi. Wanyarwanda wanataka Makao Makuu ya Jumuiya yahamishiwe Nairobi (eti ndio kati). Hivi kwenda Nairobi kuna maslahi gani kwa jumuiya? Baadhi ya

hawa ndio wanaoshinikiza uraia wa nchi mbili. Napinga kwa nguvu zangu zote. Hatuna uchache wa watu; Jeshi la Polisi au Wizara isiruhusu uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharamia Ziwa Tanganyika: Hapa silipongezi Jeshi la Polisi kwa sababu haliwasaidii wavuvi Ziwa Tanganyika. Wavuvi wanaporwa mali zao wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya uvuvi. Doria ya polisi haipo. Tumeletewa maboti ya doria pale Kigoma, lakini yana zaidi ya miezi minane sasa, hayafanyi kazi lakini katika kumbukumbu za Wizara zinaonesha kuwa tunayo maboti ya doria pale Kigoma wakati hayapo. Kwa wakati huu niandikapo, zipo zana ambazo zimekamatwa kule DRC. Wenye mali wanatakiwa watoe malipo ili wakomboe mali zao zilizoporwa ziwani na karibu kuhatarisha maisha ya wavuvi waliotupwa majini. Natangaza maslahi, mmoja kati yao ni mtoto wa kaka yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2004 ulianzishwa mkakati wa kukipa kilimo cha muhogo umuhimu unaostahili. Yaliteuliwa Magereza 10, likiwemo lile la Ilegala pamoja na lile la Handeni. Je, mkakati huu umefikia wapi? Muhogo ni zao kubwa, lenye soko Ujeruman kama walivyofaidika wakulima wa Tandahimba miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilizungumzia suala la uraia kuhusishwa na ukabila upande wa Kigoma (Uhamiaji). Leo nalizungumzia tena suala hili. Hivi ni nchi gani uraia wa mtu unahuishwa na kabilia lake? Nilisema hapa kuwa Prof. Sarungi ni Mjaluwa wa Tanzania wakati Raila Odinga ni Mjaluwa wa Kenya, kosa liko wapi? Mheshimiwa Edward Lowasa ni Mbunge Tanzania wakati Prof. George Saitoti ni Mbunge Kenya na wote ni Wamasai, tatizo halipo; lakini kwa Kigoma, Msambya (Mbembe) ni Mbunge na Hanzuruni wa Goma (DRC) ni Mbunge, ambaye ni Mbembe. Aliyewahi kuwa Rais wa Congo Brazaville Bwana Pascal Lisuba alikuwa Mbembe. Kwa Hanzuruni na Lisuba kuwa Wabembe hakuna tatizo, lakini kwa Msambya inakuwa nongwa. Kigoma Uhamiaji wameweka unyanyasaji wa hali ya juu, kwa kabilia la Wabembe amba wengi wao wapo DRC. Napenda Mheshimiwa Waziri, anijulishe kama hayo ndio maelezo waliyopewa uhamiaji. Nipate majibu ya kina kwa hili.

**MHE. DKT. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nijikite katika kuchangia hoja iliyo mbele yetu, ambayo ni muhimu sana kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, ningependa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wa Jeshi hilo, kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na IGP ni watu wasikivu na wafuatiliaji wa mambo wanapoambiwa au wanapoombwa. Waendelee na mwendo huo huo wa uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, lakini yapo maeneo ambayo hayapendezi. Kwa mfano, suala la rushwa upande wa usalama barabarani; utakuta maaskari chungu nzima wamejipanga barabarani na kila gari

linalopita barabarani humo linasimamishwa, lakini kesi zinazopelekwa mahakamani hakuna au kama zipo chache sana; je, katika utaratibu huu wanaweza kweli kurekebisha makosa yanayojitokeza barabarani; maana madereva wanajua kabisa kwamba atakapomkuta askari wa barabarani atamhonga fedha kidogo tu bila kujali uwezo wa dereva husika, ubora wa gari, mizigo aliyobeba au gari kubeba watu kupindukia?

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vyta usafiri barabarani vinapoharibika, badala ya kuweka *Reflectors* yanawekwa matawi ya miti makubwa sana na gari hili likishapona matawi hayo ya miti yanaachwa pale pale; na askari wanaoangalia usalama wa barabara wanaangalia na bila kuchukua hatua zozote. Matawi haya wakati mwingine yanababisha ajali kwa vyombo vingine vipitavyo barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine askari hao hao husababisha ajali kutokana na utendaji mbovu, kwa mfano, utakuta askari wana simamisha magari pande zote mbili (yaani huku na kule) au wanajibanza kwenye kona na kusimamisha magari. Sasa ikitokea gari linakuja kwa kasi na lenye matatizo ya breki, inaweza kutokea ajali mbaya, ambayo imesababishwa na uzembe wa askari kwa kusimamisha magari pande zote mbili au kwenye kona. Naomba suala hili liangaliwe kwa makini sana, hata ninyi mliopewa dhamana hii mnayaona. Nawatakia utendaji mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Vituo au Askari waliopo zamu, lugha zao ni za vitisho sana, kiasi cha kuwaondolea utu. Kama tunavyofahamu, mtuhumiwa bado hajawa mkosaji mpaka vyombo vyta sheria vinapomtia hatiani. Kwa mfano, mtuhumiwa ni haki yake kupata dhamana, lakini utakuta askari anafanya ujanja wa kujizungusha zungusha kwa makusudi ili ndugu wa watuhumiwa, waanze kuwatafuta na kuwapa chochote ndipo waandikiwe dhamana. Mfano mzuri wa haya ninayozungumza ni Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya Pale Morogoro Mjini (OCS), Ndugu Magesa, ana tabia ya vitisho, mlaji rushwa mkubwa hata kwa watu wenye kipato kidogo na hana huruma hata kidogo na inaonekana anaye *godfather* kutoka Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri, mtumishi huyu hatumuhitaji kabisa katika Mkoa wetu wa Morogoro. Ushahidi wa jambo hilo ninao. Tafadhali sana mtumishi huyo aondolewe haraka iwezekanavyo.

Mimi ninaamini ninyi ni watu wasikivu na mna busara ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawatakia kazi njema sana na Mungu awape afya njema.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji, kwa kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nilipoingia Bungeni, nikichangia Wizara hii, huiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma juu ya makazi ya Askari Polisi ni

magumu. Serikali ijitahidi kuboresha makazi ya askari wake ili waweze kufanya kazi zao kwa upendo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mfanyakazi anapoomba aongezewe mshahara, hulenga anapostaa fu apate kiinua mgongo kizuri, lakini pia apate pensheni nzuri. Kwa hiyo, tuwaangalie askari wetu wanavyofanya kazi katika mazingira magumu sana, kwani wako wachache na mazingira yenye we na vitendea kazi kama magari, mafuta ni kidogo. Hata kama kituo kina gari, lakini hakuna mafuta. Hivi Serikali haioni kuwa namna hii kazi hazitofanyika vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanazozifanya za kulinda raia na mali zao na pia kupambana na wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, askari anayepambana na majambazi na akafanikiwa kumshika au kumshinda na kumnyang'anya silaha, askari huyo apewe motisha ambayo itaweza kumpa moyo zaidi kwa kazi zake. Motisha hiyo iwe ni fedha na cheo ili wengine waweze kuiga ujasiri huo wa askari wetu. Endapo atapatwa na hasara ya ulemavu au kifo; iwe fidia ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri na Watendaji, kwa kuifanya kazi ile michango yangu niliyoitoa mwaka uliopita. Nasema ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Maofisa wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Nampongeza kipekee, IGP - Mheshimiwa Said Mwema na wasaidizi wake, kwa kazi nzuri anayofanya tokea amepewa wadhifa huu na Mheshimiwa Rais. Namshukuru kwa ushirikiano mkubwa aliotupatia Wabunge wa Mkoa wa Singida, kwa kutatua kero na matatizo kadhaa tuliyomfikishia. Naomba aendelee kutusikiliza na kutusaidia.

Vilevile nampongeza sana RPC wangu/wetu, afande Kaluba, kwa kazi nzuri anayofanya Mkoani kwetu. Anajitajidi kiasi cha uwezo wake, kuhakikisha kuwa Mkoa uko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho limekuwa kero kwani wananchi wanajiliza kulikoni linachukua muda mrefu kiasi hiki? Ni mradi muhimu utakaosaidia mambo mengi. Naomba Mheshimiwa Waziri, anipatie ufumbuzi wa suala hili haraka kwani litaiweka pabaya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kijengwe Kituo cha Polisi kule Ngungira, Kata ya Sepuka mpakani na Tabora, kwani yapo matukio ya hapa na pale kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya vizuri katika michezo hasa *netball* na *football*. Nashauri waunganishe nguvu ili timu ya mpira wa miguu iliyopo kwenye Ligi Kuu ya Taifa, iwe moja tu badala kila mkoa kuwa na timu yake. Wachezaji wazuri, wapelekwe kwenye timu hiyo moja kutoka mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, daladala wanapewa kichwa na baadhi ya askari wa usalama barabarani, ndio maana wanafanya wanavyotaka. Naomba washughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii ya kuchangia kwa maadishi, kwanza, kuwapongeza Viongozi wote wa Wizara hii, pamoja na Taasisi zake zote, kwa utekelezaji wa majukumu yake ya kufaulisha amani, umoja na usalama wa raia.

Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Maswa, napenda kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wote wa Taasisi na Watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Maswa, napenda kusema kwa aina ya pekee kabisa, naungana nao kumpongeza Mheshimiwa Said Mwema, IGP, kwa uwajibikaji wake makini na kwa vitendo vya uongozi wa kuwa mtumishi wa umma, pamoja na msaidizi wake wa Makao Makuu ya Polisi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufafanua kwamba, ametoa namba ya simu yake kwa umma ili aweze kufikika na kutoa maelekezo yanayotokana na mavuno ya sauti za jamii.

Napenda vilevile kusema kwamba, Mheshimiwa Said Mwema, IGP, hana tabia ya ubaguzi wa kusikiliza raia ama kuwa na mwegemeo wa asemalo askari kwa kutangulia kusema ndio mwisho wa kusikilizwa raia dhidi ya maelezo ya maafisa ama askari wa polisi waliotangulia. Maana ya hii ni kwamba, kutangulia kusema sio dira ya ukweli.

Napenda vile vile kuthibitisha kwamba, ana ujasiri wa kusema mazuri na mabaya, kwa dhana ya kujenga mema ya kesho kwa yale yatokanayo na machukizo ya leo. Kwa hiyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha, atambue pongezi hizi na azitangaze hadharani ili patimizwe ushauri wa mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na mcheza ngoma hutunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Said Mwema (IGP), amezuia kesi za kubambikizwa wafanyabiashara huko Maswa na amesaidia wauaji wa kikongwe kukamatwa kwa kumtumia RCO wa Shinyanga aitwaye Seleman A. Nyakipande – SSP Hongera sana.

Mheshimiwa Said Mwema, pamoja na kwamba, yupo Dar es Salaam, ameweza vile vile kuibua ukweli wa makosa binafsi ya watendaji wa operesheni hamisha mifugo kupitia kamati aliyoienda. Hii imetegua hasira na hila za wafugaji dhidi ya Serikali na Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Jeshi la Polisi linajenga dhana ya kuimarisha Polisi Jamii; hivyo haya machache yanathibitisha ushirikishi jamii wa IGP, ambao ukitangazwa utaibua changamoto kwa Viongozi wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linajitahidi kuimarisha na kusogezu juhudu za utekelezaji wajibu wa kutendwa na jamii na askari kwa utekelezaji wa malengo ya usalama wa raia. Napenda kushauri kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Maswa ni pana na wigo wake hauwezi kugawanya kuwa Wilaya mbili ama majimbo mawili kwa uharaka, sasa naomba uhitaji wa pikipiki sita zisaidie kukabiliana na matukio mengi ya uhalifu katika maeneo ya vijiji 120 na kata 18.

Pamoja na mchango huu wa maandishi, naambatanisha taarifa fupi ya kubainisha matukio ya uhalifu uliotokea katika baadhi ya Kata za Maswa. Naomba jibu kwa hoja hii wakati wa kujibiwa hoja za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile kuarifu kwamba, pana malalamiko mengi dhidi ya baadhi ya Watumishi wa Jeshi la Polisi katika Wilaya ya Maswa. Hawa wanaathiri kwa kuvutia hisia ya umma kuhusu uongozi rafiki wa majukumu ya Jeshi la Polisi kwa ufungamano wa kukonga miyo ya umma kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Nakamilisha upembuzi yakinifu ambao utapambanua sura halisi ya mwenendo na mwegemeo wa tabia potufu za baadhi ya maofisa na askari wa Jeshi la Polisi Maswa.

Je, Mheshimiwa Said Mwema atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Maswa aje arejeshe Imani ya umma iliyobomolewa na watumishi askari wachache wabovu waliopo Maswa. Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango huu wa maandishi ujibiwe hasa kwa maombi yote niliyosema. Baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuandaa vizuri sana Bajeti ya Wizara na kuiwasilisha vyema Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri na maombi machache kwa Wizara na Idara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tuliambiwa tutajengewa Kituo cha Polisi cha Wilaya, lakini bado sijaona dalili zozote za ujenzi huo katika Wilaya yangu ya Namtumbo. Naomba kufahamu *status* ya mradi huo ikoje? Fedha zake zilishakwenda Mkoani Ruvuma kwa ajili ya ujenzi huo au ikoje hali ya Mradi huo?

Tunashukuru tumejengewa nyumba nzuri ya Mkuu wa Polisi Wilaya, tatizo tulilonalo ni Jengo la Kituo cha Polisi Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni usafiri; tuna gari moja tu ndio linalofanya kazi Makao Makuu ya Wilaya. Gari hilo ni la miaka mingi na ndio linatumika kama sweeper kwa Viongozi wa Serikali wa ngazi ya juu ya Wilaya wanapokuja Wilayani. Tuna eneo la tarafa ya sasa iliyopo km 220 toka Makao Makuu ya Wilaya na kuna watu wengi sana, hakuna usafiri hata wa pikipiki na gari hili ndio linalofanya kazi ya kwenda mara kwa mara huko kwa kazi mbalimbali, pamoja na kubeba mahabusu kupeleka Songea na kuwaleta Mahakamani Wilaya ya Namtumbo. Vilevile gari hilo linatumika kwa patrol na OCD analitumia hilo hilo. Hivyo, kwa kazi zote hizo, lazima inawawia vigumu katika ufanisi wa kazi za ulinzi na usalama wa raia.

Naomba katika magari yanayonunuliwa kipindi hiki, tupatiwe walau moja na pikipiki tatu na moja kwa Tarafa ya Sasawala katika Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze polisi kwa kazi nzuri wanayofanya na wanavyotekeleza na kuweka katika mipango, ushauri tunaoutoa kila mara. Pili, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusaidia msongamano wa magari Dar es Salaam; ni kazi kubwa wanayofanya lakini ninashauri lazima Serikali kwa maana ya wataalam, waanze kufikiria mpango wa kushawishi wawekezaji wenyewe uwezo, kuwekeza katika usafiri wa bahari Dar es Salaam, *Sea ferry transport*, kwa kuweka magati madogo madogo kuanzia Bagamoyo, Mbweni, Bahari Beach, Kunduchi, Mbezi beach, Kawe, Msasani, Masaki hadi Ferry.

Najua hili ni la Wizara ya Miundombinu, lakini naamini kuna Vikao vya Serikali vya kitaalam, mnakaa pamoja na Wataalam wa Jeshi la Polisi/Miundombinu, kuhusiana na usafiri barabarani. Naamini watakuwepo wawekezaji wenyewe nia hiyo; hivyo tulianzishe kuwe na *Ferry Boats* watu wengi wataacha kutumia magari *unnecessary*.

Mwisho, nawapongeza kwa kuendelea kudhibiti ujambazi; hongereni sana

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, IGP, pamoja na askari wote, hasa wa cheo cha chini, kutokana na kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda raia na mali zao na kuwafanya wananchi waweze kuishi kwa amani na kujilettea maendeleo.

Naipongeza sana Serikali kwa kuifanya Wizara hii iwe karibu na maisha ya kila siku ya wananchi, kwa kuanzisha ulinzi shirikishi na tayari tumeona matunda yake ya kufichua waovu na kwa sasa jamii na askari wamekuwa wanakwenda sambamba. Naomba watu hao waendelee kuhifadhiwa (siri).

Suala la michango kwa askari nchini limekuwa ni kero sana, kumekuwa na michango ya kuchangia Timu za Polisi, lakini michango hii haina mwisho wala kuelezwu fedha hizo zinatumika vipi.

Suala la askari kupandishwa vyeo liangaliwe upya, kwani vijana wetu wanaojiunga na Polisi, baadhi yao wanatumikia kwa bidii na uaminifu mkubwa, lakini hakuna utaratibu wa kuwapandisha vyeo au kuwapeleka kozi kwa kuwapatia vyeo.

Suala la doria kwa askari ni jambo muhimu sana, kwani kuna matukio mengi yanapotokea kama askari wanakuwa karibu na wepesi kuyakabili, lakini kutokana na kutokuwepo basi, wananchi huathiriwa sana na wahalifu bila woga, kwani wanajua hakuna askari yejote atakayetokea haraka.

Mwisho, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ila tunaiomba Serikali, iiongezee fedha Wizara hii ili iweze kufanya kazi vizuri na kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa hotuba nzuri. Napenda nimpongeze IGP, kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rufiji haina Ofisi ya Wilaya ya Jeshi la Rufiji na askari hawana nyumba za kuishi. IGP na Waziri, tafadhali rejeeni barua yangu kuhusu jambo hili.

Naomba majengo ya Ofisi ya Polisi Wilaya kule Utete/Rufiji, Nyumba za Maofisa wa Polisi na Barracks, kwa askari wetu. Tafadhali, isaidieni Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka maelezo ya Waziri kuhusu mikakati ya kuwa na Magereza yatakayokuwa yanachangia kilimo.

Kuna mpango gani wa Serikali kuanzisha Kitengo cha *Internal Affairs* ndani ya Polisi ili kiweze kudhibiti maadili ya kipolisi?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa askari wengi wanapofariki, mirathi yao haipatikani kwa ndugu zao; na kuwa kuna wengi wanaodai mirathi ya ndugu zao wanapofariki na wanapofika Makao Makuu ya Polisi kudai mirathi wanaambiwa

waelezee *Force Number*; huyu ndugu wa marehemu ataijuaje *Force Number* ya ndugu yake aliyekufa? Kwa nini askari anayekuwa zamu asitafute kwa jina lake? Kwa kuwa ndugu haijui *Force Number*; je, Serikali italitatuwaje hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna askari mmoja alikufa tangu 2000 mpaka sasa bado mirathi yake ni tata. Nimetembelea Ofisi ya Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam mwaka 2007, Hazina kwa Waziri wa Fedha kuanzia mwaka 2007 hadi 2009, lakini mpaka leo hivi malipo yanagonga mwamba!

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza kwa kazi nzuri, inayofanywa na maaskari wetu. Naomba Jeshi la Polisi, pamoja na uchache wa fedha zinazotengwa kwao, lakini suala la mawasiliano ni jambo la kupewa kipaumbele hasa katika vituo vyatya mpakani, kwani bila mawasiliano ni sawa na kuwaruhusu wahalifu kuendelea na safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uhamiaji kutoa pitcha na maeleo ya wanaoomba uraia bila kuonekana vizuri au kusomeka ni utata mtupu, ambao hatuelewi inamaanisha nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linalojitokeza hivi sasa la kuua raia kwa msemo wa bahati mbaya, linakua siku hadi siku. Kwa mtiririko huu, tabia hii inaongezeka na hivi sasa wanauwana askari na viongozi wao, kutokana na taarifa za vyombo vyatya habari. Mimi nashauri wakati wa usaili utumike vizuri, pamoja na ufundishaji wakati wakiwa depu uwe wa kinidhamu na unaojitoshaleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ambao wanawekwa katika *immigration* za mipakani na viwanja vyatya ndege, wawe na sifa maalum, kwa sababu hawa ndio kioo cha nchi. Wapo ambao hufanya kazi zao bila uelewa mkubwa na kuisababishia aibu nchi. Hii niliishudhudia Mwalimu Nyerere Airport.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalishauri Jeshi na Wizara nzima ya Mambo ya Ndani kwamba, Viongozi wake wawe wawazi kwa wapiganaji wao, kuhusu ulinzi wa nchi na uwajibikaji wao; kwa sababu umezuka mtindo wa wapiganaji kutoa hisia zao kupitia magazeti, inashusha hadhi ya jeshi zima la Polisi, hasa kupitia posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vingi vimekuwa wazi mno; hivyo kupelekea watu wa kawaida kukatisha, kitu ambacho si kizuri kwa kambi. Suala hili lirekebishwe pamoja na upatikanaji wa kupewa hati miliki.

Mchango wangu wa mwisho, napenda kujua ushirikiano wetu wa kipolisi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki upo vipi kwa sababu ilionekana wazi wakati fulani wahalifu wengi wa silaha walitokea Kenya?

Mwisho, nalipongeza jeshi katika mfumo zima wa Jeshi Shirikishi na mafunzo ya mara kwa mara kwa maofisa na maaskari. Hili linatoa ukamavu kwa jeshi letu.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Masha, Naibu Waziri Balozi Kagasheki na Viongozi Wakuu wote wa Wizara hii. Naunga mkono hoja.

Kwa kuwa Jengo la Ofisi ya OCD Tabora linavuja wakati wa mvua; ni vyema ukarabati kwa mwaka huu watengewe fedha ili Ofisi hii iweze kuwa ya kisasa na kupewa vitendea kazi.

Nyumba za Polisi Mkoani Tabora hazina hadhi kwani zilijengwa tangu mkoloni; ni vyema sasa Serikali ikaungana na JKT kujenga nyumba za kisasa ili nao wapewe heshima ya kazi yao.

Nyumba za Askari Magereza Uyui, Manispaa ya Tabora, zinakatisha tamaa kwani hazijafanyiwa ukarabati kwa miaka mingi hata miundombinu ya maji na vyoo ni tatizo.

Kwa kuwa familia za Askari Polisi huongezeka; ni vyema wakapewa gari la maji taka, kwani vyoo vyao hujaa na kufurika katika makambi yote. Fungu la ukarabati wa ofisi (kasma) irudishwe.

Mashamba ya mfano yarudishwe kwenye Magereza yote, ambayo yalikuwa ya kilimo kama vile Urambo, Sumbawanga na kadhalika, kwani mashamba hayo yalikuwa yanakidhi mahitaji ya chakula chao na kulisha nchi hii.

Ofisi za Traffic, ningeshauri zijitegemee kwa kupewa majengo yao, kwani hazina hadhi kwa mfano, Kituo cha Traffic Buguruni. Ningomba Waziri na Naibu Waziri, wajipange wakaone hali halisi ya ofisi hiyo; imekaa kama kiosk.

Waongezewe posho ya usumbufu, kwani hufanya kazi bila kujali muda wa kazi, hasa Dar es Salaam, wale wanaongoza magari ni kazi ngumu. Wapewe vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kijiografia Jimbo la Tunduru lina sifa zifuatazo:-

(i) Ni Wilaya iliyombali sana kuliko Wilaya yoyote Mkoani Ruvuma; Songea km 0; Namtumbo km 64; Mbinga km 65; na Tunduru km 264.

(ii) Ni Wilaya yenye barabara mbovu sana hasa nyakati za masika kuliko wilaya nyingine mkoani.

(iii) Ni Wilaya ambayo vijiji vyake viko mbalimbali sana na kuleta ugumu wa kuwafikia wananchi ili kupata huduma za usalama wa raia.

(iv) Ni Wilaya yenyе ukubwa wa eneo kuliko wilaya nyingine yoyote. Tunduru ina ukubwa wa square km 20,000, ambapo inayofuatia kwa ukubwa ni Namtumbo square km 18,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo yote, Wilaya ya Tunduru kwa sasa haina gari zima hatu moja. Kuna magari mawili yaliyoegeshwa kwa uchakavu, takriban zaidi ya miaka minne sasa. Gari pekee aina ya Land Rover 110, lililokuwa linasaidia kutoa huduma, nalo limeegeshwa kwenye mawe kwa kukosa matengenezo ya kati na makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza zaidi, pikipiki ambayo ilikuwa inasaidia kupunguza pengo la usafiri, nayo imechukuliwa na kupelekwa Mkoani Ofisi ya RPC.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mazingira ya Wilaya ya Tunduru, kuititia Bunge lako Tukufu, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atusaidie, aidha, kuirejesha pikipiki iliyochukuliwa ikiwa nzima irudishwe Tunduru au tuletewe pikipiki nyingine mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wizara itenge fedha za kutosha kulifanya matengenezo makubwa gari la kituo, kufanya utaratibu wa kuyauza magari mawili chakavu yaliyopo kituoni na kuleta magari mengine kwenye kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mazingira ya makazi ya Askari Polisi Tunduru ni ya kutia aibu sana. Naomba wakumbukwe walau kufanyiwa ukarabati wa majengo yao. Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, hasa kwa Zanzibar, wananchi huwekwa ndani kwa amri aidha ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa saa 24 kwa Wakuu wa Wilaya na saa 48 kwa Wakuu wa Mikoa. Kwa Tanzania Bara, ninaelewa hatua wanazopaswa kuchukua kama za maandishi kwa wale wanaowekwa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka Wizara inifahamishe Wakuu hao wa Mikoa na wa Wilaya, baada ya kuwaweka watu ndani kwa amri zao wanapaswa wafanye nini kisheria? Pia uzoefu wa uwewkaji ndani huu hufanywa Ijumaa na uzoefu pia unadhihirisha kesi zao zote mbele ya Mahakama hazijathibitisha hata kazi moja hasa katika Wilaya ya Mkoani kuwa ni kweli kwa makosa wanayoshutumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwekwa ndani kwa siku ya Ijumaa na kupelekwa Mahakamani Jumatatu, ule muda wa kisheria huwa umeshapita. Hilo ni jambo la kawaida; je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa wa Kusini Pemba umejengwa na Wilaya ya Chake chake na Wilaya ya Mkoani. Tayari nyumba za polisi Wilaya ya Chakechake zimejengwa. Kuwa kuwa Mkoani (Wilaya), kuna tatizo kubwa la makazi ya askari polisi; ni lini Wizara itajenga nyumba hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la ucheleweshaji wa mishahara pale askari wanapohamishwa. Suala hilo huwasumbua sana askari kwenye maeneo wanayopelekwa. Je, Wizara ina mkakati gani wa kulitatu hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya wafungwa na hasa mahabusu, makazi yao huko magerezani ni mabaya sana. Magereza karibu yote, yana idadi kubwa ya wafungwa na mahakimu, kinyume na uwezo wa magereza hayo katika makazi. Hili ni suala la muda mrefu. Je, serikali ina mkakati gani wa kulitatu hili? Ahsante.

**MHE. BALOZI DKT. GERTRUDE I. MONGELLA:** Ukerewe ni eneo la mazingira magumu. Wizara ifikirie kutoa motisha maalum, kwa askari wanaofanya kazi sehemu kama hizi. Hata hivyo, Wizara ihakikishe kuwa, askari wanaopangwa huko ni makini na waaminifu ili kuondoa vishawishi vya kutotimiza wajibu wao kwa kuwa mbali na mamlaka za kuwathibiti.

Naomba ujenzi wa Kituo cha Mriti kiwe na huduma kama vile nyumba za makazi na gari. Eneo hili linahudumia eneo kubwa na visiwa vingi.

Hali ya Gereza la Bugorola na Kabingo (Nansio) ni mbaya na hata nyumba za askari hazitoshi, zilizopo zimechakaa.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri inayofanywa na Wizara, Idara na Taasisi za Wizara. Naomba ufanuzi kuhusu ibara ya 49, ukurasa wa 22; ni lini Wizara itatekeleza ahadi yake ya siku nyingi kujenga Ofisi mpya ya Polisi Wilaya ya Lushoto?

Pili, je, Vituo vidogo vya Polisi Mlola na Kwai vitapangiwa askari na kuwashumia wananchi mwaka 2009/10?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa viumbi vyote, asiyé na mshirika. Mungu ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa, kanijalia uhai na uzima wa afya na kunijalia kuchangia Hotuba hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha vyema hotuba hii. Pia nimpongeze Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano mzuri na Mheshimiwa Waziri na kumuwezesha kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze IGP Mwema, Makamishna wote, Maafisa na Wapiganaji wa Jeshi la Polisi na Magereza, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu wa Jeshi la Polisi ni watu wanaofanya kazi kwa moyo wa uzalendo, kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu kuanzia ofisi, makazi na vitendea kazi na hata malipo ya wastaifu huchelewa sana, pamoja na ya uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utendaji mzuri wa ndugu zetu hawa, ninaiomba Serikali iwajengee mazingira mazuri askari wetu kwa kuwalipa madeni yao ya uhamisho, makazi mazuri, ofisi za kufanya kazi, pamoja na vitendea kazi vinavyokidhi hali na kuwaboreshea malipo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mambo haya na mengine ambayo yanalamikiwa kasi na ari ya utendaji kazi itaongezeka na nidhamu ya Jeshi hilo itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Pension au kiinua mgongo. Suala hili limezungumzwa sana kuwa ni kero na linaonekana ni kasoro katika Jeshi letu kuwa na mikondo miwili ya wastaifu; na kwa kuwa suala hilo liko kwenye Jeshi la Polisi tu; Mheshimiwa Waziri haoni kuendelea na mfumo huu anasababisha makundi na ubaguzi na pia anakwenda kinyume na dhana ya uhuru na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar iliyosema yale mazuri tuliyoyakuta tutayaendeleza na yale mabaya tutayaacha na kuondosha dhiki na dhuluma kwa Wananchi wa Taifa hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linawadhalilisha sana ndugu zetu wale wanaolipwa malipo ya kiinua mgongo kwa kulipwa malipo kidogo na huwa hawapati tena malipo mengine; ukilinganisha na wale wa pension, wanalipwa fedha nyingi na malipo yanakwendelea kila baada ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze Serikali ina kigugumizi gani kuwalipa pension askari kwa mfumo mmoja tu kama ilivyo kwa vikosi vingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeze sana Jeshi la Magereza, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuwahifadhi wahalifu na watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi hili pia hujishughulisha na kazi nyingine kama ilivyoeleza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nielezee dhana ya Taifa ya Kilimo Kwanza. Jeshi la Magereza, lina uwezo mkubwa wa kuendeleza kaulimbiu hii ya Kilimo Kwanza. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, iliwezeshe zaidi katika kilimo kwa kuwapatia fedha kwa wakati ili malengo yao yakamilike ili jeshi liweze kujitegemea kwa chakula, pamoja na kuvisaidia vikosi vingine na nchi kwa jumla. Pia liwatumie wafungwa katika mashamba na sehemu za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ina mambo mengi ya kuchangia, mimi naishia hapa, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, kwa jinsi ambavyo wanatimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukumbusha juu ya suala linaloendelea la kutayarisha vitambulisho vya uraia wa nchi. Ni vyema suala hilo likapewa msukumo wa hali ya juu, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, alihitimisha wakati akihitimisha bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kuuliza kuwa; wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swali katika Mkutano huu alisema kuwa, vitambulisho hivyo vitatolewa kwa watu walotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea; je, hii ina maana gani? Ina maana *up-dates* zitakuwa zinafanyika baada ya muda gani?

Je, hamna *possibility* ya ku-link mtu anayezaliwa au kufa na *data base* hiyo? Je, katika *features* za *data base* hiyo kuna uwezekano wa ku-track records za elimu kwa mfano mtu anayekopeshwa na akiamua kufanyia kazi nchi nyingine?

Suala la mauaji na vurugu za Tarime, vita za koo; nadhani ni vyema sasa serikali iingilie kwa nguvu zote kuhakikisha kuwa, inakomesha vurugu hizo.

Vilevile ni vyema serikali itenye pesa za kutosha ili kuhakikisha kuwa, inaondoa aibu hii. Kwa nini kusifanyike Operesheni Maalum; mbona kukirokea tatizo maeneo mengine tunafanikiwa kusaidia; kwa nini nchini kwetu inakuwa tatizo? Tuyaite majeshi kutoka nje kama tunawaonea haya; kwani Tarime ni Tanzania, tena Wilaya ndani ya Mhubiri wa Amani, Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere. Ni vyema tujitahidi na kama tatizo ni Wakenya wa mpakani, safisheni kama yaliyompata Idd Amini, kwa maana ya hao wanaoleta vurugu za wizi mpakani (wizi wa ng'ombe ).

Wizara pia ifanye mazungumzo na Wizaa ya Nishati na Madini (REA), kuangalia uwezekano wa kupelekeea umeme kwenye Gereza la Mkuza – Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri pia aweke kwenye *waiting list* yake, maombi ya kutoa mafunzo ya ulinzi shirikishi katika Kata za Mwambao wa Ziwa Nyasa, kwani ni maeneo ya mpakani; hivyo ni vyema wananchi wawe na uwezo wa kuwatambua wageni ambaa wanawenza kuwa ni wahalifu.

Pamoja na kwamba, hili lilistahili pia kujitokeza kwenye Wizara ya Miundombinu, maoni yangu ni kwamba, Wizara hiyo inapokuwa hajatimiza wajibu wao, wanaleta mzigo mkubwa wa *nan hour losses* kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mfano, kwa nini maeneo kama Kijitonyama pasijengwe *roundabout* au taa za barabarani na Ubungo Morogoro/Mandela Road pasijengwe *flyover bridge* ili kuondoa msongamano wakati wa *pick hours* na hivyo kulazimu *traffic police* kuhangaika na mikono kuongoza magari? Kweli hiyo ni kazi ya utaalalm/lazima?

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mwaka jana katika Bunge hili Tukufu, wakati nikichangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, nilielezea masikitiko yangu, juu ya bajeti ndogo ya Wizara hii. Serikali imekuwa ikitenga kila mwaka, tangu uhuru wa nchi, wakati majukumu na changamoto za Wizara zimeongezeka mara difu.

Katika mchango wangu, niliomba serikali kuelekeza nguvu zake zaidi katika bajeti ya kila mwaka kwa Jeshi la Polisi, ambalo lina changamoto kubwa ya kudhibiti na kushughulikia maadui wa ndani, tofauti na miaka 40 iliyopita ambapo nchi ilikuwa inakabiliwa na tatizo kubwa la maadui wa nchi yetu toka nje ya mipaka yetu.

Ninaiomba tena serikali ibadili mtazamo wake, badala ya ule wa zamani, ambapo fedha nyingi zilitengwa kwa majeshi mengine badala ya polisi. Hali ya usalama wa nchi imebadilika na tishio kubwa la usalama sasa ni wahalifu wa ndani, kama serikali haitabadili mtazamo huu, uhalifu utaendelea kushamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kahama, tatizo hili ni kubwa hasa kwa vile baadhi ya Maafisa wa Jeshi hilo wanahusika na hivyo kulifanya tatizo hili kuwa kubwa. Jambo la kusikitisha, licha ya malalamiko ya wananchi, baadhi ya Polisi wa kawaida na mimi mwenyewe Mbunge kulalamikia tabia hii, bado afisa anayetuhumiwa hajachukuliwa hatua na anaendelea na hulka yake hiyo na kuifanya kazi ya Mkuu mpya wa Polisi Wilaya kuwa ngumu.

Hivi ni kwa nini viongozi wa aina hii wanakumbatiwa?

**NAIBU SPIKA:** Sasa ni nafasi ya Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima nyingi sana, nachukua nafasi hii, kabla sijakwenda katika hoja ambayo tuliyonayo tangu asubuhi ya leo, kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Bukoba Mjini, kwa heshima walionipa na kwa imani waliyokuwa nayo kwangu mimi ambayo imenifikisha hapa. Kwa kweli heshima zote, ziwaendee wao kwa sababu wao ndio wameniwezesha na kunipa nafasi hii. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwapa hongera Wanajimbo wangu ambao ni waajiri wangu kwa ushindi tuliouputa katika uchaguzi uliokwisha Biharamulo kwa sababu ni jambo ambalo linawagusa sana, ni Wilaya jirani kwa hiyo nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wanajimbo wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii, nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa imani kubwa aliyonayo kwangu mimi na niseme kwamba ile imani inanifanya nifanye kazi naye na nimsaidie vizuri katika kuendesha kazi za Wizara. Lakini hapo hapo nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu Patrick Rutabanzibwa na Naibu Katibu Mkuu ambaye tumempata, lakini pia nichukue nafasi kwa kweli kuwashukuru Makamanda wote wa Vikosi vyote vya Ulinzi ambavyo viko chini ya Wizara yetu kwa kazi nzuri ambao

wanafanya na pia niwashukuru Askari wote na wafanyakazi wote wa Wizara na tulionao katika Mikoa yote ya Tanzania, kwa kazi na kujituma kwa niaba ya Taifa letu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikiliza michango mingi na ningependa nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote, niwashukuru Wabunge binafsi kila mtu kwa nafasi yake lakini nyote kwa ujumla wenu kwa ushirikiano mkubwa amba mmetupa mnatupa katika Wizara yetu, ni kitu ambacho kwa kweli nakienzi na kukiheshimu sana kwa sababu kinatusaidia katika kufanya kazi zetu. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wabunge kwa nafasi hiyo na kwa ushirikiano amba mmetupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kabla sijaenda katika michango ambayo imetolewa leo na Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi lakini pia kwa kauli ambazo zimesemwa ndani ya Bunge lako Tukufu, napenda niseme machache yafuatayo. Sisi ni watu wazima, nchi hii ni yetu, Bunge hili ni letu, mustakabali wa nchi yetu huko mikononi mwetu. Kwa hiyo niseme inapokuja katika Wizara kama yetu labda nitakuwa nakosea lakini naisema kwa nia nzuri na hakuna kitu kilichofichika katika nafsi yangu. Tunapozungumza masuala ambayo yanahu vyombo vya ulinzi na usalama katika Taifa letu ninashauri tuwe tunatumia kauli ambazo, maana yake hatuzungumzii sisi wenyewe hapa maneno haya yanakwenda katika Taifa zima, maneno haya yanakwenda nje ya Taifa la Tanzania, ni maneno ambayo yanatazamwa na yanasilizwa na dunia nzima. Sijasema kwamba yasisemwe, tuyasema lakini pako pahali tunaweza tukasemana tukaambizana upungufu lakini niseme tu kwa kweli tunapotumia lugha nyingine katika vyombo hivi na kweli ukasema mambo mengine kwa kweli hayana ushahidi na wala hayana uhakika, nasema tunachochea kitu ambapo hatimaye kama kitu kikija kikaharibika tutaharibikiwa sote, sio kwamba itakuwa ni wachache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kidogo inanitia simanzi ikielekea ama ikitafsiriwa kwamba labda sisi viongozi wa Wizara hatujali Askari wetu ama ikapewa tafsiri kwamba katika mambo yao wanayoyahu sisi hatuna habari tumekaa *ahlani wasahlani*, hamsini zetu na tumewaacha wao wanateseka, wanahangaika na kadhalika. Naomba nisema kwamba kwa kweli katika jahazi hili tumo sote na katika mwenendo amba tunakwenda ninapenda kusema kwamba kweli yapo ambayo yanatuhusu tuyazungumze na sijasema kwamba yasizungumzwe lakini pia tuchague zile *forum* kwa sababu tusije tukasema maneno mengine ambayo yanaweza yakaleta vurugu katika nchi na kama vurugu zikitokea nataka niseme kwa ukweli kabisa sio kwamba zitachagua huyu ni wa wapi ama wa wapi, tumo katika jahazi moja na mustakabali wetu ni mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli tumesikia hoja na tumezipokea hoja nyingi na nyingi kwa kweli ni za kuboresha na nyingi za kujenga na kutengeneza. Mathalani kulikuwa kuna hoja kwamba uhalifu hasa ujambazi wa kutumia silaha umeongezeka katika maeneo mbalimbali katika nchi. Hoja hii iko katika maandishi lakini pia wamezungumziwa Waheshimiwa Wabunge kama Mheshimiwa Lupembe, Mheshimiwa Telele, Mheshimiwa Sarungi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Bakar Faki, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya na Mheshimiwa Stephen Galinoma. Wao kwa kweli hoja yao ya kusema kwamba hali ya ujambazi imeongezeka, ni kweli imeongezeka kwa kipimo kipi? Ujambazi kweli

umekuwepo lakini pia hata kasi ya Askari wetu katika kukabiliana na ujambazi pia imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza hapa bila ya kificho kwamba upo uhaba wa kupata vitendea kazi na kweli nilitaka niwaambie Waheshimiwa Wabunge ndugu zangu, rafiki zangu nakumbuka *IGP* mwenyewe alisema na aliwahi kuulizwa ili nchi hii iwe katika hali ya usalama tunahitaji kikosi cha Askari wangapi? Yeye alisema ili aweze kuwa katika hali ambayo anaona kwamba ni ya usalama wa nchi yetu, anahitaji Askari 90,000. Lakini sasa hivi tunavyozungumza kikosi cha Askari wetu tulionao katika Tanzania ni 30,000 na hii ndiyo inanipeleka pale ambapo kiongozi aliyekuwa Msemaji wa Upinzani leo asubuhi alipojaribu kuweka tarakimu kuonyesha kwamba Askari mmoja kwa Tanzania anawatazama raia 1,300 hii inatokana na sababu ya vitendea kazi ambavyo atavizungumzia Mheshimiwa Waziri mwenye hoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme suala la ulinzi wa Taifa letu na suala la kupambana na majambazi, ni suala letu sote na ndiyo maana tunasema kwamba itabidi kushirikisha vyombo mbalimbali, Taasisi, Idara, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa, Wilaya na Vijiji na kadhalika. Lakini papo hapo tutajaribu kadri tuwezavyo kuwashawishi wenzetu na nafikiri ndiko tunakokwenda kwa sababu kumekuwa na hoja ambayo inahusu kujenga vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali hili ni jambo ambalo ni jema na ni jambo ambalo tunalikubali lakini tumekuwa tunasema mara kwa mara kwamba uwezo wa kwetu sisi kujenga vituo chini baada ya Wilaya tukaenda katika Kata kwa kweli itatuwia ngumu. Lakini tunadhani kama nilivyokuwa nazungumza leo asubuhi katika masuala mengine kwamba endapo katika uongozi wa Kata, kushirikiana na Halmashauri wakiona kwamba kweli ipo haja wanaweza wakachangia na Halmashauri ikaweza kusaidia kupitia katika uongozi wa Wilaya wa Polisi *OCD* na nafikiri tunaweza tukafikia pahali kwa sababu ramani za majengo ambayo yanahitajika yapo na tunaweza kabisa tukafikia pahali kunakuwa na mchango wa Halmashauri na wananchi na sisi tukaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hili la vituo vya Polisi limezungumzwa na Wabunge wengi kuna Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Juma Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Basi unaona kwa idadi hii ambayo nimeisoma, ni Wabunge wangapi wamezungumzia juu ya suala hili ambalo kweli nasema ni suala muhimu lakini ninashauri katika kupitia njia kama hiyo tunapokwenda chini tukitoka katika Wilaya tukienda chini katika Kata, tunaweza tukatumia mfumo wa kusema kwamba uongozi kule katika Kata na uongozi wa Halmashauri wakiweza basi na hii itakuwa imetuletea ile dhana yetu ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii nafikiri itakuwa inakwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapokuja katika masuala ambayo wamezungumzia Wabunge kuhusu uhaba wa vitendea kazi, hilo atalizungumzia mto hoja mwenyewe na kuhusu masuala mengine kwa sababu muda unasonga sana na ukitazama hoja zilitokea hapa ni nyingi sana tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuzijibu lakini zile ambazo hazitapata majibu hapa sio kwamba hatujataka kuzijibu lakini tutazijibu kwa njia ya maandishi kama hiyo itakuwa ni barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imetoa hoja yao hapa leo asubuhi na tumewasikiliza kwa makini sana na tumeyapokea. Imekuwepo hoja ya kusema kwamba Serikali iongeze posho na mishahara kwa Askari, hilo namwachia mto hoja atakuja kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika Kambi ya Upinzani leo asubuhi kuna matamshi ya kusema kwamba Askari wamekuwa wakiwanyanya mahabusu na pia kumekuwa na kauli katika hiyo *statement* yao ya kusema kwamba kutokana na mwenendo mzima jinsi Askari wanavyokwenda basi hiyo imewapelekea wananchi wenyе hasira kali kuweza kuchukua sheria mikononi mwao na hii ndio msemaji wa mwisho Mheshimiwa Komu wa kuweza kuchukua sheria mikononi mwao kufanya mambo wanayofanya na hii Mheshimiwa Komu ameisema hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niseme, Waheshimiwa Wabunge kwanza kusema kwamba mahabusu wananyanyaswa, hili kwa kweli linaweza kweli likatokea lakini huwezi ukasema hili ndilo jambo linalotokea wakati wote na nyakati zote na katika vituo vyote. Lakini pia haya yanapotokea yanapata *coverage*, yanasemwа katika magazeti lakini pia kuna hatua ambazo tunachukua ambazo hazisemwi. Kwa mfano, niseme hapa katika Bunge lako Tukufu, mwezi Julai 2008 kuja kufikia mwezi Machi, 2009, Askari 46 wamefukuzwa kazi baada ya kubainika kuwa walikuwa wanakiuka maadili fulani pia yakiwemo masuala ya unyanyasaji. Kwa hiyo, ni hatua ambazo tunachukua, sio kwamba Jeshi la Polisi limekaa linaangalia udhalimu unaofanywa kwa watu na kuona kwamba hakuna kitu kinachofanyika, kwa hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wananchi kuchukua sheria mikononi mwao, hili suala mimi ninaomba tulitazame kwa mapana yake na msilaumu Polisi jamani, kwa sababu Polisi wanachokifanya kwa hatua ya kwanza wanamkamata mtu, lakini wanafanya upelelezi kuhusu tuhuma ambazo zinamwandama mtu yule lakini akitoka pale yule mtu anafuata utaratibu wa sheria anakwenda Mahakamani, pale Polisi hayuko tena. Sasa kinachotokea yule mtu kama amekwenda Mahakamani ameachiliwa ama Mahakama imeona hana hatia, kwa hiyo siku mbili, au tatu watu wakamwona amerudi tena mtaani, nadhani hapo tujaribu kutazama viko vitu viwili iko *role* kweli ya Polisi ambayo inafanywa ya kumkamata mtu lakini Polisi haihukumu mtu maana yake nchi yetu ni nchi ya demokrasia ziko taratibu zake. Tunazungumzia utawala bora, tunazungumzia kufuata sheria katika utawala na hiyo ndiyo wakati mwingine inakuwa *price* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme kwamba lipo tatizo ni kweli tunaliona kwa sababu wananchi wanachukua sheria mikononi mwao lakini nisingependa kusema kwamba hili ni tatizo la Polisi. *Hasha!* Inaweza kweli kukawa kuna tatizo hili lakini huwezi ukalichukua moja kwa moja ukalitupia katika mlango wa Polisi ukasema ndio wanasababisha kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *statement* aliyoitoa Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ametaka kujua ni sababu gani za msingi zinazopeleke Askari kukaa muda mrefu kituo kimoja bila ya kuhamishwa. Kwa kweli hakuna sababu, sababu za msingi ni matatizo ya fedha, hiyo tu ndiyo sababu ya msingi. Nitawapeni mfano, katika mwaka wa fedha tulionao, *IGP* katika utaratibu wao walikuwa wamepanga kuhamisha Askari 1,000 lakini wameshindwa na kitu walichofanya wameweza kuhamisha Askari 600 tu. Ukitazama 1,000 si idadi ambayo ni kubwa sana lakini kwa kumhamisha mtu mmoja haichukui chini ya shilingi 1,000,000 na fedha kadhaa kwa hiyo kidogo inakuwa taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala mengine ambayo yamezungumziwa juu ya upungufu wa vitendea kazi. Hiyo nitamwachia Mheshimiwa Waziri ataizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba baadhi ya Wabunge wametambua mchango ambaao Polisi inafanya, kwa kweli bado tuko katika vita kubwa ya kupambana na ndugu zetu wale madhalimu wanaowaua ndugu zetu wa ulemavu wa ngozi. Kwa kweli ni juhudu kubwa lakini niseme haiwezi ikawa kazi ya Polisi peke yake. Polisi itahitaji msaada mkubwa wa raia, Polisi itahitaji kupata ushirikiano wa watu mbalimbali ili kuweza kukamilisha na hii ni jitihada ambayo tunafanya na niseme kwamba kwa kweli tunaendelea lakini tunataka ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda haraka haraka kumekuwa na masuala kwa mfano kuhusu msongamano wa wafungwa katika mahabusu na kujaribu kutazama ni njia gani za kuchukua katika kuboresha mahabusu. Hili ni suala ambalo wamezungumza Wabunge wengi Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Kapteni Chiligati na kadhalika. Sasa ni kweli tunao msongamano wa Magereza lakini pia kama mtatazama vizuri katika mahitaji yetu ambayo tunaomba katika bajeti hii, tumeomba sana na hatuwezi tukajenga Magereza yote katika nchi yetu kwa sababu nchi yetu ni kubwa lakini yale ambayo tumesema nafikiri yatakuwa karibu katika Wilaya kadhaa, tutajitahidi kadri ya uwezo wetu na kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu Askari Magereza, inapokuja katika suala la vitendea kazi na maslahi yao na kadhalika, hilo namwachia Mheshimiwa Waziri atakuja kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda haraka haraka, Mheshimiwa Mwadini Jecha, yeye katika hoja zake za maandishi amezungumzia kwa mfano suala la ujenzi wa

Ofisi Kuu Zanzibar ambao ni ya Makao Makuu ya Uhamiaji na anataka kujua hizi fedha ambazo wanajengea kama mwisho wa shughuli zitaweza kurejeshwa kule. Ninapenda kuchukua fursa hii kumwambia Mheshimiwa Jecha kwamba fedha ambazo zinajengea jengo hili zinatokana na utaratibu ambao tumekubaliana maana hili ni suala la Muungano. Katika utaratibu wa gawio ile *retention* ambayo wanapata Zanzibar na niseme mimi mwenyewe nilivyokuja Zanzibar nimeona kazi ambayo wanaifanya na nataka niupongeze uongozi wa Zanzibar kule kwa kweli wamefanya kazi nzuri, nawaona kabisa kwamba fedha zinakwenda katika kazi ambayo ilitarajiwa. Sasa mambo mengine nafikiri wataendelea katika *framework* ile ya Muungano kuona wanakwenda namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *IGP* kuja Pemba, hiyo namwachia Mheshimiwa Waziri atazungumzia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Telele amesema Wilaya ya Ngorongoro haina Ofisi ya Uhamiaji na licha ya kusema kwamba iko karibu na mpaka na Kenya na kadhalika. Nimwambie Mheshimiwa Telele kwamba hili ni tatizo sio kwamba tatizo la Ngorongoro peke yake lakini liko sehemu nyingi. Lakini niseme kwamba hilo tumelichukua na uwezo utakavyokuwa ukijitokeza ndivyo tutakavyokuwa tunafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya amezungumzia juu ya fedha kiasi gani ambacho tunakitoza kuhusu *visa* ya *single* na *multiple*. Suala hili nafikiri hata Mheshimiwa Rais alilitolea tamko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, nachukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa namna ambavyo umeendesha mjadala huu. Pia napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wamechangia hoja ya Wizara yangu kuanzia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla kuanza kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Mzee William Walwa, aliyekuwa Mwenyekiti wa Wazee, jiji la Mwanza, aliyefariki dunia siku ya tarehe 06 Julai, 2009, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii, kumshukuru sana mke wangu Stella, watoto wangu Chela, Amani na Junior, kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, ninawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Nyamagana kwa kuendelea kuniamini na kunivumilia katika kipindi chote ambacho nipo mbali nao kwa sababu ya kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Ninawashukuru pia Madiwani wa Jimbo langu, viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Matawi, Kata, Wilaya na Mkoa kwa ushirikiano wanaonipatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge 143 wamechangia hoja hii na Wabunge 101 walichangia kwa maandishi na Wabunge 14 wamechangia hoja hii kwa kuzungumza. Aidha, Wabunge 28 walichangia kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa naomba kuwatambua wachangiaji kuanzia waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mohamed Rajabu Soud, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Alhaj Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu na Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Benson M. Mpesa, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Mariam S. Mfaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Kapt. John Z. Chilligati, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngiwilizi, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Tatou Ntimizi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Juma Said Omar na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Bakar Khamis Faki, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa

Stephen Galinoma, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Bujiku Phillip Sakila, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Manju Salum Msambya, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Fatma Maghimbii, Mheshimiwa Luaga J. Mpina na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Kidawa H. Salehe, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mcemba, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhil, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Prof. Dr. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Mheshimiwa Fuya Kimbita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia masuala mbalimbali kuhusu Wizara yangu wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Ibrahim M. Sanya, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mheshimiwa Masudi Abdallah Salim, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa na Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, naomba niweke wazi kwamba kutokana na uwingi wa hoja tulizozipata, haitakuwa rahisi kujibu hoja zote kwa muda ambao nimepangiwa. Kwa kuzingatia hali hiyo, nitajitahidi kujibu kadri uwezo wangu na ninaahidi kwamba hoja zote zitajibiwa kwa maandishi na vitabu vyta majibu vitawasilishwa Ofisi ya Bunge ili kila Mbunge apate.

**NAIBU SPIKA:** Unaanza kuhesabiwa muda wako sasa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo ya jumla katika maeneo mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wamechangia kama ifuatavyo. Naomba kuanza na Mkao wa Mara. Toka nimekuwa Naibu Waziri na mpaka nimekuwa Waziri kamili, nimepata nafasi ya kutembelea Mkao wa Mara na hususan Wilaya za Tarime na Rarya mara tatu. Lazima niseme pamoja na kuwa na marafiki wengi ambao wanatokea katika Wilaya hizo, kazi iliyonipeleka huko, haikuwa kazi ya furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kitabu hapa, ni *dissertation* ambayo imeandaliwa na Ndugu Iddi Ramadhani ambayo inaongelea tatizo la mapigano katika eneo la Tarime ambayo imeanza kabla ya ukoloni, katika kipindi cha ukoloni mpaka leo hii tunavyoongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba tatizo la mapigano ya koo na wizi wa mifugo katika Wilaya ya Rarya na Tarime, si tatizo ambalo limeanza leo wala si tatizo ambalo litaisha kesho. Lakini ninachowenza kuwaahidi ni kwamba kwa muda ambao nitakaopewa kusimamia Wizara hii, nitafanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba haya mapigano tunayatafutia suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishatangaza kwamba tutaandaa Mkao wa Kipolisi Maalum katika Kanda hii na naomba nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa Wizara yangu imeanzisha Mkao wa Kipolisi utakaojulikana kama Mkao wa Tarime/Rarya. Kamanda wa Polisi, SSP Constantine Massawe, ameteuliwa kuwa Kaimu Kamanda wa Mkao huo na uteuzi huo umeanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao huu utakuwa na Wilaya na Tarafa zifuatazo ambazo kila mmoja itaongozwa na *OCD*. Wilaya ya Tarime, Wilaya ya Rarya, Tarafa ya Shirati, Tarafa ya Nyamwaga, Tarafa ya Kinesi na Tarafa ya Sirari. Lakini ningependa kusema pamoja na kazi tutakayoifanya kuongeza nguvu ya askari katika Mkao wa Mara bila ndugu zangu wa Mkao wa Mara kubadili tabia, hakuna kitakachofanikiwa. (*Makofii*)

Ninawaomba sana ndugu zangu wa Mkao wa Mara tushirikiane tubadilishe tabia ili tuhakikishe kwamba watu wetu katika Wilaya za Tarime na Rarya wanakaa kwa amani na utulivu. Pale ambapo nguvu za Polisi zitahitajika zitakuwa zimepatikana, lakini naomba kusisitiza kwamba kinachohitajika hapa zaidi ni kubadilisha mawazo, tabia na fikra za ndugu zetu ambao wako huko. Kwa hilo ninawaombeni msaada wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la maslahi ya askari. Napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wameongea kwa uchungu sana kuhusu matatizo ambayo askari wangu chini ya Wizara yangu wanayoyapata. Ni wazi kabisa kwamba hawa askari wawe askari wa Magereza, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Idara ya Uhaniaji wanafanya kazi katika hali ngumu sana. Hilo lazima nikiri na naomba kuwafahamisha kwamba uchungu ambao Waheshimiwa Wabunge ambao wameonyesha hapa ndiyo uchungu ambao mimi ninaupata kila siku. Hawa ni askari wangu ambao ninawatembelea kila siku, mimi

pamoja na mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri, *IGP* na viongozi wengine wa Wizara yetu kila siku ya Mungu tukiamka tunafikiria namna ya kuweza kuboresha maslahi ya askari wetu.

Suala la makazi, suala la posho na vitendea kazi. Tunatambua kabisa kwamba wanatakiwa kupewa zaidi. Sio kwamba hatujui na sio kwamba hatujali, tunatambua kwamba tuna bajeti ndogo na ndani ya bajeti hiyo tunajaribu kubana hapa na pale ili kuhakikisha kwamba kile ambacho tunawenza kukifanya tunafanya. Hata na sisi, mimi na Naibu Wabunge tungependa sana kuwa na bajeti kubwa zaidi. Naomba msifikirie kwamba inafikia nyakati tunapangiwa bajeti kubwa halafu sisi ndiyo tunasema hapana msitugawie, haiko hivyo. Sisi tungependa sana kupata pesa zaidi. Hakuna tabu tunayoipata mimi na Naibu Waziri pamoja na *IGP* na Katibu Mkuu wangu pale tunapowatembelea askari wetu na kabla hawajaanza kutueleza matatizo yao, matatizo yao tunayafahamu. Mengine yanaonekana wazi na ndiyo maana tunajitahidi kadri ya uwezo wetu kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaulizia posho za askari kwamba zimeongezeka kiasi gani? Kabla sijataja na sitataja zimeongezeka kiasi gani, nitakachosema ni kwamba hata pale zilipofika inawezekana hazitoshi. Tungependa wapate zaidi lakini ndiyo uwezo tulionao. Lakini tunashukuru kwamba angalau posho za askari zimepanda kwa asilimia 100. Hilo sio kitu kidogo, ningefurahi sana kama ningeweza kupata mafanikio ya posho kupanda kwa asilimia 200, lakini haikuwezekana. Naomba muwe na uhakika kwamba nitaendelea kuomba na pale ambapo nitaweza kuwaongezea posho askari nitajitahidi kadri ya uwezo wangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za askari zinatia aibu. Nalifahamu hilo sio kwamba sijui na katika jitihada ya kuhakikisha kwamba Wizara yangu ingepata pesa zaidi, nilipata nafasi ya kumchukua Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kumpeleka aone askari pale Kigoto Mwanza wanaishi vipi. Waziri wa Fedha alitoa machozi alivyooona hali ya askari. Lakini hali ni ngumu! Ndiyo hivyo najitahidi kadri ya uwezo wangu pamoja na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kufanya kila ninachowea kuhakikisha kwamba maslahi ya askari yanaboreshwa. Tunashirikiana na *NSSF* sasa hivi kujenga nyumba za Polisi, tunatumia nguvu zetu sisi wenyewe, pale Iringa Mjini nyumba za Magereza kuna ghorofa moja zuri sana ambalo lina nafasi ya askari 16 limejengwa na askari Magereza tena kwa ubora kabisa na ufanisi mzuri sana. (*Makofî*)

Tunaendelea kufanya kila jitihada kuhakikisha kwamba askari wetu wanapata nyumba nzuri, wanapata makazi mazuri kwa sababu ukweli ni kwamba tunawajali. Hivi sasa hapa tulipo Wizara yangu inashirikiana na Serikali ya China kwa kupitia Hazina kujaribu kuangalia uwezekano wa kupata mkopo wa kuweza kujenga nyumba kwa ajili ya askari wetu wote, sio tu wa Polisi, lakini askari Magereza, wenzetu wa Uhamiaji pamoja na Zimamoto na Uokoaji. Naomba mtambue kabisa kwamba hata sisi tunachokiona kinatumiza. Kuna sehemu nyingine ukienda kwenye Magereza yetu huwezi kutofautisha ile selo ya mfungwa na nyumba ya Waden, sio kwamba sijui na ndiyo maana mimi Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Makanda hatulali tunajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba hali hii tunaibadilisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatembelea vikosi vyetu vyote hapa nchini na tunapeana majukumu. Kuna maombi maalum hapa ambayo yametoka kwamba *IGP* aende Zanzibar. Nimeongea nae, nimemwagiza baada ya *session*, hii ataenda Unguja na atafika Pemba. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba nchi yetu ni kubwa, tupo viongozi wengi wa ngazi ya juu ndani ya Wizara yetu na tutagawana majukumu. Kwa mfano, mimi nilikwenda Pemba. Ni kweli sikumaliza ziara ya Pemba na nitarejea tena Pemba kuona baadhi ya askari baada ya Bunge hili. Lakini Naibu wangu yeche aliwenda Zanzibar, *IGP* atakwenda sehemu nyingine na Masha atakwenda sehemu nyingine. Hivi ndivyo tutakavyofanya kazi. Lakini kutokana na ombi maalum nawahakikishia askari wa Zanzibar na Pemba *IGP* atakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niongelee suala la umri wa kustaafu ndani ya Majeshi yetu, ni jambo ambalo tumeshalionia. Tumepeleka mapendekezo mbele ili kuhakikisha kwamba umri wa kustaafu unaongezeka kama ilivyofanyika kwa wenzetu katika Jeshi la Wananchi. Hiyo kazi inafanyika hivi sasa na huu mchakato utakapokuwa unaendelea, kwa wale ambao walikuwa wanakaribia kustaafu tunawaombea Mikataba ili waendelee kufanya kazi.

Naomba kuongelea magari na nasema magari kwa sababu kati ya Wabunge 141 ambao wamechangia karibu wote wameomba magari kwa ajili ya Wilaya zao. Naomba hili niliongelee kwa ujumla. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu asubuhi kwa bahati mbaya kutokana na utaratibu wa ununuzi Wilaya zile zilizohidiwa magari mwaka jana likiwemo Jimbo la kaka yangu Mheshimiwa Blandes, Mheshimiwa Blandes alinibana kwenye vifungu mwaka jana, alikuwa anataka magari. Naomba nimhakikishie pamoja na kwamba hayupo hapa, lakini katika magari yanayokuja, gari lake lipo na atapata. Watu wote walioahidiwa mwaka jana watapata magari yao. Lakini sio tu hivyo naomba kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wilaya yoyote ile ambayo haina gari itapata gari katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, huna haja tena ya kuniomba kwenye vifungu. Kama unajua huna gari ujue utapata. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nami nitahakikisha hivyo, kwamba mtu haombi gari kwenye kifungu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya mauaji ya walemovu wa ngozi. Hili ni jambo ambalo linatia aibu na kama nilivyo sema asubuhi, Wizara yangu itafanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba tunamkamata mpaka yule mtu wa mwisho ambaye anahuksika katika mauaji haya ya kikatili. Askari wetu, Makamanda wao na viongozi wao wengine hatutalala mpaka hii kazi inakamilika. Lakini napenda kuwafahamisha kwamba sio kwamba kazi haifanyiki hivi sasa tunavyoongea, mpaka sasa hivi kuna jumla ya watu 41 wenye ulemavu wa ngozi ambao wameuawa katika kipindi cha mwaka 2007 – 2009. Baada ya upelelezi wa matukio haya, jumla ya kesi 26 zinaendelea katika Mahakama kama ifuatavyo:-

Kesi 14, upelelezi wake umekamilika na watuhumiwa wamefikishwa Mahakama Kuu na zinaendelea kusikilizwa. Kesi 12 zinaendela kutajwa katika Mahakama mbalimbali, wakati huo Polisi wakiendelea kukamilisha upelelezi wake. Watuhumiwa 53 wamekamatwa kuhusiana na mauaji hayo na kuhusu mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi ambao umetokea hivi karibuni huko Mkoani Mwanza mtuhumiwa mmoja amekwishakamatwa. Kama nilivyoeleza, mauaji haya kwa kweli yanalitia doa Taifa letu, tutaendelea kulifanyia kazi hilo na kwa wale wote ndugu zetu 41 ambao wameuawa naomba sana Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi katika michango yao ya maandishi wameulizia kuhusu vitambulisho vya raia. Katika michango yao kuna hoja kuu tatu ambazo zimejitokeza. Hoja ya kwanza kwanini imechelewa? Hoja ya pili, kwanini Waziri aliingilia? Hoja ya tatu, kwanini inapelekwa katika Baraza la Mawaziri?

Kwanza napenda kusema kwamba hoja ya vitambulisho vya raia iliibuliwa mwaka 1968, Waziri huyu alikuwa hajazaliwa na mama yangu mzazi alikuwa na miaka 19. So, tuanzie hapo. Kwa sababu watu wanaosema Masha ndiyo kachelewesha, naomba tuanze kusema, sio kweli. Mwaka 1968 hoja hii ilivyoibuliwa tukaenda mpaka mwaka 1986 ndiyo Sheria ikatungwa, tukatoka mwaka 1986 mpaka mwaka 1995 ambapo kwa mara ya kwanza zabuni ilitolewa. Kwa sababu ambazo naamini wote hapa tunazifahamu, hiyo *tender* haikuweza kufanyika, tukaangia katika awamu ya pili ya *tender* ya vitambulisho. Mwezi Novemba mwaka 2004 Wizara ya Mambo ya Ndani iliingia katika hati ya maelewano na Kampuni binafsi ya *Gotham International* ili kufanya upembuzi yakinifu wa mradi na kutoa ushauri juu ya namna ya kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari 2007, Serikali ilikubali ushauri na ikamteua Ndugu Gotham kampuni yake kuwa mshauri elekezi katika mradi huu. Hapo ndipo Masha alipokuja kufahamu huu mradi. Karibu miaka 30 ilikuwa imepita toka umeibuliwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Komu ameuliza swali zuri sana. Ameuliza hivi, kwenye mradi wa vitambulisho kuna nini? Kwa kipindi cha kama mwaka mmoja na nusu hata mimi mwenyewe nauliza, hivi kwenye huu mradi kuna nini? Inawezekana swali langu lina chimbuko tofauti kidogo na hilo la Mheshimiwa Komu, lakini na mimi kwa muda mrefu nimekuwa nikijiuliza kwenye mradi wa vitambulisho, hivi jamani, kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mimi katika majibu ambayo tumeshawahi kutoa ndani ya Bunge hili Tukufu tumeeleza kwamba mchakato unaendelea. Lakini inaelekea kwamba Waheshimiwa bado hawajaridhika kwamba mchakato huu unaendelea. *Issue* ya vitambulisho vya Taifa imefika katika hatua ya Kamati ya Zabuni, yaani *Tender Board* kupeleka mapendekezo yake kwa Katibu Mkuu wa Wizara ambaye kisheria yeye ndiye anasimamia suala la vitambulisho chini ya Sheria ya Manunuzi.

Mimi kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi niliuliza swali kwa Katibu Mkuu wangu pale ambapo Bodi ya Zabuni ilikuwa imekamilisha kazi yake na swali langu lilitokana na kile ambacho nilikiona kimetendeka katika mchakato ambacho niliona kulikuwa kuna dosari. Nauliza swali lile la Mheshimiwa Komu kwamba kuna nini kwenye mradi huu? Kwa sababu kama Waziri mwenye dhamana ambaye ndiye anajibu hoja zenu ndani ya Bunge hili, nilichofanya ni kuuliza swali ili pale mtakaponiuliza na mimi niweze kujibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ajabu ni kwamba kuuliza kwangu swali kuhusu mchakato nayo ilikuwa kosa. Nimeuliza swali kuhusu mchakato ambapo mimi ndiyo ninapewa kazi ya kuwajibu ninyi Wabunge ndani ya Bunge hili, lakini naambiwa kwamba Masha ulikuwa hutakiwi kuuliza. Mchakato ultakiwa kuendelea.

Sasa cha ajabu inakuwaje kwamba Bunge linaweza likaniuliza mimi lakini mimi Waziri mwenye dhamana nisiweze kuwaliza watendaji wangu? Kesho na kesho kutwa nisipowauliza watendaji wangu ni kitu gani wanachokifanya kwenye hiyo *tender* nitasulubiwa na Bunge hili. Cha ajabu niliweka pamba masikioni nilivyokuwa naulizwa na nikaendelea kuuliza swali langu na nikamuagiza Katibu Mkuu kupeleka hoja hizo kwa *PPRA*. Taasisi inayoshughulikia manunuvi kwa ajili ya Serikali hapa mjini. Cha ajabu ni kwamba *PPRA* ilirudi na ikasema kwamba hoja zote nilizozitoa zilikuwa sahihi. Ndiyo maana na mimi narudi kuuliza kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *PPRA* wamethibitisha kwamba hoja ambazo Waziri mwenye dhamana aliuliza zilikuwa sahihi, kuna nini? Mimi ningeomba kufahamu. Cha ajabu ni kwamba leo hii huu ni mradi wa Serikali tunataka kupeleka taarifa ya utekelezaji kwenye Baraza la Mawaziri kwa sababu hapa tutakachokuwa tunatumia ni pesa za wananchi wa Tanzania. Kuna hoja inazunguka ndani ya Bunge hili kwamba hata Rais na Baraza lake hawatakiwi kupewa taarifa kuhusu mradi huu, lakini Bunge lipewe taarifa Rais asipewe! Kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyooleza mchakato huu unaendelea. Katibu Mkuu ambaye ndiye amasimamia mchakato mzima wa manunuvi, anaomba ushauri *PPRA*, yeye ndiye ameomba sasa hivi ameomba pia ushauri kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili *paper* ya kwenda kwenye Baraza la Mawaziri iandaliwe ikamilike ili tumalize mchakato huu. Sasa tukianza kuibua maswali mengine ya kusema tuitishe Kamati, hili sijui lipelekwe Wizara nyingine, watakaochelewesha mradi huu ni ninyi sio sisi. Mimi naomba tupewe nafasi kukamilisha mradi huu wa vitambulisho. Ushauri wa *PPRA* tumekwishaupokea, ushauri kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndiyo unakamilisha, akishamaliza tunapeleka kwenye Baraza la Mawaziri, tunawafahamisha jamani yaliyosibu ni haya. Tukishayapata hayo tunamrudishia Katibu Mkuu afanye maamuzi yake kama inavyotakiwa kisheria na tunaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu ni kwamba Bunge lako Tukufu litaturuhusu kufanya kazi yetu na ili tumalize mchakato huu jinsi tulivyopanga ili kama

tulivyoahidi katika Hotuba yetu ya Bajeti tuanze utekelezaji wa mradi wa vitambulisho katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. (*Makofii*)

(*Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kazi hii iliyopo mbele yetu niwakumbushe kuhusu kifungu 104(1) na (2). Kifungu 104 (1) kinamwezesha Mwenyekiti kuongeza dakika 30 baada ya muda wa Bunge kwisha. Kifungu 104 kinamwezesha Mwenyekiti kama zimebakia dakika 10 baada ya kuongeza dakika 30 na kabla ya kwisha hizo 30 kama hatujamaliza kazi tunafunga mazungumzo tunapitisha vifungu vyote kwa pamoja yaani *guillotine*. Naomba hii tuelewane.

### Matumizi ya Kawaida

#### Fungu 14 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kif. 3001 - *Fire and Rescue Services* . . . Sh. 3,751,820,400/=

Kif. 3002 - *Fire and Rescue Services*  
Training Inst... . . . . . Sh. 574,522,600/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### Fungu 28 - Jeshi la Polisi

Kif. 2001 - *Police Main Force* . . . Sh. 120,706,500,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhahula kama ni mshahara wa Waziri bado.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 - *Police Marine* . . . . . Sh. 2,608,736,000/=

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko subvote 2002 kifungu 220300 - *fuel, oils lubricants* ambazo ni Shilingi milioni 445.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hii *Police Marine* kule Zanzibar nakumbuka ilikuwepo, hivi sasa sijui kama ipo na haya mafuta ni kwa ajili ya vyombo gani? Je, *Police Marine* Zanzibar wana vyombo gani baharini? Mbona hali iko ngumu kule! Hebu atupe ufanuzi zinakwenda wapi zote hizi na upande ule mwingine wa muungano zitapatikana wapi kwa ajili ya vyombo gani?

**MWENYEKITI:** Unaona swali hili halihitaji mshahara wa Waziri anauliza hizi ni za kazi gani? Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa ni kwa ajili ya *Police Marine* kote nchini ikiwemo na Zanzibar na kule Zanzibar iko Boti ya *Police Marine* ambayo inaitwa MV. Mamba bahati mbaya Boti hazitoshii kuongeza sio katika Bajeti hii, lakini kwa bajeti hii tumetenga fedha kwa ajili ya kukarabati boti nyingi zaidi katika *Police Marine* ambazo tunazo nchini kote.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2003 - *Railway Police Division* .... Sh. 474,121,400/=  
Kif. 2004 - *Police Signals Branch* ..... Sh. 5,527,849,100/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2005 - *Police Zanzibar* ..... Sh. 12,875,251,700/=

**MHE. KIDAWA ALI SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *item 220300 - fuel, oil and lubricant*. Katika mchango wangu wa maandishi nimeelezea kuwa kule Zanzibar sasa kumetokea uhalifu wa aina mpya ambao haukuzoeleka ambao ni wa ujambazi wa kutumia silaha za moto.

Zamani ulikuweko wizi wa visu tu na mapanga na hali hii inahitaji Jeshi letu la Polisi kuwezeshwa ili kuweza kupambana na uhalifu huo na kufuutilia matukio kila yanapotokea kwa maana ya magari, pikipiki, vifaa vya mawasiliano na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri labda anieleze kwa nini bajeti ya mafuta imepungua kwa Shilingi milioni 27.9 ukilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita na matatizo bado yanakuwa kama nilivyozungumza?

**NAIBU SPIKA:** Swali zuri. Mheshimiwa Waziri jibu!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika hivi vifungu ambavyo viko hapa, kile cha mwaka jana hiyo ni *approved estimates*, haiambatani na pesa ambazo zimekuja kutumika kwenye *actual expenditure* ambayo ilifanyika. Kwa hiyo, tunapoomba *estimates* za mwaka huu, zinaendana na matumizi halisi ya mwaka jana. Lakini ikitokea kwamba tutahitaji pesa zaidi na inawezekana kabisa kwamba itahitajika, tutajitahidi kufanya *re-allocation* kama tunavyofanya siku zote na kujibana hapa na pale ili kuwaongezea mafuta.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na*

*Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2006 – *Police Airwing*.... .... .... .... Tsh.1,787,299,300/=  
Kif. 2007 – *TAZARA Police* .... .... .... .... Tsh. 597,970,100/=

*(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na  
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2008 – *Field Force Unit*.... .... .... .... Tsh. 6,712,404,000/=

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki *Field Force Unit*, katika mchango wangu wa maandishi nimemwomba Mheshimiwa Waziri aweze kutufafanulia kuhusiana...

**MWENYEKITI:** Taja *Subvote na item.*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** *Basic Salaries pensionable posts. Operations* ambazo askari wa *Field Force* wanafanya hasa hasa kitu ambacho nina *experience* nacho ni nyakati za uchaguzi, fedha wanazolipwa ni kidogo sana. Kwa mfano, Tarime, walikuwa wanalipwa kwa siku moja Sh. 1000/=. Juzi Boharamulo, nimeongea na vijana wa *Field Force*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, sio hapo!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Ni wapi?

**MWENYEKITI:** Hilo ni swali la *Policy*, kwa sababu hapa tunazungumzia mshahara wa *Field Force Unit*, haya ndio masuala ya *pensionable post*. Kwa hiyo, unasema Tarime wangeongezewa mishahara? Hili ni suala la kisera, nenda kule kwenye mshahara wa Waziri.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *subvote 221000 - travel in country*. Kwa sbabu hawa askari huwa wanasa firishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kwa hiyo *travel in country* ni pamoja na *Per diems* na...

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umebadili hiyo?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Ni *subvote 221000*.

**MWENYEKITI:** Ehe, eleza tukusikie!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Sasa nilikuwa napenda kufahamu, katika hizi shilingi milioni 280 ambazo zimewekwa hapa, kuna nyongeza maalum ya *subsistence allowance* ambayo askari wetu wanalipwa wanapokwenda kwenye *operations* maalum. Kama nilivyo eleza hapo awali, taarifa tulizozipata kwa askari waliokuwepo wakati wa uchaguzi mdogo Tarime walikuwa wanalipwa Sh. 1000/= kwa siku. Wakati wa uchaguzi

mdogo Biharamulo, juzi walikuwa wanalipwa Sh. 3000/= kwa siku, wakati wafanyakazi wengine wote wa Serikali wakisafiri nje ya vituo vyao vyta kazi wanalipwa kuanzia Sh. 30,000/= mpaka sh. 80,000/= kutokana na maeneo wanayokwenda. Kwa hiyo, nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri anifafanulie: Je, hizi Shilingi milioni 280 za *travel in country* kwa vijana wanaokwenda kwenye *operations* maalum, malipo yao ni shilingi ngapi kwa siku? Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Uulize kwamba ndio hizi zinazohusika? Mheshimiwa Waziri, naomba maelezo! Anachouliza ni kwamba hizi ndizo hizo zinazohusika na *operations* hizo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba, askari katika Wizara yangu wana *operations* za aina mbalimbali. Kuna *operations* ambazo tunazilipia sisi moja kwa moja na kuna *operations* ambazo zinatoka katika vifungu vingine maalum. Labda nikubaliane na Mheshimiwa Zitto kwamba ni kweli posho ambayo wanapewa, hiyo *allowance* katika kipindi cha *operations* sio kubwa na tungependa kupata posho kubwa zaidi kama nilivyoeleza huko awali. Lakini, hali halisi ndio hii na tumejitahidi, kuna baadhi ya posho nyingine zimeweza kuongezeka, lakini tutajitahidi kaddri ya uwezo wetu miaka inavyokwenda, bajeti inavyoongezeka kuongeza posho za askari.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2009 – *Traffic Police* ..... .... .... .... .... Tsh.1,652,889,400/=  
Kif. 2010 – *Police Airport* ..... .... .... .... .... Tsh. 566,534,100/=  
Kif. 2011 – *Police Dog and Horses* ..... .... Tsh. 987,757,300/=  
Kif. 2012 – *DSM Special Zone* ... .... .... .... Tsh.9,816,545,400/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 3001 – *Police College Moshi*.... .... .... Tsh.4,288,905,400/=

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *sub item 221000 - printing, advertising and information supplies and services*. Kwa kuwa hiki ni Chuo cha Polisi Moshi na mimi naamini wanahitaji sana kufanya *printing* pamoja na masuala mengine yanayohusiana na *information*, lakini ukiangalia katika kifungu hicho hakijapewa fedha. Sasa nilikuwa naomba kuuliza ni kwa nini? Hiki Chuo kitawezeha shughuli zake za *printing*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Swali sahihi!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kumfahamisha kwamba kasma hiyo ilibadilika na ukiangalia katika

kifungu 220100 ile *office and general supplies and services*, utaona imepanda kutoka Sh. 1,500,000/= kwenda kwenye Shilingi milioni 40. Hizo pesa zimehamishiwa kule.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *subvote* 3001 hiyo, kifungu kidogo 221300 - *education material supply and services*. Hivi Vyuo vyote ambavyo vinatoa mafunzo kwa askari wetu viko upande wa Tanzania Bara na kule Zanzibar, nafikiri kama zamani nakumbuka pale Ziwani tu ndio kuna chuo. Lakini kasma yake siioni popote. Hivi nya Bara vinapotengewa moja kwa moja, vile nya Zanzibar pesa yake inapitia wapi? Hebu nionyeshe na kama kiko chuo!

**MWENYEKITI:** Ni swali sahihi. Mnaanza kuyawezza haya mambo! Mheshimiwa Waziri, umelielewa swali lake?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Nilikuwa sijalipata vizuri swali!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, rudia!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nasema hivi, hili Jeshi la Polisi ni Jeshi la Muungano na kuwa Vyuo...

**MWENYEKITI:** Una-refer kwenye kifungu kidogo cha 221300.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** *Yah, education, material supply and services.* Ni kwamba Jeshi la Polisi vyuo vingi viko huku nya kuwapata mafunzo askari wetu. Kule Zanzibar zamani nakumbuka pale Ziwanii kilikuwepo na huku vinaonekana vyuo vyote vimetengewa hela moja kwa moja na vinaonekana kwenye vifungu, kile cha Zanzibar sikioni, hakijatengewa. Kama kipo, nifahamishe kiko wapi kile Chuo cha Zanzibar kinachotoa mafunzo kwa askari wetu?

**MWENYEKITI:** Kwamba Je, hapa zipo ama kama hazipo ziko wapi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi askari wetu toka Zanzibar wanakuja kufanya *training* hapa Bara.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni hicho hicho.

*(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – Police College ... .... .... Tsh.1,340,876,100/-

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 4001*, zimetengwa shilingi milioni 552 kwa ajili ya *Police Vehicles Maintenance Unit*. Kule Kigoma sisi tuna tatizo kubwa sana katika Ziwa Tanganyika.

**MWENYEKITI:** Ngoja tuwe pamoja, hatukuelewa unaongelea *sub item* gani.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Jumla ya shilingi milioni 552 ambazo zimetengwa kwa ajili ya *Police Vehicles Maintenance Unit*. Napenda nifahamu, fedha hizi ni pamoja na maboti ya Polisi kuzuia wizi katika Ziwa Tanganyika? Wavuvi wetu wanaibiwa sana mali zao na inabidi wavuvi wao wenyewe wachange pesa na mitumbwi yao na maboti yao kwa jili ya kwenda kukamata mali zao ambazo zinapelekwa upande wa pili wa mpaka katika nchi ya *DRC*. Je, fedha hizi kuna utengenezaji wa maboti ya Polisi ili kuzuia ujangili katika Ziwa Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Hapana! Kwa sababu imeandikwa *basic salaries, pensionable posts, basic salaries, non-pensionable posts, total* yake ndio hiyo.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 5001 – *Police Medical Unit* .... .... .... Tsh.2,040,864,300/=  
Kif. 6001 – *Police Building Brigade* .... .... Tsh.3,223,704,900/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 7001 – *Criminal Investigation Division*.... .... .... .... .... .... Tsh15,415,390,300/=

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Programme 70 - Crime Prevention, Item 410400 - Acquisition of Specialized Equipment* ambayo imetengewa Sh. 2,639,000,000/=.

Katika kujumuisha hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema suala la ulinzi ni letu pamoja na ukweli kwamba nakubali ni lazima tusaidiane ili kuzuia huo uhalifu, lakini sasa imefika *stage* kwamba hawa wahalifu wanatumia vifaa vya moto na sisi kama kwetu huko visiwani hatujazoea masuala haya na hata haturuhusiwi kuwa na silaha: Sasa hiki kifungu, katika hizi *specialized equipment*, sasa na sisi Mheshimiwa Waziri atakubaliana nasi kwamba iko haja sasa wafanyabiashara huko visiwani nao wapate hivyo vifaa vya moto ili na sisi tuweze kuisaidia Polisi kulindana na huu ujambazi? Ahsante!

**MWENYEKITI:** Kwamba hizi hela zitatumika pia kuwapa wafanyabiashara kufanya ulinzi? unamaana hiyo? Haiwezekani! Hebu Mheshimiwa Waziri, unawenza kujibu! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kifungu hiki hakihusiani kabisa na silaha za watu binafsi. Hivi ni vifaa maalum kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Lakini, pili, kwa suala la wananchi Zanzibar kushika silaha, hapa kwenyewe Bara najaribu kutafuta namna ya kudhibiti zaidi.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 7002 – *Stock Theft Prevention Unit...* Tsh. 495,621,700/=

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 29 – JESHI LA MAGEREZA**

Kif. 1001 – *Prisons Headquarters ... ...* Tsh. 8,193,484,600/=

Kif. 2001 – *Parole Department ... ...* Tsh. 408,838,800/=

Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation... ... ...* Tsh. 84,653,323,700/=

Kif. 2003 – *Resettlement of Offenders ... ... ...* Tsh. 1,109,435,400/=

Kif. 3001 – *Prisons Staff College... ...* Tsh. 1,348,869,100/=

Kif. 3002 – *Prisons Driving School... ...* Tsh. 219,645,600/=

Kif. 3003 – *Prisons Trade School... ...* Tsh. 493,044,600/=

Kif. 3004 – *Prisons College Kiwira... ...* Tsh. 965,033,900/=

Kif. 4001 – *Prison Building Brigade... ...* Tsh. 1,316,572,700/=

Kif. 4002 – *Prison Industries... ... ...* Tsh. 496,997,600/=

Kif. 4003 – *Prison Farms... ... ...* Tsh. 1,033,393,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MWENYEKITI:** Nenda Fungu 93, tumalize huko halafu tatarudi huku, maana mengine huko tutalala huko huko. (*Kicheko*)

#### **FUNGU 93 – IDARA YA UHAMIAJI**

Kif. 2001 – *Immigration Zanzibar ... ...* Tsh. 2,619,326,000/=

Kif. 2002 – *Immigration Mainland... ... ... ... ...* Tsh. 22,745,808,476/=

Kif. 2003 – *Regional Immigration Offices... ... ... ...* Tsh. 2,746,114,000/=

Kif. 2004 – *TZ Regional Immigration*

*Training Academy... ... ... ... Tsh. 572,855,524/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na  
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **FUNGU 51 – WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Kif. 1001 – *Administration and  
General ..... .... .... .... .... .... Tsh.1,874,047,300/=*

**MWENYEKITI:** Simameni wote kabisa! Nimeandika Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Siyame, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Killimbah msiwe na tatizo. Mheshimiwa Dr. Mahenge, Mheshimiwa Luhahula, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Kyendesya, Mheshimiwa Hafidh Ali, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mpesa, Mheshimiwa Nyami, Mheshimiwa Yono, usijali nitachanganya wakati tukiwaiteni mradi muwe brief. Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Maghimbiri, Mheshimiwa Salum, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Mwera, Mheshimiwa Ameir, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, aa Mheshimiwa Mpina nimekuruka! Tumeandika wote? Tunaanza na Mheshimiwa Zitto kwa sababu hata kuchagia ulikuwa haupo! (*Kicheko*)

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri! Kwanza, kwa kuwa sikuchangia na nina dakika tatu, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa askari waliokuwa kwenye *operations* Biharamulo, walitoa ushirikiano mkubwa sana. Kwa hiyo, kwa niaba ya askari walikuwa Biharamulo, napenda kukupongeza. (*Makofî*)

Pili, umejieleza sana kuhusu vitambulisho, tutafuatilia. Tatu, nimekuletea katika mchango wangu wa maandishi hoja ya askari ambao ni wapiga kura wangu Kigoma wanatoka Kata ya Bitale ambao kwa maeleo ambayo wamenipatia na ambayo nimeipatia Wizara, walifukuzwa kazi kinyume na taratibu za Jeshi la Polisi. Nafahamu kwamba ulikuwa na hoja nyingi sana za kujibu, lakini kwa hili kwa sababu linahusu wapiga kura moja kwa moja, ningependa kupata ufanuzi kutoka kwako na ni vipi ambavyo askari hawa watapata haki zao. Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Kabwe ametuletea maeleo kuhusu wale wapiga kura wake wawili. Isingekuwa rahisi katika muda huu mfupi kuweza kutoa jibu ambalo lingekidhi kutohana na suala la kwamba ni watu halisi wenye mahitaji halisi ambayo inabidi tuyafuatilie. Mimi namwomba tu anipatie muda, baada ya Bunge hili tutaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tupate jawabu lao.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Kila anayesimama ni ajenda moja tu. Habari ya shukrani na wale waliokufa acheni tu, hapa sio penyewe. (*Kicheko*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka nipate maelezo tu kwamba Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga Chuo cha Maafisa Upelelezi hapa Dodoma. Sasa nataka nipate maelezo, Je, mpango umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hapa hata Naibu wako anaweza kusaidia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mpango bado upo.  
(*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hayo ndiyo majibu ya kitaalam, siyo maneno maneno!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nimeulizia misingi ya kikatiba ya matumizi ya Polisi katika *operations* mbalimbali, kwa mfano, *operation* ya kufukuza wafugaji wa ng'ombe Kilosa, wafugaji wa ng'ombe Loliondo. Halafu natakata kuelewa, ni kwa nini hapajawa na *operation* ya kufunga Mgodi wa North Mara baada ya kuona kwamba yule mwekezaji ameweuka sumu katika Mto na Serikali imekubali hilo jambo? Nataka kujua misingi ya kutumia *operations* hizi ni ipi kikatiba na inakuwa rahisi zaidi kutumia kwa wananchi, lakini sio kwa makampuni yanayowekeza.

**MWENYEKITI:** Anauliza tu *operations* zina misingi gani? Hiyo ilikuwa mifano. Haya Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba kuna utulivu na amani ndani ya nchi yetu popote pale bila kuangalia kwamba ni wananchi, makampuni na kadhalika. Kitu ambacho ningependa kumfahamisha ni kwamba, kwa suala hili la North Mara Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajibu maswali ya papo kwa papo alinielekeza niende kule. Nilimtuma Naibu wangu ambaye alikwenda. Baada ya hapo, Mawaziri wenzangu wengine wameelekea kule na ndio wamerudi. Mimi ningefikiria kwamba kwa sababu wamerudi tu jana, nipewe nafasi ya kufanya kazi. Kama ikihitajika kupeleka Jeshi la Polisi na nina imani ndio maana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniambia niende kule kwa mara ya kwanza. Tutaifanya kazi jinsi tunavyopaswa.

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tunduma, Wilayani Mbozi mpakani na Zambia ambao kwa uchache tu mchana una watu wasiopungua 200,000 na usiku wako kwenye 70,000 hivi, siku za hivi karibuni na hata hapo nyuma umekubwa na matukio ya ujambazi na vurugu nyingi pamoja na kwamba kuna ulinzi shirikishi. Kwa kuwa tumekuwa tukileta maombi kwamba vituo na idadi ya askari Polisi viongezwe, lakini hadi sasa tuna kituo kimoja tu. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba huu ni wakati muafaka Mji huu kuweza kupewa hadhi ya kipolisi ili kuweza kukabiliana na matukio haya ambayo ni hatari kwa maisha na mali za watu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba hivi karibuni kuna tukio ambalo limetokea pale ambalo linasikitisha sana. Kwa bahati mbaya kuna mtu ambaye ameuawa na bado tunajaribu kubaini kama alikuwa jambazi au la. Ninachotaka kusema ni kwamba labda itabidi tufanye tathmini ya kina kuona kama kuna haja ya kuongeza vituo vya Polisi pale. Nitakachomwahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kati yangu mimi au Mheshimiwa Naibu Waziri, tutakwenda pale na viongozi wetu wa Jeshi la Polisi kuangalia hali halisi ili kutoa uamuzi.

**MWENYEKITU:** Ahsante! Mheshimiwa Zambi jirani yake huko kwenye majimbo huko.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi, mwaka jana nimekuwa naongelea kuhusu kukarabati kituo cha Polisi ambacho ndio kiko Makao Makuu ya Wilaya pale Vyawa. Kituo hiki kimejengwa karibu miaka ya 1960 na kilikuwa kituo tu kama cha kuwakusanya manamba kwa ajili ya kwenda kwenye mashamba ya mkonge na maeneo mengine, leo ndio kituo cha Polisi na kiko kwenye hali mbaya kuanzia kituo chenyewe, lakini pia na nyumba za watumishi. Nami nafurahi kwamba *IGP* Mwema ameshawahi kuwa *RPC* Mbeya, anakijua kilivyo, sina hakika kama Waziri amekwenda huko.

Lakini mwaka jana wakati Naibu Waziri alipokuwa anajibu maswali alisema kwamba kituo hiki kiko kwenye programu ya ukarabati, lakini kila nikifutilia sioni kama kuna dalili yoyote kwa ajili ya kile kituo pamoja na nyumba za Polisi ili ziweze kukarabatiwa vizuri. Sasa naomba kujua, Wizara inanieleza nini leo lakini pia na askari wale ambao wanaishi katika hali ambayo siyo nzuri sana pamoja na kitu okwa ujumla na nyumba zao?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoleza nilivyokuwa nachangia hoja hii, Wizara yangu inatambua kabisa kwamba tuna vituo vingi ambavyo viko katika hali mbaya. Kituo ambacho anakiongelea Mheshimiwa Mbunge, yeeye anasema kimejengwa mwaka wa 1960, lakini tukienda Lushoto tuna kituo cha kwanza kabisa cha Polisi hapa nchini ambacho kimejengwa nacho kiko katika hali mbaya zaidi. Sasa, mimi kitu ambacho ningesema ni kwamba lazima tuangalie namna ya kutumia rasilimali tulizonazo katika vituo vyetu vyote ili kujaribu kuboresha hali halisi tuliyonayo. Ninachomwahidi ni kwamba tutakwenda, tayari tumeshaahidi kwamba tutakwenda Tunduma na katika kwenda Tunduma, tutakwenda katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, tutaangalia na kama ukarabati ni ule ambao hautachukua fedha nyingi, tutajaribu kuangalia wapi tubane ili tuendelee na ukarabati kama alivyoahidiwa katika jibu alilopewa na Naibu Waziri katika swali lake kwenye Bunge lako Tukufu.

**MWENYEKITU:** Ahsante! Niende upande huu, Mheshimiwa Hafidh Ali!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilimpongeza sana Mheshimiwa

Waziri na hata katika kauli yake kwamba kila Wilaya hivi sasa itapata gari kutokana na bajeti. Lakini kwenye mchango wangu pamoja na maswali ambayo tayari nimeshauliza katika Bunge hili kiasi mara tano, mimi nina kesi maalum katika kituo cha Polisi cha Mazizini. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alishatembelea eneo la Jimbo langu ambalo kijiografia ni eneo liliko pwani linalopitisha magendo ya aina zote kuanzia bangi, dawa za kulevyta, wezi wa aina zote na hivi sasa zimeingia silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nadhani hakunijibu katika *special case* yangu ambayo nimempa katika kituo hiki cha Mazizini. Je, katika hizo Wilaya ambazo zitapatiwa hiyo gari, kituo hiki maalum na hasa tukielekea kwenye uchaguzi, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja hivi sasa kutupatia gari kupunguza uhalifu ambaao unatokea katika Jimbo langu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tulisema magari amaeahidi tumbane baadaye ambapo tutakuta hakuna magari. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Shellukindo

**MHE.BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo aliyoeleza Mheshimiwa Waziri kuhusu vitambulisho, Tanzania na Watanzania Kiuchumi na Kisiasa tunahitaji vitambulisho mapema iwezekanavyo, mchakato mzima wa kupita kwenye Baraza la Mawaziri kwa utaratibu ambaao tuliuona sisi katika ile *area* ya uzabuni ni kwamba tayari inapita kwenye Baraza la Mawaziri, kwa hiyo, inapofika pale kwenye hatua ya kutangaza *Tender*, tayari ile kazi imekwishamalizika. Ndani ya kamati ambayo mimi nimo ambapo tunahusika na Wizara hii tuliarifiwa kwamba masuala yote ya zabuni, sheria inasema kabisa ni masuala ya siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamizi Mkuu ni Katibu Mkuu, lakini sisi tulipokuwa pale tuliambiwa na Waziri kwamba yeye alilazimika, aliona kuna dosari kuna baadhi ya watu wamelalamika. Hawa watu waliolalamika walijuaje hali ile hali ni siri? Sasa Mheshimiwa hadi kufikia juzi asubuhi, sisi wengine tunakereketwa kwa sababu moja ya sababu hizo zilinitoa Bunge la Afrika ya Mashariki kuja hapa ni kusimamia yale ambayo tulikuwa tunaona ndani ya nchi yetu hayaendi tushirikiane na Wabunge wengine ili tuyasukume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la vitambulisho tunaloliona sisi hapa sasa hivi tunataka vitambulisho. Mimi nimefuatilia hadi juzi asubuhi nimearifiwa kwamba hakuna kinachoendelea, sasa hivi wale Watumishi wote wamekaa wanashubiri ambapo itabidi kwamba uandikwe huo mchakato, waraka uende Baraza la Mawaziri ambapo hatujui itakuwa ni lini. Inatisha zaidi Waziri anapouliza yeye mwenyewe mwenye dhamana: Je kuna nini? Sasa kama hajui mchakato utakwenda kweli? Sisi tunahitaji vitambulisho, *common Market* imeanza na mengineyo, mimi naomba tupewe maelezo kabla ya Bunge halijakwisha ama sivyo mimi nina nia kabisa ya kuleta hoja mahsus.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nilipokuwa nachangia hoja hii niliuliza swali na swali langu ni kwamba kuna nini? Ninarudia tena kumwuliza Mheshimiwa Shellukindo atueleze, kuna nini? Ameeleza kwamba amekuja kwenye Wizara yangu kuulizia mchakacho wa uandaaji wa Waraka wa

Baraza la Mawaziri, Waraka wa Baraza la Mawaziri ni la kwangu? Hujaja kwangu Mama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Baraza la Mawaziri ni siri. Mimi kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nimepewa dhamana ya kusimamia shughuli zote ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ndio maana ninaulizwa na Bunge lako Tukufu hapa kipi kinachoendelea. Sasa nimeshaeleza kwamba mchakato unaendelea, waraka nimeeleza kwamba tunasubiri ushauri kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Ninaomba kuuliza, kuna nini kinachowafanya baadhi ya Wabunge wasiitake Wizara yangu kupata ushauri wa kisheria ili kuweza kuendelea mbele? Kule nyuma tulitaka kukatazwa kwenda *PPRA*. Niliuliza kuna nini *PPRA* walijibu kwamba hoja nilizozitoa zilikuwa sahihi. Sasa leo hii tunaomba kupata ushauri toka kwa mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini watu bado wanatuhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea kuuliza kuna nini? Miaka miwili iliyopita nilivyokuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini baadhi ya Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mbunge walihoji *Intergrity* yangu nilivyokuwa nasimamia Kamati ya Madini.

Nilikaa kimya kwa kipindi cha miaka miwili, baada ya miaka miwili Wabunge hao hao walikuja kusema kwamba Masha alikuwa sahihi kipindi kile. Masha huyo hajabadilika, ni Masha huyo huyo kwenye hili. Naamini niko sahihi, nitaendelea kulisimamia suala hili, mchakato unaendelea (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri. Hapa tunazungumza na Watanzania. Ukiniliza mimi hata kama Naibu Spika, haya mnayosema kuna nini, kuna nini, siwaelewii kabisa. Kwasababu Serikali itajibu hayo yaliyoko chini chini huko Watanzania wa kawaida *including* mimi na baadhi ya Wabunge wengine hapa hawajui. Hawajui kabisa! Sasa ni vizuri mkajibu kazi mnayofanya Mheshimiwa Waziri.

Sasa ni vizuri nyie mkajibu kazi mnayofanya Mheshimiwa Waziri, hayo ya kuna nini wengine hao watagundulika baadaye, lakini mtusaidie sisi Watanzania vitambulisho vitapatikana? *Ful stop.* Naomba tuwe hivyo, hii nyingine, maswali yenu yote mnafahamiana nyinyi wenye kwa vijembe huko huko. (*Vicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini Watanzania wanataka kufahamu kwamba vitambulisho vitakuwepo? Mheshimiwa Waziri mnayofanya kazi, mna shida kutakuwa na maneno mengi. Nyinyi msiyasikilize hayo yote, mtashindwa kufanya kazi. Jibu kile ambacho Watanzania wanakutegemea ufanye. Sasa vitambulisho vitapatikana ? Ndio swalii la msingi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti asubuhi hii vitapatikana. *Pilot project* itafanyika katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani tumeelewa sisi, vingine hatuelewi. Tunaendelea. Mheshimiwa Mpesa.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa miji yetu katika mchango wangu wa maandishi nilisema hivi sasa Miji yetu inakabiliwa na ongezeko kubwa la Vijana ambao wamemaliza shule na vyuo na hawana ajira. Lakini katika Jiji la Mbeya kumezuka mtindo wa kuwafanya vijana hawa kama kitega Uchumi. Ukifika wakati baadhi ya maaskari ndani ya Jiji la Mbeya wanaanza kuanzisha msako wa kwamba hawa ni wazuzuraji na vijana hawa wanapopelekwa kwenye Vituo ya Polisi hawatolewi mpaka zimepatikana pesa. Mtindo huu umekuwa ukijirudiarudia na ndio maana nasema vijana hawa wamebekwa kama vitega uchumi. Sasa na maeneo haya ni pamoa na maeneo ya Pambogo kule Iyela, Mwanjelwa, Isanga, Ilemi na maeneo mengi pamoa na Nzovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri, hizi fedha wanazotozwa hawa vijana zinaingia katika maduhuli ya Serikali? Kwa sababu imekuwa ni kero kubwa sana kwa wanandugu kwenda kuwakomboa hawa vijana na wakitoa pesa wanaachiwa kuanzia Sh. 5000/=, Sh. 10,000/= mpaka Sh. 20,000=/. Je, mtindo huu utakoma lini? Nilitaka nipate tamko la Mheshimiwa Waziri juu ya hali hii.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia tatizo ambalo Mheshimiwa Mpesa amelieleza. Siyo sahihi kwa jeshi la Polisi kupokea pesa kwa hali hiyo na kama ni kweli tutaifanyia kazi. Nilivyoeleza hapo awali, nitafika Mbeya, tutafanya Ziara kamili katika Mkoa na tutaangalia matatizo yote ambayo yanausibu Mkoa wa Mbeya.

**MHE. PONSIAO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri. Nilikuwa naomba kufahamu kuhusiana na madai ya muda mrefu sana ya malimbikizo ya askari wetu wa Mkoa wa Rukwa katika majeshi yote Polisi, Magereza, Uhamiaji na hata Zimamoto.

**MWENYEKITI:** Malimbikizo ya nini?

**MHE. PONSIAO D. NYAMI:** Malimbikizo mbalimbali ya madai yao hawajalipwa na vilevile ukitazama makazi ya maaskari wote katika Mkoa wa Rukwa hakuna majengo yoyote ambayo yamekuwa yakijengwa kwa ajili yao na vitendea kazi vyao mara nyingi vinakuwa ni shida, wakati Mkoa wa Rukwa uko pembezoni na unabeba wakimbizi na maharamia kutoka nchi za jirani, sizitaji lakini zipo kama mbili hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni hatua gani hasa ambazo Mkoa wa Rukwa mtajaribu kuutazama ili maaskari wetu hao wasiendelee kupata shida?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba suala la malimbikizo siyo la Mkoa wa Rukwa peke yake kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Hata na mimi katika majibu yangu ni suala ambalo linakabili Taifa letu katika Mikoa yote ya askari, Lakini niseme pia kwamba

Mheshimiwa Rais alikwishatoa agizo kwamba kila jitihada ifanyike, malimbikizo ya madeni haya ya askari yalipwe. Sasa nataka nikwambie tu kwamba tuko katika mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa fedha kuona tutalifanya nini, lakini ni jambo ambalo linajulikana mpaka ngazi ya juu kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendea kazi Mheshimiwa Waziri amelizungumzia hili, tutakwenda kwa mujibu wa fedha zinavyopatikana. Lakini nia ya kuwapatia askari wetu vitendea kazi ili waweze kudumisha amani ambayo tunaitaka sana katika nchi yetu iko palepale. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa avute subira na tutajitahidi kufanya tutakayoweza kufanya lakini ni tatizo ambalo linakabili nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu kwa wa kifungu 104(1) nitaongeza dakika 30 na kama tukienda kama hatujamaliza zikibakia dakiaka 10 baada ya hizi dakika 30, basi tutapitisha vifungu vyetu kwa pamoja. Mheshimiwa Yono.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi niliandika kwa uchungu sana kuhusu suala la Kituo cha Polisi cha Ilembula ambacho kinahitaji ujenzi wa haraka sana. Lakini kwenye hotuba yake nzuri Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani - ndugu yangu Mheshimiwa Masha alielezea kuhusu Vituo vya Polisi vya Makambako na Kituo cha Ilembula kinaripoti Makambako, sasa nilikuwa naomba nipate ufanuzi: Je, katika ujenzi wa ofisi ni pamoja na kituo cha polisi cha Ilembula ambako kwenye Jimbo la Njombe Magharibi kuna matukio mengi sana ya uhalifu wa kutumia silaha za moto, majanga ya radi watu wanakufa pamoja na ajali mbalimbali? Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi tutakachoendelea nacho ni Makamabako. Tunaweza tukaangalia huko mbele ya safari kuhusu Kituo cha Ilembula lakini kwa sasa hivi haiko katika mipango yetu.

**MHE. ANNA M. KOMU - MSEMAJI KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilikuwa nataka kuelewa. Kwasababu niliangalia kwenye kile kitengo cha matengenezo ya magari sijaona fungu lilowekwa kwa ajili ya ununuzi wa vipuri, yaani spea za magari. Sasa nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie hili fungu la ununuzi wa vipuri vya matengenezo ya magari, hivi huwa linawekwa wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lipo, lakini tumeliacha, liko katika upande wa *Vote 28* katika *subvot* 2001 na ukitazama pale utaona katika kifungu kinachosema 230(400) utaona ndio pale swalii lake linaingia. Siyo kwamba tumelisahau lakini liko katika kasma nyininge.

**MHE.MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchango wangu wa maandishi nilijaribu kuielezea Wilaya ya Tunduru ki-geografia na ukubwa wa eneo na matatizo yanayojiri katika kituo chetu cha Polisi. Pamoja na matatizo ya magari ambayo Mheshimiwa Waziri ametolea ufanuzi, lakini kuna tatizo la

pikipiki ambayo ndiyo kifaa pekee ambacho tulikuwa tunakitumia sasa hivi kama kifaa cha usafiri, pikipiki ile imechukuliwa imepelekwa Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kijiografia Tunduru ina umbali wa kilomita 264 kutoka Makao Makuu ya Mkoa. Sasa hivi haina gari, haina pikipiki wala baiskeli: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akachukua hatua zipi za haraka kuhakikisha kwamba Wilaya ya Tunduru ambayo iko mpakani kabisa na nchi ya Msambiji na ina umbali huo ninaoueleza inaweza kupata usafiri wa haraka iwezekanavyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mtutura kama ifuatavyo. Kama alivyoeleza kuhusu suala la gari tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakiksha kwamba Wilaya zote ambazo hazina magari watapata. Kuhusu suala la pikipiki ombi lake nimelisikia tutamtafutia pikipiki.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeelezea juu ya kituo cha Shelui. Kituo cha Shelui ni kituo cha muda mrefu sana na eneo la Shelui ni eneo ambalo lina wakazi wengi sana na hivi sasa hata Halmashauri ya Wilaya ya Iramba tumeweka kwenye mpango wa kuwa mji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na kituo hiki cha Shelui cha Polisi toka kilipoanzishwa hakijawahi kujengewa amari kwa ajili ya utunzaji wa silaha.

Nimelieleza hili suala toka mwaka 2007/2008 na leo narudia na Mheshimiwa Waziri amekuwa akiniahidi kwamba watahakikisha kwamba wanajenga amari pale katika Kituo cha Shelui na baya zaidi ni tukio lililojitekeza hivi juzi wananchi walivamiwa katika hoteli iliyopo pale *stand* Shelui na wale Polisi walipofuatwa walishindwa kwenda kukabiliiana na wale majambari kutokana na ukosefu wa silaha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi kuhusiana na hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwa kweli tunajitahidi na ninaomba tuione hivyo. Maana yake kila Mbunge ni haki yake, hata na mimi, hata na wewe na mwingine anataka kila kitu kifanyike kwake, lakini uwezo unakuwa ni mdogo. Ndio maana nikasema kwamba tutajitahidi mpaka ngazi ya Wilaya inapotelemka kule chini wananchi, Halmashauri tujitahidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Killimbah hili tulizungumze, tutazame mchango ambao wanawenza wakaweka wao na sisi tunawenza tukaweka mchango gani tuweze kutengeneza hiyo.

**MHE. FATUMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami katika mchango wangu wa maandishi nililizia juu ya polisi mmoja ambaye amefariki na mpaka leo ni zaidi ya miaka mitatu hajalipwa. Najua ni muda mfupi wa kunipa majibu maana yake mchango wenywewe ulikuwa wa maandishi, lakini kwasababu nimetumwa na wapiga kura ambao ni ndugu zake na ameacha watoto wachanga na wanahitaji watoto wale kusoma itabidi Mheshimiwa nikuombe unipe jibu nikawaambie nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie pia naomba niulize kuwa mtu akifa inakaa muda mrefu kabla hajalipwa hasa kule kwetu. Mheshimiwa Waziri kuna nini huko? (*Vicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba ujibu hili la pili. Lile lingine litafuata maana yake hata jina hulifahamu. Jibu hili la pili kwamba watu wakifa wanalipwa kwa muda gani? Ni hilo tu basi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningesema kwamba kama askari akifa akiwa kazini kuna *death gratuity* ambayo anastahili kupewa na ni suala tu la kushirikiana na ofisi yetu tufanye kazi hizi haraka. Hatuna nia ya kuwachelewesha askari wetu na hasa familia zao kupata mafao yao. Tunafahamu kabisa kwamba ucheleweshaji unatokea siyo tu Zanzibar lakini hata bara, naomba tushirikiane tufuatilie kwa pamoja ili tuweze tukatafuta stahili. Karibu sana ofisini kwangu Mheshimiwa Maghimbi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali haya ya mtu mmoja mmoja mjifunze kwenda kwa Mawaziri maana hapa hawawezi kujibu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufanuzi juu ya zoezi la uboreshaji daftari la wapiga kura Kisiwani Pemba ambapo vikosi vya SMZ vinakuwa na silaha za moto na vitisho katika zoezi hili la kiraia. Sasa jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao ni la Jeshi la Polisi: Je, kuna nini?

**MWENYEKITI:** Sasa mnaitengeneza wimbo! Mheshimiwa Waziri jibu swali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kwamba ni kweli katika majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ni kulinda amani na kuhakikisha kwamba kuna utulivu. Lakini pia katika Zanzibar kuna vikosi vingine ambavyo viko kisheria chini ya Sheria za Zanzibar ambapo pia vina majukumu hayo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Katika mchango wangu wa maandishi nilzungumzia katika suala la uhaniaji. Kuna wageni wanaokuja kutoka nje huwa wanapata *visa* zao kutoka kwenye Balozi zinazohusika na kuna wanaokuja hapa Tanzania wanapata *visa* wakati wakiingia mfano *Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *form* zile za kujaza, yaani *form Na.10 ile arrival form*. Katika sababu zinazowaruhusu wageni kuingia nchini sababu sio mojawapo ambayo imenitia utata kidogo ni wale wanaokuja kutafuta kazi wakiingia nchini. Katika *form* hii nawauliza, kama wanatafuta kazi ningependa kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri: Je, Kuna watu ambao wanakuja kutoka nje na wanapata kibali cha kufanya kazi nchini wakati wanaingia tu *Airport*?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye akifika pale *Airport* anapata kibali cha kufanya kazi hapa nchini, hilo

halipo. Ni kweli kabisa katika hiyo *form* iko sehemu ambayo inasema kwamba mtu aingie katika hali ya kutafuta kazi, hii *form* ni *form* ambayo ianatumika katika Afrika ya Mashariki yote na tayari Serikali yetu kupitia Wizara yangu imeshaanza maongezi na nchi zetu jirani za Afrika ya Mashariki ili hicho kipengele tukibadilishe, hata sisi pia tunaona hakifai.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi niliomba maelezo au ufanuzi kuhusu ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri humu ndani kufuatia matukio ya ujambazi pale Makete kwenye Kata ya Lupalilo kijiji cha Pandala ambapo wananchi hao waliwakilisha matatizo kwa Mheshimiwa Rais tarehe 3 Agosti, 2008. Pia Rais akaigiza kwamba atahakikisha kuwa polisi wanapelekwa pale na kwamba pale kuna kituo kimejengwa kwa nguvu za wananchi na vitu vilivyobaki vidogo wananchi wamekuwa tayari kukaa na polisi waweze kuchangia waweze kukamilisha na polisi waende pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Naibu Waziri aliahidi kwamba baada ya lile Bunge lililopita angehakikisha *RPC* anakaa na wahusika na ikiwezekana askari waende pale mara moja kuwasaidia wananchi wa pale Tandalo. Naomba ufanuzi

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli anavyosema Dr Mahenge. Nilizungumza naye lakini ni kwamba ni suala la muda na ningeomba tukishamaliza Bunge hili tutakuwa tumepata wasaa na tutafuatilia hilo suala lake. Sio kwamba tumelipuuza ni majukumu tu na shughuli tulizonazo.

**MHE . EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo sana na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi hasa katika Wilaya ya Bukombe ambavyo wanajitahidi ingawaje hawajabahatika kupewa motisha yoyote hata iliyotangazwa na *IGP*. Lakini wakati Waziri wa Ulinzi anajibu hapa swali langu alieleza kwamba wao wako tayari kusaidiana na Jeshi la Polisi hasa katika ulinzi wa amani katika maeneo yetu ambayo yana ujambazi mwingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa nikieleza hapa kuwa ukitaka kwenda kwenye Kata zangu mbili ni mpaka uombe Mungu. Sasa ninachotaka kuuliza hapa Mheshimiwa Waziri atufafanulie kwasababu hata wananchi kule wanategemea jibu. Atakuwa tayari sasa kushirikiana na Jeshi la Wananchi kwenda kulinda maeneo ya Ushirombo - Runzewe na Runzewe – Bwanga na Runzewe – Nyakanazi maeneo yenye ujambazi mkubwa sana na ambako hata ye ye aliopembelea kule ye ye siku nne nyuma alikuta kuna ujambazi mfululizo? Naomba ufanuzi, watatusaidiaje ili hata mimi Mbunge mwenzenu ninapokwenda kutembelea kule nisilazimike kuchukua Polisi kuni-escort ili nifanye kazi kwa amani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Luhahula kama ifutavyo:- Ni kweli mimi mwenywewe nimetembelea Jimbo la Bukombe, nimeona hali halisi, ukweli wana tatizo

kubwa la uhaba wa askari na vitendea kazi. Ni ukweli kabisa kwamba kuna ujambazi ambao inabidi ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vitu tulivyopanga nilivyoondoka pale ni kuangalia namna ya kuweza kuimarisha ulinzi katika Jimbo la Bukombe na tutafanya hivyo. Ibibidi kushirikiana na Jeshi la Ulinzi tutaliangalia kwa undani lakini kwa sasa hivi hatuamini kwamba Jeshi la Polisi limeshindwa kazi ni kwamba linahitaji kuongezewa vitendea kazi na tunahitaji kuongeza watu.

**MHE .HABIB J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, niliwahi kueleza kuhusu mambo ya uvunjaji wa haki za binadamu na hasa ukitendeka ndani ya Jeshi la Polisi. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anatoa mchango wake alituasa kuhusu matamshi ambayo na hili ni jeshi letu na ninakubaliana naye lakini kutokana na madaraka ya Bunge ya kifungu 63(3) na (a) (b) inabidi tuseme mambo mengine. Huu uvunjaji wa haki za binadamu naomba ninukuu kitabu cha taarifa cha 2006 – 2007 tuliipata hivi karibuni ya haki za binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema malalamiko dhidi ya Jeshi la Polisi, lalamiko kuhusu ajira, kufukuzwa kazi, Polisi kutesa na kuua, rufaa ya kupinga kufukuzwa kazi, kupigwa risasi, yako mengi mno, sasa ukurasa wa 284 na hizi zote yamekwenda kwa *IGP*. Kuna uvunjaji wa haki za binadamu zaidi ya huo ambao wametuma wapiga kura wetu na wengine ndio hawa askari kwamba kuna moja kubwa zaidi ambalo pia utakuta askari kwenye kota zile analala chumba kimoja na watoto wakubwa. Kuna haki nyingine ya Mama na Bwana hazipati kufanya kazi, huu ni uvunjaji mwengine wa haki za binadamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imepiga. Mheshimiwa Waziri nilikuwa nashangaa utanukuu kweli dakika tatu zikatosha haya!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja amabayo iko mbele yetu hapa siku ya leo kwa nilieleza wazi kabisa kwamba Wizara tangu inatambua kwamba baadhi ya Askari wetu wanaishi katika hali mbaya. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tunalitambua hilo, tunalifanyia kazi na ndio maana tupo katika mchakato mzima wa kujitahidi kujenga nyumba kwa ajili ya askari wetu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nilieleza juu ya baadhi ya maaskari wasiokuwa waaminifu wakitumia madaraka yao vibaya kwa ajili ya kujinufaisha. Nilitoa mifano miwili hai ambayo niliwakabidhi, nadhani leo ni siku ya 370 toka nikabidhi hiyo taarifa wakati wa kipindi cha bajeti kilichopita kuhusu jinsi Bwana Amos Mnguru alivyofilisiwa mali zake kwa kuporwa mifugo yake 50 na mifugo hiyo ikaenda Kituo cha Polisi na ikatoka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nikatoa mfano wa Mwalimu Abrahamu Mongo ambaye ye ye aliikutwa akiandaa *lesson notes* kule Mitundu kwa ajili ya kwenda darasani akawekwa chini ya Ulinzi, akawekwa kwenye gari akasafirishwa akielekea Kituo cha

Polisi Manyoni. Njiani kabla ya kufika Itigi gari likapinduka akavunjika mguu, huyu mtu akalazwa Gasper, wakamtelekeza pale alipopata nafuu kidogo kwenda Kituo cha Polisi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumwomba radhi Mheshimiwa Lwanji kwamba amekaa mwaka mzima bila kupata jibu. Ninachomuahidi *IGP*, amemskia yupo humu ndani na kupitia Bunge lako Tukufu namwagiza katika wiki hii jibu lipatikane na Mheshimiwa Lwanji tutakujibu.

**MHE.FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. *Item* hiyo hiyo kifungu kidogo 220 (400) - *medical supplies and services*. Mwaka 2007/2008, 2008/2009 hatukupata pesa yoyote, imeandikwa sifuri 2009/2010 kimepewa Sh. 800,000/=.

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Mbunge, tuko kwenye mshahara wa Mawaziri tu, wewe zungumza unachotaka kusema.

**MHE. FROLENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kimepewa Sh. 800,000/=: Je, hizi pesa zitawahudumia watumishi wote wa pale *headquarters* ama kitawahudumia wakubwa tu? Kwa sababu Sh. 800,000/= ni ndogo sana. Siku hizi tunajua maradhi yalivyo, magonjwa yamekuwa mengi. Utakuta watapata wachache wakubwa, lakini hawawezi kuwahudumiwa watumishi wa chini jambo ambalo linaweza likaleta malalamiko mengi kwa viongozi wao. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Mbunge, tukiwa kwenye kifungu cha Waziri ni sera. Wewe unaweza kuzungumza chochote pale. Sasa kuingia hapa ni *administration and general*. Swali lako ungeuliza ni kitu gani unachouliza. Ongea tu kwa uhuru bila hata vifungu hapa kwa sababu ni mahali pa sera. Simama tena uulize.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Fedha hizi naona ni kidogo sana hazitoshi.

**MWENYEKITU:** Kwa matibabu ya nani?

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Kwa matibabu ya watumishi wa *headquarters*. Yaani watumishi wote pale *headquarter*.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ningombwa kukiri kwamba inawezekana kabisa kwamba hizo fedha zimetengewa pale hazitatosha kukidhi mahitaji ya matibabu ya askari pamoja na wafanyakazi raia ambao wako pale *headquarters*. Niseme tu kwamba kwa wafanyakazi raia wao wako chini ya Bima ya Afya na kwa wafanyakazi askari maagizo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba wote watibiwe na Serikali moja kwa moja. (*Makofî*)

**MWENYEKITU:** Kuna vifungu vingi pale vinavyohusiana na *hospital service* viko humo humo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi yako mengi niliyazungumzia ambayo kwa kweli katika Mji wa Musoma inapaswa Wizara ya Mambo ya Ndani iyashughulikie kwa ajili ya kuwanusuru wananchi wangu. Lakini mbali na hayo niliweza kumwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuja mwenyewe binafsi katika Mji wa Musoma. Kwa sababu amekuwa akija Mara lakini akienda Mkoa wa Kipolisi la Ranya pamoja na Tarime.

**MWENYEKITU:** Uliza swali, dakika chache mno.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Sasa kati ya mambo ambayo ni kero kubwa pale ni pamoja na kwamba hizo nyumba zenyewe tunazosema za Maaskari pale kwangu wanalala kwenye *holly*. Sasa sijui wao wanazaa vipi. Lakini mbali na hiyo ziko zile *barrier* nyingi ambazo zinazuia hata chakula kuingia.

**MWENYEKITU:** Swali la nyumba, basi linatosha. Ni swali moja tu Mheshimiwa Waziri.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Swali langu nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri atakuja lini? Je, yuko tayari kuja Musoma ili tukae tuangalie?

**MWENYEKITU:** Naona umezungumza mpaka Dar es Salaam.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba katika mwaka huu wa fedha itabidi nifike tena Ranya na Tarime na huko huko nikiwa nakwenda nitaelekeea huko Musoma Mjini.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilielezea kazi nzuri inayofanywa na Polisi Wilaya ya Kahama licha ya matatizo ya usafiri na idadi ndogo. Lakini pia nilielezea tatizo la kiutawala ambalo wananchi wanalilalamikia, mimi nimelilalamikia Waziri analifahamu na Polisi, Mkoa na Wilaya wanalifahamu. Ningependa kupata ufanuzi lini tatizo hili litatuliwa? Ahsante.

**MWENYEKITU:** Mheshimiwa Mbunge, Waziri hakuelewa tatizo la utawala gani kwamba kuna nini katika utawala?

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Waziri analifahamu, lakini tatizo kuna mtu pale ambaye kazi yake kila Mara Mkuu wa Polisi anayeletwa wa Wilaya anaondolewa katika kipindi kifupi kadri inavyowezekana. Ni tatizo.

**MWENYEKITU:** Haya Mheshimiwa Waziri nasikia unalijua.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba nimefika pale katika Jimbo la Mheshimiwa Lembeli na

inawezekana kwamba tatizo hilo analolisema lilinipita, lakini tukitoka kwenye Bunge hili nitakaa na Mheshimiwa Lembeli nilielewe hilo tatizo kwa undani na nimfikishie *IGP*.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na katika mchango kwa Waziri Mkuu nilieleza namna gani majambazi yamekuwa yakinambana na wananchi na yakiwa yanawazidi wananchi mchana na nikaeleza namna gani askari wamekuwa wakishindwa kupamba na majambazi wakiwa wamezidiwa hata mchana nikataku kujua kwamba: Je, Serikali ina juhudzi gani ili kuwasaidia wananchi hao kwa sababu mchana hawa Maaskari wamekuwa wakizidiwa? Je, sasa Serikali ina juhudzi gani za kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanasaidiwa na Polisi? Wanaweza wakapambana nao kuweza kukabiliana nao kwa vile wale majambazi wamekuwa wakitumia silaha kubwa. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa najibu hoja hapa mbele ya Bunge lako Tukufu nilieleza wazi kwamba tumeanzisha Mkoa wa Kipolisi wa Tarime – Ranya kwa kutambua kabisa tatizo la ujambazi, wizi wa mifugo na mapigano ya koo. Naamini kabisa kwamba hii kazi ambayo tumeanza rasmi sasa hivi na kwa kuwa tutakuwa tuna *OCD* sita kama nilivyoeleza katika hayo maeneo ambayo niliyataja hapo awali naamini tatizo hili litapungua.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa maandishi nilizungumzia kuhusu mfumo wa kuwalipa wastaifu wa Jeshi la Polisi, kiinua mgongo. Mfumo huu tumezungumza mara nyingi katika Bunge hili na kupata majibu tofauti tofauti na pia tabia hii inafanywa na Jeshi la Polisi tu. Nilitaka kujua, Serikali ina kigugumizi gani kuondoa mfumo huu wa kiinua mgongo na askari wote sasa kuwalipa mfumo mmoja wa pensheni?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina kigugumizi tulishaliongelea leo hili suala mfumo huu wa pensheni pamoja na *gratuity* itaendelea.

**MHE. NURU A. BAFAHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi kuhusu utaratibu unaotumika na askari wa usalama barabarani katika makutano ya barabara ambako kuna sehemu kuna taa barabarani. Utakuta pale ndiyo askari wanasmama na zile sehemu ambazo hakuna mataa hawasimami askari na husababisha msongamano na wakati mwengine ajali kutokea. Kuna nini? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Bafadhili hakuna chochote hapo. Isipokuwa nikuambie tu kweli ni malalamiko ambayo ni sahihi na tutayafanya kazi. Siyo lugha tu ya kusema tutayafanya kazi, kihakika tutayafanya kazi. Ahsante.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tatizo la Meatu sisi ni matukio mengi yanayopelekeea Polisi kukosa mafuta kwa ajili ya kuhudhuria kwenye matukio hayo. Mafuta ambayo tunapangiwa kwa mwezi hayatoshi. Wilaya ya

Meatu ina matukio mengi ya ujambazi, ina matukio mengi ya mauaji ya vikongwe na ina matukio mengi ya wizi wa mifugo. Hata sasa hivi ninavyozungumza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nenda kwenye swali.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninachozungumza ni kwamba ng'ombe wameibiwa, lakini Polisi wetu wamekosa mafuta ya kuwafuatilia. Sasa wakati nachangia kwa maandishi nilimtaka Waziri anisaidie kwa sababu tulishaleta maombi ya kuomba kwamba angalau tuongezewe mafuta katika kipindi hiki cha mpito ambapo Wilaya ina matukio mengi. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumthibishia Mheshimiwa Mpina kwamba ikitokea kuna mahitaji ya mafuta ya ziada pale Meatu naomba anifahamishe, tutajihidi kumfikishia katika kipindi hicho. Sisi kama Wizara tutafanya tathimini kuangalia upya namna tunavyogawa mafuta katika Wilaya zetu nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kutumia kifungu 104(2) *guillotine*.

## **FUNGU 51 – WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Kif. 1001 – <i>Administration and General</i> .. . . . .	Tshs. 1,874,047,300/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> ... . . . . .	Tshs. 387,072,400/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> ... . . . . .	Tshs. 413,312,800/=
Kif. 1004 – <i>Probation and Community Services Division</i> ... . . . . .	Tshs. 1,251,708,000/=
Kif. 1005 – <i>Information, Education and community</i> ... . . . . .	Tshs. 126,920,700/=
Kif. 1006 – <i>Management Information System Unit</i> ... . . . . .	Tshs. 102,683,900/=
Kif. 1007 – <i>Internal Audit unit</i> ... . . . . .	Tshs. 155,178,700/=
Kif. 1008 – <i>Procurement Management Unit</i> ... . . . . .	Tshs. 212,136,700/=
Kif. 1009 – <i>Complaints Division</i> ... . . . . .	Tshs. 637,423,200/=
Kif. 1010 – <i>Legal Services Division</i> ... . . . . .	Tshs. 146,213,700/=
Kif. 3001 – <i>Fire and Rescue Services</i> ... . . . . .	Tshs. 0
Kif. 3002 – <i>Fire and Resare Services Training Institution</i> ... . . . . .	Tshs. 0
Kif. 4001 – <i>Refugees unit</i> ... . . . . .	TShs.822,785,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilitajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## **KITABU CHA NNE**

## FUNGU LA 14 – JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

Kif. 3002 – <i>Fire and Rescue</i>		
<i>Services</i>	... ... ... ... ...	Tshs. 2,500,000/=
Kif. 3002 – <i>Fire Services Training</i>		
<i>Institution</i>	... ... ... ... ...	Tshs. 500,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilitajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## FUNGU 28 – JESHI LA POLISI

Kif. 2001 – <i>Police Mainforce</i>	... ... ...	Tshs. 22,471,815,000/=
Kif. 2002 – <i>Police Marine</i>	... ... ...	Tshs. 399,000,000/=
Kif. 5001 – <i>Police Medical Unit</i>	... ...	Tshs. 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilitajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupitia kifungu kwa kifungu bila mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kufikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yamepita na tunawatakia kazi njema kuanzia watendaji wote wapigaji na Wizara.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma alisimama hapa kutaka mwongozo wa Spika kuhusu kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Soud asubuhi. Mheshimiwa Soud alisema hivi: “Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Bunge lako hili nataka kuzungumzia suala la vitambulisho lakini kwa kupitia Bunge lako hili nataka niombe kwanza sana Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kitambulisho chake kimekaa muda mrefu, anaitwa akakichukue. Kwa hiyo, angalau akifuatilie hicho cha Uzanzibar.”

Sasa maelezo niliyopewa ni kwamba Waziri wa Serikali ya Mapinduzi nadhani katika mazungumzo yao alitamka kwamba kuna vitambulisho fulani havijawahi

kuchukuliwa, kimoja nadhani cha Kiongozi wa Upinzani Bungeni na cha Shoka Khamis Juma. Sasa Shoka hapa ameonyesha kitambulisho halisi alichonipa hapa. Sasa mimi sikuona ubaya wa *statement* hii. Ni kama yeye alivyosikia kwenye redio wanatangaza akawa anamwomba Shoka Khamis Juma aende akachukue na amekichukua. Ni kitambulisho halisi Bwana Shoka Khamis Juma alichonacho. Kwa hiyo, naomba tusiingie kwenye malumbano maana yake lugha hii ni ya *Hansard* siyo lugha ambayo mimi nimetoa. Siku hizi watu wetu wanafanya kazi nzuri sana *Hansard*. Ni lugha iliyoko ya *Hansard* haina maudhi wala haina nini, ni kwamba ukakichukue sasa kumbe wewe uliwahi yeye hakujua. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kesho saa na nusu Kamati ya Uongozi ya Bunge itakutana katika Ukumbi wa Spika. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 2.15 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 9 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)